# HALI YA UCHUMI WA TAIFA

# KATIKA MWAKA 2013

## YALIYOMO


**ORODHA YA MAJEDWALI ........ IX**

**KIREFU/TAFSIRI YA MANENO ........ XIV**

**MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KWA MWAKA 2013 ........ XVIII**

**SURA YA I ........ 1**

**HALI YA UCHUMI WA TAIFA ........ 1**

UKUAJI WA UCHUMI ........ 1
MWENENDO WA BEI ........ 6
UKUZAJI RASILIMALI ........ 8

**SURA YA 2 ........ 38**

**HALI YA UCHUMI DUNIANI NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA ........ 38**

UKUAJI WA UCHUMI DUNIANI ........ 38
MWENENDO WA BIASHARA DUNIANI ........ 39
HALI YA UCHUMI WA NCHI ZA AFRIKA KUSINI MWA JANGWA LA SAHARA ........ 39
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ........ 41
UMOJA WA AFRIKA NA TUME YA UCHUMI YA BARA LA AFRIKA ........ 41
SHIRIKISHO LA BIASHARA ULIMWENGUNI ........ 42

**SURA YA 3 ........ 43**

**SEKTA YA NJE ........ 43**

UTANGULIZI ........ 43
BIDHAA ZILIZOUZWA NJE ........ 43
*Bidhaa Asilia ........ 43*
*Bidhaa Zisizo Asilia ........ 45*
MAPATO YA HUDUMA ........ 48
BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA NJE ........ 48
*Bidhaa za Kukuza Mitaji ........ 48*
*Bidhaa za Kati ........ 48*
*Bidhaa za Matumizi ya Kawaida ........ 49*
MALIPO YA HUDUMA ........ 49
MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI MBALIMBALI ........ 49
MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE ........ 53
AKIBA YA FEDHA ZA KIGENI ........ 55
SOKO LA FEDHA ZA KIGENI KWA MABENKI ........ 55
THAMANI YA FEDHA YA TANZANIA ........ 55

**SURA YA 4** .......... **69**

**FEDHA ZA SERIKALI** .......... **69**

UTANGULIZI .......... 69
MWENENDO WA MAPATO .......... 70
*Mapato ya Ndani* .......... *70*
*Misaada na Mikopo Nafuu* .......... *70*
MIKOPO YA KIBIASHARA YA NDANI .......... 71
MIKOPO YA KIBIASHARA KUTOKA NJE .......... 71
MATUMIZI .......... 71

**SURA YA 5** .......... **81**

**FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA** .......... **81**

UJAZI WA FEDHA NA KARADHA .......... 81
MIKOPO YA BENKI ZA BIASHARA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI .......... 82
AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA .......... 83
MWENENDO WA VIWANGO VYA RIBA .......... 84
MABORESHO KATIKA SEKTA YA BENKI .......... 85
MAENDELEO YA UKUAJI WA SOKO LA MIKOPO YA NYUMBA TANZANIA .......... 86
MAMLAKA YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SEKTA YA HIFADHI YA JAMII .......... 89
MFUKO WA PENSHENI KWA WATUMISHI WA UMMA .......... 90
MFUKO WA TAIFA WA HIFADHI YA JAMII .......... 91
MFUKO WA AKIBA YA WAFANYAKAZI WA SERIKALI .......... 92
MFUKO WA PENSHENI WA MASHIRIKA YA UMMA .......... 92
MFUKO WA PENSHENI WA SERIKALI ZA MITAA .......... 93
MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA .......... 94
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA BIMA TANZANIA .......... 96
MAENDELEO YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA .......... 98
BENKI YA POSTA .......... 99

**SURA YA 6** .......... **106**

**RASILIMALI WATU** .......... **106**

IDADI YA WATU .......... 106
MGAWANYIKO WA WATU KIMKOA .......... 106
NGUVUKAZI NA AJIRA .......... 109

**SURA YA 7** .......... **115**

**UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI** .......... **115**

UWEKEZAJI MITAJI YA KIGENI YA MOJA KWA MOJA .......... 115
UBORESHAJI WA MAZINGIRA WEZESHI KWA SEKTA BINAFSI .......... 116
UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI .......... 117
MFUKO WA UWEZESHAJI WANANCHI .......... 118

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira ....................................................118

**SURA YA 8 ....................................................................................................120**

**MASUALA MTAMBUKA ......................................................................................120**

UKIMWI ....................................................................................................120
Mazingira ....................................................................................................121
Utawala Bora ....................................................................................................123
Jinsia ....................................................................................................124
Usalama wa Raia....................................................................................................125

**SURA YA 9 ....................................................................................................128**

Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato....................................................128
Kuboresha Maisha na Ustawi wa Jamii ....................................................132
Utawala Bora na Uwajibikaji....................................................133

**SURA YA 10 ....................................................................................................136**

**MCHANGO WA GESI NA MAFUTA KATIKA UCHUMI..............................................136**

Historia ya Utafutaji wa Mafuta na Gesi Nchini....................................................136
Sheria, Sera na Kanuni Katika Masuala ya Gesi na Mafuta Nchini .......................139
Maeneo Yaliyogunduliwa Mafuta na Gesi, Kiwango cha Uzalishaji na Matumizi ....................................................................................................139
Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi....................................................141
Mradi wa LNG (*Liquified Natural Gas*)....................................................143
Ushirikishwaji wa Wananchi Katika Shughuli za Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi ....................................................................................................143
Umuhimu na Mchango wa Mafuta na Gesi katika Uchumi ....................................................144
Changamoto na mikakati iliyowekwa na Serikali kukabiliana nayo .....................147
Matarajio ....................................................................................................149

**SURA YA 11 ....................................................................................................152**

**KILIMO NA USHIRIKA ....................................................................................................152**

Kiwango cha Ukuaji....................................................................................................152
Uzalishaji wa Mazao ya Chakula....................................................................................................152
Uzalishaji wa Mazao ya Biashara ....................................................................................................153
Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta....................................................................................................153
Uwekezaji katika Shughuli za Kiuchumi za Kilimo....................................................154
Kilimo cha Umwagiliaji....................................................................................................154
Huduma za Ugani na Mafunzo ....................................................................................................155
Shughuli za Utafiti....................................................................................................156
MIFUGO ....................................................................................................156
*Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake....................................................................................................156*
*Biashara ya Mifugo na Mazao Yake ....................................................................................................158*

Maendeleo ya Ushirika ... 160

**SURA YA 12 ... 170**

**MALIASILI NA UTALII ... 170**

Kiwango cha ukuaji ... 170
Misitu na Nyuki ... 170
Wanyamapori ... 172
Utalii ... 175
Malikale ... 176
Uvuvi ... 178

**SURA YA 13 ... 192**

**MADINI ... 192**

Kiwango cha Ukuaji ... 192
Utafutaji Madini ... 192
Uendelezaji wa Uchimbaji Mdogo wa Madini ... 192
Uchimbaji na Uuzaji Madini ... 194
Thamani ya Mauzo ya Madini ... 195

**SURA YA 14 ... 198**

**VIWANDA NA BIASHARA ... 198**

Kiwango cha Ukuaji ... 198
Viwanda Vidogo ... 198
Gharama za Uzalishaji ... 198
Maendeleo ya Teknologia kwa Wajasiriamali ... 199
Utoaji wa Elimu kwa Wajasiriamali Wanaosindika Mazao ... 200
Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa ... 200

**SURA YA 15 ... 209**

**UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI ... 209**

UJENZI ... 209
*Kiwango cha Ukuaji ... 209*
*Mtandao wa Barabara ... 209*
*Matengenezo ya Barabara na Madaraja ... 210*
*Bodi ya Mfuko wa Barabara ... 211*
*Bodi ya Usajili wa Makandarasi ... 211*
*Bodi ya Usajili ya Wahandisi ... 212*
*Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ... 213*
*Baraza la Taifa la Ujenzi ... 214*
*Wakala wa Majengo Tanzania ... 215*
*Wakala wa Ufundi na Umeme ... 215*

MAENDELEO YA ARDHI ....................................................................................................215
*Upimaji wa Mipaka ya Vijiji*...............................................................................................*215*
*Ukaguzi, Uhakiki na Utayarishaji wa Hatimiliki*..............................................................*217*
*Utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji na Hati za Hakimiliki za Kimila*..............................*218*
*Usajili wa Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria*...................................................................*218*
*Upimaji wa Mashamba na Viwanja*.....................................................................................*218*
*Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya*.........................................................................*219*
*Mipango ya Matumizi ya Ardhi*...........................................................................................*220*
MAENDELEO YA MAKAZI ................................................................................................220
*Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara*.......................................................................*220*

**SURA YA 16 .......................................................................................................................222**

**MAWASILIANO NA UCHUKUZI ...................................................................................222**

KIWANGO CHA UKUAJI.........................................................................................................222
USAFIRI WA BARABARA .......................................................................................................222
USAFIRI WA MAJINI...............................................................................................................224
KAMPUNI YA RELI TANZANIA (TRL) ..................................................................................224
MAMLAKA YA RELI YA TANZANIA NA ZAMBIA (TAZARA) ................................................224
USAFIRI WA ANGA.................................................................................................................225
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA ..........................................................228
UCHUKUZI KWENYE MAZIWA .............................................................................................230
KAMPUNI YA MELI YA CHINA NA TANZANIA .....................................................................230
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA ..........................................................................230
HUDUMA ZA MAWASILIANO.................................................................................................231
*Shirika la Posta Tanzania*....................................................................................................*231*
*Mawasiliano kwa Njia ya Sauti na Takwimu*.......................................................................*233*
TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO ......................................................................234
*Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano*.......................................................................................*234*
SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU ...................................................................................235
*Udhibiti wa Mionzi* ...............................................................................................................*235*
*Vyombo vya Habari* ..............................................................................................................*235*

**SURA YA 17 .......................................................................................................................244**

**NISHATI ..............................................................................................................................244**

KIWANGO CHA UKUAJI.........................................................................................................244
UFUAJI WA UMEME ...............................................................................................................244
UTAFUTAJI MAFUTA NA GESI...............................................................................................249
UAGIZAJI NA MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA...................................................................252
NISHATI MBADALA ...............................................................................................................254
*Maporomoko Madogo ya Maji* .............................................................................................*254*
*Nishati ya Mionzi ya Jua*.......................................................................................................*255*
*Tungamotaka (Biomass)* .......................................................................................................*255*

*Jotoardhi* ... *256*

**SURA YA 18** ... **257**

**MAJI** ... **257**

Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji ... 257
Huduma ya Maji Vijijini ... 258
Huduma za Maji Mijini ... 258

**SURA YA 19** ... **261**

**ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** ... **261**

Elimu ya Awali ... 261
Elimu ya Msingi ... 262
Elimu ya Sekondari ... 264
Elimu ya Ualimu ... 265
Elimu ya Watu Wazima na Mfumo Usio Rasmi ... 266
Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu ... 267
Elimu ya Ufundi na Mafunzo ... 267
Elimu ya Ufundi Stadi ... 268
Elimu ya Juu ... 268

**SURA YA 20** ... **275**

**AFYA** ... **275**

Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya ... 275
Elimu ya Afya kwa Wananchi ... 276
Afya ya Uzazi na Mtoto ... 277
Mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria ... 278
Mpango wa Damu Salama ... 278
Magonjwa ya kuambukiza na ya mlipuko ... 278
Chakula na Lishe ... 278
Huduma za Ustawi wa Jamii ... 279

**SURA YA 21** ... **283**

**MAENDELEO YA JAMII** ... **283**

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ... 283
Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ... 283
Benki ya Wanawake ... 284
Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ... 284
Maendeleo ya Watoto ... 284
Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ... 285

**Ukurasa**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali A: Takwimu Muhimu Katika Uchumi – Tanzania Bara ................ .xx

Jedwali B: Mwenendo wa Viashiria vya Kiuchumi, 2006 – 2013…........xxi

Jedwali 1: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika)...................................................... 10

Jedwali 1A Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko – Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za miaka inayohusika)........................................................ 11

Jedwali 2: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa kwa Bei za Soko (bei za miaka inayohusika) ................................. 12

Jedwali 2A: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko- Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za miaka inayohusika)....................................................... 13

Jedwali 2B: Pato la Taifa (PLT) na Matumizi yake, kwa bei za soko (bei za miaka inayohusika)........................................................ 14

Jedwali 3: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (bei za mwaka 2001)............................................. 15

Jedwali 3A: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za mwaka 2001) .................................................................. 16

Jedwali 4: Ukuaji wa Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (bei za mwaka 2001) ...................................... 17

Jedwali 4A: Ukuaji wa Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za mwaka 2001) .................................................................. 18

Jedwali 4B: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko (bei za mwaka 2001) ..................................... 20

Jedwali 4C: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko -Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za mwaka 2001) .................................................................. 23

Jedwali 4D: Pato la Taifa (PLT) na matumizi yake, kwa bei za soko (bei za mwaka 2001) ................................................................. 24

Jedwali 5: Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya shughuli (bei za miaka inayohusika)................................................................25

Jedwali 6: Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya shughuli(bei za mwaka2001).26

Jedwali 7: Ukuzaji Rasilimali (sekta za umma na binafsi)........................... 27

Jedwali 8: Fahirisi ya bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini Dar es Salaam (2001=100) ........... 28

Jedwali 9: Fahirisi ya bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini Dar es Salaam (2001=100) ........... 29

Jedwali 10: Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na wafanyakazi wa kima cha kati Dar es Salaam (2001=100).................................................................................. 30

Jedwali 11: Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na Wafanyakazi wa kima cha kati Dar es Salaam (2001=100)........ 31

Jedwali 12: Fahirisi ya gharama ya maisha ya wenye kipato cha juu Dar es Salaam (2001=100) ........................................... 32

Jedwali 13: Fahirisi ya gharama ya maisha wenye kipato cha juu Dar es Salaam (2001=100).................................................... 33

Jedwali 14: Fahirisi ya bei ya bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2001=100) ...................... 34

Jedwali 15: Fahirisi ya Bei ya Bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2001=100) ...................... 35

Jedwali 16: Fahirisi mbali mbali za bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini – Tanzania Bara (2001=100) .......................... 37

Jedwali 17: Thamani ya Bidhaa za biashara baina ya Tanzania na nchi za nje (Sh. Milioni)........................................................ 56

Jedwali 18: Kiasi na thamani ya bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh. Milioni) .................................................................... 57

Jedwali 19: Kiasi na thamani ya bidhaa za asilia na zisizo asilia zilizouzwa nchi za nje....................................................... 58

Jedwali 20: Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh./tani) .................................................................. 63

Jedwali 21: Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (US $/tani)................................................................. 64

Jedwali 23: Aina na thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za nje (Sh. Milioni).............................................................. 66

Jedwali 24: Mizania ya malipo na nchi za nje (US$ milioni) ........................ 67

Jedwali 25: Mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali (Sh. Milioni).... 77

Jedwali 26: Mgawanyo wa Matumizi ya Serikali kwa huduma mbalimbali (Sh. Milioni)........................................................... 79

Jedwali 27: Mwenendo wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania Bara...... 101

Jedwali 28: Viwango vya ukuaji wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania Bara...................................................................... ..102

Jedwali 29: Mwenendo wa Viwango vya ubadilishaji kati ya Shilingi na Dola ya Marekani.................................................................... 103

Jedwali 30: Mikopo ya benki za biashara kwa Shughuli za Kiuchumi... ..... 104

Jedwali 31: Mwenendo wa amana katika benki za biashara ...................... 105

Jedwali 32: Viwango vya wastani vya riba (asilimia) ............................... 105

Jedwali 33: Idadi ya watu nchini Tanzania kimkoa (2005-2013)............... 111

Jedwali 34: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC): Miradi iliyopitishwa .... 119

Jedwali 35: Uzalishaji wa miwa na sukari Nchini.................................... ...161

Jedwali 36: Pamba iliyonunuliwa na mauzo nchini .................................... 162

Jedwali 37: Eneo lililopandwa michai na majani mabichi yaliyopatikana .......................................................................... 163

Jedwali 38: Kahawa iliyonunuliwa na mauzo nchini ................................. 164

Jedwali 39: Eneo lililopandwa mkonge na katani iliyopatikana ................. 165

Jedwali 40: Tumbaku iliyonunuliwa na mauzo nchini ................................ 166

Jedwali 41: Maua ya pareto yaliyonunuliwa na mauzo ya bidhaa za pareto nchini ........................................................... 167

Jedwali 42: Korosho zilizonunuliwa na mauzo nchini. ............................... 168

Jedwali 43: Muhtasari wa kiasi cha mazao muhimu ya biashara yaliyonunuliwa........................................................................ 169

Jedwali 45: Idadi ya Wageni Waliotembelea Makumbusho ya Taifa .......... 181

Jedwali 47: Mauzo ya bidhaa za misitu na nyuki katika masoko ya nchi za nje .............................................................. 182

Jedwali 48: Mwenendo wa biashara ya ndege, wanyamapori na vipusa nchi za nje...................................................................... 183

Jedwali 48A: Mwenendo wa biashara ya wanyama hai na uwindaji wa kitalii ..... 184

Jedwali 48B: Idadi ya Wawindaji wa Kitalii ..... 184

Jedwali 50: Uzalishaji katika sekta ya uvuvi ..... 185

Jedwali 51: Mauzo ya mazao ya uvuvi nchi za nje ..... 186

Jedwali 51A: Muhtasari wa Mauzo ya Mazao ya Uvuvi Nchi za Nje ..... 187

Jedwali 51B: Mwelekeo wa Mauzo ya Sangara Nje ya Nchi ..... 187

Jedwali 52: Mwenendo wa Biashara ya Utalii ..... 188

Jedwali 53: Idadi ya Watalii walioingia nchini na kiasi cha fedha zilizopatikana ..... 189

Jedwali 55: Idadi ya wageni waliotembelea Vituo vya Utalii ..... 190

Jedwali 55A: Wageni waliotembelea Vituo vya Makumbusho ..... 191

Jedwali 56: Uchimbaji wa madini: Kiasi kilichopatikana ..... 196

Jedwali 57: Madini yaliyouzwa nchi za nje ..... 197

Jedwali 58: Matumizi ya saruji nchini ..... 202

Jedwali 59: Uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani ..... 203

Jedwali 60: Viwanda - Idadi ya Watu walioajiriwa ..... 204

Jedwali 61: Viwanda - Gharama za kazi ..... 205

Jedwali 62: Viwanda - Muhtasari wa matokeo ..... 206

Jedwali 63: Viwanda - Muhtasari wa matokeo kimkoa ..... 207

Jedwali 65: Vigezo vya Ufanisi katika Sekta ya Viwanda ..... 208

Jedwali 67: Shirika la Reli Tanzania (TRL) ..... 237

Jedwali 68: Reli ya Uhuru (TAZARA) ..... 238

Jedwali 69: Usafirishaji kwa Meli ..... 239

Jedwali 70: Huduma za Posta ..... 242

Jedwali 73: Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ..... 243

Jedwali 74: Uwezo wa mitambo ya umeme na kiasi cha umeme uliotengenezwa kwa vituo ..... 246

Jedwali 75: Mauzo ya umeme kwa watumiaji mbalimbali ......................... 247

Jedwali 76: Mauzo ya umeme kwa mikoa.................................................... 248

Jedwali 77: Uzalishaji wa maji na mapato yatokanayo na maji ..............260

Jedwali 80: Shule za sekondari za Serikali - Idadi ya wanafunzi kwa kidato ............................................................ ..... ..........270

Jedwali 81: Shule za sekondari za binafsi - Idadi ya wanafunzi kwa kidato .................................................................................. 274

Jedwali 84: Idadi ya Vituo vya Kutolea Huduma za afya nchini ................. 280

Jedwali 85: Huduma za Afya: waliofaulu mafunzo ya Afya....................... 281

Jedwali 87: Idadi ya Vitanda katika Hospitali zote Nchini....................282

## KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| ASDP | - | Agricultural Sector Development Programme (Program ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo) |
| AfDB | - | African Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Afrika) |
| ARVs | - | Anti-retrovirals ( Dawa za Kupunguza Makali ya UKIMWI) |
| TAA | - | Tanzania Airpots Authority (Mamlaka ya Viwanja vya Ndege) |
| AU | - | African Union (Umoja wa Afrika) |
| BoT | - | Bank of Tanzania (Benki Kuu ya Tanzania) |
| Cif | - | Cost, insurance and freight (Thamani ya bidhaa ikijumuisha gharama za usafiri na bima) |
| CPI | - | Consumer Price Index (Fahirisi ya Bei za Walaji) |
| CRDB | - | Benki ya CRDB |
| COICOP | - | Classification of Individual Consumption by Purpose |
| COMESA | - | Common Market for Eastern and Southern Africa (Soko la Pamoja la Nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika) |
| CUM | - | City Urgent Mail (Kampuni ya usambazaji barua za haraka Mijini) |
| CHMT | - | Council Health Management Team (Kamati za Afya za Halmashauri) |
| CHF | - | Community Health Fund (Mfuko wa Jamii wa Afya) |
| DSE | - | Dar es Salaam Stock Exchange (Soko la Hisa la Dar Es Salaam) |
| DADPs | - | District Agricultural Development Plans (Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya) |
| ECA | - | Economic Commission for Africa (Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika) |
| EAC | - | East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki) |
| EPZA | - | Export Processing Zone Authority (Mamlaka ya Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje) |
| EPZ | - | Export Processing Zones (Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje) |
| EWURA | - | Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati) |
| EFD | - | Electronic Fiscal Divices Machines (Mashine za Kielektroniki) |
| f.o.b | - | free on board (Thamani ya Bidhaa bila Kujumuisha Gharama za Usafiri na Bima |
| FDI | - | Foreign Direct Investment (Uwekezaji wa Mitaji ya Kigeni) |
| GEPF | - | Government Employees Provident Fund (Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali) |
| GBS | - | General Budget Support (Misaada na Mikopo ya Bajeti) |
| GDP | - | Gross Domestic Product (Pato la Taifa) |
| HBS | - | Household Budget Survey (Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya) |

| | | |
|---|---|---|
| IFMS | - | Integrated Financial Management System (Mfumo Tungamanishi wa Usimamizi wa Fedha) |
| LGRP | - | Local Government Reform Programme (Programu ya Maboresho katika Serikali za Mitaa) |
| LAPF | - | Local Authorities Pensions Fund (Mfuko wa Pension wa Serikali za Mitaa) |
| LSRP | - | Legal Sector Reform Programme (Programu ya Maboresho katika Sekta ya Sheria) |
| MTEF | - | Medium Term Expenditure Framework (Mfumo wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Serikali) |
| $M_2$ | - | Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana) |
| $M_3$ | - | Extended Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi) |
| IMF | - | International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa) |
| MDGs | - | Millenium Development Goals (Malengo ya Maendeleo ya Milenia) |
| MKUKUTA | - | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania |
| MPAMITA | - | Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania |
| MKURABITA | - | Mpango wa Kurasimisha Biashara na Mali za Wanyonge Tanzania |
| MMEM | - | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi |
| MMES | - | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari |
| MMS | - | MKUKUTA Monitoring System (Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA) |
| MSCL | - | Marine Services Company Ltd (Kampuni ya Huduma za Meli) |
| MSMEs | - | Medium, Small and Micro Enterprises (Viwanda vya Kati, Vidogo na Vidogo sana) |
| MUKEJA | - | Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii |
| MEMKWA | - | Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Waliyoikosa |
| MMAM | - | Mpango Maalum wa Afya ya Msingi |
| MW | - | Mega Watts |
| NDC | - | National Development Corporation (Shirika la Maendeleo la Taifa) |
| NSSF | - | National Social Security Fund (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii) |
| NFRA | - | National Food Reserve Agency (Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula) |
| NASCAP | - | National Anti-Corruption Strategy and Action Plan (Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa) |
| NGO’s | - | Non-Governmental Organisations (Asasi Zisizo ya Kiserikali) |
| NHIF | - | National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya) |
| NIC | - | National Insurance Corporation (Shirika la Bima la Taifa) |

| | | |
|---|---|---|
| NMB | - | National Microfinance Bank (Benki ya Taifa ya Mikopo Midogo) |
| OSBP | - | One - Stop - Border Posts ( Vituo vya Pamoja Mipakani) |
| PSRP | - | Public Service Reform Program (Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma) |
| PRS | - | Poverty Reduction Strategy (Mkakati wa Kupunguza Umaskini) |
| PAP | - | Priority Action Plan (Vipaumbele vya Utekelezaji). |
| PSPF | - | Public Service Pensions Fund (Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma) |
| PPF | - | Parastatal Pensions Fund (Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma) |
| PFMRP | - | Public Financial Management Reform Programme (Program ya Maboresho ya Fedha za Umma) |
| RAHCO | - | Railway Holding Company (Kampuni Miliki ya Rasilimali za Reli) |
| RUBADA | | Rufiji Basin Development Authority (Mamlaka ya Uendeshaji wa Bonde la Mto Rufiji) |
| RITA | - | Registration, Insolvency and Trusteeship Agency (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini) |
| SIDO | - | Small Industries Development Organization (Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo) |
| SAGCOT | - | Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania ( Ukanda wa Kilimo Kusini mwa Tanzania) |
| SACCOS | - | Savings and Credit Cooperative Societies (Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo) |
| SADC | - | Southern Africa Development Community (Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika) |
| SMEs | - | Small and Medium Enterprises (Viwanda Vidogo na vya Kati) |
| SELF | - | Small Enterpreneurs Loan Facility (Mradi wa Kuhudumia Biashara Ndogondogo) |
| SSRA | - | Social Security Reguratory Authority (Mamlaka ya Usimamizi na udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii) |
| SUMATRA | - | Surface and Marine Transport Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini) |
| TMRC | - | Tanzania Mortgage Refinancing Company ( Kampuni ya Utoaji Mikopo ya Nyumba) |
| TaESA | - | Tanzania Employment Service Agency (Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania) |
| TANESCO | - | Tanzania Electricity Supply Company (Shirika la Umeme Tanzania) |
| TANROADS | - | Tanzania Roads Agency (Mamlaka ya Barabara Tanzania) |

| | | |
|---|---|---|
| TAZARA | - | Tanzania Zambia Railway Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia) |
| TDHS | - | Tanzania Demographic and Health Survey (Utafiti wa Afya na Demografia Tanzania) |
| TIRA | - | Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania) |
| TCAA | - | Tanzania Civil Aviation Authority (Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania) |
| TMA | - | Tanzania Meteorology Agency (Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania) |
| TCRA | - | Tanzania Communications Regulatory Authority (Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania). |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TICTS | - | Tanzania International Container Terminal Services (Kampuni ya Kupakua Makontena katika Bandari ya Dar es Salaam) |
| TRC | - | Tanzania Railways Corporation (Shirika la Reli Tanzania) |
| TRL | - | Tanzania Railways Company Limited (Kampuni ya Reli Tanzania) |
| TTCL | - | Tanzania Telecomunications Company Limited (Kampuni ya Simu Tanzania) |
| UPU | - | Universal Postal Union |
| UAE | - | United Arab Emirates (Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu) |
| UFI | - | Global Association of the Exhibition Industry – Fomerly known, Union Des Foires Internationales (Shirika la Maonesho ya Dunia) |
| UNIDO | - | United Nations Industrial Development Organization (Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda) |
| UKIMWI | - | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| VVU | - | Virusi Vya Ukimwi |
| WEF | - | World Economic Forum (Mdahalo wa Uchumi Duniani) |

## MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KWA MWAKA 2013

| TAREHE | MWEZI | MATUKIO |
|---|---|---|
| 07 | Feb | Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania azindua mfumo wa usajili na utambuzi wa watu na utoaji wa vitambulisho vya taifa. |
| 31 | Mei | Rais atangaza kuanzishwa kwa chombo cha kusimamia ufuatiliaji wa utekelezaji wa program na miradi ya maendeleo kwenye maeneo ya kimkakati ya kitaifa kijulikanacho kama *"President's Delivery Bureau PDB*". |
| 24 | Mei | Rais azindua Mpango wa Matokeo Makubwa sasa. |
| 13 | Juni | Siku ya bajeti kwa Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki. |
| 28 | Juni | Rais Jakaya Mrisho Kikwete azindua Mkutano wa Kimataifa wa Majadiliano ya Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote (*Smart Partnership*). |
| 1-2 | Julai | Rais wa Marekeni Barack Obama afanya ziara ya siku mbili Tanzania na kuzindua Mpango wa Umeme Afrika (*Power Africa*). |
| 30 | Novemba | Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa pamoja watia saini itifaki ya Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki. |
| 29 | Oktoba | Waziri Mkuu azindua matokeo ya awali ya Taarifa ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2011/12. |
| 13 | Desemba | Serikali yatoa tangazo (Tangazo la Serikali Na. 443) kuyaalika makundi mbalimbali kuwasilisha mapendekezo ya majina kwa ajili ya uteuzi katika Bunge Maalum la Katiba kwa mujibu wa Kifungu Na. 22(1c) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. |
| 30 | Desemba | Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania apokea rasimu ya pili ya mapendekezo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. |

Jedwali Na. A

**TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA**

| Maelezo | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013p | 2012-13 Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watu (milioni) | 39.5 | 40.7 | 41.9 | 43.2 | 43.6 | 44.8 | 2.8 |
| Pato la Taifa kwa Bei za miaka inayohusika (Sh. milioni) | 24754457.1 | 28212646.0 | 32293479.0 | 37532962.2 | 44717663.3 | 53174678.3 | 18.9 |
| Pato la Taifa kwa Bei za mwaka 2001 (Sh. milioni) | 14828344.8 | 15721301.0 | 16828563.0 | 17913803.1 | 19155764.9 | 20489149.6 | 7.0 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika (Sh.) | 627097.2 | 693470.1 | 770464.3 | 869436.3 | 1025038.4 | 1186199.8 | 15.7 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za 2001 (Sh.)** | 375642.0 | 386431.4 | 401499.2 | 414966.2 | 439097.1 | 457063.9 | 4.1 |
| Kasi ya Upandaji Bei (asilimia) | 10.3 | 12.3 | 5.5 | 12.7 | 16.0 | 7.9 | -50.6 |
| Urari wa Biashara ya Bidhaa (US$ milioni) | -3433.5 | -2536.1 | -2841.2 | -4729.6 | -4429.9 | -5680.2 | 28.2 |
| Urari wa Bidhaa,Huduma na Uhamisho wa Mali (US$ milioni) | -1703.1 | -1809.9 | -1960.1 | -3992.2 | -3792.0 | -4657.1 | 22.8 |
| Saruji Iliyotumika (Tani '000) | 1755.8 | 1940.8 | 2312.0 | 2408.8 | 2581.4 | 2345.6 | -9.1 |
| Umeme Uliouzwa (KWH milioni) | 4425.4 | 4802.1 | 5137.8 | 5156.2 | 5855.7 | 5997.3 | 2.4 |
| Utalii (Mapato US$ milioni) | 1354.0 | 1159.8 | 1254.5 | 1324.8 | 1712.8 | 1806.3 | 5.5 |
| Reli: Uchukuzi Mizigo (Tani '000) | 954.0 | 570.0 | 805.0 | 386.0 | 413.0 | 430.0 | 4.1 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Msingi ('000) * | 84372.4 | 84415.5 | 84193.0 | 83633.9 | 8247.2 | 8231.9 | -0.2 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Sekondari ('000) * | 1222.4 | 1466.4 | 1638.7 | 1711.1 | 1884.3 | 1804.1 | -4.3 |
| Hospitali: Idadi ya Vitanda | 37228.0 | 40118.0 | 45241.0 | 48480.0 | 47484.0 | 49755.0 | 4.8 |
| **Mauzo Nje ya Mazao Muhimu ya Biashara (mil. US$)** | | | | | | | |
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | |
| Kahawa | 103.32 | 111.66 | 117.31 | 142.64 | 186.61 | 170.99 | -8.4 |
| Pamba | 80.87 | 111.15 | 97.79 | 61.64 | 164.93 | 111.73 | -32.3 |
| Katani | 15.68 | 6.73 | 10.90 | 16.93 | 18.37 | 16.93 | -7.8 |
| Chai | 41.96 | 34.50 | 49.79 | 47.17 | 56.06 | 56.91 | 1.5 |
| Tumbaku | 175.92 | 127.29 | 232.38 | 281.24 | 350.05 | 307.02 | -12.3 |
| Korosho | 69.37 | 71.51 | 96.92 | 106.99 | 142.58 | 162.41 | 13.9 |
| Karafuu | 13.52 | 14.73 | 7.61 | 28.88 | 38.08 | 42.96 | 12.8 |
| **Bidhaa zisizo Asilia** | | | | | | | |
| Madini | 1186.74 | 1274.83 | 1561.18 | 2283.41 | 2197.79 | 1861.16 | -15.3 |
| Bidhaa za Viwanda | 741.83 | 506.49 | 964.05 | 861.52 | 1037.34 | 1072.07 | 3.3 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | 184.69 | 154.98 | 150.36 | 137.67 | 160.56 | 130.55 | -18.7 |
| Mazao ya Mboga na Maua | 45.67 | 33.34 | 30.77 | 36.40 | 31.33 | 28.13 | -10.2 |
| Bidhaa zilizouzwa tena (Re-export) | 285.52 | 282.86 | 338.15 | 330.15 | 181.70 | 172.77 | -4.9 |
| Bidhaa nyinginezo | 160.29 | 120.36 | 132.48 | 98.32 | 555.66 | 517.63 | -6.8 |
| **Ujazi wa Fedha** | | | | | | | |
| Ujazi wa Fedha-M3 (Sh. bilioni) [2] | 7458.8 | 8780.1 | 11012.7 | 13021.3 | 14647.1 | 16106.8 | 10.0 |
| Karadha (Sh. bilioni) | 6753.9 | 7857.6 | 9522.8 | 10958.1 | 13719.0 | 16293.0 | 18.8 |
| **Fedha za serikali** | **2008/09** | **2009/10** | **2010/11** | **2011/12** | **2012/13** | **2013/14** | **2012/13-13/14 Badiliko (%)** |
| Mapato ya Kawaida ya Serikali (Sh. bilioni) | 4293075 | 4661540 | 5736266.1 | 7221408.6 | 8442610.8 | 11537522.6 | 36.7 |
| Matumizi ya Kawaida ya Serikali (Sh. bilioni) | 4681459 | 5562443 | 6690370.0 | 6989806.6 | 9043323.0 | 11065984.0 | 22.4 |
| Matumizi ya Maendeleo ya Serikali (Sh. bilioni) | 2130.4 | 2611.3 | 2749037.2 | 3774721.7 | 4499695.2 | 5644989.1 | 25.5 |

Chanzo: Wizara ya Fedha

* Kwa shule za serikali na binafsi

** Kuanzia 1998 ni kwa bei za mwaka 2001

[1] Kwa mwaka wa masomo unaoishia mwaka unaohusika

[2] Kwa tafsiri pana (M3)

\- Takwimu hazikupatikana

\- [P] Takwimu za Awali

## Jedwali Na. B: Mwenendo wa Viashiria vya Ukuaji wa Uchumi, 2006 - 2013

| | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PATO LA TAIFA** | | | | | | | | |
| Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa (mp) | 6.7% | 7.1% | 7.4% | 6.0% | 7.0% | 6.4% | 6.9% | 7.0% |
| Ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika (mp) | 12.4% | 16.8% | 18.3% | 13.8% | 14.5% | 16.2% | 19.1% | 18.9% |
| **MWENENDO WA BEI** | | | | | | | | |
| Kasi ya upandaji bei (mwisho wa kipindi) | 6.7% | 6.4% | 13.5% | 12.2% | 5.6% | 19.8% | 12.1% | 5.6% |
| Kasi ya upandaji bei (Wastani wa mwaka) | 7.3% | 7.0% | 10.3% | 12.1% | 7.6% | 12.6% | 16.0% | 7.9% |
| GDP deflator inflation (fc) | 4.5% | 8.9% | 10.1% | 7.2% | 7.3% | 9.2% | 11.7% | 11.5% |
| GDP deflator inflation (mp) | 5.3% | 9.0% | 10.1% | 7.4% | 6.9% | 9.2% | 11.4% | 11.2% |
| **UJAZI WA FEDHA** | | | | | | | | |
| Kiwango cha ukuaji wa M3 | 21.5% | 20.5% | 19.8% | 17.7% | 25.4% | 18.2% | 13.1% | 10.0% |
| Kiwango cha ukuaji wa M2 | 16.7% | 27.2% | 24.4% | 20.8% | 21.8% | 15.0% | 16.0% | 10.9% |
| Kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi | 40.1% | 43.1% | 44.6% | 9.6% | 20.0% | 27.2% | 18.2% | 15.3% |
| **UWIANO WA MIZANIA YA MALIPO YA NJE NA PATO LA TAIFA** | | | | | | | | |
| Bidhaa zilizouzwa nje | 13.4% | 13.2% | 17.3% | 15.2% | 18.8% | 21.1% | 21.0% | 21.7% |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 24.1% | 24.3% | 26.9% | 23.8% | 27.6% | 30.6% | 30.2% | 29.3% |
| Bidhaa zilizonunuliwa kutoka nje | 27.1% | 28.8% | 33.8% | 27.0% | 31.0% | 40.8% | 36.2% | 33.2% |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 35.8% | 37.1% | 41.9% | 35.0% | 39.1% | 49.9% | 44.5% | 42.7% |
| Akiba ya fedha za kigeni (miezi) | 5.0 | 4.8 | 4.3 | 5.7 | 5.4 | 3.7 | 3.8 | 4.5 |
| **UWIANO WA BAJETI YA SERIKALI NA PATO LA TAIFA** | | | | | | | | |
| **Mwaka wa Fedha** | **2005/06** | **2006/07** | **2007/08** | **2008/09** | **2009/10** | **2010/11** | **2011/12** | **2012/13** |
| Mapato ya ndani | 12.4% | 14.1% | 15.9% | 16.2% | 15.4% | 16.3% | 17.6% | 17.1% |
| Matumizi | 23.5% | 23.0% | 22.8% | 25.7% | 27.0% | 26.6% | 26.2% | 26.0% |
| Matumizi ya Kawaida | 15.7% | 16.2% | 14.9% | 17.7% | 18.3% | 19.0% | 17.0% | 18.5% |
| Matumizi ya Maendeleo | 7.7% | 6.9% | 7.9% | 8.0% | 8.6% | 7.6% | 9.2% | 7.5% |
| Misaada | 6.0% | 5.0% | 6.9% | 4.7% | 4.6% | 4.7% | 4.5% | 2.8% |
| Nakisi (kabla ya misaada) | -10.8% | -9.9% | -8.6% | -9.3% | -11.0% | -11.6% | -9.6% | -8.9% |
| Nakisi (baada ya misaada) | -4.8% | -4.9% | -1.7% | -4.5% | -6.4% | -6.9% | -5.0% | -6.1% |
| Mikopo ya nje | 3.3% | 3.7% | 3.2% | 3.6% | 4.6% | 3.4% | 4.2% | 3.5% |
| Mikopo ya ndani (kutoka benki) | 0.8% | 0.1% | -1.4% | 0.8% | 1.9% | 2.6% | 0.2% | 1.4% |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu

# SEHEMU YA KWANZA

# MAENDELEO YA UCHUMI JUMLA

# SURA YA I

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA

## Ukuaji wa Uchumi

1. Mwaka 2013, Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9 mwaka 2012. Ukuaji huu ulitokana na kuimarika kwa sekta zinazochangia Pato la Taifa kwa kiasi kikubwa hususan sekta za kilimo, ujenzi na biashara. Ukuaji wa viwango vya juu ulijionesha katika shughuli ndogo za kiuchumi za: mawasiliano (asilimia 22.8); fedha (asilimia 12.2); ujenzi (asilimia 8.6); na biashara (asilimia 8.3). Pamoja na kuwa na viwango vikubwa vya ukuaji, sekta za mawasiliano na fedha bado zinachangia kiwango kidogo katika Pato la Taifa cha chini ya wastani wa asilimia 2.5.

2. Pato la Taifa mwaka 2013 lilikuwa shilingi 53,174,678 milioni kwa bei za mwaka husika. Aidha, idadi ya watu Tanzania Bara ambayo inakua kwa wastani wa asilimia 2.7 ilikadiriwa kuwa watu 44,827,757 mwaka 2013. Hivyo, Pato la wastani la kila mtu lilikuwa shilingi 1,186,200 mwaka 2013 ikilinganishwa na shilingi 1,025,038 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 15.7

3. Kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za kilimo ambazo hujumuisha mazao, ufugaji na misitu na uwindaji kilikuwa asilimia 4.3 mwaka 2013 sawa na ilivyokuwa mwaka 2012. Kuimarika kwa kiwango cha ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa shughuli za uwindaji wa kitalii na kuongezeka kwa huduma za ugani hasa katika shughuli za uendelezaji wa mifugo. Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za uzalishaji mazao kiliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 4.5 mwaka 2013 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 2012. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kutokuwepo kwa mtawanyiko mzuri wa mvua na kwa wakati muafaka. Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za mifugo kiliongezeka kutoka asilimia 3.1 mwaka 2012 hadi asilimia 3.8 mwaka 2013. Ongezeko la kasi ya ukuaji lilitokana na upatikanaji wa maji na malisho ya kutosha kwa ajili ya mifugo, kuongezeka kwa huduma za ugani katika shughuli za uendelezaji mifugo, na kuongezeka kwa thamani ya mifugo na bidhaa zake. Shughuli ndogo za kiuchumi katika misitu na uwindaji zilikua

kwa kiwango cha asilimia 3.3 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 2.4 mwaka 2012 kutokana na kuongezeka kwa wawindaji wa kitalii.

4. Kiwango cha ukuaji wa Pato lililotokana na shughuli za kilimo sehemu ya kuuza kilikua kwa asilimia 5.2 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 4.1 mwaka 2012 kutokana na jitihada za serikali za kuhamasisha kilimo cha kisasa na kibiashara na kuimarisha huduma za masoko ili kuondokana na kilimo cha kijungujiko. Kwa upande wa sehemu isiyo ya kuuza, kiwango cha ukuaji kilipungua na kuwa asilimia 2.5 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 4.3 mwaka 2012. Shughuli za kilimo zilichangia asilimia 24.5 ya Pato la Taifa mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 24.7 mwaka 2012.

5. Shughuli za kiuchumi katika uvuvi zilikua kwa kiwango cha asilimia 2.2 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2012. Hii ilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa samaki kutokana na uharibifu wa mazingira ya mazalia ya samaki. Mchango wa shughuli za uvuvi katika Pato la Taifa umeendelea kubaki asilimia 1.4 kwa miaka minne mfululizo.

6. Shughuli za kiuchumi katika viwanda na ujenzi zilikua kwa asilimia 7.5 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2012. Kushuka kwa ukuaji huo kulitokana na kiwango kidogo cha ukuaji katika shughuli ndogo zote isipokuwa shughuli ndogo za ujenzi. Hata hivyo, mchango wa shughuli za kiuchumi za viwanda na ujenzi katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 22.2 mwaka 2013 kutoka asilimia 22.1 mwaka 2012.

7. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani kilikuwa asilimia 7.7 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2012. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kwa uzalishaji katika baadhi ya viwanda hususan vya rangi na dawa za pareto. Hata hivyo mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa uliongezeka mwaka 2013 kufikia asilimia 8.5 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2012.

8. Ukuaji katika shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe ulishuka kutoka asilimia 7.8 mwaka 2012 hadi asilimia 6.9 mwaka 2013. Hii ilitokana na kuwepo kwa ongezeko dogo la uzalishaji kufuatia kufungwa kwa migodi ya dhahabu ya Tulawaka na Resolute. Mchango wa shughuli za kiuchumi za madini

na uchimbaji mawe katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 3.5 mwaka 2012 hadi asilimia 3.3 mwaka 2013.

9. Shughuli za kiuchumi katika ujenzi zilikua kwa asilimia 8.6 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2012. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi na ukarabati wa: barabara na madaraja ikiwemo barabara ya mabasi yaendayo kasi jijini Dar es Salaam; ujenzi unaondelea wa viwanja vya ndege; na majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi. Aidha, mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa uliongezeka na kuwa asilimia 8.3 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 2012.

10. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi kilikuwa asilimia 4.4 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 6.0 mwaka 2012. Upungufu katika kiwango cha ukuaji ulitokana na kupungua kwa ufuaji wa umeme wa maji kutokana na uchakavu wa mitambo. Aidha, uzalishaji wa umeme wa mafuta ambao ni wa gharama umepungua kufuatia jitihada za serikali za kuelekeza uwekezaji zaidi katika uzalishaji wa umeme wa gesi kufuatia kugunduliwa kwa gesi huko Mtwara na Lindi ambayo ndiyo chanzo cha uhakika zaidi na cha gharama nafuuu. Katika mwaka 2013, chanzo cha gesi asilia ndicho kilichoongoza kwa kuzalisha karibu asilimia 50 ya umeme wote uliozalishwa baada ya kuanza uzalishaji wa gesi katika visima vya Songosongo na Mnazi Bay. Uzalishaji wa umeme wa gesi asilia uliongezeka kwa asilimia 22.5 mwaka 2013 kufikia saa za gigawati 2,980.5. Shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi zilichangia asilimia 1.8 katika Pato la Taifa mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 1.9 mwaka 2012.

11. Mwaka 2013, kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi za usambazaji maji ilipungua kidogo na kuwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2012. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na uchakavu wa miundombinu ya maji. Hata hivyo Serikali iliendelea na jitihada za kuboresha miundombinu ya maji ikiwemo kuchimba visima na upanuzi/ukarabati wa mitambo ya maji ya Ruvu juu na Ruvu chini. Mchango wa shughuli za usambazaji maji katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 0.3 kwa mwaka wa tatu mfululizo.

12. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika utoaji huduma kilikuwa asilimia 8.2 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 8.0 mwaka 2012. Hata

hivyo, mwenendo wa kasi ya ukuaji ulikuwa unatofautiana baina ya shughuli ndogo za kiuchumi. Mchango wa shughuli za utoaji huduma katika Pato la Taifa uliongezeka na kuwa asilimia 44.3 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 43.9 mwaka 2012.

13. Shughuli za biashara (uuzaji jumla na rejareja) na matengenezo zilikua kwa asilimia 8.3 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 7.7 mwaka 2012. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na kuboreshwa kwa mazingira ya ufanyaji biashara nchini na kuongezeka kwa biashara ya kikanda. Shughuli ndogo za biashara na matengenezo zilichangia asilimia 12.1 ya Pato la Taifa mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 12.3 mwaka 2012.

14. Shughuli ndogo za mahoteli na migahawa (ikijumuisha utalii) zilikua kwa asilimia 6.3 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 4.8 mwaka 2012. Ukuaji huo ulitokana na mikakati ya Serikali ya kuboresha huduma za utalii na kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi na hivyo kuongezeka kwa idadi na kiwango cha matumizi ya watalii. Idadi ya watalii nchini iliongezeka kwa asilimia 5.5 kutoka watalii 1,077,058 mwaka 2012 na kufikia watalii 1,135,884 mwaka 2013. Mchango wa shughuli za huduma za mahoteli na migahawa katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 2.5 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2012.

15. Shughuli za kiuchumi katika huduma za uchukuzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 6.2 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2012. Kupungua kwa shughuli za kiuchumi za uchukuzi kulitokana na kupungua kwa usafirishaji wa shehena za mizigo kwa njia ya anga na reli. Mchango wa huduma za uchukuzi katika Pato la Taifa uliongezeka na kuwa asilimia 5.8 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2012.

16. Shughuli za kiuchumi za huduma za mawasiliano katika mwaka 2013 zilikua kwa kiwango kikubwa zaidi ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi. Kiwango cha ukuaji cha shughuli hizi kilikuwa asilimia 22.8 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 20.6 mwaka 2012. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa wateja na matumizi ya huduma za mawasiliano ya simu za mkononi na kuimarishwa kwa miundombinu ya huduma za mawasiliano.

Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 2.4 mwaka 2013 kutoka asilimia 2.3 mwaka 2012.

17. Mwaka 2013, shughuli za kiuchumi katika huduma za fedha zilikua kwa asilimia 12.2 ikilinganishwa na asilimia 13.2 mwaka 2012. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kwa mikopo kwa sekta binafsi; na kasi ndogo ya ongezeko la mahitaji ya kifedha kwa ajili ya uwekezaji; huduma za bima; na huduma za kibiashara. Mchango wa shughuli za huduma za fedha katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.8 kwa mwaka wa nne mfululizo.

| Gabon | 6.9 | 5.5 | 5.9 | 1.3 | 2.7 | 0.5 | 13.2 | 14.0 | 10.6 |
| Republic of Congo | 3.4 | 3.8 | 4.5 | 1.8 | 5.0 | 4.6 | 5.8 | -1.3 | -1.2 |
| Chad | 0.1 | 8.9 | 3.6 | 1.9 | 7.7 | 0.2 | -5.6 | -8.3 | -8.1 |
| Cameroon | 4.1 | 4.6 | 4.6 | 2.9 | 2.4 | 2.1 | -2.9 | -4.0 | -4.4 |
| South Sudan | 1.4 | -47.6 | 24.4 | 47.3 | 45.1 | 0.0 | 18.4 | -27.7 | 2.2 |
| **Nchi za Kipato cha Kati** | **4.8** | **3.4** | **2.7** | **5.6** | **6.0** | **6.0** | **-3.1** | **-5.5** | **-6.1** |
| Botswana | 6.1 | 4.2 | 3.9 | 8.5 | 7.5 | 5.8 | -0.2 | -4.9 | -0.4 |
| Cape Verde | 4.0 | 2.5 | 1.5 | 4.5 | 2.5 | 3.3 | -45.4 | -39.4 | -36.4 |
| Ghana | 15.0 | 7.9 | 5.5 | 8.7 | 9.2 | 11.7 | -9.1 | -12.2 | -13.2 |
| Lesotho | 4.3 | 6.0 | 5.8 | 5.0 | 6.2 | 5.3 | -8.6 | -4.2 | -1.3 |
| Mauritius | 3.8 | 3.3 | 3.1 | 6.5 | 3.9 | 3.5 | -13.3 | -7.9 | -9.1 |
| Namibia | 5.7 | 5.0 | 4.3 | 5.0 | 6.5 | 6.2 | -3.5 | -2.6 | -4.6 |
| Senegal | 2.1 | 3.5 | 4.0 | 3.4 | 1.4 | 0.8 | -7.9 | -10.3 | -9.3 |
| Seychelles | 7.9 | 2.8 | 3.6 | 2.6 | 7.1 | 4.3 | -26.6 | -24.8 | -17.7 |
| South Africa | 3.6 | 2.5 | 1.9 | 5.0 | 5.7 | 5.8 | -2.3 | -5.2 | -5.8 |
| Swaziland | -0.6 | 1.9 | 2.8 | 6.1 | 8.9 | 5.6 | -8.6 | 4.1 | 5.5 |
| Zambia | 6.8 | 7.2 | 6.0 | 8.7 | 6.6 | 7.0 | 3.7 | 3.8 | 1.2 |
| **Nchi za Kipato cha Chini** | **6.5** | **6.2** | **6.8** | **18.9** | **8.5** | **5.8** | **-10.2** | **-12.2** | **-11.3** |
| Benin | 3.3 | 5.4 | 5.6 | 2.7 | 6.7 | 1.0 | -7.8 | -7.9 | -14.5 |
| Burkina Faso | 5.0 | 9.0 | 6.8 | 2.8 | 3.8 | 2.0 | -1.2 | -0.8 | -7.2 |
| Ethiopia | 11.4 | 8.5 | 9.7 | 33.2 | 24.1 | 8.0 | -0.7 | -6.5 | -6.1 |
| Gambia | -4.3 | 5.3 | 6.3 | 4.8 | 4.6 | 5.2 | -15.6 | -17.0 | -17.0 |
| Kenya | 4.4 | 4.6 | 5.6 | 14.0 | 9.4 | 5.7 | -11.2 | -10.4 | -8.3 |
| Madagascar | 1.5 | 2.5 | 2.4 | 10.0 | 5.8 | 5.8 | -5.6 | -6.2 | -4.6 |
| Malawi | 4.3 | 1.9 | 5.0 | 7.6 | 21.3 | 27.7 | -5.8 | -4.0 | -3.4 |
| Mali | 2.7 | 0.0 | 1.7 | 3.1 | 5.3 | -0.6 | -6.0 | -3.3 | -3.3 |
| Niger | 2.3 | 11.1 | 3.6 | 2.9 | 0.5 | 2.3 | -22.3 | -15.4 | -17.2 |
| Rwanda | 8.2 | 8.0 | 5.0 | 5.7 | 6.3 | 4.2 | -7.2 | -11.4 | -7.3 |
| Sierra Leone | 6.0 | 15.2 | 16.3 | 18.5 | 13.8 | 9.8 | -44.9 | -36.7 | -14.2 |
| Tanzania | 6.4 | 6.9 | 7.0 | 12.7 | 16.0 | 7.9 | -14.5 | -15.9 | -14.3 |
| Uganda | 6.2 | 2.8 | 6.0 | 18.7 | 14.0 | 5.4 | -12.5 | -10.5 | -11.7 |
| Mozambique | 7.3 | 7.2 | 7.1 | 10.4 | 2.1 | 4.2 | -24.4 | -45.6 | -41.9 |

Chanzo:-Shirika la Fedha Duniani (IMF), Aprili 2014.

## USHIRIKIANO WA UCHUMI KIMATAIFA

### Jumuiya ya Afrika Mashariki

39. Kikao cha kumi na tano cha wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kilifanyika Uganda mwezi Novemba 2013, ambapo uenyekiti ulikabidhiwa kwa nchi ya Kenya kutoka Uganda. Katika kikao hicho, pamoja na mambo mengine, wakuu wa nchi wanachama walitia saini itifaki ya kuanzisha sarafu moja kwa nchi za Afrika Mashariki. Masuala ya msingi yaliyotakiwa kutekelezwa kwenye mpango wa uanzishaji wa sarafu moja kwa nchi za Afrika Mashariki ni kukamilisha hatua za awali za mtangamano za umoja wa forodha na soko la pamoja. Aidha, masuala mengine ni kufikia vigezo vya muunganiko wa uchumi mpana na kuanzisha Taasisi muhimu za kusimamia utekelezaji wa sarafu moja kwa nchi husika.

40. Katika uendelezaji wa miundombinu ya barabara na reli ndani ya Jumuiya, usanifu wa kina wa barabara ya Arusha – Holili/Taveta – Voi inayounganisha Tanzania na Kenya ulikamilika. Mkataba wa ujenzi wa barabara hiyo ulitiwa saini mwezi Mei 2013 kati ya Benki ya Maendeleo ya Afrika na nchi za Kenya na Tanzania. Aidha, katika kutekeleza mpango kabambe wa kuendeleza reli ndani ya Jumuiya, usanifu wa kina wa reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali/Kezi – Gitegi – Musongati inayojumuisha nchi za Burundi, Rwanda na Tanzania ulikamilika.

41. Mwaka 2013, mpango-kazi wa utekelezaji wa sera na mkakati wa maendeleo ya viwanda kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikamilika. Mpango-kazi huo unabainisha hatua za kuchukuliwa katika kuendeleza viwanda vya kimkakati ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, katika kuendeleza sekta ya kilimo rasimu ya sera ya upatikanaji wa chakula iliandaliwa ikiwa ni hatua ya kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### Umoja wa Afrika na Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika

42. Ukuaji wa uchumi wa Afrika unakabiliwa na changamoto za kuongeza fursa za ajira na kupunguza kiwango cha umasikini. Hii inatokana na kuendelea kutegemea sekta ya kilimo ambayo mazao yake yanauzwa nje bila kuyaongezea thamani. Aidha, kilimo chenyewe kinategemea mvua ambayo haitabiriki na bei za mazao ya kilimo hayana uhakika katika soko la ndani na nje. Katika

kukabiliana na changamoto hiyo, Umoja wa Afrika na Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika uliandaa mada iliyohusu "Ujenzi wa Viwanda kwa Afrika inayochipukia" (Industrialization for Emerging Africa) katika kikao chao cha sita cha pamoja kilichofanyika Abidjan - Ivory Coast Machi 2013. Mambo yaliyojadiliwa kulingana na mada hiyo ni pamoja na: Kuongeza kasi ya ujenzi wa viwanda Afrika; Ujenzi wa viwanda na mabadiliko ya kimuundo Afrika; Mpangilio wa ujenzi wa viwanda; na Ugharamiaji wa ujenzi wa viwanda.

43. Katika kikao hicho, nchi za Afrika zilishauriwa kutekeleza mambo kadhaa ili kufanikisha ujenzi wa viwanda kwa lengo la kutoa ajira na kuongeza thamani kwa mazao ghafi. Baadhi ya mambo hayo ni: Kubuni na kutekeleza sera za ujenzi wa viwanda zenye mtazamo wa umiliki wa kitaifa na kuongeza thamani ya mazao ghafi; Kubuni na kutekeleza sera maalum za kulinda viwanda vichanga; Matumizi ya sera za kupunguza uuzaji nje mazao na malighafi na badala yake kuongeza thamani ya mazao hayo; Kuchukua hatua madhubuti za kuongeza vyanzo mbalimbali vya nishati kwa lengo la kuongeza tija na ushindani; na Kuweka kipaumbele cha ugharamiaji ujenzi wa viwanda katika mipango ya maendeleo. Vile vile, Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na taasisi nyingine za fedha za maendeleo zilishauriwa kushiriki kugharamia miradi ya viwanda vya kitaifa na kikanda.

**Shirikisho la Biashara Ulimwenguni**

44. Katika kikao cha tisa cha Shirikisho la Biashara Duniani kilichofanyika Desemba 2013, Mawaziri wa nchi wanachama 159 wa Shirikisho walikubaliana kuwa na "Mpango wa Bali" (Bali Package) kwa lengo la kuziwezesha kibiashara nchi wanachama. "Mpango wa Bali" unajumuisha hatua mbalimbali za kuboresha biashara duniani. Hatua hizo ni pamoja na kuziruhusu nchi zinazoendelea kuwa na fursa zaidi ya kuzalisha chakula cha akiba, kuinua kiwango cha biashara kwa nchi changa na kusaidia maendeleo ya nchi changa kibiashara. Nchi wanachama wa Shirikisho waliridhia "Makubaliano ya Urahisishaji wa Biashara" ambayo yanalenga kuharakisha taratibu na kuongeza tija katika shughuli za forodha kupitia ushirikiano baina ya forodha na mamlaka mbalimbali za biashara. Aidha, makubaliano hayo yanajumuisha utoaji wa elimu ya biashara na misaada ya kiufundi kwa nchi wanachama.

# SURA YA 3

# SEKTA YA NJE

**Utangulizi**

45. Mwaka 2013, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma nje haukuwa wa kuridhisha ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2012. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilipungua kwa asilimia 1.7 kutoka Dola za Kimarekani milioni 8,675.6 mwaka 2012 hadi Dola milioni 8,532.0. Upungufu huu ulichangiwa zaidi na kupungua kwa mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia zikiwemo tumbaku, kahawa, pamba na katani. Kwa upande mwingine, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 6.6 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 13,517.6 kutoka Dola milioni 12,678.0 mwaka 2012.

**Bidhaa Zilizouzwa Nje**

46. Mwaka 2013, thamani ya mauzo ya bidhaa zilizouzwa nje ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 5,348.9 ikilinganishwa na Dola milioni 5,889.2 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 9.2. Upungufu huu ulitokana na kushuka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa asilia pamoja na mauzo ya dhahabu nje. Kiasi hiki cha mauzo ya bidhaa nje kwa mwaka 2013 kinajumuisha bidhaa zisizorekodiwa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 697.7.

**Bidhaa Asilia**

47. Mwaka 2013, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia ilipungua hadi Dola za Kimarekani milioni 868.9 kutoka Dola milioni 956.7 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 9.2. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha mauzo ya tumbaku, pamba na katani kilichouzwa nje sambamba na kushuka kwa wastani wa bei ya kahawa, katani, chai na karafuu katika soko la dunia, na kupelekea thamani ya mauzo nje nayo kupungua.

**Kahawa**

48. Thamani ya mauzo ya kahawa ilipungua kwa asilimia 8.4 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 171.0 mwaka 2013 kutoka Dola milioni 186.6 mwaka 2012. Hii ilitokana na kupungua kwa wastani wa bei ya kahawa katika soko la dunia kutoka Dola za Kimarekani 3,403.2 kwa tani mwaka 2012 hadi Dola 2,872.7 kwa tani mwaka 2013. Hata hivyo, kiasi cha kahawa iliyouzwa nje

kiliongezeka kwa asilimia 8.5 kutoka tani 54,800 mwaka 2012 hadi tani 59,500 mwaka 2013.

**Pamba**

49. Mwaka 2013, thamani ya mauzo ya pamba ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 111.7 ikilinganishwa na Dola milioni 164.9 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 32.3. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha pamba kilichouzwa nje kutoka tani 132,000 mwaka 2012 hadi tani 89,000 mwaka 2013. Hata hivyo, wastani wa bei ya pamba katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 0.5 hadi kufikia Dola za Kimarekani 1,256.0 kwa tani ikilinganishwa na Dola 1,249.7 kwa tani mwaka 2012.

**Katani**

50. Mwaka 2013, thamani ya mauzo ya katani nje ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 16.9 kutoka Dola milioni 18.4 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 7.8. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa kiasi cha katani kilichouzwa nje kwa asilimia 6.8 na kushuka kwa wastani wa bei ya katani katika soko la dunia kwa asilimia 1.1. Kiasi cha katani kilichouzwa nje mwaka 2013 kilikuwa tani 12.6 ikilinganishwa na tani 13.5 zilizouzwa mwaka 2012. Aidha, wastani wa bei ya katani katika soko la dunia kwa mwaka 2013 ulikuwa Dola za Kimarekani 1,341.6 kwa tani ikilinganishwa na Dola 1,357.1 kwa tani mwaka 2012.

**Chai**

51. Thamani ya chai iliyouzwa nje iliongezeka kwa asilimia 1.5 kutoka Dola za Kimarekani 56.1 mwaka 2012 hadi Dola milioni 56.9 mwaka 2013. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha chai iliyouzwa nje kutoka tani 27,200 mwaka 2012 hadi tani 28,800 mwaka 2013. Hata hivyo, wastani wa bei ya chai katika soko la dunia ulipungua kwa asilimia 4.0 na kufikia Dola za Kimarekani 1,977.9 kwa tani ikilinganishwa na Dola 2,061.2 kwa tani mwaka 2012.

**Tumbaku**

52. Thamani ya mauzo ya tumbaku nje ilipungua kwa asilimia 12.3 mwaka 2013 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 307.0 ikilinganishwa na Dola milioni 350.1 mwaka 2012. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha mauzo ya tumbaku nje kutoka tani 105,600 mwaka 2012 hadi tani 67,800 mwaka 2013, sawa na

upungufu wa asilimia 35.7. Hata hivyo, wastani wa bei ya tumbaku katika soko la dunia kwa mwaka 2013 uliongezeka kwa asilimia 36.5 na kuwa Dola za Kimarekani 4,526.1 kwa tani ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 3,316.0 kwa tani mwaka 2012.

**Korosho**

53. Mwaka 2013, thamani ya mauzo ya korosho nje ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 162.4 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 142.6 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 13.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha korosho kilichouzwa nje sambamba na kupanda kwa wastani wa bei ya korosho katika soko la dunia. Kiasi cha korosho kilichouzwa nje kiliongezeka kwa asilimia 12.5 kutoka tani 130,900 mwaka 2012 hadi tani 147,300 mwaka 2013. Aidha, wastani wa bei ya korosho katika soko la dunia ulikuwa Dola 1,102.5 kwa tani mwaka 2013 ikilinganishwa na Dola 1,089.3 kwa tani mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 1.2.

**Karafuu**

54. Mwaka 2013, thamani ya mauzo ya karafuu nje iliongezeka kwa asilimia 12.8 hadi Dola za Kimarekani milioni 43.0 kutoka Dola milioni 38.1 mwaka 2012. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha karafuu kilichouzwa nje kufuatia kuongezeka kwa uzalishaji. Aidha, kiasi cha karafuu kilichouzwa nje kiliongezeka kwa asilimia 19.6 kutoka tani 3,400 mwaka 2012 hadi tani 4,100 mwaka 2013. Hata hivyo, wastani wa bei ya karafuu katika soko la dunia ilishuka kwa asilimia 5.7 na kufikia Dola za Kimarekani 10,562.8 kwa tani mwaka 2013 kutoka Dola 11,198.5 kwa tani mwaka 2012.

**Bidhaa Zisizo Asilia**

55. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia ilipungua kwa asilimia 9.2 kutoka Dola za Kimarekani milioni 4,164.4 mwaka 2012 hadi Dola milioni 3,782.3 mwaka 2013. Hii, ilitokana na kupungua kwa thamani ya mauzo ya dhahabu nje.

**Madini**

56. Thamani ya mauzo ya madini nje ilipungua kwa asilimia 15.3 kutoka Dola za Kimarekani milioni 2,197.8 mwaka 2012 na kufikia Dola milioni 1,861.2 mwaka 2013. Upungufu huu ulitokana na kushuka kwa thamani ya mauzo ya dhahabu kufuatia kupungua kwa kiasi cha dhahabu iliyouzwa nje sambamba na kushuka kwa wastani wa bei ya dhahabu katika soko la dunia. Mauzo ya

dhahabu yalipungua kwa asilimia 18.2 kutoka Dola za Kimarekani milioni 2,117.4 mwaka 2012 hadi Dola milioni 1,732.9 mwaka 2013. Pamoja na thamani ya mauzo ya dhahabu kupungua, dhahabu iliendelea kutoa mchango mkubwa katika bidhaa zisizo asilia. Mwaka 2013, dhahabu peke yake ilichangia asilimia 45.8 ya mauzo yote ya bidhaa zisizo asilia. Kwa upande mwingine, thamani ya mauzo ya almasi na madini mengine nje iliongezeka mwaka 2013 ikilinganishwa na mwaka 2012.

**Bidhaa za Viwandani**

57. Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani iliongezeka hadi Dola za Kimarekani milioni 1,072.1 mwaka 2013 kutoka Dola milioni 1,037.3 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Hii ilitokana zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya nyuzi za pamba nje ambazo thamani yake iliongezeka kwa asilimia 88.8 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 10.9 mwaka 2013 kutoka Dola milioni 5.8 mwaka 2012. Aidha, mauzo ya bidhaa za viwandani yalichangia asilimia 28.3 ya mauzo yote ya bidhaa zisizo asilia.

**Samaki na Mazao ya Samaki**

58. Mwaka 2013, thamani ya mauzo ya samaki na mazao ya samaki nje ilipungua kwa asilimia 18.7 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 130.6 mwaka 2013 kutoka Dola milioni 160.6 mwaka 2012. Hali hii ilitokana na upatikanaji duni wa samaki na mazao yake kufuatia uchakavu na uduni wa vifaa vya uvuvi na uharibifu wa mazalio ya samaki kutokana na uvuaji usioruhusu samaki kuzaliana.

**Mazao ya Mboga na Maua**

59. Mwaka 2013, thamani ya mauzo ya mazao ya mboga na maua nje ilikuwa Dola za kimarekani milioni 28.1 ikilinganishwa na Dola milioni 31.3 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 10.2. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa kasi ya mahitaji ya mazao ya mboga na maua kufuatia kupungua kwa mahitaji katika soko la dunia na kuongezeka kwa ushindani kutoka nchi nyingine.

**Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje**

60. Thamani ya mauzo ya bidhaa nyinginezo zilizouzwa nje mwaka 2013 ilipungua kwa asilimia 6.9 kutoka Dola za Kimarekani milioni 555.7 mwaka 2012 hadi Dola za Kimarekani milioni 517.6.

## Jedwali Na.3.1: Thamani, Kiasi na Bei ya Bidhaa Zilizouzwa Nje

| Bidhaa | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | Badiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | |
| **Kahawa** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 111.2 | 101.6 | 142.6 | 186.6 | 171.0 | -8.4% |
| Kiasi (‘000 tani) | 56.0 | 35.6 | 39.0 | 54.8 | 59.5 | 8.5% |
| Bei (US$ kwa tani) | 1984.6 | 2853.1 | 3654.9 | 3403.2 | 2872.7 | -15.6% |
| **Pamba** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 111.0 | 84.0 | 61.6 | 164.9 | 111.7 | -32.3% |
| Kiasi (‘000 ttani) | 99.4 | 67.6 | 40.3 | 132.0 | 89.0 | -32.6% |
| Bei (US$ kwa tani) | 1116.7 | 1241.9 | 1529.0 | 1249.7 | 1256.0 | 0.5% |
| **Katani** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 6.7 | 10.9 | 16.9 | 18.4 | 16.9 | -7.8% |
| Kiasi (‘000 tani) | 8.2 | 11.6 | 13.8 | 13.5 | 12.6 | -6.8% |
| Bei (US$ kwa tani) | 826.0 | 939.8 | 1223.5 | 1357.1 | 1341.6 | -1.1% |
| **Chai** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 47.2 | 49.8 | 47.2 | 56.1 | 56.9 | 1.5% |
| Kiasi (‘000 tani) | 30.6 | 27.1 | 27.1 | 27.2 | 28.8 | 5.8% |
| Bei (US$ kwa tani) | 1538.7 | 1840.2 | 1739.7 | 2061.2 | 1977.9 | -4.0% |
| **Tumbaku** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 127.4 | 232.4 | 281.2 | 350.1 | 307.0 | -12.3% |
| Kiasi (‘000 tani) | 33.8 | 53.6 | 73.3 | 105.6 | 67.8 | -35.7% |
| Bei (US$ kwa tani) | 3764.0 | 4337.0 | 3839.4 | 3316.0 | 4526.1 | 36.5% |
| **Korosho** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 68.6 | 96.9 | 107.0 | 142.6 | 162.4 | 13.9% |
| Kiasi (‘000 tani) | 95.5 | 100.6 | 96.4 | 130.9 | 147.3 | 12.5% |
| Bei (US$ kwa tani) | 718.2 | 963.2 | 1110.0 | 1089.3 | 1102.5 | 1.2% |
| **Karafuu** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 14.4 | 7.6 | 28.9 | 38.1 | 43.0 | 12.8% |
| Kiasi (‘000 tani) | 4.8 | 2.2 | 2.2 | 3.4 | 4.1 | 19.6% |
| Bei (US$ kwa tani) | 2977.9 | 3449.6 | 13162.9 | 11198.5 | 10562.8 | -5.7% |
| **Jumla (Bidhaa Asilia)** | **486.4** | **583.2** | **685.5** | **956.7** | **868.9** | **-9.2%** |
| **Bidhaa Zisizo Asilia** | | | | | | |
| **Madini** | **1274.8** | **1561.2** | **2283.4** | **2197.8** | **1861.2** | **-15.3%** |
| Dhahabu | 1229.5 | 1516.6 | 2224.1 | 2117.4 | 1732.9 | -18.2% |
| Almasi | 18.9 | 11.1 | 10.2 | 30.2 | 39.8 | 31.5% |
| Madini mengine | 26.4 | 33.5 | 49.2 | 50.2 | 88.5 | 76.3% |
| **Bidhaa za Viwandani** | **506.5** | **964.0** | **861.5** | **1037.3** | **1072.1** | **3.3%** |
| Nyuzi za Pamba | 8.1 | 11.5 | 4.8 | 5.8 | 10.9 | 88.8% |
| Kahawa Iliyozalishwa | 2.0 | 0.7 | 1.1 | 1.0 | 1.1 | 7.1% |
| Tumbaku ilizalishwa | 7.0 | 10.5 | 16.7 | 24.6 | 32.2 | 30.7% |
| Mazao ya Katani | 13.4 | 9.0 | 11.8 | 9.1 | 9.7 | 6.3% |
| Mazao mengine ya Viwandani | 476.1 | 932.4 | 827.1 | 996.8 | 1018.2 | 2.1% |
| **Samaki na Mazao ya Samaki** | **155.0** | **150.4** | **137.7** | **160.6** | **130.6** | **-18.7%** |
| **Mazao ya mboga na Maua** | **33.3** | **30.8** | **36.4** | **31.3** | **28.1** | **-10.2%** |
| **Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports)** | **282.9** | **338.2** | **330.2** | **555.7** | **517.6** | **-6.8%** |
| **Bidhaa nyinginezo** | **120.4** | **132.5** | **98.3** | **181.7** | **172.8** | **-4.9%** |
| **Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)** | **2372.9** | **3177.0** | **3747.5** | **4164.4** | **3782.3** | **-9.2%** |
| Bidhaa zisizorekodiwa | 438.9 | 564.0 | 664.9 | 768.2 | 697.7 | -9.2% |
| **JUMLA KUU (BIDHAA ZOTE)** | **3298.1** | **4324.3** | **5097.9** | **5889.2** | **5348.9** | **-9.2%** |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha

**Mapato ya Huduma**

61. Mwaka 2013, mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka kwa asilimia 14.4 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 3,188.0 ikilinganishwa na Dola milioni 2,786.4 mwaka 2012. Hii ilitokana hasa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za usafiri na usafirishaji kufuatia kuongezeka kwa idadi ya watalii waliongia nchini pamoja na kiasi cha mizigo iliyosafirishwa kwenda nchi za jirani. Mapato yatokanayo na huduma ya usafirishaji wa mizigo kwenda nchi jirani yalikua kwa asilimia 16.0 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 576.8 mwaka 2013. Sehemu kubwa ya mizigo hiyo ilisafirishwa kwenda nchi jirani za Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na Rwanda. Aidha, shughuli za usafiri zilichangia asilimia 59.0 na shughuli za usafirishaji zilichangia asilimia 24.6 ya mapato yote yatokanayo na huduma katika mwaka 2013.

**Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje**

62. Mwaka 2013, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje (f.o.b) ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 11,029.1 ikilinganishwa na Dola milioni 10,319.1 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 6.9. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa za kati na bidhaa za matumizi ya kawaida.

**Bidhaa za Kukuza Mitaji**

63. Mwaka 2013, thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoagizwa kutoka nje ilipungua kwa asilimia 6.1 hadi Dola za Kimarekani milioni 3,460.4 kutoka Dola milioni 3,686.5 mwaka 2012. Upungufu huu ulitokana na kushuka kwa thamani ya mitambo iliyoagizwa kutoka nje. Thamani ya mitambo iliyoagizwa kutoka nje ilishuka kwa asilimia 22.2 ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2012 kufuatia kupungua kwa uwekezaji mpya kwenye miradi mikubwa hasusan miradi ya madini ambayo kwa sasa mingi ipo kwenye hatua ya uzalishaji au utafiti wa awali.

**Bidhaa za Kati**

64. Thamani ya bidhaa za kati zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 20.5 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 5,205.2 mwaka 2013 kutoka Dola milioni 4,320.2 mwaka 2012. Hii ilitokana hasa na kuongezeka kwa kiasi cha bidhaa za mafuta zilizoagizwa kutoka nje  sambamba na ongezeko la wastani wa bei ya mafuta katika soko la dunia. Thamani ya bidhaa za mafuta yaliyoagizwa

kutoka nje mwaka 2013 iliongezeka kwa asilimia 27.4 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 4,308.6 kutoka Dola 3,380.6 mwaka 2012. Mafuta peke yake yalichangia asilimia 39.1 ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje mwaka 2013. Aidha, mbolea iliyoagizwa kutoka nje mwaka 2013 ilikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 160.1, ikiwa ni ongezeko la asilimia 19.6. Hata hivyo, thamani ya uagizaji wa malighafi za viwandani ilipungua kwa asilimia 8.6 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 736.6 kutoka dola milioni 805.7 mwaka 2012.

**Bidhaa za Matumizi ya Kawaida**

65. Mwaka 2013, thamani ya uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida iliongezeka kwa asilimia 2.2 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 2,361.3 kutoka Dola milioni 2,310.3 mwaka 2012. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa nyinginezo za matumizi ya kawaida. Mwaka 2013, thamani ya uagizaji wa bidhaa nyinginezo za matumizi ya kawaida iliongezeka kwa asilimia 3.7 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 1,714.9 kutoka Dola milioni 1,653.7 mwaka 2012.

**Malipo ya Huduma**

66. Mwaka 2013, malipo ya huduma yalikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2,488.5 ikilinganishwa na Dola milioni 2,358.9 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa malipo ya huduma za usafirishaji wa mizigo kufuatia kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa toka nje.

**Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali**

67. Mwaka 2013, mwenendo wa biashara baina ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani pamoja na jumuiya za kikanda zikiwemo nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za kusini mwa Afrika (SADC), na Umoja wa nchi za Ulaya (EU) haukuwa wa kuridhisha. Thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda nchi za Bara la Ulaya, America, EAC, SADC na Bara la Asia ilipungua kwa asilimia 41.4, 18.8, 18.6, 15.0, na 8.1, kwa mtiririko huo mwaka 2013. Aidha, sehemu kubwa ya mauzo ya Tanzania nje yalikwenda katika nchi ya Afrika ya Kusini iliyochangia asilimia 14.2 ya mauzo yote, ikifuatiwa na India (asilimia 14.0), Uswisi (asilimia 7.5), China (asilimia 5.8), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (asilimia 4.4) na Kenya (asilimia 4.2).

68. Kwa upande mwengine, thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka nchi mbalimbali duniani uliongezeka kwa asilimia 6.9 mwaka 2013. Sehemu kubwa ya bidhaa zilizoagizwa zilitoka katika nchi za bara la Asia  hususan nchi za India, China, na Falme za nchi za Kiarabu ambazo mwaka 2013 zilichangia asilimia 18.9, 13.1 na 9.8 ya bidhaa zote zilizoagizwa kwa mtiririko huo na pia zilikuwa na ongezeko katika thamani ya bidhaa zilizoagizwa. Kiwango cha uagizaji karibu nchi nyingine zote zikiwemo za jumuiya za kikanda kilipungua mwaka 2013 ikilinganishwa na mwaka 2012.

69. Mchanganuo wa mauzo na uagizaji wa bidhaa kati ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 3.2 na 3.3.

**Jedwali Na. 3.3: Thamani ya Bidhaa Zilizouzwa Nje (Miln USD)**

| JUMUIYA/ NCHI | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013p | 2012 -2013 (Badiliko) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **JUMUIYA YA ULAYA** | 461.9 | 440.0 | 464.0 | 553.5 | 745.4 | 898.4 | **20.5%** |
| **NCHI NYINGINE ZA ULAYA** | 533.3 | 469.0 | 687.1 | 828.5 | 816.8 | 16.9 | **-97.9%** |
| **JUMLA - BARA LA ULAYA** | **995.2** | **909.0** | **1151.1** | **1382.0** | **1562.2** | **915.3** | **-41.4%** |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | | |
| Afrika ya kusini | 232.5 | 170.9 | 416.8 | 831.1 | 967.9 | 760.5 | **-21.4%** |
| Zambia | 36.6 | 44.3 | 53.5 | 47.1 | 71.4 | 90.6 | **26.9%** |
| Swaziland | 0.6 | 20.8 | 0 | 12.5 | 2.2 | 4.1 | **86.4%** |
| Zimbabwe | 1.2 | 5.7 | 0 | 4.1 | 4.7 | 6.5 | **38.3%** |
| Msumbiji | 31.4 | 20.3 | 17.7 | 61.9 | 53.1 | 66.4 | **25.0%** |
| Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 124 | 79.9 | 137.1 | 119.5 | 181.6 | 236.2 | **30.1%** |
| Nchi nyingine za SADC | **17.1** | **32.3** | **0** | **82.6** | **141** | **44.9** | **-68.2%** |
| **JUMLA- SADC** | **443.4** | **374.2** | **625.1** | **1158.8** | **1421.9** | **1209.2** | **-15.0%** |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | | |
| Burundi | 19.5 | 23.6 | 51.0 | 30.8 | 45.8 | 45.0 | **-1.7%** |
| Kenya | 235 | 177.4 | 297.3 | 211.2 | 330.9 | 227.1 | **-31.4%** |
| Rwanda | 20.6 | 15.1 | 55.0 | 65.8 | 72.8 | 81.1 | **11.4%** |
| Uganda | 40.5 | 47.7 | 46.8 | 44.6 | 65.8 | 66.1 | **0.5%** |
| **JUMLA – EAC** | **315.6** | **263.8** | **450.1** | **352.4** | **515.3** | **419.3** | **-18.6%** |
| **Nchi nyingine za Afrika** | **96.1** | **0.6** | **5.8** | **67.9** | **47.7** | **3.5** | **-92.7%** |
| **JUMLA –AFRIKA** | **855.1** | **638.6** | **1081.0** | **1579.1** | **1984.9** | **1632.0** | **-17.8%** |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | | |
| Marekani | 55.1 | 39.5 | 46.5 | 47.5 | 66.8 | 60.5 | **-9.4%** |
| Canada | 3.8 | 6.1 | 4.6 | 5.0 | 25.2 | 12.9 | **-48.8%** |
| Nchi nyingine za Bara la Amerika | 5.4 | 0 | 0 | 7.4 | 1.7 | 2.7 | **58.8%** |
| **JUMLA- BARA LA AMERIKA** | **64.3** | **45.6** | **51.1** | **59.9** | **93.7** | **76.1** | **-18.8%** |
| **ASIA** | | | | | | | |
| China | 223.5 | 363.9 | 634.2 | 659.2 | 520.4 | 307.8 | **-40.9%** |
| India | 171.8 | 183.8 | 218.5 | 202.7 | 476.5 | 748.2 | **57.0%** |
| Japan | 136.9 | 164.7 | 209.7 | 346.8 | 296.5 | 220 | **-25.8%** |
| Umoja wa Falme za Kiarabu | 65.4 | 66.8 | 55.3 | 74.9 | 94.2 | 84.2 | **-10.6%** |
| Hong Kong | 13.4 | 85.6 | 12.6 | 11.1 | 23.1 | 30.4 | **31.6%** |
| Singapore | 11.0 | 6.4 | 13.5 | 10.9 | 24.3 | 55.7 | **129.2%** |
| **Nchi nyingine za Asia** | 52.4 | 59.1 | 56.4 | 109.1 | 209.4 | 64.7 | **-69.1%** |
| **JUMLA- ASIA** | **674.4** | **930.3** | **1200.2** | **1414.7** | **1644.4** | **1511** | **-8.1%** |
| **NCHI NYINGINEZO** | **989.8** | **774.6** | **840.9** | **662.2** | **604.0** | **1214.5** | **101.1%** |
| **JUMLA KUU** | **3,578.8** | **3,298.1** | **4,324.3** | **5,097.9** | **5,889.2** | **5,348.9** | **-9.2%** |

Chanzo: Benki Kuu na Wizara ya Fedha
P – Takwimu za Awali

## Jedwali Na. 3.4: Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa Nje (Mln USD)

| JUMUIYA/ NCHI | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013p | 2012-2013 (Badiliko, %) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI** | 1280.8 | 1076.6 | 1111.4 | 1074.4 | 1536.9 | 2759.4 | 79.5 |
| NCHI NYINGINE ZA ULAYA | 153.8 | 145.5 | 558.4 | 647.1 | 1756.3 | 218.0 | -87.6 |
| **JUMLA - BARA LA ULAYA** | **1434.6** | **1222.1** | **1669.8** | **1721.5** | **3293.2** | **3077.4** | -6.6 |
| **AFRIKA** | | | | | | | |
| **JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)** | | | | | | | |
| Afrika ya Kusini | 791.0 | 672.8 | 745.5 | 676.5 | 920.8 | 660.1 | -28.3 |
| Zimbabwe | 27.6 | 0.6 | 1.1 | 1.0 | 2.9 | 3.4 | 17.2 |
| Zambia | 27.6 | 23.3 | 29.8 | 27.0 | 39.6 | 46.2 | 16.7 |
| Msumbiji | 18.2 | 9.0 | 18.5 | 16.9 | 11.0 | 66.9 | 508.2 |
| Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | 19.6 | 1.2 | 1.1 | 1.0 | 0.9 | 0.1 | -88.9 |
| Swaziland | 76.5 | 26.3 | 31.7 | 29.0 | 34.6 | 33.9 | -2.0 |
| **Nchi nyingine za SADC** | **19.2** | **-** | **-** | **29.9** | **83.3** | **25.3** | -69.6 |
| **JUMLA –SADC** | **979.7** | **733.2** | **827.7** | **781.3** | **1098.1** | **835.9** | -23.5 |
| **JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)** | | | | | | | |
| Burundi | 0.4 | 0.3 | 0.6 | 0.6 | 3.8 | 1.5 | -60.5 |
| Kenya | 197.9 | 298.3 | 265.9 | 246.1 | 555.8 | 303.6 | -45.4 |
| Rwanda | 0.1 | 0.0 | 1.4 | 1.2 | 2.1 | 1.5 | -28.6 |
| Uganda | 6.4 | 11.9 | 17.3 | 15.9 | 106.7 | 52.5 | -50.8 |
| **JUMLA –EAC** | **204.8** | **310.5** | **285.2** | **263.8** | **668.4** | **359.1** | -46.3 |
| **Nchi nyingine za Afrika** | **71.9** | **0.3** | **0.0** | **53.2** | **56.2** | **0.6** | -98.9 |
| **JUMLA NCHI ZOTE ZA AFRIKA** | **1256.4** | **1044.0** | **1112.9** | **1098.3** | **1822** | **1195.6** | -34.2 |
| **BARA LA AMERIKA** | | | | | | | |
| Marekani | 200.4 | 136.0 | 150.6 | 138.5 | 235.5 | 211.9 | -10.0 |
| Canada | 57.1 | 35.2 | 36.4 | 33.1 | 110.1 | 91.8 | -16.6 |
| **Nchi nyingine za Bara la Amerika** | **120.3** | **91.4** | **72.0** | **68.6** | **199.1** | **34.5** | -82.7 |
| **JUMLA - BARA LA AMERIKA** | **377.8** | **262.6** | **259.0** | **240.2** | **544.7** | **338.2** | -37.9 |
| **ASIA** | | | | | | | |
| China | 711.8 | 678.1 | 846.8 | 787.6 | 1145.4 | 1444.2 | 26.1 |
| India | 891.2 | 757.3 | 864.6 | 784.5 | 867.4 | 2088.2 | 140.7 |
| Japan | 711.8 | 413.6 | 548.8 | 502.9 | 510.5 | 466.7 | -8.6 |
| Hong | 18.1 | 30.7 | 23.3 | 21.1 | 52.5 | 32.7 | -37.7 |
| Singapore | 433.0 | 188.2 | 429.3 | 390.4 | 145.6 | 200.7 | 37.8 |
| Umoja wa Falme za Kiarabu | 859.7 | 618.8 | 649.3 | 590.9 | 1010.3 | 1079.3 | 6.8 |
| Nchi nyingine za Asia | 386.0 | 438.3 | 796.0 | 959.9 | 2024.9 | 381.0 | -81.2 |
| **JUMLA- ASIA** | **4011.6** | **3125.0** | **4158.1** | **4037.3** | **5756.6** | **5692.8** | -1.1 |
| **NCHI NYINGINEZO** | **-68.1** | **180.4** | **-34.3** | **2730.2** | **-1097.4** | **725.1** | -166.7 |
| **JUMLA KUU** | **7012.3** | **5834.1** | **7165.5** | **9827.5** | **10319.1** | **11029.** | 6.8 |

Chanzo: Benki Kuu na Wizara ya Fedha

P – Takwimu za Awali

## Mizania ya Malipo na Nchi za Nje

**Urari wa Biashara ya Bidhaa**

70. Mwaka 2013, urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 5,680.2 ikilinganishwa na nakisi ya Dola milioni 4,429.9 mwaka 2012, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 28.2. Hii ilitokana na kupungua kwa mauzo ya bidhaa nje sambamba na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa.

**Urari wa Biashara ya Huduma**

71. Mwaka 2013, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya Dola za Kimarekani milioni 694.1 ikilinganishwa na ziada ya Dola milioni 427.5 mwaka 2012. Ongezeko la mapato yatokanayo na shughuli za usafirishaji na usafiri hususan biashara ya utalii kulichangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa ziada katika biashara ya huduma.

**Urari wa Biashara ya Huduma na Bidhaa**

72. Mwaka 2013, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 4,986.1 ikilinganishwa na nakisi ya Dola milioni 4,002.4 mwaka 2012 sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 24.6. Ongezeko la nakisi katika biashara ya bidhaa kulichangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa nakisi katika biashara ya bidhaa na huduma.

**Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi**

73. Mwaka 2013, urari wa mapato ya vitega uchumi ambayo yanajumuisha fidia kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba ulikuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 445.5 ikilinganishwa na nakisi ya Dola milioni 607.5 mwaka 2012, sawa na upungufu wa nakisi kwa asilimia 26.7. Hata hivyo, katika mwaka 2013 malipo ya riba yaliongezeka kwa asilimia 76.1 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 148.2 ikilinganishwa na malipo ya riba mwaka 2012.

**Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida**

74. Urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha unaofanywa na sekta binafsi, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya Dola za Kimarekani milioni 774.4 mwaka 2013 ikilinganishwa na ziada ya Dola milioni 817.8 mwaka 2012. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa

misaada kutoka nchi washirika wa maendeleo. Mwaka 2013, misaada kutoka nchi washirika wa maendeleo ilishuka kwa asilimia 12.5 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 485.5 kutoka Dola milioni 554.6 mwaka 2012. Hii ilitokana na hatua ya nchi hizi kubadilisha mfumo wa utoaji wa misaada kutoka misaada ya kawaida kwenda kwenye utaratibu wa misaada kwa miradi moja kwa moja.

**Urari wa Malipo ya Kawaida**

75. Mwaka 2013, urari wa malipo ya kawaida ambao unajumuisha urari wa biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 4,657.1 ikilinganishwa na nakisi ya Dola milioni 3,792.0 mwaka 2012, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 22.8. Kuongezeka kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida kulichangiwa zaidi na kupungua kwa mauzo ya bidhaa nje, pamoja na kushuka kwa kiwango cha misaada ya kiserikali kutoka Nchi Washirika wa Maendeleo

**Urari wa Uhamisho wa Mitaji**

76. Mwaka 2013, urari wa uhamisho wa mitaji ambao unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa mashirika ya fedha ya Kimataifa na Nchi Wahisani ulikuwa na ziada ya Dola za Kimarekani milioni 659.7 ikilinganishwa na ziada ya Dola milioni 777.2 mwaka 2012. Kupungua kwa ziada ya urari wa uhamisho wa mitaji kulitokana na kupungua kwa misaada ya kawaida ya kibajeti kutoka nchi washirika wa maendeleo.

**Urari wa Malipo ya Fedha katika Uwekezaji**

77. Mwaka 2013, urari wa malipo ya fedha katika uwekezaji, unaojumuisha uwekezaji wa mitaji ya kigeni ya moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ulikuwa na ziada ya Dola za Kimarekani milioni 4,878.2 ikilinganishwa na ziada ya Dola milioni 3,874.5 mwaka 2012, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 25.9. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa mikopo yenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Vile vile, kumekuwa na kiwango kikubwa cha uwekezaji wa moja kwa moja kwenye sekta mbalimbali kama madini na gesi asilia.

**Urari wa Malipo Yote**

78. Mwaka 2013, urari wa malipo yote ulikuwa na ziada ya Dola za Kimarekani milioni 495.7 ikilinganishwa na ziada ya Dola milioni 326.2 mwaka 2012. Ongezeko hili la ziada lilitokana na kuongezeka kwa ziada katika urari wa uhamishaji wa mitaji pamoja na urari wa malipo ya fedha katika uwekezaji ambazo ziliweza kufidia nakisi katika urari wa malipo ya kawaida.

**Akiba ya Fedha za Kigeni**

79. Hali ya akiba ya fedha za kigeni mpaka mwisho wa mwezi Desemba 2013 iliendelea kuwa ya kuridhisha. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2013, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Kimarekani milioni 4,676.2 ikilinganishwa na Dola milioni 4,069.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Kiasi hiki cha akiba ya fedha za kigeni kwa mwaka 2013 kinatosheleza uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje kwa zaidi ya miezi 4.5 (ukiondoa bidhaa na huduma ambazo zinalipiwa na fedha za uwekezaji wa moja kwa moja) ikilinganishwa na miezi 3.9 iliyofikiwa mwaka 2012. Wakati huo huo, akiba ya fedha za kigeni katika benki za biashara ilipungua kwa asilimia 2.2 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 867.3 kutoka Dola milioni 887.1 mwaka 2012.

**Soko la Fedha za Kigeni kwa Mabenki**

80. Mwaka 2013, viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni viliendelea kuamuliwa na nguvu ya soko. Kiasi cha fedha za kigeni zilizouzwa katika soko la fedha za kigeni kilikuwa Dola za Kimarekani milioni 1,743.2 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 1,375.0 mwaka 2012. Kati ya mauzo yote yaliyofanyika mwaka 2013, Dola za Kimarekani milioni 961.2 (sawa na asilimia 55.1) ziliuzwa na Benki Kuu na kiasi kilichobaki kiliuzwa na benki za biashara.

**Thamani ya Fedha ya Tanzania**

81. Mwaka 2013, thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani ilishuka kwa wastani wa asilimia 1.7 ikilinganishwa na kushuka kwa asilimia 0.9 mwaka 2012. Dola moja ya Kimarekani ilinunuliwa kwa wastani wa Shilingi za Tanzania 1,598.60 mwaka 2013, ikilinganishwa na shilingi 1,571.70 mwaka 2012. Aidha, mwishoni mwa mwaka 2013 Dola moja ya Kimarekani iliuzwa kwa Shilingi 1,578.57 ikilinganishwa na Shilingi 1,571.62 mwishoni mwa mwaka 2012.

**THAMANI YA BIDHAA ZA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI ZA NJE**

Jedwali Na.17 Shs. Million

| Aina ya Bidhaa | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Zilizouzwa Nje | 1874265 | 2156732 | 2628866 | 3194929 | 3671935 | 4050561 | 7331020 | 8653372 | 8223206 |
| Bidhaa Halisi | 1726241 | 1967358 | 2413809 | 2992530 | 3568071 | 3921648 | 7175377 | 8368496 | 7012100 |
| Zilizouzwa Tena | 148024 | 189374 | 215057 | 202399 | 103864 | 128913 | 155643 | 289875 | 1211106 |
| Zilizoagizwa | 3659962 | 5534418 | 7296763 | 8839274 | 8446721 | 11086891 | 17217173 | 18275893 | 19904472 |
| Jumla | 5534227 | 7691150 | 9925629 | 12034203 | 12118656 | 15137452 | 24548193 | 26929265 | 28127678 |
| Urari | -1785697 | -3377686 | -4667897 | -5644345 | -4774785 | -7036330 | -9886153 | -9622521 | -11681266 |
| Thamani ya Fedha (Shs/US$) | 1122.7 | 1251.9 | 1232.8 | 1196.3 | 1320.3 | 1409.3 | 1557.4 | 1571.7 | 1598.6 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Idara ya forodha na Banki Kuu ya Tanzania

**KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE**

**Jedwali Na. 18**

| Bidhaa | Kiasi(Tani) | | | | | | Thamani(sh. Milioni) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | Badiliko(%) 2012/13 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | Badiliko (%) 2012/13 |
| Kahawa | 56079 | 35359 | 40456 | 54213 | 62654 | 15.6% | 147427 | 162310 | 225748 | 292787 | 259132 | -11.5% |
| Pamba | 100361 | 74859 | 43042 | 92817 | 68274 | -26.4% | 146752 | 83999 | 61636 | 164926 | 137663 | -16.5% |
| Katani | 8151 | 11601 | 13838 | 13536 | 11928 | -11.9% | 6733 | 10903 | 16931 | 18369 | 25396 | 38.3% |
| Chai | 19191 | 44254 | 27114 | 27783 | 25585 | -7.9% | 45552 | 65479 | 72257 | 87359 | 86810 | -0.6% |
| Tumbaku | 33839 | 69095 | 74022 | 110649 | 71258 | -35.6% | 168057 | 327521 | 189834 | 348062 | 159454 | -54.2% |
| Korosho | 99313 | 132675 | 99425 | 130882 | 154997 | 18.4% | 94413 | 173572 | 162715 | 221971 | 301212 | 35.7% |
| Karafuu | 4853 | 2566 | 2306 | 5957 | 4089 | -31.4% | 19453 | 11265 | 48362 | 58281 | 68429 | 17.4% |
| Almasi (Carat) | 158838 | 367849 | 417000 | 411000 | - | - | 24988 | 14234 | 16976 | - | 63584 | - |
| Dhahabu(gms) | 34600000 | 35600000 | 40400000 | 37900000 | 35100000 | -7.4% | 1420756 | 2137344 | 3463813 | 3410746 | 2768481 | -18.8% |

Chanzo: Idara ya forodha, TRA

- Takwimu hazikupatikana

Katani imebadilishwa "code" yake na umoja wa Forodha

**KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE**

Jedwali Na. 19

| Bidhaa | Kiasi (Tani) | | | | | Badiliko(%) | Thamani (Milioni US$) | | | | | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2012/13 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2012/13 |
| Bidhaa Asilia: | | | | | | | | | | | | |
| Kahawa | 56079 | 35359 | 40455 | 54213 | 62654 | 15.6 | 111.2 | 101.6 | 142.6 | 186.6 | 171.0 | -8.4 |
| Pamba | 100361 | 83999 | 43042 | 92817 | 68274 | (26.4) | 111.0 | 84.0 | 61.6 | 164.9 | 111.7 | -32.3 |
| Katani | 8198 | 9041 | 0 | 13536 | 11928 | (11.9) | 6.7 | 10.9 | 16.9 | 18.4 | 16.9 | -7.8 |
| Chai | 19191 | 44254 | 27113 | 27783 | 25585 | (7.9) | 47.2 | 49.8 | 47.2 | 56.1 | 56.9 | 1.5 |
| Tumbaku | 33839 | 69095 | 74022 | 110649 | 71258 | (35.6) | 127.4 | 232.4 | 281.2 | 350.1 | 307.0 | -12.3 |
| Korosho | 99313 | 132675 | 117041 | 130882 | 154997 | 18.4 | 68.6 | 96.9 | 107.0 | 142.6 | 162.4 | 13.9 |
| Karafuu | 4853 | 2566 | 2306 | 5957 | 4089 | (31.4) | 14.4 | 7.6 | 28.9 | 38.1 | 43.0 | 12.8 |
| **Jumla** | | | | | | | **486.4** | **583.2** | **685.5** | **956.7** | **868.9** | **-9.2** |
| Bidhaa zisizo asilia: | | | | | | | | | | | | |
| Madini | | | | | | | 1274.8 | 1561.2 | 2283.4 | 2197.8 | 1861.2 | -15.3 |
| Bidhaa za Viwanda | | | | | | | 506.5 | 964.0 | 861.5 | 1037.3 | 1072.1 | 3.3 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | | | | | | | 155.0 | 150.4 | 137.7 | 160.6 | 130.6 | -18.7 |
| Mazao ya Mboga na Maua | | | | | | | 33.3 | 30.8 | 36.4 | 31.3 | 28.1 | -10.2 |
| Bidhaa zilizouzwa tena | | | | | | | 120.4 | 132.5 | 98.3 | 181.7 | 172.8 | -4.9 |
| Bidhaa nyinginezo | | | | | | | 282.9 | 338.2 | 330.2 | 555.7 | 517.6 | -6.8 |
| **Jumla** | | | | | | | **2372.9** | **3177.0** | **3747.5** | **4164.4** | **3782.3** | **-9.2** |
| Bidhaa Zisizorekodiwa | | | | | | | 438.9 | 564.0 | 664.9 | 768.2 | 697.7 | -9.2 |
| **JUMLA KUBWA** | | | | | | | **3298.1** | **4324.3** | **5097.9** | **5889.2** | **5348.9** | **-9.2** |

Chanzo: Idara ya Forodha, TRA


I: BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE
(US$ Milioni)
US$ Milioni
4500.00
4000.00
3500.00
3000.00
2500.00
2000.00
1500.00
1000.00
500.00
0.00
2004
2005
2006
2007
2008
2009
2010
2011
2012
2013
Bidhaa asilia
Bidhaa zisizo asilia

## II: PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NCHI ZA NJE
## (Kiasi kwa Tani '000)




IIIB: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2012
Bidhaa zilizouzwa tena 3.1%
Bidhaa Zisizorekodiwa 13.0%
Mboga na Maua 0.5%
Samaki na Mazao ya Samaki 2.7%
Bidhaa nyinginezo 9.4%
Kahawa 3.2%
Pamba 2.8%
Bidha za Viwanda 17.6%
Katani 0.3%
Chai 1.0%
Tumbaku 5.9%
Karafuu 0.6%
Korosho 2.4%
Madini 37.3%



IIIA: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2013
Bidhaa nyinginezo 9.7%
Kahawa 3.2%
Pamba 2.1%
Katani 0.3%
Chai 1.1%
Tumbaku 5.7%
Korosho 3.0%
Karafuu 0.8%
Bidhaa zilizouzwa tena 3.2%
Mboga na Maua 0.5%
Bidhaa Zisizorekodiwa 13.0%
Samaki na Mazao ya Samaki 2.4%
Bidha za Viwanda 20.0%
Madini 34.8%

## WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 20 Sh./Tani*

| Bidhaa | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | $2013^{p}$ | Badiliko (%) 2012/13 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 1812959 | 2390243 | 2668414 | 2642540 | 2628934 | 4069399 | 5580087 | 5400679 | 4135909 | -23.4 |
| Pamba | 1126467 | 1221942 | 1222475 | 1767694 | 1462236 | 1775008 | 1431997 | 1724164 | 2016331 | 16.9 |
| Katani | 879366 | 931090 | 1047444 | 946323 | 1951011 | 1986211 | 2091121 | 2102332 | 2129058 | 1.3 |
| Chai | 1322780 | 1680523 | 1581921 | 1861435 | 2373683 | 2501897 | 2664933 | 3144333 | 3392989 | 7.9 |
| Tumbaku | 2938727 | 3440586 | 2869021 | 4593309 | 4970800 | 2586996 | 2564562 | 3145641 | 2237711 | -28.9 |
| Korosho | 874903 | 1058854 | 2278459 | 1356504 | 950656 | 1284308 | 1636560 | 1695963 | 1943340 | 14.6 |
| Karafuu | 3210533 | 3285196 | 3321160 | 4202786 | 4008131 | 4390290 | 20972246 | 9783616 | 16735615 | 71.1 |
| Almasi (kwa carat) | 129576 | 138878 | 156300 | 157692 | 157319 | 38695 | 40709 | 99809 | - | - |
| Dhahabu (kwa gramu) | 24223 | 21778 | 9982 | 34504 | 40826 | 60038 | 85738 | 89993 | 78874 | -12.4 |

Chanzo:Idara ya Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

p - Takwimu za Awali

## WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 21

US$/Tani*

| Bidhaa | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | $2013^p$ | Badiliko(%) 2012/13 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 1612 | 1932 | 2165 | 2203 | 1991 | 3318 | 3609 | 3468 | 2602 | -25.0% |
| Pamba | 988 | 988 | 992 | 1321 | 1108 | 1306 | 1431 | 1353 | 1274 | -5.8% |
| Katani | 785 | 751 | 850 | 1251 | 980 | 880 | 1010 | 1250 | 1341 | 7.3% |
| Chai | 1174 | 1359 | 1283 | 1575 | 1542 | 1125 | 1741 | 2016 | 2150 | 6.7% |
| Tumbaku | 2598 | 2779 | 2327 | 3041 | 3762 | 3363 | 3799 | 2015 | 3256 | 61.5% |
| Korosho | 752 | 855 | 1848 | 730 | 720 | 730 | 914 | 1085 | 1065 | -1.9% |
| Karafuu | 2833 | 2638 | 2694 | 3578 | 3036 | 3173 | 13443 | 6211 | 10516 | 69.3% |
| Almasi (kwa carat) | 115 | 111 | 127 | 133 | 1193 | 3028 | 2395 | 2188 | - | - |
| Dhahabu (kwa gramu) | 12.30 | 17.40 | 8.10 | 1.78 | 35.34 | 42.58 | 55.01 | 57.26 | 35.10 | -38.7% |

Chanzo: Idara ya forodha, TRA

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

p - Takwimu za Awali


MWENENDO WA BEI YA PAMBA NA KAHAWA
ILIYOUZWA NCHI ZA NJE (US$/Tani)
US$
4000.0
3500.0
3000.0
2500.0
2000.0
1500.0
1000.0
500.0
0.0
2004
2005
2006
2007
2008
2009
2010
2011
2012
2013
Kahawa
Pamba

## AINA NA THAMANI YA BIDHAA ZILIZOAGIZWA TOKA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 23 Sh. Milioni

| Mwaka | Bidhaa za Matumizi ya Kawaida | Bidhaa za Kati | Bidhaa za Viwanda | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1987 | 13180 | 23819 | 41948 | 78947 |
| 1988 | 29841 | 55284 | 43950 | 129075 |
| 1989 | 34779 | 60176 | 96804 | 191759 |
| 1990* | 18783 | 116277 | 96223 | 231283 |
| 1991 | 62000 | 69710 | 139668 | 271378 |
| 1992 | 101641 | 94233 | 196791 | 392665 |
| 1993 | 194604 | 107481 | 229657 | 531742 |
| 1994 | 247076 | 128544 | 290638 | 666258 |
| 1995 | 201347 | 294224 | 275207 | 770778 |
| 1996 | 182340 | 267600 | 252501 | 702441 |
| 1997 | 301018 | 203418 | 198670 | 703106 |
| 1998 | 441025 | 155225 | 311244 | 907495 |
| 1999 | 503868 | 197271 | 360225 | 1061363 |
| 2000 | 401612 | 222399 | 444427 | 1068438 |
| 2001 | 468173 | 386317 | 648361 | 1502851 |
| 2002 | 499346 | 408872 | 697209 | 1605426 |
| 2003 | 654630 | 705729 | 846251 | 2206610 |
| 2004 | 917953 | 1024705 | 1029389 | 2972046 |
| 2005 | 937031 | 1451062 | 1341462 | 3729555 |
| 2006 | 1068550 | 1977695 | 1799855 | 4846100 |
| 2007 | 1393799 | 2441781 | 2186910 | 6022490 |
| 2008 | 1703932 | 3217747 | 3537543 | 8459222 |
| 2009 | 1836142 | 2471066 | 3319331 | 7626538 |
| 2010 | 2395659 | 3842586 | 3806139 | 10044384 |
| 2011 | 3322611 | 6462590 | 5559326 | 15344528 |
| 2012 | 3631073 | 6790046 | 5794109 | 16215229 |
| 2013 | 3774647 | 8320829 | 5531694 | 17627170 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

*Angalia: Kuanzia mwaka 1990, thamani ya bidhaa zilizoagizwa ni f.o.b. badala ya c.i.f.

**MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE**

Jedwali Na. 24 US $ milioni

| | 2004 Halisi | 2005 Halisi | 2006 Halisi | 2007 Halisi | 2008 Halisi | 2009 Halisi | 2010 Halisi | 2011 Halisi | 2012 Halisi | 2013 Matarajio |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Urari wa Biashara** | **-1009.7** | **-1321.8** | **-1946.5** | **-2634.1** | **-3433.5** | **-2536.1** | **-2841.2** | **-4729.6** | **-4429.9** | **-5680.2** |
| Zilizouzwa nje (fob) | 1473.1 | 1675.8 | 1917.6 | 2226.6 | 3578.8 | 3298.1 | 4324.3 | 5097.9 | 5889.2 | 5348.9 |
| Zilizonunuliwa toka nje (fob)* | 2482.8 | 2997.6 | 3864.1 | 4860.6 | 7012.3 | 5834.1 | 7165.5 | 9827.5 | 10319.1 | 11029.1 |
| Urari wa Huduma | 158.9 | 61.8 | 278.8 | 462.1 | 336.9 | 132.7 | 156.9 | 92.2 | 427.5 | 694.1 |
| Mapato | 1133.6 | 1269.2 | 1528.1 | 1875.7 | 1998.8 | 1854.6 | 2045.7 | 2300.3 | 2786.4 | 3183.0 |
| Malipo | 974.7 | 1207.3 | 1249.3 | 1413.7 | 1661.9 | 1722.0 | 1888.9 | 2208.1 | 2358.9 | 2488.9 |
| Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi | -119.1 | -104.1 | -94.8 | -282.1 | 559.7 | -297.8 | -326.9 | -257.1 | -607.5 | -445.5 |
| Yaliyoingia | 81.8 | 80.9 | 80.3 | 107.3 | 122.7 | 161.1 | 160.1 | 184.2 | 131.1 | 130.1 |
| Yaliyotoka | 200.9 | 185.0 | 175.1 | 389.4 | -437.0 | 458.9 | 487.0 | 441.3 | 738.5 | 575.5 |
| Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida | 586.7 | 496.4 | 588.7 | 651.5 | 833.8 | 891.2 | 1051.2 | 902.2 | 817.8 | 774.4 |
| Iliyoingia | 651.7 | 563.9 | 654.6 | 724.0 | 913.4 | 959.7 | 1130.2 | 994.9 | 923.3 | 837.3 |
| Serikalini | 582.0 | 478.5 | 559.7 | 626.9 | 588.5 | 658.4 | 798.1 | 609.7 | 554.6 | 485.5 |
| Sekta nyingine | 69.7 | 85.4 | 94.9 | 97.1 | 324.9 | 301.3 | 332.1 | 385.2 | 368.7 | 351.7 |
| Iliyotoka | 65.0 | 67.5 | 65.9 | 72.5 | 79.6 | 68.4 | 79.0 | 92.7 | 105.4 | 62.9 |
| **Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali** | **-383.2** | **-867.6** | **-1173.8** | **-1802.6** | **-1703.1** | **-1809.9** | **-1960.1** | **-3992.2** | **-3792.0** | **-4657.1** |
| Urari wa Uhamisho wa Mitaji | 460.0 | 393.2 | 5183.5 | 938.5 | 524.2 | 442.2 | 537.9 | 690.9 | 777.2 | 659.7 |
| Iliyoingia | 460 | 393.2 | 5183.5 | 938.5 | 524.2 | 442.2 | 537.9 | 690.9 | 777.2 | 659.7 |
| Iliyotoka | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Urari katika uwekezaji | 275.6 | 807.6 | -4081.6 | 873.0 | 2592.8 | 1984.4 | 3074.3 | 3424.5 | 3874.5 | 4878.2 |
| Uwekezaji katika miradi | 330.6 | 494.1 | 403.0 | 581.5 | 1383.3 | 952.6 | 1812.5 | 1229.4 | 1799.6 | 1872.4 |
| Uwekezaji katika hisa | 2.4 | 2.5 | 2.6 | 4.3 | 1.8 | 3.5 | 3.4 | 4.0 | 1.0 | 6.7 |
| Uwekezaji aina nyingine | -57.4 | 311.0 | -4487.3 | 287.1 | 1207.8 | 1028.3 | 1258.4 | 2191.1 | 2073.9 | 2999.1 |
| Makosa na Masahihisho | -146.3 | -555.4 | 532.6 | 307.8 | -391.9 | -250.5 | -1282.3 | -325.2 | -533.5 | -385.1 |
| **Urari wa Malipo yote** | **206.1** | **-222.2** | **460.8** | **316.7** | **1022.0** | **366.2** | **369.8** | **-202.0** | **326.2** | **495.7** |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Kuanzia mwaka 2006 bidhaa zilizouzwa nje zinajumuisha pia zile zisizorekodiwa (Unrecorded trade)


MWENENDO WA URARI KATIKA MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE
US $ milioni
2000.0
1000.0
0.0
-1000.0
-2000.0
-3000.0
-4000.0
-5000.0
-6000.0
-7000.0
2004
2005
2006
2007
2008
2009
2010
2011
2012
2013
Urari wa Biashara
Huduma na Uhamisho Mali
Urari wa Malipo yote

# SURA YA 4

## FEDHA ZA SERIKALI

**Utangulizi**

82. Bajeti ya mwaka 2013/14 ilizingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye: Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/14 na mfumo mpya wa utekelezaji wa vipaumbele vyenye matokeo makubwa na ya haraka; Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA II); Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010; na programu za maboresho katika sekta ya umma. Lengo likiwa ni kufikia Dira yaTaifa ya Maendeleo 2025.

83. Bajeti ya mwaka 2013/14, pamoja na mambo mengine ilijielekeza katika kufikia shabaha na malengo yafuatayo: kuongezeka kwa mapato ya ndani yatakayofikia uwiano na Pato la Taifa wa asilimia 20.2 mwaka 2013/14; kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 5.0 ya Pato la Taifa mwaka 2013/14; kuimarisha utaratibu wa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma ili kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kuimarisha uhusiano na Washirika wa Maendeleo; kuongeza mapato ya ndani kwa kuimarisha vyanzo vilivyopo na kubuni vyanzo vipya vya mapato pamoja na kuendelea kuimarisha usimamizi katika matumizi ya fedha za umma; na kuboresha mfumo wa utekelezaji wa vipaumbele na uwajibikaji.

84. Katika kipindi cha mwaka 2013/14, Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 18,249.1 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Kati ya mapato hayo, mapato ya kodi na mapato yasiyo ya kodi yalitarajiwa kufikia shilingi bilioni 11,154.1, sawa na asilimia 20.2 ya Pato la Taifa. Mapato kutokana na vyanzo vya Halmashauri yalikadiriwa kufikia shilingi bilioni 383.5, sawa na asilimia 0.7 ya Pato la Taifa. Katika kipindi hicho, Washirika wa Maendeleo walitarajiwa kutoa misaada na mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 3,855.2. Aidha, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 2,856.3 kutoka katika vyanzo vya ndani na nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, ambapo shilingi bilioni 1,156.4 ni mikopo yenye masharti ya kibiashara kuwiana na ukomo wa kukopa.

**Mwenendo wa Mapato**

**Mapato ya Ndani**

85. Katika mwaka 2013/14, sera za mapato zililenga kukusanya mapato ya ndani ya serikali kuu jumla ya shilingi bilioni 11,154, sawa na asilimia 61.1 ya bajeti yote ya Serikali. Kufikia Machi, 2014, mapato ya ndani ya serikali kuu yalifikia shilingi bilioni 7,130.076, ambayo ni sawa na asilimia 92 ya makadirio ya kipindi hicho kilichoishia Machi 2014 ya shilingi bilioni 7,750.

86. Mapato ya kodi hayakufikia lengo kutokana na kushuka kwa makusanyo hususan kwenye kodi ya zuio kutokana na kupungua kwa makusanyo kwenye shughuli za utafiti wa gesi na mafuta. Aidha, kulikuwa na mapato pungufu ya kodi ya makampuni kuliko ilivyotarajiwa kutoka kwenye baadhi ya makampuni ya madini kutokana na kushuka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia. Kadhalika, kampuni za simu za mikononi hazikukusanya tozo ya kadi za simu (*SIMcard levy*) ambayo ili tarajiwa kuiingizia Serikali mapato ya shilingi bilioni 178 katika mwaka huu wa fedha ambapo hadi kufikia mwezi Desemba, 2013 hakuna kiasi chochote cha tozo ya kadi za simu kilichokuwa kimekusanywa. Kuanzia Januari 2014, Bunge lilibadilisha tozo za kadi ya simu kuwa nyongeza kwenye ushuru wa bidhaa kwenye kadi za simu.

87. Hadi Machi 2014, mapato yasiyotokana na kodi yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 366.4 ikiwa ni asilimia 60 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 555.75 kwa kipindi hicho. Lengo la makusanyo katika kipindi husika halikufikiwa kutokana na baadhi ya tozo kutoanza kutozwa kama ilivyopendekezwa ikiwa ni pamoja na *bednight Levy* na michango isiyoridhisha kutoka kwa Mashirika na Taasisi. Aidha, hadi Machi 2014, mapato ya halmashauri yalifikia shilingi bilioni 213, sawa na asilimia 82 ya makadirio kwa kipindi husika. Kutofikiwa kwa lengo kulitokana na: kuchelewa kuanza ukusanyaji wa ada za leseni na zoezi la kuthamanisha majengo kufanyika pasipo umakini na hivyo kuathiri ukusanyaji wa kodi ya majengo.

**Misaada na Mikopo Nafuu**

88. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, jumla ya shilingi bilioni 1,201.38 zilipokelewa kama misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa ni asilimia 50 ya ahadi ya shilingi bilioni 2,390.78. Jumla ya misaada ya

kibajeti (GBS) iliyopokelewa katika kipindi cha Julai 2013 – Machi 2014 ilikuwa shilingi bilioni 495.49 zikiwa ni asilimia 64 ya ahadi ya shilingi bilioni 776.91. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 206.278 zilipokelewa kupitia misaada ya mifuko ya kisekta, ikiwa ni asilimia 78 ya makadirio ya shilingi bilioni 266.07 kwa mwaka 2013/14. Misaada iliyopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Julai 2013 – Machi 2014 ilifikia shilingi bilioni 508.4 ambayo ni asilimia 38 ya ahadi ya shilingi bilioni 1,347.80 kwa mwaka 2013/14.

**Mikopo ya Kibiashara ya Ndani**

89. Katika kipindi cha Julai 2013 – Machi, 2014, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 1,242.763 ikiwa ni asilimia 125 ya makadirio ya shilingi bilioni 996.9 zilizopangwa kukopwa kwa ajili ya kulipia Hatifungani na amana za Serikali zilizoiva (*rollover*) kwa kipindi kilichoishia Machi 2014. Aidha, hadi Machi 2014, Serikali ilikopa kiasi cha shilingi bilioni 474.6 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 99 zaidi ya kiasi kilichopangwa kukopwa kwa kipindi husika. Lengo kuu la mwaka 2013/14 ni kukopa ndani asilimia moja ya Pato la Taifa, sawa na shilingi bilioni 552.

**Mikopo ya Kibiashara kutoka Nje**

90. Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 1,156.4, sawa na Dola za Kimarekani milioni 700 kutoka kwenye vyanzo vya nje ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi, 2014, kiasi cha dola milioni 394.116 kilipatikana. Kati ya kiasi hicho, dola milioni 238.75 zimepatikana kutoka Benki ya *Credit Suisse* na HBS kwa ajili ya kugharamia miradi ya Maendeleo ya Serikali na dola milioni 83 zimepatikana kutoka Benki ya Citi kwa ajili ya kugharamia miradi ya ufuaji umeme inayoendeshwa na TANESCO. Majadiliano ya kupata kiasi kilichobaki yanaendelea na yako katika hatua za mwisho.

**Matumizi**

91. Sera za matumizi ya Serikali kwa mwaka 2013/14, zililenga yafuatayo: kuwianisha matumizi na mapato yanayotarajiwa; mafungu yatazingatia viwango vya matumizi vitakavyoidhinishwa na Bunge; kutenga fedha za kutosha katika kutekeleza miradi ya vipaumbele vilivyoainishwa; na kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi wa Umma.

92. Sera za matumizi ya mwaka 2013/14 zilizingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/14 ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kutumia kiasi cha shilingi bilioni 18,249 kwa matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 12,604 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 5,645. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 kiasi cha shilingi bilioni 11,559 kilitumika sawa na asilimia 93 ya makadirio ya kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 8,823 na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 2,735.

**Matumizi ya Kawaida**

**Mishahara**

93. Malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali kwa kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014 yalikuwa shilingi bilioni 3,356.4, sawa na asilimia 99 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi bilioni 1,401.8 zilitolewa kwa ajili ya watumishi wa wizara, idara zinazojitegemea na taasisi za serikali; shilingi bilioni 82.6 kwa watumishi wa sekretarieti za mikoa; na shilingi bilioni 1,872.1 kwa ajili ya mishahara ya halmashauri za jiji, manispaa, miji na wilaya.

**Malipo ya Deni**

94. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, malipo ya riba kwa madeni ya ndani na nje yalifikia shilingi bilioni 507.4 na shilingi bilioni 286.3 kwa mtiririko huo, ikiwa ni kiasi sawa na lengo la kipindi hicho. Aidha, kwa upande wa malipo ya mtaji, Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 1,695 ikiwa ni kiasi sawa na lengo la kipindi hicho. Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika ulipaji wa madeni kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya riba.

**Matumizi Mengineyo**

95. Matumizi mengineyo ya Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za serikali, Mikoa na Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 3,068 hadi Machi 2014, ikiwa ni asilimia 96.5 ya makadirio ya shilingi bilioni 3,179 kwa kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, matumizi yatokanayo na mapato ya ndani ya Halmashauri ni shilingi

bilioni 181. Kwa upande wa ruzuku toka mfuko mkuu wa Serikali, mafungu ya wizara yalipewa jumla ya shilingi bilioni 2,624.4, sawa na asilimia 88.6 ya makadirio ya shilingi bilioni 2,960.7 kwa kipindi hicho; mafungu ya mikoa shilingi bilioni 32.24, sawa na asilimia 86.5; na mafungu ya Halmashauri shilingi bilioni 230.47, sawa na asilimia 89.8.

**Matumizi ya Maendeleo**

96. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi, 2014 jumla ya matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 2,758.019, sawa na asilimia 5 zaidi ya lengo la kipindi hicho la shilingi bilioni 2,619. Kati ya kiasi hicho, fedha za ndani zilikuwa shilingi bilioni 1,221.848, sawa na asilimia 110 na fedha za nje zilikuwa shilingi bilioni 1,536.171, sawa na asilimia 100 ya lango la kipindi kilichoishia Machi 2014.

**Deni la Taifa**

97. Hadi Desemba 2013, deni la taifa lilikuwa limefikia Dola za Kimarekani bilioni 17.10, sawa na shilingi trilioni 27.04 ikilinganishwa na shilingi trilioni 22.71 katika kipindi kama hicho mwaka 2012, ikiwa ni ongezeko la asilimia 19.1. Ongezeko hilo lilitokana na mikopo mipya yenye masharti nafuu na ya kibiashara na malimbikizo ya riba ya deni la nje hasa kwenye nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris ambazo hazitoa misamaha ya madeni kulingana na makubaliano. Mikopo hii ilitumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo: ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es salaam; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara; ujenzi wa miundombinu ya umeme; na mradi wa maji wa Ruvu juu na Ruvu chini.

98. Kati ya kiasi cha deni la taifa hadi Desemba 2013, deni la nje lilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 12.79, sawa na shilingi trilioni 20.23 ambazo ni asilimia 74.8 ya deni la taifa. Kati ya deni la nje la taifa, Dola za Kimarekani milioni 10,563, sawa na shilingi trilioni 16.71 ni deni la Serikali na Dola za Kimarekani bilioni 2.23, sawa na shilingi trilioni 3.52 zilikuwa deni la sekta binafsi. Aidha, deni la nje la Serikali linajumuisha malimbikizo ya riba ya deni la nje ya kiasi cha dola milioni 801.7 na kiasi kilichobaki cha dola 9,761.3 ni bakaa ya deni.

99. Mikopo ya masharti nafuu kutoka Mashirika ya Fedha ya Kimataifa iliendelea kuwa chanzo kikubwa cha mikopo kutoka nje ambapo ilichangia asilimia 60 ya mikopo yote ya nje ikilinganishwa na asilimia 75 Desemba 2012. Aidha, mikopo kutoka nchi wahisani ilichangia asilimia 17 na mikopo yenye masharti ya kibiashara ilichangia asilimia 23 ya mikopo yote ya nje Desemba 2013 ikilinganishwa na asilimia 13 na 12 Desemba 2012 kwa mtiririko huo.

100. Hadi kufikia Desemba 2013, deni la ndani la Serikali linalojumuisha dhamana za muda mfupi kwa ajili ya kudhibiti ukwasi katika uchumi lilikuwa shilingi trilioni 6.81 ikilinganishwa na shilingi trilioni 6.17 Desemba 2012, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Ongezeko hilo lilitokana na mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, uchambuzi wa deni la ndani la Serikali kwa makundi yanayohodhi ulibainisha kuwa benki za biashara zinaendelea kuhodhi sehemu kubwa ya deni hilo. Hadi kufikia mwishoni mwa Desemba 2013, benki za biashara ziilikua zinahodhi asilimia 47.4 ya deni lote la ndani ikilinganishwa na asilimia 48.8 Desemba 2012, ikifuatiwa na Benki Kuu ya Tanzania asilimia 26.2 ikilinganishwa na asilimia 28.9 Desemba 2012, mifuko ya hifadhi ya jamii/makampuni ya bima asilimia 25.9 ikilinganishwa na asilimia 21.2 Desemba 2012 na watu binafsi asilimia 0.5 ikilinganishwa na asilimia 1.1 Desemba 2012.

**Kielelezo Na. 4.1: Deni la Ndani kwa Mkopeshaji- Desemba 2013**




**Uhimilivu wa Deni la Taifa**

101. Katika kutekeleza Mkakati wa Deni la Taifa, Serikali iliendelea kusimamia kwa umakini deni lake kwa kukopa zaidi kutoka vyanzo nafuu na kuchambua athari zinazotokana na mikopo mipya. Vyanzo vikuu vya mikopo nafuu ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Umoja wa nchi za Ulaya, China, India, Japani, Korea ya Kusini na Nchi za Kiarabu. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika mwezi Septemba, 2013, ilionesha kuwa deni la Taifa ni himilivu kama viashiria vya deni vinavyoonesha katika Jedwali Na.4.1

**Jedwali Na.4.1: Viashiria vya Uhimilivu wa Deni hadi mwaka 2030**

| Aina ya Kiashiria | 2013 | 2017 | 2023 | 2027 | 2030 | Ukomo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni la nje kwa sasa /Pato la Taifa | 24.83 | 25.19 | 17.00 | 14.02 | 12.54 | **50** |
| Deni la nje kwa sasa / uuzaji wa bidhaa nje | 93.80 | 92.77 | 61.69 | 50.88 | 45.49 | **200** |
| Deni la nje kwa sasa / Mapato ya ndani | 121.23 | 117.04 | 78.54 | 63.76 | 56.77 | **300** |
| Ulipaji wa deni la nje/Uuzaji wa bidhaa nje | 3.34 | 5.89 | 3.03 | 2.89 | 2.72 | **25** |
| Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani | 4.32 | 7.44 | 3.86 | 3.63 | 3.40 | **22** |
| Deni la Serikali kwa sasa/Pato la Taifa | 35.58 | 35.10 | 25.60 | 21.93 | 20.04 | **74** |

Chanzo: WizarayaFedha

**MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI**

Jedwali Na. 25

Sh. milioni

| | 2006/07 Halisi | 2007/08 Halisi | 2008/09 halisi | 2009/10 halisi | 2010/11 Halisi | 2011/12 Halisi | 2012/13 Halisi | 2013/14 Bajeti | 2013/14 Matokeo hadi March | 2013/14 Matarajio hadi Juni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri) | 2739022 | 3634581 | 4293075 | 4661540 | 5736266 | 7221409 | 8442611 | 11537523 | 7130076 | 10747230 |
| MAPATO YA NDANI | 2739022 | 3634581 | 4293075 | 4661540 | 5577986 | 7025884 | 8221776 | 11154071 | 6917076 | 10363778 |
| 1. Mapato yatokanayo na Kodi | 2529439 | 3359250 | 4043674 | 4427834 | 5293277 | 6480478 | 7729986 | 10395440 | 6550704 | 9817620 |
| Ushuru wa Forodha na Excise Duty | 765644 | 965498 | 1130860 | 1214626 | 1512135 | 1538617 | 1845218 | 2768933 | 1599261 | 2401100 |
| Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) | 861050 | 1110951 | 1333789 | 1488452 | 1632863 | 2072621 | 2374977 | 2991086 | 1922983 | 2841532 |
| Bidhaa toka nje | 431614 | 550289 | 641392 | 729040 | 905611 | 1082918 | 1240149 | 1494836 | 938765 | 1420094 |
| Bidhaa za ndani | 429436 | 560661 | 692397 | 759412 | 727252 | 989703 | 1134829 | 1496251 | 984218 | 1421438 |
| Kodi ya Mapato | 790877 | 1028902 | 1257861 | 1388778 | 1719790 | 2311350 | 3036110 | 3681997 | 2461768 | 3605900 |
| Kodi nyingine | 218581 | 382792 | 462544 | 499497 | 601448 | 732303 | 706910 | 1387587 | 928592 | 1359836 |
| Marejesho (Refunds Accounts) | -106713 | -128893 | -141380 | -163519 | -172959 | -174414 | -233231 | -434164 | -361901 | -390748 |
| 2. Mapato yasiyotokana na Kodi | 209583 | 275331 | 249401 | 233707 | 284709 | 545406 | 491790 | 758631 | 366372 | 546159 |
| 3. Mapato ya Halmashauri | | | | | 158280 | 195525 | 220835 | 383452 | 213000 | 383452 |
| | | | | | | | | | | |
| B. JUMLA YA MATUMIZI | 4474680 | 5208996 | 6811827 | 8173749 | 9439407 | 10764528 | 13543018 | 16710973 | 9493308 | 14862397 |
| 1. Matumizi ya Kawaida | 3137469 | 3398024 | 4681459 | 5562443 | 6690370 | 6989807 | 9043323 | 11065984 | 6735289 | 9217407 |
| 2. Matumizi ya Maendeleo | 1337211 | 1810972 | 2130368 | 2611306 | 2749037 | 3774722 | 4499695 | 5644989 | 2758019 | 5644989 |
| Fedha za ndani | 503291 | 567421 | 906023 | 1004530 | 984555 | 1872312 | 2314718 | 2952920 | 1221848 | 2952920 |
| Fedha za nje | 833920 | 1243551 | 1224345 | 1606776 | 1764482 | 1902410 | 2184977 | 2692069 | 1536171 | 2692069 |
| | | | | | | | | | | |
| C. NAKISI/SALIO (A-B) | -1735658 | -1574415 | -2518752 | -3512209 | -3703141 | -3543120 | -5100407 | -5173450 | -2363232 | -4115166 |
| | | | | | | | | | | |
| D. KUZIBA NAKISI | 1735660 | 1574415 | 2518752 | 3512209 | 3703141 | 3543120 | 5100407 | 5173450 | 2363232 | 4115166 |
| 1. Fedha kutoka nje | 1689337 | 2302805 | 2201485 | 2784944 | 2776309 | 3590357 | 3942498 | 4621166 | 2300925 | 4112660 |
| Ruzuku | 971547 | 1573195 | 1257283 | 1405288 | 1627425 | 1855097 | 1447013 | 2124096 | 995105 | 1746984 |
| Basket support | 47331 | 200628 | 151370 | 194071 | 220681 | 172212 | 280936 | 266070 | 206278 | 159220 |
| Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL | 266946 | 365038 | 331315 | 558320 | 173806 | 246850 | 543817 | 620573 | 339785 | 589544 |
| Mikopo ya miradi | 433203 | 209342 | 488795 | 695597 | 643395 | 595414 | 734389 | 844461 | 482554 | 692103 |
| Mikopo ya masharti ya kibiashara | | | | | 153948 | 801282 | 1063006 | 1156400 | 394116 | 1156400 |
| Kulipia madeni ya nje (Amortization Foreign | -29690 | -45399 | -27278 | -68331 | -42946 | -80497 | -126663 | -390433 | -116914 | -231591 |
| 2. Fedha za Ndani | 46323 | -728390 | 317267 | 727265 | 926832 | -47237 | 1157910 | 552284 | 62307 | 2507 |
| Mikopo isiyo ya mabenki | 212475 | -19795 | 1108 | -24754 | 337494 | 263614 | 401391 | 55228 | -37881 | 55228 |
| Mikopo ya mabenki | 25533 | -316755 | 212567 | 593023 | 906837 | 71250 | 667930 | 497056 | 413472 | 497056 |
| Mikopo ya ndani (Rollover) | | | | 714315 | 720249 | 1326852 | 1734535 | 1147576 | 1242763 | 1622891 |
| Mapato ya Ubinafsishaji | 0 | 0 | 45000 | 9659 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Marekebisho (Adjustment to Cash) | -60370 | -78308 | 275298 | 595034 | 162629 | -198539 | 439984 | 0 | 297347 | 60853 |
| Kulipia madeni ya ndani (amortization) | 0 | -14648 | 0 | -723776 | -720249 | -1326852 | -1734535 | -1147576 | -1242763 | -1622891 |
| Expenditure float | -131315 | -298884 | -216706 | -436236 | -480127 | -183562 | -351395 | 0 | -610630 | -610630 |

Chanzo: Wizara ya Fedha


MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI
Sh. milioni
20000000
15000000
10000000
5000000
0
-5000000
-10000000
2006/07
2007/08
2008/09
2009/10
2010/11
2011/12
2012/13
2013/14
MAPATO YA NDANI
B. JUMLA YA MATUMIZI
C. NAKISI/SALIO (A-B)

**MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI**

Jedwali Na. 26 Sh. Milioni

| Fungu | Melezo | 2012/2013 | | | 2013/2014* | | | 2014/2015* | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
| **701** | **Huduma za kawaida** | **6,552,891** | **871,073** | **7,423,964** | **7,865,795** | **925,639** | **8,791,434** | **9,029,085** | **750,216** | **9,779,301** |
| 70111 | Utawala na shughuli za bunge | 284,570 | 13,316 | 297,886 | 286,570 | 30,216 | 316,787 | 303,850 | 35,875 | 339,724 |
| 70112 | Fedha na masuala ya kodi | 401,148 | 341,810 | 742,959 | 1,453,635 | 294,484 | 1,748,119 | 959,933 | 78,564 | 1,038,497 |
| 70113 | Mambo ya nje (CS) | 128,419 | 13,261 | 141,680 | 101,990 | 28,000 | 129,990 | 150,981 | 30,000 | 180,981 |
| 70121 | Misaada ya kiuchumi kutoka nje | 1,474 | 0 | 1,474 | 1,683 | 0 | 1,683 | 1,936 | 0 | 1,936 |
| 70122 | Misaada ya kiuchumi kupitia Mashirika ya Kimataifa | 126 | 0 | 126 | 244 | 0 | 244 | 425 | 0 | 425 |
| 70131 | Huduma za Umma | 77,903 | 49,986 | 127,889 | 86,180 | 101,123 | 187,304 | 106,119 | 76,284 | 182,403 |
| 70132 | Huduma za Mipango na Takwimu | 472,742 | 167,446 | 640,188 | 480,399 | 60,048 | 540,447 | 544,913 | 76,944 | 621,857 |
| 70133 | Huduma nyinginezo za kawaida (CS) | 139,325 | 18 | 139,343 | 176,554 | 1,320 | 177,874 | 258,776 | 5,823 | 264,599 |
| 70140 | Utafiti wa Msingi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70150 | Utafiti na Maendeleo Huduma za Umma | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70160 | Huduma za Umma zizizotajwa hapo juu | 8,553 | 0 | 8,553 | 4,351 | 1,959 | 6,310 | 4,870 | 2,699 | 7,569 |
| 70170 | Deni la taifa (CS) | 3,341,691 | 0 | 3,341,691 | 3,319,018 | 0 | 3,319,018 | 4,354,865 | 0 | 4,354,865 |
| 70180 | Uhamishaji Fedha ndani ya Serikali | 1,696,941 | 285,236 | 1,982,176 | 1,955,170 | 408,487 | 2,363,658 | 2,342,417 | 444,028 | 2,786,445 |
| **702** | **Ulinzi** | **798,933** | **229,700** | **1,028,633** | **854,237** | **245,582** | **1,099,819** | **1,016,711** | **245,645** | **1,262,356** |
| 70210 | Huduma za Ulinzi wa Kijeshi | 798,933 | 229,700 | 1,028,633 | 854,237 | 245,582 | 1,099,819 | 1,016,711 | 245,645 | 1,262,356 |
| 70220 | Huduma za Ulinzi wa Kiraia | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70230 | Misaada ya nje ya ulinzi (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70240 | Utafiti na maendeleo ya ulinzi (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70250 | Huduma za ulinzi zisizotajwa hapo juu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **703** | **Usalama wa Raia** | **752,128** | **58,439** | **810,567** | **733,463** | **224,357** | **957,821** | **827,068** | **270,815** | **1,097,883** |
| 70310 | Huduma za polisi (CS) | 489,964 | 46,102 | 536,065 | 436,919 | 160,180 | 597,099 | 493,193 | 212,809 | 706,002 |
| 70320 | Huduma za zimamoto (CS) | 8,070 | 0 | 8,070 | 10,540 | 0 | 10,540 | 10,787 | 0 | 10,787 |
| 70330 | Mahakama (CS) | 114,532 | 11,723 | 126,255 | 168,199 | 61,810 | 230,009 | 183,360 | 56,393 | 239,753 |
| 70340 | Magereza (CS) | 139,346 | 615 | 139,961 | 117,643 | 2,367 | 120,010 | 139,319 | 1,613 | 140,931 |
| 70350 | Huduma za Utafiti na Maendeleo Usalama wa Raia | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70360 | Huduma Usalama wa Raia zizizotajwa hapo juu | 217 | 0 | 217 | 163 | 0 | 163 | 410 | 0 | 410 |
| **704** | **Shughuli za kiuchumi** | **734,282** | **1,631,808** | **2,366,090** | **962,304** | **2,663,531** | **3,625,835** | **1,153,586** | **2,269,079** | **3,422,665** |
| 70411 | Shughuli za kiuchumi na biashara (CS) | 14,399 | 49,630 | 64,029 | 15,265 | 58,886 | 74,151 | 19,701 | 82,342 | 102,044 |
| 70412 | Masuala ya kazi (CS) | 10,711 | 0 | 10,711 | 12,337 | 0 | 12,337 | 14,307 | 3,000 | 17,307 |
| 70421 | Kilimo (CS) | 181,123 | 85,123 | 266,246 | 303,925 | 145,452 | 449,377 | 312,360 | 112,202 | 424,561 |
| 70422 | Misitu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70423 | Uvuvi na uwindaji (CS) | 6,456 | 2,614 | 9,070 | 7,849 | 0 | 7,849 | 8,050 | 0 | 8,050 |
| 70431 | Makaa ya mawe na nishati Nyingine | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70432 | Petroli na gesi asilia (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70433 | Nishati ya Nyukilia | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70434 | Nishati Nyingine | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70435 | Umeme (CS) | 43,048 | 604,764 | 647,812 | 44,879 | 1,131,653 | 1,176,532 | 34,120 | 923,805 | 957,925 |
| 70436 | Nishati isiyo ya Umeme | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70441 | Uchimaji Madini yasiyo ya Nishati | 28,954 | 0 | 28,954 | 14,144 | 0 | 14,144 | 20,352 | 0 | 20,352 |
| 70442 | Uzalishaji viwandani (CS) | 5,789 | 4,194 | 9,983 | 5,886 | 6,225 | 12,110 | 5,622 | 2,769 | 8,391 |
| 70443 | Ujenzi (CS) | 40,444 | 37,424 | 77,868 | 42,667 | 52,855 | 95,523 | 58,242 | 44,417 | 102,659 |
| 70451 | Usafiri wa barabara (CS) | 373,702 | 771,493 | 1,145,194 | 476,337 | 983,749 | 1,460,086 | 634,900 | 788,496 | 1,423,396 |
| 70452 | Usafiri wa majini (CS) | 429 | 54,919 | 55,348 | 551 | 255,720 | 256,271 | 687 | 261,730 | 262,417 |
| 70453 | Usafiri wa reli (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70454 | Usafiri wa anga (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70455 | Njia nyingine za usafiri (CS) | 1,502 | 2,639 | 4,141 | 1,608 | 6,547 | 8,155 | 3,227 | 24,690 | 27,917 |
| 70460 | Mawasiliano (CS) | 8,313 | 3,128 | 11,440 | 10,776 | 10,695 | 21,472 | 12,729 | 5,245 | 17,974 |
| 70471 | Huduma za Biashara na Utunzaji Mizigo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70472 | Hoteli na migahawa (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70473 | Utalii (CS) | 6,874 | 0 | 6,874 | 12,384 | 1,000 | 13,384 | 12,331 | 1,200 | 13,531 |
| 70474 | Miradi ya maendeleo (multi-purpose) (CS) | 3,319 | 680 | 3,999 | 3,709 | 3,600 | 7,309 | 4,702 | 13,600 | 18,302 |
| 70481 | Utafiti katika shughuli za kiuchumi, biashara na kazi (CS) | 41 | 0 | 41 | 67 | 0 | 67 | 212 | 1,355 | 1,567 |
| 70482 | Utafiti na maendeleo ya kilimo, misitu, uvuvi na uwindaji (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 50 | 0 | 50 |
| 70483 | Utafiti na maendeleo ya mafuta na nishati (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70484 | Utafiti na maendeleo ya uchimbaji madini, uzalishaji viwandani na ujenzi (CS) | 0 | 1,000 | 1,000 | 0 | 1,000 | 1,000 | 0 | 2,000 | 2,000 |
| 70485 | Utafiti na maendeleo ya usafiri (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70486 | Utafiti na maendeleo ya mawasiliano (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70487 | Utafiti na maendeleo ya viwanda vingine (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70490 | Shughuli nyingine za kiuchumi zisizotajwa hapo juu (CS) | 9,178 | 14,201 | 23,379 | 9,922 | 6,149 | 16,071 | 11,993 | 2,228 | 14,221 |

**Jedwali linaendelea ukurasa unaofuata...**

Jedwali Na. 26 linaendelea

| Fungu | Melezo | 2012/2013 | | | 2013/2014* | | | 2014/2015* | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
| **705** | **Hifadhi ya mazingira** | **620,754** | **186,297** | **807,051** | **858,219** | **295,992** | **1,154,211** | **1,005,215** | **309,861** | **1,315,076** |
| 70510 | Hifadhi ya taka | 122 | 0 | 122 | 109 | 0 | 109 | 122 | 0 | 122 |
| 70520 | Hifadhi ya maji taka | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70530 | Kupunguza Uhalibifu wa mazingira | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70540 | Hifadhi ya viumbehai na mazingira | 14,454 | 360 | 14,814 | 19,163 | 2,860 | 22,023 | 20,837 | 4,507 | 25,344 |
| 70550 | Utafiti na maendeleo ya hifadhi ya mazingira (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70560 | Huduma nyingine za hifadhi ya mazingira zisizotajwa hapo juu (CS) | 606,179 | 185,937 | 792,116 | 838,947 | 293,132 | 1,132,079 | 984,256 | 305,354 | 1,289,610 |
| **706** | **Nyumba na huduma za jamii** | **224,807** | **242,794** | **467,601** | **239,574** | **638,300** | **877,874** | **271,725** | **485,194** | **756,919** |
| 70610 | Maendeleo ya nyumba (CS) | 6,058 | 3,257 | 9,315 | 8,377 | 63,306 | 71,683 | 14,386 | 21,852 | 36,238 |
| 70620 | Maendeleo ya jamii (CS) | 6,712 | 197,089 | 203,801 | 11,293 | 272,997 | 284,290 | 12,477 | 213,429 | 225,906 |
| 70630 | Usambazaji maji (CS) | 6,383 | 10,218 | 16,601 | 8,197 | 242,497 | 250,695 | 9,742 | 207,078 | 216,820 |
| 70640 | Taa za barabarani (CS) | 170 | 0 | 170 | 316 | 0 | 316 | 321 | 0 | 321 |
| 70650 | Utafiti wa nyumba na maendeleo ya jamii (CS) | 1,998 | 0 | 1,998 | 2,196 | 400 | 2,596 | 2,383 | 500 | 2,883 |
| 70660 | Nyumba na huduma za jamii zisizotajwa hapo juu (CS) | 203,485 | 32,230 | 235,715 | 209,196 | 59,099 | 268,295 | 232,416 | 42,335 | 274,751 |
| **707** | **Afya** | **295,667** | **85,714** | **381,381** | **282,327** | **112,805** | **395,131** | **334,717** | **77,373** | **412,090** |
| 70711 | Madawa (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70712 | Bidhaa nyingine za madawa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70713 | Huduma za tiba na vifaa tiba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70721 | Huduma za tiba za jumla | 25 | 0 | 25 | 72 | 0 | 72 | 882 | 141 | 1,023 |
| 70722 | Huduma maalumu za tiba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70723 | Huduma za meno (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70724 | Huduma za wakunga wasaidizi | 214,942 | 69,468 | 284,410 | 209,546 | 84,226 | 293,772 | 241,848 | 57,065 | 298,913 |
| 70731 | Huduma za hospitali (IS) | 6,679 | 717 | 7,396 | 6,590 | 1,507 | 8,097 | 8,720 | 1,902 | 10,622 |
| 70732 | Huduma za Hospitali Maaalum | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70733 | Huduma za Vituo vya Kujjifungulia wajawazito | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70734 | Huduma za Wakunga na Wakunga wa jadi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70740 | Huduma za afya (IS) | 5,121 | 6,530 | 11,651 | 6,051 | 15,374 | 21,425 | 7,965 | 5,491 | 13,456 |
| 70750 | Utafiti na maendeleo ya huduma za afya (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70760 | Huduma za afya zisizotajwa hapo juu (CS) | 68,901 | 8,999 | 77,900 | 60,068 | 11,697 | 71,764 | 75,302 | 12,775 | 88,076 |
| **708** | **Burudani, utamaduni na dini** | **9,587** | **2,520** | **12,107** | **12,434** | **6,700** | **19,134** | **13,253** | **13,550** | **26,803** |
| 70810 | Huduma za burudani na michezo (IS) | 1,822 | 1,660 | 3,482 | 2,504 | 0 | 2,504 | 3,016 | 7,280 | 10,296 |
| 70820 | Huduma za utamaduni (IS) | 7,358 | 860 | 8,218 | 9,387 | 6,700 | 16,087 | 9,657 | 6,120 | 15,777 |
| 70830 | Huduma za utangazaji na uchapishaji (CS) | 42 | 0 | 42 | 81 | 0 | 81 | 86 | 0 | 86 |
| 70840 | Dini na huduma nyingine za kijamii (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70850 | Utafiti na maendeleo katika burudani, utamaduni na dini (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70860 | Huduma nyingine za burudani, utamaduni na dini zisizotajwa hapo juu | 364 | 0 | 364 | 461 | 0 | 461 | 495 | 150 | 645 |
| **709** | **Elimu** | **656,129** | **136,014** | **792,143** | **643,215** | **135,560** | **778,775** | **375,880** | **639,428** | **1,015,308** |
| 70911 | Elimu ya Awali (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70912 | Elimu ya Msingi (IS) | 847 | 3,596 | 4,443 | 1,304 | 3,302 | 4,606 | 642 | 15,406 | 16,047 |
| 70921 | Elimu ya sekondari (Kidato I -IV) (IS) | 10,325 | 79,570 | 89,895 | 8,441 | 64,660 | 73,101 | 15,753 | 188,859 | 204,612 |
| 70922 | Elimu ya sekondari (Kidato V -VI (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70930 | Elimu baada ya sekondari isiyo ya Chuo Kikuu | 7,648 | 0 | 7,648 | 5,815 | 1,900 | 7,715 | 6,976 | 4,000 | 10,976 |
| 70941 | Daraja la awali Elimu ya Chuo Kikuu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70942 | Daraja linalofuata Elimu ya Chuo Kikuu | 0 | 1,000 | 1,000 | 0 | 1,220 | 1,220 | 0 | 3,200 | 3,200 |
| 70950 | Elimu isiyopambanuliwa (IS) | 23,586 | 755 | 24,341 | 24,640 | 10,700 | 35,340 | 24,657 | 2,698 | 27,355 |
| 70960 | Huduma za ziada kwa elimu (IS) | 611,474 | 51,094 | 662,567 | 601,158 | 53,778 | 654,937 | 325,534 | 425,265 | 750,799 |
| 70970 | Utafiti wa Elimu (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70980 | Huduma za elimu zisizotajwa hapo juu (CS) | 2,249 | 0 | 2,249 | 1,856 | 0 | 1,856 | 2,318 | 0 | 2,318 |
| **710** | **Kinga ya Jamii** | **220,170** | **194,767** | **414,936** | **152,441** | **393,822** | **546,263** | **177,170** | **381,938** | **559,108** |
| 71011 | Ugonjwa (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71012 | Ulemavu (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71020 | Wazee (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71030 | Wahanga | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71040 | Familia na Watoto (IS) | 166,054 | 19,485 | 185,539 | 102,001 | 26,140 | 128,140 | 119,160 | 25,585 | 144,745 |
| 71050 | Ukosefu wa ajira (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71060 | Nyumba (IS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71070 | Huduma za Jamii zizizotajwa hapo juu | 451 | 587 | 1,038 | 505 | 0 | 505 | 743 | 725 | 1,468 |
| 71080 | Utafiti wa kinga ya jamii (CS) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 71090 | Huduma za kinga ya jamii zisizotajwa hapo juu (CS) | 53,665 | 174,694 | 228,359 | 49,935 | 367,682 | 417,617 | 57,268 | 355,628 | 412,896 |
| | **Jumla Kuu** | **10,865,347** | **3,639,126** | **14,504,473** | **12,604,009** | **5,642,288** | **18,246,296** | **14,204,410** | **5,443,100** | **19,647,510** |

Chanzo: ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Makadirio

CS - Huduma za Umma zinazotolewa na Serikali na wanaonufaika ni watu wote

IS - Huduma za Umma zinzotolewa na Serikali na wanaonufaika ni wanakaya

## SURA YA 5

## FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA

### Ujazi wa Fedha na Karadha

102. Mwaka 2013, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea na sera ya kudhibiti ujazi wa fedha ili kuzuia mfumuko wa bei. Katika kipindi hicho, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikuwa shilingi bilioni 16,106.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 14,647.1 mwaka 2012, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 10.0. Ukuaji huu ni chini ya lengo lililowekwa la asilimia 15.0 kwa mwaka 2013. Hii ilitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa rasilimali katika fedha za ndani kwenye mabenki ambayo ilikua kwa asilimia 15.5 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 22.3 mwaka 2012. Aidha, katika kipindi hicho, kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi nayo ilipungua na kuwa asilimia 15.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 18.2 mwaka 2012. Vile vile, madai halisi ya mabenki kwa serikali kuu yalikua kwa asilimia 26.5 mwaka 2013 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 37.3 mwaka 2012. Wakati huo huo, rasilimali halisi katika fedha za kigeni katika mabenki zilikua kwa asilimia 2.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.0 mwaka 2012.

103. Mwaka 2013, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) uliongezeka na kufikia shilingi bilioni 11,890.6 kutoka shilingi bilioni 10,724.5 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Aidha, karadha nchini iliongezeka kwa asilimia 18.8 kutoka shilingi bilioni 13,719.0 mwaka 2012 hadi shilingi bilioni 16,293.1 mwaka 2013. Kati ya hizo, shilingi bilioni 5,900.4 zilikuwa mikopo kwa Serikali Kuu na mikopo kwa sekta binafsi ilikuwa shilingi bilioni 10,387.9.

**Mikopo ya Benki za Biashara kwa Shughuli za Kiuchumi**

104.Katika kipindi kilichoishia Desemba 2013, mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 10,392.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9,010.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 15.3. Mikopo kwa sekta binafsi ilikuwa sawa na wastani wa asilimia 19.5 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na asilimia 20.1 kwa mwaka 2012. Ukuaji wa mikopo kwenye shughuli za kilimo, huduma za kifedha, majengo na ujenzi, biashara, umeme na biashara za watu binafsi ulipungua ikilinganishwa na mwaka 2012. Aidha, mikopo katika shughuli za madini na uchimbaji mawe, viwanda, uchukuzi na mawasiliano, utalii pamoja na mahoteli na migahawa uliimarika. Hata hivyo, sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli za biashara ambazo zilipata wastani wa asilimia 21.3 ya mikopo yote iliyoelekezwa katika sekta binafsi mwaka 2013 ikifuatiwa na biashara za watu binafsi asilimia 17.2.

**Kielelezo Na 5.1: Mchango wa Mikopo ya Benki za Biashara kwa Shughuli za Kiuchumi**




## Amana Katika Benki za Biashara

105. Mwaka 2013, amana katika benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 9.9 na kufikia shilingi bilioni 14,115.5 kutoka shilingi bilioni 12,847.3 mwaka 2012. Kati ya hizo, sekta binafsi ilichangia shilingi bilioni 13,323.0, sawa na asilimia 94.4 ya amana zote. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni katika amana zote ulipungua na kufikia asilimia 29.9 mwaka 2013 kutoka asilimia 30.2 mwaka 2012.

**Mwenendo wa Viwango vya Riba**

106. Mwaka 2013, mwenendo wa riba za amana mbalimbali na zile za mikopo ziliimarika ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2012. Kiwango cha riba kwa amana za muda maalum kiliongezeka kutoka wastani wa asilimia 8.67 Desemba 2012 hadi asilimia 8.71 Desemba 2013. Hata hivyo, riba ya mikopo kwa ujumla iliongezeka kutoka wastani wa asilimia 15.68 Desemba 2012 hadi asilimia 16.01 Desemba 2013. Aidha, riba ya mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 14.09 Desemba 2012 hadi kufikia asilimia 13.78 Desemba 2013, wakati riba za amana za mwaka mmoja ziliongezeka kufikia wastani wa asilimia 11.12 Desemba 2013 kutoka asilimia 11.06 katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Kutokana na mwenendo huo, tofauti kati ya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 3.03 Desemba 2012 na kufikia asilimia 2.66 Desemba 2013.

107. Kutokana na kupungua kwa ukwasi kwenye mabenki hasa katika kipindi cha mwisho wa mwaka 2013, riba zilizotozwa katika soko la fedha kati ya mabenki ziliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 8.58 mwezi Desemba 2013 ikilinganishwa na asilimia 5.80 mwezi Desemba 2012. Wakati huo huo, riba kwenye dhamana za serikali ziliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 15.20 ikilinganishwa na asilimia 12.85 mwaka 2012.

108. Dhamana za Serikali zenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 3,341.3 ziliuzwa mwaka 2013 ikilinganishwa na dhamana zenye thamani ya shilingi bilioni 2,620.0 zilizouzwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 27.5. Aidha, mauzo ya hati fungani katika mwaka 2013 yalipungua kwa asilimia 11.1 kufikia shilingi bilioni 755.9 ikilinganishwa na mauzo ya mwaka 2012 ya shilingi bilioni 850.

**Maboresho Katika Sekta ya Benki**

109. Mwaka 2013, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa leseni za kufanya biashara nchini kwa benki mpya tatu. Benki hizo ni FINCA Tanzania Ltd iliyoanza kutoa huduma mwezi Januari 2013, UBL Bank Tanzania Ltd iliyoanza kutoa huduma mwezi Mei 2013 na Maendeleo Bank Plc iliyoanza kutoa huduma mwezi Septemba 2013. Kufuatia hali hiyo, hadi kufikia mwezi Desemba 2013, idadi ya benki za biashara nchini iliongezeka na kufikia 52 kutoka 49 zilizokuwepo mwaka 2012. Wakati huo huo, matawi ya benki yaliongezeka kutoka 552 hadi 609. Mashine za kutolea fedha (ATMs) ziliongezeka kutoka 1,367 mwaka 2012 kufikia 1,452 mwaka 2013. Aidha, kufuatia kukamilika kwa mwongozo wa uwakala wa huduma za kibenki mwezi Februari 2013, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa leseni ya kuziruhusu benki ya CRDB, Benki ya Posta, *Equity Bank* na Benki ya Wananchi Dar es salaam kutoa huduma hii. Utaratibu huu wa uwakala umepanua wigo wa huduma za kibenki na hivyo kuwafikia wananchi wengi zaidi mijini na vijijini na kwa gharama nafuu. Vile vile, benki nyingi zimeendeleza ushirikiano na makampuni ya simu katika kutoa huduma za kifedha na malipo kupitia simu za mikononi.

110. Tathmini ya awali ya mabenki nchini kwa mwaka 2013 inaonesha kuwa benki nyingi ni salama na zinaweza kuhimili misukosuko ya kifedha. Vile vile, takwimu zinaonesha kuwa, benki nyingi zimetimiza masharti mapya ya kuongeza mtaji kutoka shilingi bilioni 5 hadi shilingi bilioni 15 hata kabla ya tarehe ya mwisho iliyopangwa ambayo ni Februari 2015. Aidha, uwiano wa mitaji kwa mali iliyowekezwa katika mabenki ulikuwa ni asilimia 18.3 ikilinganishwa na kiwango cha chini kinachotakiwa kisheria cha asilimia 12.

111. Katika kipindi cha mwaka 2013, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua. Uwiano kati ya mikopo chechefu na jumla ya mikopo yote katika benki za biashara ulipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2013 kutoka wastani wa asilimia 7.4 wa mwaka 2012. Kiwango cha mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu ikilinganishwa na kiwango cha amana zinazoweza kuhitajika katika muda mfupi kilifikia asilimia 38.1. Kiwango hiki ni kikubwa kikilinganishwa na asilimia 36.5 kwa mwaka 2012 na kiwango cha asilimia 20 au zaidi kinachohitajika kisheria.

112.Hadi kufikia Desemba 2013, Benki ya Rasilimali Tanzania iliidhinisha jumla ya miradi ya kilimo 15 iliyokuwa na thamani ya shilingi bilioni 4.45. Hivyo, jumla ya miradi iliyoidhinishwa tangu dirisha hilo lilipoanza kazi Mei 2010 imefikia 168. Hadi Desemba 2013, jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 281.9 iliombwa ambapo mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 56.7 iliidhinishwa, sawa na asilimia 20.1 ya mikopo iliyoombwa. Aidha, hadi kufikia Aprili 2014, Serikali ilishatoa jumla ya shilingi bilioni 42 za kuongeza mtaji kwenye Dirisha la Kilimo.

113. Hadi kufikia Desemba 2013, mikopo iliyotolewa kupitia Dirisha la Kilimo ilifikia jumla ya shilingi bilioni 41.9 ambapo thamani ya mikopo iliyorejeshwa hadi Desemba 2013 ilikuwa shilingi bilioni 13.1. Kasi ya urejeshaji wa mikopo iliyoiva siyo ya kuridhisha na Serikali kupitia Benki ya Rasilimali Tanzania inaendelea kuwafuatilia kwa karibu waliokopeshwa ili warejeshe mikopo hiyo kwa wakati iweze pia kuwasaidia watu wengine. Miongoni mwa sababu zilizochangia kutorejeshwa mikopo kwa wakati ni ufanisi duni katika sekta ya kilimo uliotokana na hali mbaya ya hewa, kushuka kwa bei za mazao na uharibikaji wa zana za kilimo kama matrekta na mbegu. Hadi Desemba 2013, mikopo ya dirisha la kilimo ilitolewa kwenye mikoa 23 na wilaya 72.

114.Mwaka 2013, Serikali iliendelea na mchakato wa kukamilisha uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania yenye lengo la kuwapatia wakulima mikopo yenye masharti nafuu ya muda mfupi, wa kati na mrefu. Mwezi Desemba 2013, Serikali ilizindua Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ambayo inasimamia hatua za uanzishwaji wa Benki hii. Hadi kufikia Machi 2014, Bodi ilifanya usaili wa nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Benki na Wakuu wa Idara tano wa kuanzia. Aidha, Serikali ilitoa shilingi bilioni 10 kuongezea mtaji wa benki hiyo na kufikia shilingi bilioni 100.

**Maendeleo ya Ukuaji wa Soko la Mikopo ya Nyumba Tanzania**

115.Mwaka 2013, soko la mikopo ya nyumba lilikua kutokana na kuongezeka kwa kasi ya uwekezaji kwenye nyumba za makazi. Hadi kufikia Desemba 2013, sekta ya benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 156.5 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ikilinganishwa na shilingi bilioni 107.2 zilizotolewa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 46. Vile vile, mikopo ya

nyumba iliongezeka kutoka 1,889 mwaka 2012 na kufikia 2,784 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 47.4. Ongezeko la mikopo ya nyumba lilitokana na: kuwepo kwa viwango vizuri vya riba; kuongezeka kwa uelewa juu ya mikopo ya nyumba miongoni mwa wakopaji; uhamasishaji wa umma uliofanywa na mabenki kuhusiana na mikopo ya nyumba; na kuanzishwa kwa utoaji wa mikopo ya nyumba kwenye benki ambazo hazikuwa zikitoa huduma hiyo hapo awali kama vile CRDB na *Exim Bank*.

116. Mwaka 2013, jumla ya taasisi 18 za benki zilikuwa zikitoa mikopo ya nyumba. Soko la mikopo ya nyumba kwa mwaka 2013 lilikuwa na wakopeshaji wakubwa watatu, ambao kwa pamoja walichangia wastani wa asilimia 60.1 ya mikopo yote ya nyumba iliyotolewa. Wakopeshaji hao ni: Benki ya Azania (asilimia 24.3), Benki ya Stanbic (asilimia 20.74), na Benki ya Kibiashara ya Afrika (asilimia 15.1).

**Jedwali Na. 5.1: Mwenendo wa Soko la Mikopo ya Nyumba kwenye Benki hadi Desemba 2013**

| Mkopeshaji | Mikopo iliyotolewa | Kiwango cha Mikopo (Shs. Bilioni) | Umiliki wa Soko (%) |
|---|---|---|---|
| Azania Bank Limited | 701 | 38.04 | 24.3 |
| Stanbic Bank (T) Limited | 114 | 32.46 | 20.74 |
| Commercial Bank of Africa (T) Limited | 144 | 23.63 | 15.1 |
| Equity Bank Tanzania Limited | 20 | 11.75 | 7.51 |
| EFC Tanzania M.F.C. Limited | 679 | 8.65 | 5.53 |
| Barclays Bank (T) Limited | 60 | 7.11 | 4.54 |
| DCB Commercial Bank Plc | 580 | 6.47 | 4.13 |
| Bank of Africa Tanzania Limited | 44 | 5.86 | 3.74 |
| African Banking Corporation (T) Limited | 31 | 5.49 | 3.51 |
| I & M Bank Tanzania Limited | 25 | 3.85 | 2.46 |
| Exim Bank Tanzania Limited | 13 | 2.93 | 1.87 |
| KCB Bank Tanzania Limited | 15 | 2.89 | 1.85 |
| National Microfinance Bank (T) Plc | 16 | 2.39 | 1.53 |
| Citibank Tanzania Limited | 14 | 2.36 | 1.51 |
| CRDB Bank Plc | 35 | 1.34 | 0.85 |
| Akiba Commercial Bank Limited | 290 | 0.83 | 0.53 |
| NIC Bank Tanzania Limited | 1 | 0.25 | 0.16 |
| First National Bank Tanzania Limited | 2 | 0.23 | 0.14 |
| **Jumla** | **2,784** | **156.53** | **100** |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

117. Pamoja na kuongezeka kwa thamani ya mikopo iliyotolewa, soko la mikopo ya nyumba nchini bado ni dogo ikilinganishwa na nchi nyingine. Wastani wa kiwango cha mikopo ya nyumba kwa Pato la Taifa ni asilimia 0.36. Kiwango hiki ni kidogo ikilinganishwa na viwango vya nchi jirani za Afrika ya Mashariki ambapo Kenya (asilimia 2.4), Rwanda (asilimia 2.4) na Uganda (asilimia 1.0). Aidha, mahitaji ya nyumba na mikopo ya nyumba ni makubwa lakini yanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa nyumba za gharama nafuu.

**Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa sekta ya Hifadhi ya Jamii**

118. Mwaka 2012/13, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) iliendelea kusimamia mifuko sita ya hifadhi ya jamii. Hii inajumuisha mifuko mitano ya pensheni (PPF, NSSF, LAPF, PSPF, GEPF) na mmoja wa bima ya afya (NHIF). Jumla ya wanachama katika mifuko kwa pamoja ilifikia 1,869,888 mwaka 2012/13 ikijumuisha wanachama 536,829 wa Mfuko wa Bima ya Afya ikilinganishwa na wanachama 1,674,932 wakiwemo wanachama 474,760 wa Mfuko wa Bima ya Afya mwaka 2011/12. Wanachama wa mifuko ya pensheni wanakadiriwa kuwa asilimia 6 ya nguvu kazi ya Tanzania Bara. Mchanganuo wa wanachama kwa aina ya mfuko ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

**Jedwali Na.5.2 : Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

| Mwaka | LAPF | PPF | PSPF | NSSF | GEPF | NHIF | Mifuko ya Pensheni tu | Mifuko yote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2005/06 | 53,015 | 66,305 | 222,258 | 380,693 | 25,678 | 275,865 | 747,949 | 1,023,814 |
| 2006/07 | 56,479 | 72,770 | 2,39,374 | 408,970 | 27,333 | 295,205 | 804,926 | 1,100,131 |
| 2007/08 | 63,302 | 84,186 | 256,774 | 449,039 | 29,779 | 316,460 | 883,080 | 1,199,540 |
| 2008/09 | 66,394 | 104,684 | 266,045 | 371,911 | 30,227 | 332,650 | 839,650 | 1,171,911 |
| 2009/10 | 73,833 | 156,239 | 288,055 | 383,808 | 35,279 | 373,326 | 937,214 | 1,310,540 |
| 2010/11 | 80,529 | 180,046 | 306,514 | 521,629 | 41,879 | 468,611 | 1,130,597 | 1,599,208 |
| 2011/12 | 91,852 | 202,198 | 309,767 | 543,685 | 52,670 | 474,760 | 1,200,172 | 1,674,392 |
| 2012/13 | 104,840 | 247,418 | 322,184 | 599,575 | 59,042 | 536,829 | 1,333,059 | 1,869,888 |

Chanzo: Mifuko Hifadhi ya Jamii

119. Mwaka 2012/13, thamani ya mali za mifuko ilikuwa shilingi bilioni 6,190.51 ikilinganishwa na shilingi bilioni 5,357.21 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 15.5. Ongezeko hili lilitokana na ukuaji wa thamani ya vitega uchumi na kuongezeka kwa michango ya wanachama. Thamani ya vitega uchumi vya mifuko yote iliongezeka kutoka shilingi bilioni 4,245.49 mwaka 2011/12 hadi shilingi bilioni 5,348.63 mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la asilimia 25.9. Aidha, michango ya wanachama kwa mifuko yote iliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 1,602.57 mwaka 2012/13 kutoka shilingi bilioni 1,364.21 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 17.4. Kutokana na

uchanga wa sekta ya fedha nchini, mifuko imewekeza katika maeneo machache yenye athari ndogo kama vile dhamana za muda maalumu, hisa na majengo. Aidha mwaka 2012/13 sehemu kubwa ya uwekezaji katika vitega uchumi vya mifuko ilikua kwenye dhamana za muda maalumu sawa na asilimia 67.8 ambapo uwekezaji katika majengo ni asilimia 19.5.

120.Mwaka 2012/13, jumla ya wanachama 86,995 walipata mafao ya pensheni ikilinganishwa na wanachama 72,751 mwaka 2011/12. Aidha jumla ya shilingi bilioni 1,131.4 zililipwa kama mafao kwa wanachama hao mwaka 2012/13 ikilinganishwa na shilingi bilioni 733.63 zilizolipwa mwaka 2011/12 sawa na ongezeko la asilimia 54.2. Uwiano wa mafao yanayolipwa na thamani ya mali za mifuko ulikua asilimia 18.3 na uwiano wa mafao kwa michango ya wanachama ulikua asilimia 70.6.

**Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma**

121.Mwaka 2013, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma uliendelea kutekeleza malengo makuu ya Mfuko ili kuweza kufanikisha Dira ya Mfuko ya kuwa chaguo katika tasnia ya hifadhi za jamii nchini. Mwaka 2013, Mfuko ulisajili jumla ya wanachama 18,781 na kufanya idadi ya wanachama waliosajiliwa kuongezeka na kufika 322,184 kutoka wanachama 309,767 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 4.0.

122.Mwaka 2013, Mfuko ulilipa jumla ya mafao sita yenye thamani ya jumla ya shilingi milioni 607,446.8 kwa wanachama wake ikilinganishwa na mafao ya shilingi milioni 355,980.3 yaliyolipwa mwaka 2012. Mafao hayo ni: malipo ya kustaafu kwa umri ambayo ni asilimia 70.4 ya mafao yaliyolipwa, pensheni kwa wastaafu (asilimia 18.0), mafao ya kifo (asilimia 8.7), pensheni ya wategemezi (asilimia 2.9), mafao ya kujitoa (asilimia 0.06) na msaada wa mazishi (asilimia 0.05).

123.Hadi kufikia Desemba 2013, thamani ya rasilimali na uwekezaji halisi wa Mfuko ilikuwa shilingi milioni 1,248,653.36, sawa na ongezeko la asilimia 14.9 ikilinganishwa na shilingi milioni 1,086,279.7 mwaka 2012. Aidha, thamani ya mapato yatokanayo na vitega uchumi mwaka 2013 ilikuwa shilingi milioni 202,235.41 ikilinganishwa na shilingi milioni 79,166.6 mwaka 2012.

**Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii**

124. Mwaka 2012/13, wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii waliongezeka kwa asilimia 10.3 kufikia 599,575 ikilinganishwa na wanachama 543,685 mwaka 2011/12. Vile vile, michango iliyokusanywa kutoka kwa wanachama ilikuwa na thamani ya shilingi milioni 476,107.47 ikilinganishwa na shilingi milioni 420,245.20 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 13.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wanachama na waajiri wapya 1,819 kuwasilisha michango kwa wakati.

125. Mwaka 2012/13, mafao yaliyotolewa kwa wanachama yalikuwa na thamani ya shilingi milioni 228,049.37 ikilinganishwa na shilingi milioni 178,691.9 zilizotolewa na Mfuko mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 27.6. Aidha, idadi ya wanachama waliolipwa mafao mwaka 2012/13 ilikuwa 67,055 ikilinganishwa na wanachama 136,395, sawa na upungufu wa asilimia 50.8. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya wanachama wa fao la kujitoa baada ya kuelimishwa na kuelewa kuhusu umuhimu wa mifuko ya jamii katika maisha yao ya baadaye. Mwaka 2013, Mfuko uliendesha semina 2,018 nchi nzima kwa lengo la kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa mifuko ya jamii katika maisha ya baadaye ikilinganishwa na semina 553 mwaka 2012.

126. Thamani ya uwekezaji katika vitega uchumi vya Mfuko iliongezeka hadi shilingi milioni 2,059,076.28 mwaka 2012/13 kutoka shilingi milioni 1,800,118.8 mwaka 2011/12, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 14.4. Vile vile, thamani ya uwekezaji katika dhamana za Serikali iliongezeka kwa asilimia 11.8 kufikia shilingi milioni 350,647.1 mwaka 2012/13 kutoka shilingi milioni 313,747.5 mwaka 2011/12. Aidha, mapato kutokana na uwekezaji katika vitega uchumi yalikuwa shilingi milioni 231,061.3 mwaka 2012/13 ikilinganishwa na shilingi milioni 398,669.9 mwaka 2011/12, sawa na upungufu wa asilimia 42.0. Kupungua kwa mapato ya vitega uchumi kulitokana na mabadiliko yaliyotokana na sababu za kitathmini. Mfuko hufanya tathmini ya vitega uchumi vyake kila baada ya miaka mitatu ambapo katika tathmini iliyofanyika mwaka 2012 ilionekana kuwa thamani ya vitega uchumi vyake (hususan majengo) ilikuwa imeongezeka. Hata hivyo, mapato halisi ya vitega uchumi (ikijumuisha dhamana za Serikali, dhamana za makampuni, mikopo, amana za muda maalum, majengo na hisa) yaliongezeka kwa asilimia 38.0 kutoka shilingi milioni 139,989.2 mwaka 2011/12 hadi shilingi milioni 193,156.8 mwaka 2012/13. Vilevile, katika

mwaka 2012/13, thamani halisi ya mali za Mfuko kwa ajili ya mafao zilikuwa shilingi milioni 2,239,866.67 ikilinganishwa na shilingi milioni 1,970,636.1 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 13.7.

**Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali**

127. Mwaka 2012/13, thamani ya rasilimali ya Mfuko iliongezeka hadi kufikia shilingi milioni 198,435.07 kutoka shilingi milioni 154,410.99 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 28.5. Aidha, wanachama wa Mfuko waliongezeka kutoka 52,670 mwaka 2011/12 hadi kufikia wanachama 59,042 mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la asilimia 12.1.

128. Makusanyo kutoka kwa wanachama yaliongezeka kutoka shilingi milioni 30,149.12 mwaka 2011/12 hadi shilingi milioni 36,816.18 mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la asilimia 22.1. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wanachama. Vile vile, mafao yaliyolipwa na Mfuko kwa wanachama yaliongezeka kutoka shilingi milioni 5,247.25 mwaka 2011/12 hadi shilingi milioni 9,161.62 mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la asilimia 74.6.

129. Mwaka 2012/13, mapato yatokanayo na vitega uchumi yaliongezeka hadi shilingi milioni 18,253.99 kutoka shilingi milioni 11,538.15 mwaka 2011/12, ikiwa ni ongezeko la asilimia 58.2. Hii ilipelekea kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji wa Mfuko katika vitega uchumi kutoka shilingi milioni 137,746.75 mwaka 2011/12 hadi shilingi milioni 179,552.6 mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la asilimia 30.3.

**Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma**

130. Mwaka 2013, idadi ya wanachama wanaochangia katika Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma iliongezeka na kufikia 247,418 kutoka wanachama 203,981 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 21.3. Aidha, mapato ya Mfuko yatokanayo na makusanyo ya michango kutoka kwa wanachama yalikuwa shilingi bilioni 278.57 ikilinganishwa na shilingi bilioni 235.89 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 18.1.

131. Mwaka 2013, uwekezaji wa Mfuko katika vitega uchumi mbalimbali uliendelea kuimarika. Hadi kufikia Desemba 2013, Mfuko uliwekeza jumla ya shilingi bilioni 1,329.18 kutoka shilingi bilioni 1,022.43 zilizowekezwa mwaka

2012, sawa na ongezeko la asilimia 30. Ukuaji mkubwa wa thamani ya uwekezaji ilikuwa kwenye hisa za makampuni ambapo ulikua kwa asilimia 87.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi kikubwa kwa thamani ya hisa za makampuni katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam.

**Jedwali Na. 5.3: Thamani ya Uwekezaji ya Vitega Uchumi vya Mfuko (Sh.Biln)**

| Aina ya Uwekezaji | 2012 | 2013 | Ukuaji (%) |
|---|---|---|---|
| Mali zenye faida inayojulikana kabla ya kuwekeza | 721.52 | 869.39 | 20.5% |
| Hisa za Makampuni | 150.62 | 281.82 | 87.1% |
| Majengo | 99.07 | 104.18 | 5.2% |
| Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja | 51.22 | 73.79 | 44.1% |
| **Jumla** | **1,022.43** | **1,329.18** | **30.0%** |

132.Mapato ya Mfuko yanayotokana na uwekezaji yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 111.15 mwaka 2012 hadi shilingi bilioni 305.2 mwaka 2013. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa thamani ya hisa za makampuni katika soko la mitaji, pamoja na kujumuishwa kwa mapato yatokanayo na riba katika mkopo kwa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma baada ya kusainiwa mkataba kati ya Serikali na Mfuko wa Pensheni ya Mashirika ya Umma.

133.Malipo ya pensheni kwa wastaafu kwa mwaka 2013 yalikuwa shilingi bilioni 131.97 ikilinganishwa na shilingi bilioni 99.39 zilizolipwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 32.7. Hii imetokana na kuongezeka kwa malipo ya kujitoa pamoja na malipo ya mkupuo yaliyofanywa na Mfuko kwa wafanyakazi mbalimbali waliostaafu pamoja na kuongezeka kwa wastaafu.

**Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa**

134.Idadi ya wanachama wa Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa iliongezeka na kufikia 104,840 mwaka 2012/13 ikilinganishwa na wanachama 91,852 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 14.1. Aidha, michango kutoka kwa wanachama ilikua kwa asilimia 33.8 kufikia shilingi bilioni 119.175

mwaka 2012/13 ikilinganishwa na shilingi bilioni 89.06 mwaka 2011/12. Hii ilitokana na kuongezeka kwa usajili wa wanachama wapya. Mafao yaliyolipwa kwa wanachama mwaka 2012/13 yaliongezeka kwa asilimia 48.4 na kufikia shilingi bilioni 56.87 kutoka shilingi bilioni 38.3 mwaka 2011/12. Aidha, thamani ya uwekezaji katika vitega uchumi vya Mfuko iliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 570.35 mwaka 2012/13 kutoka shilingi bilioni 490.36 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 16.3.

**Jedwali Na.5.4: Idadi ya Wanachama, Michango na Malipo ya Mafao**

| Mwaka | Wanachama | Michango (Tshs. Biln) | Malipo ya Mafao (Ths. Biln) |
|---|---|---|---|
| 2005/06 | 53,015 | 15.9 | 6.98 |
| 2006/07 | 56,479 | 23.71 | 6.50 |
| 2007/08 | 63,302 | 32.21 | 9.29 |
| 2008/09 | 66,394 | 47.05 | 14.89 |
| 2009/10 | 73,833 | 54.24 | 22.51 |
| 2010/11 | 80,529 | 80.51 | 26.50 |
| 2011/12 | 91,253 | 89.06 | 38.30 |
| 2012/13 | 104,840 | 119.2 | 56.9 |

Chanzo: Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**

135. Mwaka 2012/13, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uliendelea kupanua utoaji wa huduma ili kuongeza wigo kwa wananchi, kuboresha huduma za matibabu hasa vijijini na kuharakisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM, 2007-2017). Aidha, mabadiliko ya kisheria yaliyofanywa katika Mfuko yalipelekea kupanuka kwa wigo wa uanachama na hivyo kuongezeka kwa idadi ya wanachama kufikia 536,829 (sawa na wanufaika 2,963,269) mwaka 2012/13 kutoka wanachama 474,760 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 13.1. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulipewa jukumu la kusimamia Mfuko wa Afya ya Jamii. Mwaka 2012/13, idadi ya kaya zilizo wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii ilipungua kwa asilimia 15.3 kufikia 543,621 (sawa na wanufaika 3,261,726) kutoka kaya 641,753 mwaka 2011/12. Upungufu huu ulitokana na baadhi ya kaya kujitoa kufuatia kuwepo kwa hali ya upungufu wa madawa katika baadhi ya vituo vya kutolea huduma za

afya pamoja na usimamizi hafifu wa vyombo vya usimamizi kwenye ngazi ya Halmashauri.

136. Hadi kufikia Juni 2013, Mfuko ulikuwa unahudumia jumla ya wanufaika 6,225,022 ikilinganishwa na wanufaika 6,353,312 waliohudumiwa mwaka 2011/12, sawa na upungufu wa asilimia 2.0. Hii ilitokana na kupungua kwa idadi ya wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii. Aidha, katika kipindi hicho, mafao yaliyotolewa kwa wanufaika wa Mfuko yalikuwa shilingi milioni 97,924.61 ambazo ni sawa na asilimia 94.3 ya madai ya shilingi milioni 103,800.09.

137. Mwaka 2012/13, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uliendelea kukusanya mapato yake kutoka katika sehemu kuu tatu ambazo ni; michango inayotokana na makato ya mishahara ya wanachama; mapato yatokanayo na vitega uchumi; na mapato mengineyo. Sehemu kubwa ya mapato ya Mfuko yanatokana na michango ya wanachama ambapo iliongezeka na kufikia shilingi milioni 207,502.1 kutoka shilingi milioni 163,457.46 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 26.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wanachama na marekebisho ya mishahara ya wafanyakazi. Mapato yanayotokana na thamani ya uwekezaji katika vitega uchumi vya Mfuko yaliongezeka kwa asilimia 43.9 kutoka shilingi milioni 38,034.64 mwaka 2011/12 hadi shilingi milioni 54,739.24. Vile vile, mapato mengineyo ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yaliongezeka na kufikia shilingi milioni 2,291.78 mwaka 2012/13 kutoka shilingi milioni 1,417.87 mwaka 2011/12. Pia Mfuko ulipokea kiasi cha shilingi milioni 2,000 kutoka Serikalini kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Mfuko wa Afya wa Jamii.

138. Mwaka 2012/13, Mfuko ulikuwa na ongezeko la vituo vya afya 411 vilivyosajiliwa kwa kipindi cha mwaka mzima. Ongezeko hilo limepelekea Mfuko wa Taifa ya Bima Afya kuwa na jumla ya vituo vilivyosajiliwa 5,837 hadi kufikia Juni 2013, ikilinganishwa na vituo 5,426 vilivyosajiliwa hadi kufikia mwaka 2011/12. Kati ya vituo vilivyosajiliwa 2012/13, vituo 4,662 sawa na asilimia 79.8 vilikuwa vituo vya Serikali; vituo 612 (10.5%) madhehebu ya dini; vituo 566 (9.7%) mashirika yasiyo ya kiserikali na maduka ya dawa.

**Jedwali Na.5.5: Jumla ya Vituo vya Afya Vilivyosajiliwa**

| Aina ya Kituo | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | Ukuaji (%) |
|---|---|---|---|---|
| Zahati | 4,555 | 4,242 | 4,513 | 6.39 |
| Vituo vya Afya | 552 | 549 | 591 | 7.65 |
| Hospitali | 235 | 232 | 238 | 2.5 |
| Maduka ya dawa | 331 | 403 | 495 | 22.83 |
| **Jumla** | **5,673** | **5,426** | **5,837** | **7.6** |

Chanzo: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

**Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania**

139. Mwaka 2013, idadi ya kampuni zilizosajiliwa kufanya biashara ya bima nchini iliongezeka na kufikia 30 kutoka kampuni 28 zilizosajiliwa mwaka 2012. Vile vile, kampuni zilizosajiliwa kufanya biashara ya uwakala wa bima zilifikia 400, na kampuni 100 zilisajiliwa kufanya biashara ya udalali wa bima nchini.

140. Mwaka 2013, mauzo ya bima yalifikia shilingi bilioni 481.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 415.6 zilizouzwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 15.9. Kati ya mauzo hayo, shilingi bilioni 51.7 (asilimia 10.7) zilikuwa za bima ya maisha na shilingi bilioni 430 (asilimia 89.3) zilikuwa za bima ya kawaida. Sababu zilizopelekea ukuaji wa mauzo ya bima ni kuongezeka kwa uelewa wa umma juu ya umuhimu wa kukata bima kufuatia utoaji wa elimu ya bima kwa wananchi pamoja na kuongezeka kwa madai ya bima.

**Jedwali Na. 5.6: Mauzo ya Bima kwa Mwaka 2008 – 2013 (Sh. Bilioni)**

| Mauzo | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bima za Kaiwaida** | **164.497** | **209.559** | **255.7** | **305.3** | **367.6** | **430.04** |
| Ukuaji | 17.4% | 27.4% | 22.04% | 19.4% | 20.4% | 17.0% |
| Mchango kwa jumla ya mauzo | 86.2% | 90.6% | 89.10% | 89.20% | 88.50% | 89.30% |
| **Bima za Maisha** | **26.338** | **21.678** | **31.2** | **36.8** | **48.0** | **51.7** |
| Ukuaji | 31.1% | -17.7% | 44.0% | 17.9% | 30.4% | 7.7% |
| Mchango kwa jumla ya mauzo | 13.8% | 9.4% | 10.88% | 10.80% | 11.50% | 10.70% |
| **Jumla ya Mauzo** | **190.835** | **231.237** | **287.0** | **342.1** | **415.6** | **481.73** |
| Ukuaji | 19.3% | 21.2% | 24.1% | 19.2% | 21.5% | 15.9% |

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima

141.Mwaka 2013, madai ya bima za kawaida kutoka kwa wateja yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 110.4 kutoka shilingi bilioni 96.6 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Vile vile, madai ya bima za maisha yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 14.4 mwaka 2012 hadi shilingi bilioni 15.2 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ufanisi kwenye makampuni ya bima na kupungua kwa urasimu katika ufuatiliaji wa madai ya bima.

142.Mwaka 2013, thamani ya mali za makampuni ya bima iliongezeka kwa asilimia 12.0 kufikia shilingi bilioni 504.6 kutoka shilingi bilioni 450.5 mwaka 2012. Ongezeko hili lilitokana na kukua kwa biashara ya bima na kuongezeka kwa uwekezaji wa ada za bima katika amana za Serikali na mabenki. Aidha, thamani ya madeni ya makampuni ya bima iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 360.1 kutoka shilingi bilioni 317.8 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 13.3. Madeni ya makampuni ya bima yaliongezeka kutokana na ukuaji wa mauzo ambao ulipelekea kampuni kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa fidia zinazotarajiwa. Mwenendo huu umepelekea makampuni ya bima kuwa na ziada ya mali zenye thamani ya shilingi bilioni 144.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 132.7 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 8.9.

**Jedwali Na. 5.7: Thamani ya Mali na Madeni ya Kampuni za Bima (Sh.Bln)**

| Mali na Madeni | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumla ya Mali** | **289.456** | **320.611** | **355.7** | **416.1** | **450.5** | **504.6** |
| Ukuaji | 26.6% | 10.8% | 10.9% | 17.0% | 8.3% | 12.0% |
| **Jumla ya Madeni** | **202.238** | **219.022** | **247.8** | **289.3** | **317.8** | **360.1** |
| Ukuaji | 34.2% | 8.3% | 13.1% | 16.7% | 9.9% | 13.3% |
| **Ziada ya Mali** | **87.218** | **101.589** | **108** | **126.9** | **132.7** | **144.5** |
| Ukuaji | 9.0% | 16.5% | 6.3% | 17.5% | 4.6% | 8.9% |

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima

**Maendeleo ya Masoko ya Mitaji na Dhamana**

143. Mwaka 2013, Soko la Hisa la Dar es Salaam lilianzisha dirisha maalum kwa ajili ya kukuza na kuimarisha masoko ya wajasiriamali wadogo. Hali hii inatoa fursa za uwekezaji kwa wajasiriamali wadogo, ikiwa ni pamoja na kujiandikisha na kuwekeza mitaji yao (IPOs) katika soko la hisa. Benki ya Maendeleo imeshakaribisha uwekezaji kupitia ununuzi wa hisa zake chini ya mpango huu. Hadi kufikia Desemba 2013, wawekezaji waliosajiliwa na soko la hisa walifikia 192,391 ambapo wawekezaji wa ndani ya nchi walikuwa 191,324 na wa nje ya nchi walikuwa 467.

144. Hadi kufikia Desemba 2013, kampuni 18 zilikuwa zimeorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ikilinganishwa na kampuni 17 zilizokuwa zimeorodheshwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Hii ilitokana na kuorodheshwa kwa Benki ya Maendeleo iliyoanzishwa mwaka 2013. Kati ya hizo, kampuni za ndani ni 12 na za nje ni sita. Aidha, hadi Desemba 2013, thamani ya hisa zote zilizoorodheshwa katika soko la Hisa la Dar es Salaam zilifikia shilingi bilioni 16,464.3, ikiwa ni ongezeko la asilimia 24.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 13,197.3 Desemba 2012. Ongezeko hili lilitokana na kupanda kwa bei ya hisa za kampuni za TBL kwa asilimia 176; NMB (asilimia 130); kampuni ya sigara (asilimia 99); benki ya CRDB (asilimia 75); na SWISSPORT (asilimia 54).

145. Mwaka 2013, jumla ya hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 252.4 ziliuzwa na kununuliwa ikilinganishwa na hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 50.43 zilizouzwa na kununuliwa mwaka 2012. Ongezeko hili lilitokana na

kupunguza muda wa uhawilishaji na malipo ya dhamana toka siku tano mpaka tatu; kuongezeka kwa muda wa soko toka masaa mawili mpaka manne; na kuongezeka kwa uelewa juu ya masoko ya mitaji na dhamana.

146. Mwaka 2013, hatifungani zenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 3,635.4 ziliuzwa katika soko la hisa ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,924.34 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 24.3. Hatifungani za Serikali Kuu na hatifungani za hazina ziliuzwa katika soko la pili, wakati hatifungani za kampuni ziliuzwa na kununuliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam.

**Jedwali Na. 5.8: Hatifungani za Soko la Hisa la Dar es Salaam (Sh. Biln)**

| Aina ya Hisa | 2012 | 2013 | Ukuaji (%) |
|---|---|---|---|
| Hatifungani za Serikali Kuu | 2,606.88 | 3,290.51 | 26.2% |
| Hatifungani za Hazina | 241.77 | 302.29 | 25.0% |
| Hatifungani za Kampuni | 75.67 | 42.57 | -43.7% |
| **Jumla** | **2,924.32** | **3,635.37** | **24.3%** |

Chanzo: Soko la Hisa la Dar es Salaam

**Benki ya Posta**

147. Mwaka 2013, Benki ya Posta Tanzania ilitekeleza miradi mbali mbali yenye lengo la kuongeza uwezo na ubora wa utoaji huduma. Maeneo yaliopewa kipaumbele ni pamoja na: ukarabati wa matawi; mradi wa TPB popote; ukuzaji wa mtaji; na kushirikisha vyombo vingine katika kutoa huduma. Katika kipindi hicho, amana za wateja ziliongezeka na kufikia shilingi milioni 169,297 kutoka shilingi milioni 138,287 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 22.4. Ongezeko hili lilitokana na kupanuka kwa wigo wa kutoa huduma.

148. Mwaka 2013, thamani ya uwekezaji katika dhamana za Serikali iliongezeka na kufikia shilingi milioni 45,735 kutoka shilingi milioni 38,146 zilizowekezwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 19.9. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa viwango vya riba kwenye dhamana pamoja na kuanzisha uwekezaji kwenye dhamana binafsi. Thamani ya mikopo iliyotolewa na Benki ya Posta ilikuwa shilingi milioni 117,539, sawa na ukuaji wa asilimia 22.5 kutoka shilingi milioni 95,914 mwishoni mwa mwaka 2013. Hii ilitokana na

maboresho yaliyofanyika katika mfumo wa ukusanyaji wa mikopo yenye lengo la kuhakikisha kwamba wadaiwa wanarejesha mikopo kwa wakati ili iweze kutumika kukopesha wengine. Aidha, mwaka 2013, Benki ya Posta ilianzisha aina mpya ya mikopo kwa ajili ya wafanyakazi ambapo hadi Desemba 2013 mikopo iliyotolewa ilikuwa na thamani ya jumla ya shilingi milioni 5,049.

**Jedwali Na. 5.9: Thamani ya Rasilimali katika Dhamana (Shilingi milioni)**

| Kitega Uchumi | 31/12/2010 | 31/12/2011 | 31/12/2012 | 31/12/2013 |
|---|---|---|---|---|
| Dhamana za Serikali za muda mfupi (Bills) | 16,876 | 16,113 | 10,000 | 15,894 |
| Dhamana za Serikali | 26,036 | 33,348 | 28,146 | 29,404 |
| Dhamana binafsi | | | | 437 |
| **Jumla ya dhamana** | **42,912** | **49,461** | **38,146** | **45,735** |
| **Badiliko (%)** | **-** | **15.3%** | **(22.9%)** | **19.9%** |

Chanzo: Benki ya Posta Tanzania

**Jedwali Na. 5.10: Thamani ya Mikopo ya Benki (Shilingi milioni)**

| Aina ya Mkopo | 31/12/2010 | 31/12/2011 | 31/12/2012 | 31/12/2013 |
|---|---|---|---|---|
| Mikopo ya Biashara | 4,338 | 4,665 | 6,589 | 7,655 |
| Mikopo ya Watumishi | 58,857 | 57,892 | 85,113 | 95,444 |
| Mikopo midogo midogo | 1,634 | 1,525 | 4,106 | 7,471 |
| Mikopo ya Uwezeshaji | 255 | 413 | 106 | 1,920 |
| Mikopo ya Wafanyakazi | | | | 5,049 |
| **Jumla** | **65,084** | **64,495** | **95,914** | **117,539** |
| **Badiliko (%)** | **-** | **(0.9)** | **48.7** | **22.5** |

Chanzo: Benki ya Posta Tanzania

149. Mwaka 2013, mapato ya Benki yalikuwa shilingi milioni 38,359 ikiwa ni ongezeko la asilimia 25.4, kutoka shilingi milioni 30,587 mwaka 2012. Ongezeko hilo lilitokana na: usimamizi madhubuti wa matumizi ya benki; kupanuka kwa uwekezaji katika mikopo; na kuongezeka kwa wigo wa huduma pamoja na aina ya huduma zinazotolewa na Benki.

**MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA**

Jedwali Na. 27

**Sh. Bilioni**

| | Kipindi kinachoishia mwezi Desemba | | | | | | Badiliko 2012-2013 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | Kiasi | % |
| **Fedha ya msingi (M0)** | **2,276.4** | **3,009.1** | **3,497.8** | **4,111.9** | **4,525.6** | **5,027.8** | **502.2** | **11.1%** |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **3,158.3** | **3,590.8** | **4,521.4** | **5,572.0** | **6,538.6** | **7,218.1** | **679.6** | **10.4%** |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 2,310.2 | 3,012.6 | 3,520.7 | 3,676.0 | 4,186.0 | 4,672.4 | **486.5** | **11.6%** |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **5,468.5** | **6,603.4** | **8,042.2** | **9,247.9** | **10,724.5** | **11,890.6** | **1,166.0** | **10.9%** |
| Amana za fedha za kigeni | 1,990.3 | 2,176.7 | 2,970.5 | 3,773.4 | 3,922.6 | 4,216.2 | **293.6** | **7.5%** |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **7,458.8** | **8,780.1** | **11,012.7** | **13,021.3** | **14,647.1** | **16,106.8** | **1,459.7** | **10.0%** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)** | **4,086.8** | **4,939.5** | **6,125.6** | **6,273.6** | **6,396.0** | **6,576.3** | **180.3** | **2.8%** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)** | **3,372.0** | **3,840.6** | **4,887.1** | **6,747.7** | **8,251.1** | **9,530.4** | **1,279.4** | **15.5%** |
| Karadha Nchini | 6,753.9 | 7,857.6 | 9,522.8 | 10,958.1 | 13,719.0 | 16,293.0 | **2,574.0** | **18.8%** |
| Madai halisi kwa serikali kuu | -335.0 | 128.4 | 806.7 | 1,471.3 | 2,019.4 | 2,554.6 | **535.2** | **26.5%** |
| Mikopo kwa serikali kuu | 2,197.8 | 2,865.8 | 3,531.0 | 3,335.7 | 4,708.6 | 5,900.4 | **1,191.7** | **25.3%** |
| Mikopo kwa sekta isiyo serikali | 4,556.2 | 4,991.9 | 5,991.8 | 7,622.3 | 9,010.4 | 10,392.7 | **1,382.3** | **15.3%** |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | -849.2 | -1,279.6 | -1,911.4 | -2,345.9 | -2,778.7 | -3,416.8 | **-638.1** | **23.0%** |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## VIWANGO VYA UKUAJI WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

**Jedwali Na. 28**

| | Kipindi kinachoishia mwezi Desemba | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
| **Fedha ya msingi (M0)** | **21.1%** | **28.5%** | **17.1%** | **24.9%** | **21.1%** | **32.2%** | **16.2%** | **17.6%** | **10.1%** | **11.1%** |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **22.7%** | **31.8%** | **12.0%** | **29.1%** | **21.9%** | **13.7%** | **25.9%** | **23.2%** | **17.3%** | **10.4%** |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 15.3% | 37.2% | 23.8% | 24.6% | 28.1% | 30.4% | 16.9% | 4.4% | 13.9% | 11.6% |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **19.8%** | **33.9%** | **16.7%** | **27.2%** | **24.4%** | **20.8%** | **21.8%** | **15.0%** | **16.0%** | **10.9%** |
| Amana za fedha za kigeni | 1.1% | 36.9% | 32.5% | 7.0% | 8.8% | 9.4% | 36.5% | 27.0% | 4.0% | 7.5% |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **13.5%** | **34.8%** | **21.5%** | **20.5%** | **19.8%** | **17.7%** | **25.4%** | **18.2%** | **12.5%** | **10.0%** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)** | **8.5%** | **6.7%** | **35.7%** | **0.7%** | **12.2%** | **20.9%** | **24.0%** | **2.4%** | **2.0%** | **2.8%** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)** | **37.6%** | **142.1%** | **-2.4%** | **66.9%** | **30.6%** | **13.9%** | **27.2%** | **38.1%** | **22.3%** | **15.5%** |
| Karadha Nchini | 24.1% | 47.7% | 23.4% | 31.7% | 24.6% | 16.3% | 21.2% | 15.1% | 25.2% | 18.8% |
| Madai halisi kwa serikali kuu | 150.7% | -170.6% | -247.1% | 13.2% | 4.7% | -138.3% | 528.4% | 82.4% | 37.3% | 26.5% |
| Mikopo kwa serikali kuu | 14.3% | 77.7% | 7.5% | 25.7% | -3.2% | 30.4% | 23.2% | -5.5% | 41.2% | 25.3% |
| Mikopo kwa sekta isiyo serikali | 32.3% | 26.0% | 39.6% | 36.4% | 44.6% | 9.6% | 20.0% | 27.2% | 18.2% | 15.3% |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | -5.5% | -32.4% | 84.3% | -48.0% | 240.1% | 50.7% | 49.4% | 22.7% | 18.5% | 23.0% |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI

Jedwali Na.29

| | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shs/Dola mwisho wa mwaka | 1,165.51 | 1,261.64 | 1,132.09 | 1,280.30 | 1,313.29 | 1,453.54 | 1,566.66 | 1,571.62 | 1578.57 |
| Badiliko la thamani ya shilingi (%) | 11.8 | 8.2 | -10.3 | 13.1 | 2.6 | 10.7 | 7.8 | 0.3 | 0.4 |
| Shs/Dola wastani wa mwaka | 1,132.23 | 1,254.17 | 1,239.04 | 1,206.32 | 1,307.23 | 1,401.79 | 1,557.44 | 1,571.70 | 1598.6 |
| Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (%) | 3.9 | 10.8 | -1.2 | -2.6 | 8.4 | 7.2 | 11.1 | 0.9 | 1.7 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**MIKOPO YA BENKI ZA BIASHARA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**

Jedwali Na. 30

| Aina ya Shughuli | Kipindi kinachoishia mwezi Desemba (Sh. Milioni) | | | | | | Ukuaji (%) | Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | | |
| Uzalishaji katika Kilimo | 515936.0 | 467097.1 | 691210.3 | 912331.8 | 938915.0 | 965140.6 | 2.8 | 9.5 |
| Huduma za Kifedha | 122001.1 | 105843.7 | 142600.1 | 177691.8 | 231269.4 | 251255.0 | 8.6 | 2.5 |
| Madini na Uchimbaji Mawe | 37727.8 | 18926.3 | 33943.7 | 39175.7 | 55158.0 | 96739.0 | 75.4 | 1.0 |
| Viwanda | 612670.6 | 565775.5 | 786470.6 | 928746.6 | 991795.9 | 1160593.7 | 17.0 | 11.4 |
| Majengo na Ujenzi | 142992.8 | 148713.4 | 182071.6 | 320938.2 | 410748.0 | 514408.4 | 25.2 | 5.1 |
| Uchukuzi na Mawasiliano | 320600.6 | 457407.2 | 533990.3 | 545243.5 | 610053.9 | 727538.0 | 19.3 | 7.2 |
| Biashara | 737105.8 | 926626.3 | 1014177.8 | 1523962.2 | 1843242.7 | 2162191.4 | 17.3 | 21.3 |
| Utalii | 29165.5 | 27097.6 | 37665.7 | 49730.4 | 60152.3 | 113394.5 | 88.5 | 1.1 |
| Mahoteli na Migahawa | 150978.4 | 187204.6 | 263046.3 | 361039.7 | 363033.4 | 371008.5 | 2.2 | 3.7 |
| Umeme | 183487.0 | 193609.6 | 156528.3 | 166672.8 | 338035.1 | 403022.7 | 19.2 | 4.0 |
| Watu Binafsi | 928510.5 | 1063142.9 | 1242763.5 | 1557495.5 | 1778743.2 | 1744954.0 | -1.9 | 17.2 |
| Sekta Nyinginezo | 595294.9 | 644369.9 | 713954.0 | 815729.5 | 1101473.5 | 1643118.0 | 49.2 | 16.2 |
| **Jumla** | **4376471.1** | **4805814.0** | **5798422.1** | **7398757.6** | **8722620.4** | **10153363.7** | **16.4** | **100.0** |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA**

Jedwali Na.31 — **Sh. Bilioni**

| | Kipindi Kinachoishia mwezi Desemba | | | | | | | | | | | | | Badiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2001** | **2002** | **2003** | **2004** | **2005** | **2006** | **2007** | **2008** | **2009** | **2010** | **2011** | **2012** | **2013** | **2011/12 ( %)** |
| **Amana za Sekta Binafsi** | | | | | | | | | | | | | | |
| Amana za Hundi/Zinazaohamishika | 339.8 | 441.4 | 541.7 | 662.3 | 898.1 | 969.5 | 1,424.8 | 1,715.7 | 2,019.4 | 2,617.9 | 3,329.5 | 4,114.4 | 4,442.2 | 8.0 |
| Amana za Akiba na za Muda Maalum | 548.5 | 623.3 | 735.1 | 848.9 | 1,165.9 | 1,444.5 | 1,803.9 | 2,307.9 | 3,011.9 | 3,505.2 | 3,664.2 | 4,113.7 | 4,664.7 | 13.4 |
| Amana za fedha za kigeni | 563.3 | 764.3 | 921.3 | 934.8 | 1,289.0 | 1,709.9 | 1,828.6 | 1,989.3 | 2,158.8 | 2,926.4 | 3,722.0 | 3,882.4 | 4,216.0 | 8.6 |
| **Jumla** | **1,451.6** | **1,828.9** | **2,198.1** | **2,446.0** | **3,353.0** | **4,123.9** | **5,057.3** | **6,012.9** | **7,190.1** | **9,049.5** | **10,715.8** | **12,110.5** | **13,323.0** | 10.0 |
| Amana za Serikali | 80.0 | 102.8 | 125.2 | 152.1 | 206.6 | 230.1 | 325.2 | 401.7 | 662.6 | 699.3 | 626.6 | 736.8 | 792.6 | 7.6 |
| **Jumla za Amana zote** | **1,531.5** | **1,931.7** | **2,323.3** | **2,598.0** | **3,559.6** | **4,354.0** | **5,382.5** | **6,414.5** | **7,852.7** | **9,748.8** | **11,342.4** | **12,847.3** | **14,115.5** | 9.9 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA**

Jedwali Na. 32 — **Asilimia**

| **Aina ya Riba** | Kipindi Kinachoishia Mwezi Desemba | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2003** | **2004** | **2005** | **2006** | **2007** | **2008** | **2009** | **2010** | **2011** | **2012** | **2013** |
| Riba ya Benki Kuu (Bank rate) | 12.34 | 14.42 | 19.33 | 20.07 | 16.40 | 15.99 | 3.70 | 7.58 | 12.00 | 12.00 | 16.00 |
| Riba za Amana | | | | | | | | | | | |
| Amana za akiba | 2.45 | 2.60 | 2.60 | 2.59 | 2.65 | 2.74 | 2.83 | 2.43 | 2.90 | 2.88 | 3.04 |
| Amana za muda maalum | 3.87 | 4.39 | 5.28 | 7.17 | 8.37 | 6.63 | 6.36 | 6.09 | 7.12 | 8.67 | 8.71 |
| Riba za mikopo | | | | | | | | | | | |
| Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja | 15.65 | 14.23 | 15.65 | 15.67 | 15.01 | 13.56 | 13.96 | 14.37 | 13.78 | 14.09 | 13.78 |
| Mikopo ya muda wa kati na mrefu | 13.83 | 14.80 | 14.98 | 16.36 | 15.31 | 16.05 | 14.38 | 14.92 | 14.21 | 15.68 | 16.01 |
| Riba za Hawala za Hazina | | | | | | | | | | | |
| Siku 91 | 7.57 | 9.63 | 14.70 | 14.39 | 9.90 | 11.20 | 6.06 | 5.24 | 12.61 | 11.89 | 13.62 |
| Siku 182 | 7.61 | 9.87 | 14.71 | 14.95 | 10.15 | 12.13 | 6.59 | 6.20 | 16.39 | 12.96 | 15.46 |
| Siku 364 | 7.93 | 10.67 | 15.72 | 15.61 | 12.95 | 12.79 | 8.83 | 7.67 | 18.66 | 13.69 | 15.63 |

Chanzo:Benki Kuu ya Tazania

# SURA YA 6

# RASILIMALI WATU

## Idadi ya Watu

150. Mwaka 2013, idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa 46,170,150 ikilinganishwa na watu 44,928,923 mwaka 2012. Kati ya hao, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 44,827,757 sawa na asilima 97.1 ya watu wote na Tanzania Zanzibar watu 1,342,394. Aidha, mchanganuo wa watu kwa jinsia unaonesha kuwa wanawake walikuwa 23,058,933 sawa na asilimia 51.3 ya watu wote na wanaume walikuwa 21,869,990 sawa na asilimia 48.7. Makadirio haya yalitokana na maoteo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 ya ukuaji wa idadi ya watu kwa wastani wa asilimia 2.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.9 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002.

## Mgawanyiko wa Watu Kimkoa

151. Mwaka 2013, mkoa wa Dar es salaam ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu ikilinganishwa na mikoa mingine, ukiwa na takribani watu 4,617,000 sawa na asilimia 10.0 ya watu wote Tanzania Bara. Mkoa wa Mwanza ndio uliofuatia kwa kuwa na watu 2,856,258 (asilimia 6.4); na Mbeya watu 2,781,971 (asilimia 6.2). Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es salaam ilitokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaohamia kutoka mikoa mingine. Aidha, mkoa wa Katavi ulikuwa na watu 583,160 (asilimia 1.3) ambayo ni idadi ndogo zaidi ya watu ikilinganishwa na mikoa mingine ya Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, mkoa uliokuwa na idadi kubwa zaidi ya watu ni Mjini Magharibi (619,144), sawa na asilimia 46.12 ya watu wote Tanzania Zanzibar na mkoa uliokuwa na idadi ndogo zaidi ya watu ni Kusini Unguja uliokuwa na watu 117,923 sawa na asilimi 8.8.

152. Msongamano wa watu Tanzania Bara ulikuwa watu 51 kwa kilometa moja ya mraba, huku kukiwa na tofauti kimkoa. Kwa Tanzania Bara, msongamano wa watu ulikuwa mkubwa zaidi kwa Mkoa wa Dar es Salaam uliokuwa na watu 3,314 kwa kilometa moja ya mraba ikifuatiwa na Mwanza (145), Kilimanjaro (126) na Kagera (89). Aidha, Mkoa uliokuwa na idadi ndogo ya watu kwa kilometa ya mraba ulikuwa mkoa wa Lindi uliokuwa na watu 13 kwa kilometa

moja ya mraba ukifuatiwa na mikoa ya Rukwa na Njombe iliyokuwa na watu 15 kwa kilometa moja ya mraba. Kwa upande wa Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa watu 2,692 wakati ambapo Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu 138 kwa kilometea moja ya mraba. Kwa wastani, msongamano wa watu Tanzania ulikuwa watu 52 kwa kilometa moja ya mraba.

**Jedwali Na. 6.1: Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012**

| Mkoa | Idadi ya Watu | | | Wastani wa Ongezeko la Idadi ya Watu (2002 - 2012) | Msongamano wa Watu kwa kilometa moja ya Mraba | Wastani wa Idadi ya Watu kwa Kaya | Uwiano wa Kijinsi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Wanaume | Wanawake | | | | |
| **Tanzania** | **44,928,923** | **21,869,990** | **23,058,933** | **2.7** | **51** | **4.8** | **95** |
| **Tanzania Bara** | **43,625,354** | **21,239,313** | **22,386,041** | **2.7** | **49** | **4.8** | **95** |
| Dodoma | 2,083,588 | 1,014,974 | 1,068,614 | 2.1 | 50 | 4.6 | 95 |
| Arusha | 1,694,310 | 821,282 | 873,028 | 2.7 | 45 | 4.5 | 94 |
| Kilimanjaro | 1,640,087 | 793,140 | 846,947 | 1.8 | 124 | 4.3 | 94 |
| Tanga | 2,045,205 | 992,347 | 1,052,858 | 2.2 | 77 | 4.7 | 94 |
| Morogoro | 2,218,492 | 1,093,302 | 1,125,190 | 2.4 | 31 | 4.4 | 97 |
| Pwani | 1,098,668 | 537,826 | 560,842 | 2.2 | 34 | 4.3 | 96 |
| Dar es Salaam | 4,364,541 | 2,125,786 | 2,238,755 | 5.6 | 3,133 | 4 | 95 |
| Lindi | 864,652 | 414,507 | 450,145 | 0.9 | 13 | 3.8 | 92 |
| Mtwara | 1,270,854 | 599,648 | 671,206 | 1.2 | 76 | 3.7 | 89 |
| Ruvuma | 1,376,891 | 668,684 | 708,207 | 2.1 | 22 | 4.5 | 94 |
| Iringa | 941,238 | 452,052 | 489,186 | 1.1 | 27 | 4.2 | 92 |
| Mbeya | 2,707,410 | 1,297,738 | 1,409,672 | 2.7 | 45 | 4.3 | 92 |
| Singida | 1,370,637 | 677,995 | 692,642 | 2.3 | 28 | 5.3 | 98 |
| Tabora | 2,291,623 | 1,129,730 | 1,161,893 | 2.9 | 30 | 6 | 97 |
| Rukwa | 1,004,539 | 487,311 | 517,228 | 3.2 | 44 | 5 | 94 |
| Kigoma | 2,127,930 | 1,028,994 | 1,098,936 | 2.4 | 57 | 5.7 | 94 |
| Shinyanga | 1,534,808 | 750,841 | 783,967 | 2.1 | 81 | 5.9 | 96 |
| Kagera | 2,458,023 | 1,205,683 | 1,252,340 | 3.2 | 97 | 4.7 | 96 |
| Mwanza | 2,772,509 | 1,360,381 | 1,412,128 | 3 | 293 | 5.7 | 96 |
| Mara | 1,743,830 | 840,020 | 903,810 | 2.5 | 80 | 5.6 | 93 |
| Manyara | 1,425,131 | 717,085 | 708,046 | 3.2 | 32 | 5.2 | 101 |
| Njombe | 702,097 | 329,359 | 372,738 | 0.8 | 15 | 4.1 | 88 |
| Katavi | 564,604 | 279,682 | 284,922 | 3.2 | 28 | 5.5 | 98 |
| Simiyu | 1,584,157 | 759,891 | 824,266 | 1.8 | 63 | 6.9 | 92 |
| Geita | 1,739,530 | 861,055 | 878,475 | 2.6 | 81 | 6.1 | 98 |
| **Tanzania Zanzibar** | **1,303,569** | **630,677** | **672,892** | **2.8** | **530** | **5.1** | **94** |
| Kaskazini Unguja | 187,455 | 92,114 | 95,341 | 3.2 | 399 | 4.8 | 97 |
| Kusini Unguja | 115,588 | 57,880 | 57,708 | 2 | 135 | 4.4 | 100 |
| Mjini Magharibi | 593,678 | 283,590 | 310,088 | 4.2 | 2,581 | 5.2 | 91 |
| Kaskazini Pemba | 211,732 | 103,222 | 108,510 | 1.3 | 369 | 5.3 | 95 |
| Kusini Pemba | 195,116 | 93,871 | 101,245 | 1.1 | 588 | 5.4 | 93 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Nguvukazi na Ajira**

153. Mwezi Julai 2013, Serikali ilizindua taarifa ya matokeo ya Utafiti wa Ajira na Mapato (*Employment and Earnings Survey*) uliofanyika mwaka 2012. Kwa mujibu wa matokeo ya Utafiti huo uliohusisha sekta rasmi peke yake yalionesha kuwa ajira nchini ziliongezeka kwa asilimia 13.8 kufikia 1,550,018 ikilinganishwa na ajira 1,362,559 kutokana na Utafiti kama huo uliofanyika mwaka 2011. Utafiti huu ulionesha kuna ongezeko la ajira za masharti ya muda mrefu kutoka ajira 1,102,473 mwaka 2011 hadi kufikia 1,323,733 mwaka 2012. Ajira za muda mfupi zilipungua kwa asilimia 13 kutoka 260,086 mwaka 2011 hadi kufikia 226,285 mwaka 2012. Kupungua kwa ajira za masharti ya muda mfupi kunamaanisha kuongezeka kwa kazi za staha, ambazo zinakuwa na maslahi mazuri ikijumuisha masuala ya hifadhi ya jamii, likizo, na bima za afya. Aidha, uwiano wa ajira kati ya sekta binafsi na sekta ya umma ulionesha kuwa sekta binafsi ilitoa nafasi nyingi za ajira (asilimia 64.2) ikilinganishwa na sekta ya umma (asilimia 35.8). Vile vile, uwiano wa ajira kwa jinsia haukuwa na mabadiliko makubwa kwani wanawake walikuwa ni asilimia 37.3 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 37.8 mwaka 2011 wakati ajira za wanaume zilishuka na kufikia asilimia 62.7 kutoka asilimia 62.2 katika kipindi hicho. Matokeo ya Utafiti huo yalizidi kubainisha kuwa, kati ya ajira 1,550,018 zilizokuwepo katika mwaka 2012, kulikuwa na vijana wenye umri wa miaka 15-24 wapatao 37,972 waliokuwa kwenye ajira, sawa na asilimia 2.4 ya ajira zote. Hii ni kutokana na kuwa sehemu kubwa ya vijana wa umri huo wanakuwa bado wako shuleni/vyuoni.

**Jedwali Na 6.2: Mchanganuo wa Jumla ya Ajira kwa Jinsia**

| Waajiriwa | Mwaka | | |
|---|---|---|---|
| | **2010** | **2011** | **2012** |
| Wanaume | 810,427 | 845,569 | 947,545 |
| Wanawake | 465,883 | 513,527 | 564,501 |
| Chini ya Miaka 18 | 672 | 3,463 | 37,927 |
| **Jumla** | **1,276,982** | **1,362,559** | **1,550,018** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

154. Sekta ya ulinzi na utawala iliendelea kutoa mchango mkubwa katika ajira ingawa mchango wake ulipungua kufikia asilimia 18.5 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 23.4 mwaka 2011. Sekta ya viwanda ilifuatia ambapo

mchango katika ajira uliongezeka kufikia asilimia 16.8 mwaka 2012 kutoka asilimia 13.9 mwaka 2011 na elimu imechangia asilimia 16.4 ikilinganishwa na asilimia 11.3 mwaka 2011. Mwaka 2012, sekta ya ulinzi na utawala iliajiri watu 286,327; sekta ya viwanda watu 260,974; na sekta ya elimu watu 254,538 ikilinganishwa na ajira 318,210; 188,403; na 154,528 mwaka 2011 kwa mtiririko huo.

**Jedwali Na. 6.3: Mchanganuo wa Ajira kwa Mikoa (% ya Mchango)**

| Mkoa | Sekta Binafsi | | | Sekta ya Umma | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2010 | 2011 | 2012 | 2010 | 2011 | 2012 | 2010 | 2011 | 2012 |
| Dodoma | 0.9 | 0.9 | 1.2 | 1.6 | 1.5 | 1.4 | 2.6 | 2.4 | 2.6 |
| Arusha | 4.0 | 4.3 | 4.2 | 1.2 | 1.1 | 1.1 | 5.2 | 5.4 | 5.3 |
| Kilimanjaro | 3.4 | 3.1 | 4.4 | 1.4 | 2.1 | 2.0 | 4.8 | 5.2 | 6.4 |
| Tanga | 2.1 | 2.2 | 3.0 | 1.7 | 1.8 | 1.8 | 3.8 | 4.0 | 4.8 |
| Morogoro | 8.4 | 10.6 | 6.0 | 3.8 | 3.5 | 3.1 | 12.2 | 14.1 | 9.1 |
| Pwani | 0.6 | 0.6 | 0.7 | 1.1 | 1.3 | 1.1 | 1.7 | 1.9 | 1.8 |
| Dar es Salaam | 25.7 | 25.5 | 25.8 | 7.2 | 8.1 | 7.2 | 32.9 | 33.6 | 33.0 |
| Lindi | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 1.0 | 0.8 | 1.0 | 1.3 | 1.1 | 1.3 |
| Mtwara | 1.1 | 1.2 | 1.4 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 1.9 | 2.0 | 2.2 |
| Ruvuma | 0.7 | 1.1 | 1.2 | 0.9 | 0.8 | 0.8 | 1.6 | 1.9 | 2.0 |
| Iringa | 1.8 | 1.5 | 2.1 | 2.3 | 1.7 | 1.8 | 4.1 | 3.2 | 3.9 |
| Mbeya | 3.0 | 2.6 | 3.1 | 2.3 | 2.2 | 2.2 | 5.3 | 4.8 | 5.3 |
| Singida | 0.7 | 0.6 | 0.7 | 0.9 | 0.9 | 0.9 | 1.6 | 1.5 | 1.6 |
| Tabora | 0.6 | 0.3 | 0.5 | 1.2 | 1.3 | 1.3 | 1.9 | 1.6 | 1.8 |
| Rukwa | 0.3 | 0.4 | 0.4 | 0.7 | 0.4 | 0.7 | 1.0 | 0.8 | 1.1 |
| Kigoma | 0.5 | 0.8 | 0.9 | 1.1 | 0.9 | 1.1 | 1.6 | 1.7 | 2.0 |
| Shinyanga | 1.5 | 1.4 | 1.7 | 2.3 | 2.8 | 2.6 | 3.8 | 4.2 | 4.2 |
| Kagera | 1.0 | 1.1 | 1.1 | 0.9 | 1.2 | 1.1 | 1.8 | 2.3 | 2.2 |
| Mwanza | 4.9 | 3.1 | 3.2 | 1.8 | 1.7 | 1.8 | 6.8 | 4.8 | 5.0 |
| Mara | 0.7 | 0.7 | 1.2 | 1.6 | 1.5 | 1.4 | 2.3 | 2.2 | 2.5 |
| Manyara | 1.5 | 0.8 | 1.1 | 0.6 | 0.5 | 0.7 | 2.0 | 1.3 | 1.8 |
| **Jumla (%)** | 63.7 | 63.1 | 64.2 | 36.3 | 36.9 | 35.8 | 100.0 | 100.0 | 100 |
| **Jumla ya Ajira** | **813,297** | **859,435** | **995,705** | **463,685** | **503,124** | **554,313** | **1,276,982** | **1,362,559** | **1,550,018** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

155. Mkoa wa Dar es salaam unaongoza katika kuajiri watu wengi katika sekta rasmi ambapo jumla ya watu 511,596 (sawa na asilimia 33) kati ya watu 1,550,018 wameajiriwa katika Mkoa wa Dar es Salaam mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 33.6 mwaka 2011. Hii inafuatiwa na Mkoa wa Morogoro ambapo wameajiriwa watu 141,416 ambao ni sawa na aslimia 9.1 na mkoa wa mwisho kwa kuajiri watu ni Rukwa wenye jumla ya ajira rasmi 17,557 sawa na asilimia 1.1.

156. Matokeo ya utafiti huo pia yalionesha kuwa jumla ya watu 74,474 waliajiriwa mwaka 2011/12 ikilinganishwa na watu 47,637 walioajiriwa mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 56.3.Kati ya hao, wanaume walikuwa 45,835 na wanawake 28,639 (asilimia 38.5). Kwa upande wa aina ya ajira, idadi kubwa ya walioajiriwa walikuwa katika kada za mafundi na wataalam washiriki ambao walikuwa 31,191 (sawa na asilimia 41.9 ya waajiriwa wote) wakifuatiwa na watoa huduma ambao walikuwa 19,594 (asilimia 26.3) na Wataalamu (Professionals) ajira 12,134 sawa na asilimia 16.3. Sekta ya elimu iliongoza kwa kuajiri idadi kubwa ya wafanyakazi wapya katika kipindi cha mwaka 2012 ambao walikuwa 19,745, sawa na asilimia 26.5, ikifuatiwa na utengenezaji wa bidhaa na usindikaji viwandani wafanyakazi 16,703 sawa na asilimia 22.4. Aidha, utafiti ulibaini kuwa kulikuwa na fursa za ajira 126,073 katika sekta rasmi mwaka 2012, nyingi (asilimia 60.5) zikiwa za kitaalam.

157. Mwaka 2013, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) uliandikisha jumla ya watafuta kazi 1,707 ikilinganishwa na watafuta kazi 1,625 walioandikishwa mwaka 2012. Kati ya watafuta kazi walioandikishwa mwaka 2013, watafuta kazi 683 waliunganishwa kwa waajiri wenye fursa za ajira. Wakala pia uliwaunganisha watanzania wanaotafuta kazi nje ya nchi kwa kuweka utaratibu madhubuti wa kuhakikisha kuwa wanaajiriwa bila kuwepo na aina yeyote ya unyanyashaji wala ubaguzi kwa kuzingatia Sheria za nchi na Miongozo ya Shirika la Kazi Duniani. Utaratibu huu umewezesha Wakala kwa kushirikiana na taasisi binafsi za ajira na Balozi katika nchi husika kupitia na kuridhia mikataba ya Watanzania 652 waliopata ajira kwenye nchi za Saudi Arabia, Falme za Nchi za Kiarabu, Oman, India, Denmark na Qatar.

158. Mwaka 2013, Wakala uliwatembelea waajiri 103 na kusajili nafasi 106 za kazi zenye fursa za ajira 366. Aidha, Wakala uliendelea kutoa mafunzo ya

kuwajengea uwezo watafuta kazi 350 ili waweze kuhimili ushindani na changamoto za soko la ajira. Mafunzo hayo yalihusu namna ya kubaini vyanzo vya taarifa juu ya fursa mpya za ajira kama vile matangazo kwenye magazeti, vyombo vya habari, tovuti, majarida na kuwatembelea waajiri; jinsi ya kuandika wasifu binafsi; jinsi ya kufanya vyema kwenye usaili na dondoo muhimu za kujibu vyema maswali ya usaili. Vile vile, Wakala ulikagua wakala binafsi za ajira zipatazo 43 ikilinganishwa na wakala binafsi 18 zilizokaguliwa mwaka 2012. Kati ya hizo, wakala 25 zilikidhi vigezo vya kutoa huduma za ajira.

## IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA: 2005-2013

**Jedwali 33**

| Mkoa | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012** | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 1786073 | 1896786 | 1951071 | 2004544 | 2058630 | 2111764 | 2163817 | 2083588 | 2127416 |
| Arusha | 1427904 | 1475489 | 1522975 | 1570394 | 1617728 | 1664780 | 1711624 | 1694310 | 1741396 |
| Kilimanjaro | 1435847 | 1503014 | 1535975 | 1569212 | 1602530 | 1635870 | 1669174 | 1640087 | 1669051 |
| Tanga | 1716271 | 1753284 | 1837661 | 1880389 | 1923468 | 1966908 | 2010480 | 2045205 | 2091341 |
| Morogoro | 1881113 | 1929087 | 1975160 | 2021713 | 2068426 | 2115275 | 2162197 | 2218492 | 2271310 |
| Pwani | 944145 | 968637 | 991586 | 1014968 | 1038654 | 1062574 | 1086658 | 1098668 | 1122685 |
| Dar es Salaam | 2799241 | 2801675 | 2881548 | 2961150 | 3040118 | 3118132 | 3194903 | 4364541 | 4617000 |
| Lindi | 816815 | 851764 | 869522 | 887434 | 905480 | 923607 | 941884 | 864652 | 872758 |
| Mtwara | 1176112 | 1220248 | 1246089 | 1271912 | 1297751 | 1323568 | 1349235 | 1270854 | 1286501 |
| Ruvuma | 1192680 | 1235161 | 1268738 | 1303330 | 1338800 | 1375017 | 1412084 | 1376891 | 1406411 |
| Iringa | 1553392 | 1617696 | 1649200 | 1679828 | 1709225 | 1737382 | 1764285 | 941238 | 951964 |
| Mbeya | 2201206 | 2346388 | 2423635 | 2502258 | 2581792 | 2662156 | 2743084 | 2707410 | 2781971 |
| Singida | 1150367 | 1222810 | 1258545 | 1294584 | 1330931 | 1367481 | 1404065 | 1370637 | 1402820 |
| Tabora | 1887507 | 2004115 | 2086048 | 2170926 | 2258664 | 2349374 | 2443049 | 2291623 | 2359642 |
| Rukwa | 1251697 | 1302278 | 1349579 | 1398866 | 1450118 | 1503184 | 1558200 | 1004539 | 1037259 |
| Kigoma | 1910592 | 1970750 | 1601020 | 1669078 | 1740111 | 1814158 | 1891173 | 2127930 | 2179598 |
| Shinyanga | 3060176 | 3277784 | 3411023 | 3549342 | 3692941 | 3841787 | 3998664 | 1534808 | 1566734 |
| Kagera | 2206814 | 2210217 | 2293093 | 2379637 | 2469904 | 2563870 | 2661671 | 2458023 | 2537021 |
| Mwanza | 3196714 | 3168904 | 3265729 | 3364378 | 3464566 | 3566263 | 3669380 | 2772509 | 2856258 |
| Mara | 1461270 | 1572068 | 1631031 | 1692449 | 1756442 | 1822866 | 1891907 | 1743830 | 1787279 |
| Manyara | 1141376 | 1198051 | 1241994 | 1288280 | 1337015 | 1388295 | 1441771 | 1425131 | 1471083 |
| Njombe | | | | | | | | 702097 | 707698 |
| Katavi | | | | | | | | 564604 | 583160 |
| Simiyu | | | | | | | | 1584157 | 1613580 |
| Geita | | | | | | | | 1739530 | 1785824 |
| **Tanzania Bara** | **36197312** | **37526206** | **38291222** | **39474672** | **40683294** | **41914311** | **43169305** | **43625354** | **44827757** |
| Kaskazini Unguja | 146221 | 155066 | 160175 | 165544 | 171150 | 177095 | 183209 | 187455 | 193551 |
| Kusini Unguja | 99678 | 103191 | 105456 | 107811 | 110183 | 112612 | 115035 | 115588 | 117923 |
| Mjini Magharibi | 441446 | 461759 | 447716 | 459502 | 471341 | 483205 | 495054 | 593678 | 619144 |
| Kaskazini Pemba | 196221 | 216174 | 224951 | 234142 | 243759 | 253999 | 264677 | 211732 | 214502 |
| Kusini Pemba | 186651 | 207348 | 216479 | 226055 | 236072 | 246601 | 257577 | 195116 | 197274 |
| **Zanzibar** | **1070217** | **1143538** | **1154777** | **1193054** | **1232505** | **1273512** | **1315552** | **1303569** | **1342394** |
| **Tanzania** | **37267529** | **38669744** | **39445999** | **40667726** | **41915799** | **43187823** | **44484857** | **44928923** | **46170151** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Takwimu za matokeo ya sensa mwaka 2012

# SEHEMU YA PILI

# UENDELEZAJI SEKTA BINAFSI

## SURA YA 7

## UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

### Uwekezaji Vitega Uchumi Nchini

159.Mwaka 2013, Kituo cha Uwekezaji Rasilimali kilisajili jumla ya miradi 885 yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 88.24 ikilinganishwa na miradi 869 yenye thamani ya dola bilioni 11.42 mwaka 2012. Ongezeko hili lilitokana na kusajiliwa kwa miradi mikubwa ya miundombinu ya reli na bandari. Miradi hiyo ilitoa fursa za ajira 202,487 ambazo ni ongezeko la asilimia 16.1 ikilinganishwa na fursa za ajira 174,412 mwaka 2012. Kati ya miradi hiyo 885 iliyosajiliwa mwaka 2013, miradi 417 (asilimia 47.1) inamilikiwa na watanzania, miradi 184 (asilimia 20.8) ni ya wageni na miradi 284 (asilimia 32.1) ni ya ubia. Aidha, miradi mipya miongoni mwa iliyosajiliwa mwaka.

### Mgawanyiko wa Miradi Kisekta na Umiliki

160.Mwaka 2013, uwekezaji kisekta ulilenga kuinua miundombinu ambapo miradi yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 80 ilisajiliwa ili kutekeleza miradi mikubwa ya miundombinu ya bandari na reli. Sekta iliyofuata ilikuwa ya uzalishaji viwandani iliyokuwa na thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 2.0 na sekta ya majengo ya biashara iliyokuwa na thamani ya dola bilioni 1.7.

### Uwekezaji Mitaji ya Kigeni ya moja kwa moja

161.Mwaka 2013, thamani ya mitaji ya kigeni ya moja kwa moja ilikadiriwa kuwa Dola za Kimarekani milioni 1,879.4, sawa na ongezeko la asilimia 4.4 ikilinganishwa na dola milioni 1,799.6 mwaka 2012. Ongezeko hili lilitokana na uwekezaji mkubwa unaondelea katika sekta ndogo za gesi na petroli.

**Jedwali Na.7.1 Thamani ya Uwekezaji Mitaji ya Kigeni yaMoja kwa Moja**

| Mwaka | 2003 | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiasi (Dola Milioni) | 308.2 | 330.6 | 447.6 | 616.6 | 653.4 | 744 | 558.4 | 1800 | 1330 | 1799.6 | 1872.4 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

*Takwimu za Makadirio

**Uboreshaji wa Mazingira Wezeshi kwa Sekta Binafsi**

162. Mwaka 2013, Serikali iliendelea na juhudi za kuboresha mazingira wezeshi kwa sekta binafsi ili kuiwezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Katika kutekeleza hilo, Serikali iliandaa na kuratibu Sera ya Maendeleo ya Sekta Binafsi Tanzania kwa kuzingatia changamoto zilizopo na uzoefu wa nchi nyingine. Sambamba na hili, Serikali iliratibu na kusimamia urekebishaji wa mfumo uliopo katika sekta binafsi kwa lengo la kuufanya kuwa wa kisasa na wenye uwezo wa kutatua changamoto zinazojitokeza. Hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya sekta binafsi ni pamoja na:

***a) Uanzishaji na Ufungaji wa Biashara***

163. Mwaka 2013, Serikali kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni, iliweka kwenye mtandao sampuli ya taarifa na maelezo muhimu yanayohitajika katika kuanzisha kampuni (*Memorandum and Article of Association Model*) kwa lengo la kuwarahisishia wafanyabiashara kuandaa taarifa hizo wenyewe. Hii imeondoa gharama kubwa iliyokuwa inalipwa kwa wataalam kwa ajili ya kuandaa nyaraka hizi. Sambamba na hili, Wakala umeanza kupokea maombi ya usajili wa majina ya biashara na makampuni kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara kwa njia ya mtandao. Hatua hii pia imeondoa usumbufu kwa wafanyabiashara kusafiri kutoka mikoani kwenda makao makuu Dar es salaam kwa ajili ya usajili wa biashara na kampuni.

164. Mwaka 2013, Serikali iliondoa masharti ya kupitishia maombi ya leseni za biashara katika ofisi za afya na mipango miji kama kigezo cha kupata leseni. Udhibiti wa masharti ya afya, usalama na mazingira kwa sasa unatekelezwa nje ya taratibu za kupata leseni za biashara. Aidha, Serikali iliboresha masijala za wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(Registration, Insolvency and Trusteeship Agency - RITA)* ambapo imeziwezesha kutunza kumbukumbu zote katika mfumo wa TEHAMA sambamba na kuunganisha masijala za wilaya na za makao makuu kwa lengo la kurahisisha huduma zinazotolewa na Wakala.

***b) Upatikanaji wa Vibali vya Ujenzi***

165. Mwaka 2013, Serikali ilipitia taratibu za kiutawala, sheria na kanuni zinazohusiana na vibali vya ujenzi kwa lengo la kuangalia uwezekano wa

kuondoa urasimu katika mfumo wa utoaji wa vibali vya ujenzi na kuongeza ufanisi. Mchakato huo uliweza kupunguza muda na gharama za upatikanaji wa vibali bila kuathiri ubora na usalama wa majengo. Aidha, kamati za madiwani zinazoidhinisha vibali vya ujenzi na ramani ziliwekewa utaratibu wa uhakika wa vikao na Halmashauri zilielekezwa kuhakikisha zinafanya mikutano iliyopangwa ili kuondoa kero ya kuchelewesha vibali vya ujenzi. Vile vile, Halmashauri ziliagizwa kuhakikisha kuwa: (i) ukaguzi wa maeneo ya ujenzi kabla na baada ya ujenzi unafanyika kwa wakati mmoja ikihusisha timu za wataalam kutoka taasisi zote zinazohusika; (ii) Ramani zinapowasilishwa, siku hiyo hiyo zinapitiwa na wataalam waandamizi ili kuhakiki ukamilifu wa vigezo; na (iii) ramani zisizotimiza vigezo zinarejeshwa siku hiyo hiyo kwa wahusika kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

### *c) Ulinzi wa Mikataba ya Biashara*

166. Mwaka 2013, katika jitihada za Serikali za kupunguza urasimu, gharama, mlundikano wa kesi na muda unaotumika katika kuendesha kesi za migogoro ya kibiashara, mambo yafuatayo yalitekelezwa: (i) kutenganisha Idara ya *"Civil & International Law"* na kuwa na idara mbili ambazo ni Idara ya Madai na Usuluhishi na Idara ya Mikataba; (ii) kuboresha mfumo wa sheria za kesi na madai kwa jumla ya sheria 9 na kanuni 8; (iii) kuanza kutumika kwa mfumo wa TEHAMA *(Electronic Court Case Management System*) kwa ajili ya shughuli za Mahakama Kuu – kitengo cha Mahakama ya Biashara; na (iv) kuanza kutumika kwa mfumo mbadala wa utatuzi wa migogoro *(Alternative Dispute Resolution – ADR)* unaolenga kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani.

### Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

167. Mwaka 2013, Serikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi liliendelea kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali iliridhia Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mkakati huu unasimamia utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji kwa wadau mbalimbali kwa kuainisha malengo, kazi zinazotakiwa kufanyika, watekelezaji, ufuatiliaji na upimaji wa matokeo.

**Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi**

168. Mwaka 2013, Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi ilitoa mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya shilingi bilioni 9.2 kwa wajasiriamali 9,651 (wanaume 5,869; wanawake 3,782) ikilinganishwa na shilingi bilioni 8.5 zilizotolewa kwa wajasiriamali 8,497 (wanaume 5,331 na wanawake 3,166) mwaka 2012. Mikopo hiyo ilitolewa kupitia vyama 51 vya akiba na mikopo (SACCOS) katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Singida, Rukwa, Manyara, Ruvuma, Dodoma, Pwani, Tanga, Mbeya na Kagera. Katika mikoa ya Lindi na Mtwara, mikopo iliwekezwa katika mashamba ya zao la korosho ikiwa ni pamoja na kuongeza ukubwa wa mashamba kutoka wastani wa ekari 10 mwaka 2012 hadi ekari 20 mwaka 2013. Hadi kufikia Desemba 2013, marejesho ya mikopo yalikuwa asilimia 83 ya mikopo iliyotolewa. Marejesho hayakufikia lengo la asilimia mia kutokana na kukosekena kwa soko mahususi la korosho katika mikoa ya Mtwara na Lindi ambako ndiko mikopo mingi ilitolewa.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira**

169. Mwaka 2013, Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira ulikuwa umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 50.06 ikilinganishwa na shilingi bilioni 49.65 mwaka 2012. Mikopo hiyo iliweza kuwanufaisha wajasiriamali 76,546 ikilinganishwa na wajasiriamali 72,197 mwaka 2012. Hadi kufikia Desemba 2013 mikopo iliyokuwa imerejeshwa ni asilimia 84 ya mikopo iliyotolewa.

## KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC): MIRADI ILIYOPITISHWA

Jedwali Na.34

| Sekta | 2012 | | | | | | | | 2013 | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | A | B | C | D | E | F | G | H | A | B | C | D | E | F | G | H |
| Kilimo na Ufugaji | 60 | 51 | 9 | 28 | 19 | 13 | 51939 | 821.8 | 43 | 31 | 12 | 15 | 12 | 16 | 20635 | 529.2 |
| Maliasili | 2 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 110 | 5.6 | 6 | 5 | 1 | 2 | 3 | 1 | 2526 | 73.3 |
| Utalii | 209 | 161 | 48 | 144 | 31 | 34 | 10788 | 741.2 | 186 | 153 | 33 | 93 | 38 | 55 | 10745 | 664.3 |
| Uzalishaji Viwandani | 225 | 184 | 41 | 86 | 74 | 65 | 24039 | 2976.4 | 258 | 225 | 33 | 95 | 75 | 88 | 26927 | 2343.4 |
| Bidhaa za Petroli na Madini | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 64 | 8.1 | 2 | 2 | - | - | - | 2 | 98 | 2.6 |
| Majengo ya Biashara | 128 | 113 | 15 | 78 | 30 | 20 | 57541 | 838.9 | 132 | 120 | 12 | 77 | 20 | 35 | 9130 | 1728.0 |
| Usafirishaji | 163 | 139 | 24 | 92 | 35 | 36 | 17076 | 855.0 | 182 | 149 | 33 | 107 | 24 | 51 | 16473 | 842.4 |
| Huduma | 15 | 15 | 0 | 1 | 7 | 7 | 1892 | 424.3 | 8 | 5 | 3 | 1 | 3 | 4 | 570 | 29.9 |
| Kompyuta | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 67 | 7.0 | 1 | 1 | - | - | 1 | - | 50 | 1.9 |
| Asasi za Fedha | 7 | 4 | 3 | 3 | 2 | 2 | 755 | 67.1 | 4 | 4 | - | 1 | - | 3 | 6979 | 9.9 |
| Mawasiliano | 4 | 2 | 2 | 2 | 0 | 2 | 803 | 2969.7 | 9 | 8 | 1 | 1 | 2 | 5 | 2244 | 944.7 |
| Rasilimaliwatu | 33 | 29 | 4 | 20 | 4 | 9 | 1781 | 95.0 | 32 | 27 | 5 | 14 | 5 | 13 | 2813 | 177.2 |
| Nishati | 7 | 7 | 0 | 2 | 2 | 3 | 4529 | 1344.1 | 8 | 6 | 2 | 4 | - | 5 | 2593 | 823.1 |
| Miundombinu ya kiuchumi | 7 | 6 | 1 | 5 | 1 | 1 | 2901 | 261.5 | 7 | 6 | 1 | 2 | - | 5 | 100369 | 80035.1 |
| Utangazaji | 6 | 6 | 0 | 5 | 0 | 1 | 127 | 4.5 | 7 | 7 | - | 5 | 1 | 1 | 335 | 31.3 |
| Jumla | 869 | 718 | 151 | 469 | 205 | 195 | 174412 | 11420.1 | 885 | 749 | 136 | 417 | 184 | 284 | 202487 | 88236.3 |

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

A Jumla ya Miradi Iliyopitishwa

B Miradi Mipya

C Miradi ya Zamani (Upanuzi na Ukarabati)

D Miradi ya Nchini

E Miradi ya Nje

F Miradi ya Ubia

G Jumla ya Ajira

H Jumla ya Thamani ya Uwekezaji (USD. Milioni)

# SURA YA 8

## MASUALA MTAMBUKA

### UKIMWI

170.UKIMWI umekuwa tishio kubwa kwa malengo ya ajira na ufanisi wa soko la ajira. Ukosefu wa wafanyakazi kutokana na maradhi yatokanayo na UKIMWI au kutokana na majukumu ya kuuguza waathirika unaweza kusababisha kushuka kwa uzalishaji mali, kupungua kwa mapato na kupotea kwa ujuzi na utaalam. Katika ngazi ya kaya, kuugua kwa mwanakaya kunamaanisha kupoteza kazi na kipato alichokuwa akiingiza mwanakaya huyo. Aidha, inamaanisha kuongezeka kwa gharama za matibabu na kupelekea kuacha kazi au shule kwa wanakaya wengine ili kumhudumia mgonjwa. Katika ngazi ya Taifa, UKIMWI unaathiri kwa namna mbalimbali uchumi wa nchi. Ongezeko la gharama za huduma za afya na za hifadhi ya jamii, pamoja na upungufu wa faida kwa mashirika na taasisi na kukosekana kwa mapato kwa wafanyakazi husababisha upungufu wa mapato ya Serikali, kutokufikiwa kwa malengo ya bajeti na kuyumba kwa uchumi wa nchi nzima. Hali hii, sambamba na kushuka kwa akiba za watu binafsi hupelekea kushuka kwa nafasi za ajira mpya. Hivyo, Serikali inachukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa inatokomeza maambukizi mapya ya VVU.

171.Mwaka 2013, Serikali ilianzisha mpango unaoitwa *‘Option B plus’* unaolenga kuwapatia wajawazito wenye maambukizi ya VVU dawa za kupunguza makali ya VVU kwa wakati. Hii ni katika kutekeleza Mpango wa kutokomeza maambukizi mapya ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Aidha, mafunzo na warsha zilitolewa kwa watoa huduma na viongozi wa ngazi mbalimbali za mikoa na wilaya kwa lengo la kuwawezesha kuandaa mipango endelevu ya kutokomeza maambukizi mapya ya VVU.

172.Mwaka 2013, Serikali kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania iliwapatia ‘chakula dawa’ watu wenye virusi vya UKIMWI. Watu wenye virusi vya UKIMWI walipimwa hali zao za lishe na waliobainika kuwa na utapiamlo waliingizwa kwenye programu ya “chakula dawa”. Programu hii inatekelezwa katika vituo vyote vya matunzo na tiba katika mikoa ya Arusha, Dodoma na Singida. Aidha, watoa huduma 2,530 walipata mafunzo ya jinsi ya kuchukua vipimo na kutoa “chakula dawa” kwa wagonjwa. Jumla ya watu 26,868

wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye utapiamlo walipata matibabu ya utapiamlo kwa kutumia “chakula dawa”.

173. Mwaka 2013, Serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iliandaa mkakati wa tatu wa Taifa wa UKIMWI (NMSF III 2013-2018) ambao ulizinduliwa tarehe 01/12/2013. Mkakati huu ulitayarishwa kwa ushirikiano na wataalam wa Kitaifa na Kimataifa ambao walifanya mapitio na uchambuzi wa kina juu ya changamoto, mafanikio yaliyokwishapatikana na hatua zinazofuata. Hivyo, Mkakati huu unaendeleza mafanikio ya juhudi katika kinga dhidi ya VVU na UKIMWI katika kipindi cha miaka kumi iliyopita na kubainisha hatua za kuchukua katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Aidha, Mkakati huu umebainisha majukumu ya wadau wote ikiwa ni pamoja na hatua za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji.

174. Mwaka 2013, Serikali iliandaa Mkakati wa Kupunguza Unyanyapaa na Ubaguzi 2013-2017. Katika mkakati huu yameainishwa maeneo makuu 13 ya utekelezaji kwa ajili ya kushughulikia visababishi, viashiria, na madhara ya unyanyapaa na ubaguzi. Afua zote za kimkakati zimeainisha maeneo muhimu yanayochangia kushamiri kwa unyanyapaa na madhara yake na kuelekeza hatua za kuchukua katika ngazi mbalimbali

**Mazingira**

175. Mwaka 2013, Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Mazingira ya mwaka 1997 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 ili kuleta maendeleo endelevu. Katika kipindi hiki, miongozo mitatu (3) kwa ajili ya kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 iliandaliwa na hivyo kufanya Sheria iwe na miongozo 7 kati ya 19 inayohitajika ikilinganishwa na miongozo minne iliyoandaliwa mwaka 2012. Miongozo hiyo ni: Mwongozo wa kuandaa tathmini ya kimkakati ya mazingira; Mwongozo wa kuhuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika sera na mipango; na mwongozo wa maandalizi ya mipango ya mazingira ya kisekta na Serikali za Mitaa.

176. Mwaka 2013, Serikali iliendelea kuhimiza wananchi kupanda na kutunza miti ili kuhifadhi mazingira. Katika kipindi hicho, jumla ya miti 145,156,884 ilipandwa katika mikoa 17 nchini ikilinganishwa na miti 111,994,448 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 29.6. Kati ya hiyo, miti 108,171,349 ilistawi, sawa na asilimia 74.5 ya miti iliyopandwa mwaka 2013 ikilinganishwa na

asilimia 80.7 ya miti iliyostawi mwaka 2012. Wilaya 25 zilipanda miti na kustawi kwa zaidi ya asilimia 80 ikilinganishwa na Wilaya 23 mwaka 2012. Wilaya hizo ni Mufindi, Kilolo, Nkasi, Pangani, Uyui, Urambo, Sikonge, Igunga, Kilindi, Handeni, Lushoto, Muheza, Tanga, Monduli, Ngorongoro, Muleba, Misenyi, Karagwe, Biharamulo, Chato, Kilombero, Sumbawanga, Temeke, Mbinga na Lindi.

177. Mwaka 2013, Serikali iliendelea kuwahimiza wawekezaji kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika uwekezaji kwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kabla ya kutekeleza miradi yao. Katika kipindi hicho, jumla ya miradi 239 ya uwekezaji ilisajiliwa na kufanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira. Kati ya hiyo, miradi 207 ilipata hati za Tathmini ya Athari kwa Mazingira baada ya kukidhi vigezo ikilinganishwa na miradi 213 mwaka 2012.

178. Mwaka 2013, Serikali iliendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali kwa ajili ya kuhifadhi wa bioanuwai. Miradi hii ni pamoja na:

(i) Mradi wa kuhifadhi mazingira katika maeneo ya mfumo wa ikolojia wa Gombe Kigoma na Masito Mpanda ambao unatekelezwa katika eneo la kilomita za mraba 12,047: Katika kipindi hicho: Mipango ya matumizi bora ya ardhi iliandaliwa katika vijiji 6 na kufanya vijiji vyote 49 katika eneo hili kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi; Kaya 5,950 zilihamasishwa kutengeneza majiko banifu na kutengenza majiko 6,150 katika vijiji 27 ikiwa ni hatua ya kupunguza uvunaji holela wa misitu kwa ajili ya kuni na mkaa; Wakulima 79 walihamasishwa kuanzisha mashamba- misitu (*agro-forestry*); Vijiji vitano vinavyozunguka msitu wa Masito-Ugalla vilipatiwa mizinga ya nyuki 200 ya kisasa; na Wadau 55 walipewa mafunzo kuhusu uangalizi wa misitu na matumizi ya teknolojia ya kufuatilia matukio ya moto katika misitu kwa njia ya komputa na simu.

(ii) Mradi wa kuhifadhi mazingira ya bonde la Ziwa Tanganyika ambao unatekelezwa katika mikoa ya Kigoma na Rukwa: Katika utekelezaji wa mradi huu, mipango ya matumizi bora ya ardhi iliandaliwa kwa vijiji sita (6) vya mfano, ambavyo ni: Nyange (Kibondo); Titye (Kasulu); Ilagala (Kigoma); Karema (Mpanda); Korongwe (Nkasi); na Kisumba (Sumbawanga). Aidha, kupitia mradi huu, vijiji 16 vya mfano vilipatiwa mizinga ya nyuki ya kisasa na vifaa vya kuchakata asali kwa lengo la

kuwawezesha wananchi kuwa na shughuli mbadala za kiuchumi na kuhifadhi misitu.

(iii) Mradi wa usimamizi wa matumizi endelevu ya ardhi ambao unatekelezwa katika vijiji 72 vya Mkoa wa Kilimanjaro. Mradi huu unalenga kuhakikisha kuwa juhudi za kuleta maendeleo ya kiuchumi na kupunguza umasikini zinaenda sambamba na kulinda na kuhifadhi mazingira. Katika kipindi hicho, matuta yenye urefu wa mita 510 na mita 30,530 yalitengenezwa katika Wilaya za Hai na Mwanga mtawalia ili kukinga mmomonyoko wa udongo. Aidha, makinga maji tisa (9) yamejengwa katika kijiji cha Sango, Manispaa ya Moshi ili kuzuia uharibifu uliopo kwenye eneo hilo. Ili kukabiliana na ukame, matenki matano (5) ya kuvuna maji yalijengwa katika Wilaya ya Rombo (3) na Wilaya ya Hai (2). Vile vile, mfereji wa Gunge katika Wilaya ya Same, wenye urefu wa mita 300 ulitengenezwa na wananchi wanaotumia mfereji waliongezeka kutoka 200 mwaka 2012 hadi 250 mwaka 2013.

**Utawala Bora**

179. Mwaka 2013, Serikali kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliendelea na juhudi za kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora katika jamii. Katika jitihada za kuimarisha utawala bora, mwaka 2013, Tume ikishirikiana na Asasi Zisizo za Kiserikali ilizindua Mwongozo unaolenga kuongeza uelewa wa watendaji, wananchi na viongozi kuhusu utawala bora na haki za binadamu. Aidha, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Utawala Bora iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi ambapo ilitekeleza Mpango kazi wa mwaka mmoja. Miongoni mwa mambo yaliyotekelezwa mwaka 2013 kupitia Mpango huo ni kupitishwa kwa marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura Na. 398.

180. Mwaka 2013, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliwatumia viongozi wa umma 13,119 fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni. Hadi kufikia Desemba 2013, jumla ya viongozi 8,400 walirejesha fomu zao. Kati ya hao, viongozi 3,801 walikuwa wa siasa na viongozi 5,319 walikuwa wa utumishi wa umma. Viongozi wa siasa ambao hawakurejesha fomu zao walikuwa 1,170 na viongozi wa utumishi wa umma walikuwa 2,829.

Urejeshwaji mdogo wa fomu ulitokana na ongezeko la viongozi wapya uliofanyika mwezi Septemba 2013. Aidha, orodha ya viongozi wanaowajibika na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na.13 ya mwaka 1995 kupitia Tangazo la Serikali Na. 260 la mwezi Septemba 2013, iliongezeka kufikia 8,148 kutoka 4,104 waliokuwepo awali. Idadi ya viongozi wa siasa walikuwa 4,971

**Jinsia**

181. Mwaka 2013, Serikali ilifanya vikao na wadau mbalimbali kujadili namna ya kujumuisha masuala ya jinsia katika mipango, mikakati, sera na programu mbalimbali za Kisekta. Katika vikao hivyo, pamoja na masuala mengine wadau walikubaliana kufuatilia uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika Wizara zinazotekeleza mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa. Aidha, vikao vitatu vya Kamati ya Kitaifa ya Kuzuia na Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake, Watoto na walemavu wa ngozi vilifanyika ili kuratibu na kusimamia shughuli za kuzuia na kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia. Vile vile, tathmini ya utendaji wa Kamati za Ulinzi na Usalama katika mkoa wa Manyara kuhusiana na kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake na watoto ilifanyika. Tathmini hiyo ilionesha kuwa Kamati husika zinahitaji kujengewa uwezo zaidi ili ziweze kufanya kazi zake kikamilifu.

182. Mwaka 2013, Benki ya Wanawake Tanzania ilitoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake na wanaume, yenye thamani ya jumla ya shilingi milioni 9,163.85 kwa wateja 9,380 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 1,939.63 iliyotolewa kwa wateja 14,663 mwaka 2012. Kati ya wateja waliopata mikopo mwaka 2013, wanawake walikuwa 7,395, sawa na asilimia 78.8. Aidha, Benki ilitoa mafunzo ya ujasiriamali na uendeshaji wa biashara kwa wateja 8,858. Vile vile, Benki ilipanua wigo wa shughuli zake kwa kufungua tawi lingine eneo la Kariakoo na kufungua vituo vya kutolea mikopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, na Mwanza. Jumla ya wanawake 9,380 walipatiwa mikopo katika vituo hivyo.

183. Katika mwaka wa fedha wa 2013/14, Serikali ilitenga shilingi bilioni 2 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Katika kipindi cha Julai – Desemba 2013, Mfuko ulikuwa umepatiwa shilingi milioni 515.63. Kati ya kiasi kilichopatikana, shilingi milioni 347.0 sawa na asilimia 62 zilipelekwa katika Halmashauri 31 kwa ajili ya kuwakopesha wanawake wajasiriamali

kuendesha biashara zao. Aidha, shilingi milioni 103.13 zilitumika kwa ajili ya ufuatiliaji katika mikoa 9 ya Arusha, Manyara, Singida, Pwani, Tanga, Katavi, Rukwa, Morogoro na Kagera.

**Usalama wa Raia**

184. Mwaka 2012/13 hali ya ulinzi na usalama nchini ilikuwa tulivu kwa ujumla wake, licha ya kuendelea kuwepo kwa baadhi ya matukio ya kihalifu na uvunjifu wa amani katika maeneo mbalimbali nchini. Changamoto kubwa ni makosa ya jinai ambayo ingawa hayaongezeki kwa kasi lakini bado yako juu.

185. Mwaka 2012/13, makosa ya jinai yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi nchini yalipungua kwa asilimia moja kufikia makosa 65,154 ikilinganishwa na makosa 65,798 yaliyoripotiwa mwaka 2011/12. Aidha, makosa dhidi ya maadili ya jamii yaliyoripotiwa mwaka 2012/13 yalipungua kwa asilimia 7.1 na kuwa 12,714 ikilinganishwa na makosa 13,683 yaliyoripotiwa mwaka 2011/12. Haya yanajumuisha makosa yote yanayopingana na maadili mema ya jamii kama vile biashara na matumizi ya madawa ya kulevya na rushwa. Hata hivyo, matukio ya kuwania mali yaliyoripotiwa mwaka 2012/13 yaliongezeka kwa asilimia 0.4 kufikia 41,278 ikilinganishwa na matukio 41,103 yaliyoripotiwa mwaka 2011/12. Vile vile, makosa dhidi ya binadamu yaliyoripotiwa mwaka 2012/13 yalikuwa 11,162 ikilinganishwa na makosa 11,012 yaliyoripotiwa mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Haya ni makosa yanayoelekezwa kwenye nafsi ya binadamu kama vile mauaji, kubaka, kulawiti na wizi wa watoto.

186. Mwaka 2012/13, jumla ya ajali 23,800 ziliripotiwa ikilinganishwa na ajali 23,499 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 1.3. Aidha, ajali zilizosababisha vifo katika kipindi hicho zilikuwa 3,382 ikilinganishwa na ajali 3,321 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 1.8. Vile, vile, majeruhi wa ajali hizo katika kipindi hicho walikuwa 20,826 ikilinganishwa na majeruhi 19,696 mwaka 2011/12, sawa na ongezeko la asilimia 5.7. Hata hivyo, vifo kutokana na ajali hizo vilipungua kwa asilimia 1.9 na kufikia 3,972 mwaka 2012/13 ikilinganishwa na vifo 4,049 mwaka 2011/12.

187. Hadi Juni, 2013, magereza yote nchini yalikuwa na uwezo wa kuhifadhi wahalifu/watuhumiwa 29,552 ikilinganishwa na wahalifu/watuhumiwa 32,494

waliokuwepo magerezani. Idadi hii inaonesha kuwepo kwa wahalifu/watuhumiwa 2,942 zaidi ya uwezo wa magereza. Kati ya idadi hiyo, waliohukumiwa kifungo walikuwa 15,343 na mahabusu wenye kesi katika mahakama mbalimbali walikuwa 17,151. Kwa wastani, magereza nchini yalikuwa na wafungwa 4,185 mwaka 2012/13 zaidi ya uwezo wake, sawa na asilimia 14.2 zaidi ya uwezo wa magereza.

188. Katika mwaka 2013, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kupunguza msongamano wa wafungwa pamoja na kuboresha huduma za magereza. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na: Kutumia vikao vya Bodi ya Parole; Vifungo vya nje; Misamaha ya Rais; Kuharakisha usikilizwaji wa kesi za mahabusu hasa waliokaa muda mrefu gerezani; na Ujenzi na ukarabati wa mabweni.

189. Mwaka 2012/13, vikosi vya huduma ya zimamoto na uokoaji viliendelea kukabiliana na majanga ya moto kwa lengo la kuokoa maisha ya watu na mali zao. Katika kipindi hicho, jumla ya miito ya matukio 528 ilipokelewa ikilinganishwa na miito 642 iliyopokelewa mwaka 2011/12. Aidha, katika kukabiliana na matukio ya moto, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liliendelea na zoezi la ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kwenye maeneo mbalimbali. Ukaguzi huo ulienda sambamba na utoaji elimu ya kujikinga na moto na namna ya kutumia vifaa vya kuzima moto vinavyowekwa sehemu za kazi. Mwaka 2012/13, jumla ya maeneo 7,336 yalikaguliwa ikilinganishwa na maeneo 29,582 yaliyokaguliwa mwaka 2011/12.

190. Mwaka 2012/13, wahamiaji haramu 3,732 walikamatwa ikilinganishwa na wahamiaji 6,293 waliokamatwa mwaka 2011/12. Aidha, wageni walioingia nchini kwa halali katika kipindi hicho walikuwa 1,054,987 ikilinganishwa na wageni 910,143 walioingia nchini mwaka 2011/12. Vile vile, wageni 973,503 walitoka nchini mwaka 2012/13 ikilinganishwa na wageni 939,852 waliotoka nchini mwaka 2011/12. Idadi ya wakimbizi waliokuwa nchini mwaka 2012/13 walikuwa 101,414,jumla ya wakimbizi 701 walipelekwa nchini Marekani chini ya usimamizi wa UNHCR na shirika la kimataifa la wakimbizi (IOM).

191. Jumla ya hati za ukaazi 30,913 zilitolewa mwaka 2012/13 ikilinganishwa na hati za ukaazi 14,127 zilizotolewa mwaka 2011/12. Aidha, jumla ya hati za

kusafiria 56,959 zilitolewa kwa watanzania mwaka 2012/13 ikilinganishwa na hati 42,582 zilizotolewa mwaka 2011/12. Kati ya hizo, hati za kawaida zilikuwa 54,988, hati za kibalozi (383), hati za watumishi (207), na hati za Afrika Mashariki (1,381).

192. Hadi Desemba 2013, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilingiza taarifa za watumishi 290,000 kwenye mfumo wa kompyuta ikiwa ni pamoja na picha na alama za vidole. Watumishi hawa ni kutoka Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kutoka Zanzibar na mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, mwaka 2013, Mamlaka ilitoa vitambulisho kwa makundi maalum na kwa baadhi ya watumishi wa umma walioko mkoa wa Dar es Salaam. Vile vile, uchambuzi wa maombi ya wananchi 220,000 walioandikishwa katika wilaya ya Kilombero iliyoteuliwa kuwa ya majaribio ulifanyika na taarifa za uchambuzi kuingizwa kwenye kompyuta. Kadhalika, jumla ya wakazi 2,159,822 wa mkoa wa Dar es Salaam waliandikishwa na kuhakikiwa na kamati za ulinzi na usalama za kata na utaratibu wa kuingiza taarifa zao kwenye mfumo wa kompyuta unaendelea. Kwa upande wa Zanzibar, Mamlaka iliandikisha jumla ya wakazi 160,645.

# SURA YA 9

# MAENDELEO YA JUHUDI ZA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI

## Utangulizi

193. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 20012/13, Serikali iliendelea na utekelezaji wa MKUKUTA-II kama nyenzo ya kufikia malengo yaliyowekwa ifikapo mwaka 2015, katika juhudi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Katika kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji wa MKUKUTA-II (2010/11, 2011/12 na 2012/13), taarifa mabalimbali zinazoelezea mafanikio na changamoto zilizojitokeza zimekuwa zikiandaliwa chini ya "Mpango wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA". Taarifa hizi ni pamoja na; Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA (MAIR 2010/11,2011/12, 2012/13), Taarifa ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu (PHDR 2011); Taarifa itokanayo na maoni ya watu (*Views of the People's Report 20012*); na taarifa za tafiti na uchambuzi/sensa mbalimbali kama vile taarifa ya viashiria vya UKIMWI na Malaria ya mwaka 2011/12 na taarifa ya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ya mwaka 2011/12.

194. Katika kupima utekelezaji wa MKUKUTA-II, viashiria mbalimbali vimeainishwa katika nguzo tatu ambazo ni Ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; Kuboresha maisha na ustawi wa jamii; na Utawala bora na Uwajibikaji. Uchambuzi wa mwenendo wa viashria hivyo katika mwaka wa tatu wa utekelezaji ni kama inavyoelezwa hapa chini:

## Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato

195. Mwaka 2013, uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.9 mwaka 2012. Shabaha ya MKUKUTA-II ni kuwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 8 hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2015. Ukuaji wa pato la ndani la taifa kwa mwaka 2013 ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya mawasiliano iliyokua kwa asilimia 22.8; sekta ya fedha (asilimia 12.2); sekta ya ujenzi (asilimia 8.6); na sekta ya biashara (asilimia 8.3).

196.Katika kupunguza umaskini wa kipato, Serikali iliendelea na utekelezaji wa programu ya ajira nchini, kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa ajili ya kuwezesha vijana kujiajiri wenyewe na kusimamia sheria za kazi. Kutokana na hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali, jumla ya nafasi za ajira 274,030 zilipatikana mwaka 2012/13 ukilinganisha na nafasi za ajira 250,678 mwaka 2011/12 kupitia programu na miradi ya maendeleo katika sekata ya umma na binafsi. Fursa hizo za ajira zilipatikana katika maeneo yafuatayo: Sekta ya umma (56,746); Sekta binafsi (rasmi) nafasi 8,603 na programu na miradi ya maendeleo (208,681) kama inavyoonekana katika jedwali Na. 9.1. Aidha, katika hatua nyingine ya kupunguza umaskini wa kipato, Serikali iliwezesha zaidi ya vikundi 502 katika Mikoa 17, vikiwa na jumla ya wanachama 5,385 (Wanawake 2,519 na Wanaume 2,866) kwa kuvipatia mitaji na mafunzo ya ujasiriamali.

**Jedwali 9.1: Nafasi za ajira zilizopatikana mwaka 2012/2013**

| **Miradi ya Maendeleo** | **Nafasi za ajira** |
|---|---|
| TASAF | 50,246 |
| SIDO | 2,436 |
| TANROADS | 1,033 |
| Sekta ya Mawasiliano | 86,702 |
| TIC | 59,010 |
| EPZA | 9,254 |
| Serikali | 56,746 |
| Sekata binafsi (rasmi) | 8,603 |
| **Jumla** | **274,030** |

Chanzo: Wizara ya Kazi na Ajira

197.“Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2011/12” umeboresha mbinu za ukusanyaji na ukokotoaji wa viashiria vya umaskini. Utafiti wa mwaka 2011/12 umekusanya taarifa nyingi zikiwemo mpya zilizokusanywa kwa mara ya kwanza kama vile huduma za afya, maji na huduma nyingine za kijamii. Mbinu za kitakwimu zilizotumika mwaka 2011/12 zilitumika pia kukokotoa viashiria vya 2007 kwa ajili ya kuweza kupima mwelekeo wa umaskini. Kufuatia kutumika kwa mbinu mpya za ukusanyaji na ukokotoaji wa viashiria

vya umaskini, takwimu za viashiria vya umaskini zilizotokana na utafiti wa mwaka 2006/07 nazo zilibadilika ili kupata ulinganifu.

198. Matokeo ya "Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya" kwa Tanzania Bara yalionesha kuwa idadi ya watanzania waliomo katika viwango vya chini vya mahitaji ya msingi vilipungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2007 hadi asilimia 28.2 mwaka 2011/12. Katika Jiji la Dar es Salaam, umaskini ulipungua kutoka asilimia 14.1 mwaka 2007 hadi asilimia 4.1 mwaka 2011/12 na maeneo mengine ya mijini umaskini ulipungua kutoka asilimia 22.7 hadi asilimia 21.7 katika kipindi hicho. Kwa ujumla, kiwango cha umaskini kimepungua kwa asilimia 6.2 katika kipindi cha mwaka 2007 hadi 2011/12. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa asilimia 9.7 ya watu wote waishio Tanzania Bara wapo chini ya mstari wa umaskini wa chakula.

**Jedwali Na 9.2. Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini**

| Hali ya Umaskini | | Maeneo | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Hali ya Umaskini** | **Mwaka wa Utafiti** | **Dar es Salaaam** | **Maeneo mengine ya mijini** | **Maeneo ya Vijijini** | **Tanzania Bara** |
| Chakula | 2007* | 3.2 | 8.9 | 13.5 | 11.8 |
| | 2011/12 | 1.0 | 8.7 | 11.3 | 9.7 |
| Mahitaji ya Msingi | 2007* | 14.1 | 22.7 | 39.4 | 34.4 |
| | 2011/12 | 4.1 | 21.7 | 33.3 | 28.2 |

Chanzo: Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya - 2007 na 2011/12

*Takwimu zimeboreshwa kwa kutumia mbinu mpya za ukokotoaji

199. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2011/12 unaonesha kuwa hali ya utofauti wa kipato ulipungua kufikia kipimo cha Gini cha 0.34 kwa Tanzania Bara ikilinganishwa na 0.35 mwaka 2007. Kwa kawaida, tofauti ya kipato hupimwa kwa kutumia kipimo cha tofauti ya kipato katika jamii maarufu kama "kizio cha Gini". Kipimo cha Gini huanzia sifuri (0) kama hakuna tofauti ya kipato mpaka moja (1) kama kuna tofauti kubwa ya kipato. Aidha, tafiti mbalimbali zimeonesha kwamba kuna uhusiano wa karibu kati ya idadi ya watu kwenye kaya na hali ya umaskini katika kaya. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2011/12 ulionesha uwiano huu,

ambapo hali ya umaskini imekuwa ikiongezeka kulingana na jinsi idadi ya watu katika kaya inavyoongezeka kama kielelezo 9.1 kinavyoonesha.

**Kielelezo Na 9.1: Uhusiano wa Kiwango cha Umaskini kwa Idadi ya Watu, Tanzania Bara, 2011/12**




200.Kuhusu viashiria vya umaskini visivyo vya kipato, kumekuwa na ongezeko la uwiano wa kaya zinazoishi katika makazi yaliyo jengwa kwa vifaa vya kisasa kama vile zege, mawe, saruji na vyuma. Matokeo ya utafiti wa mwaka 2011/12 yalionesha kuwa asilimia 66 ya kaya zinaishi katika nyumba zenye paa za kisasa ikilinganishwa na asilimia 55 ya kaya mwaka 2007. Vivyo hivyo, asilimia 73 ya kaya zinaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa kuta imara mwaka 2011/12 ikilinganishwa na asilimia 33 za mwaka 2007. Kuta imara zinajumuisha kuta zilizojengwa kwa mawe, matofali ya saruji, au matofali ya kuchoma na paa za kisasa ni zile zilizojengwa kwa mabati. Aidha, kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo wa mwaka 2011/12, asilimia 18 ya kaya za Tanzania Bara zinaishi katika nyumba zilizounganishwa na umeme wa gridi ya Taifa, sawa na ongezeko la asilimia 6 ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2007. Vile vile, kuhusu umiliki wa mali, utafiti unaonesha kuwa asilimia 4 ya kaya zinamiliki pikipiki, asilimia 55 zinamiliki redio, na katika asilimia 57 ya kaya zote kuna angalau mwanakaya mmoja anayemiliki simu ya mkononi. Viashiria vya umiliki wa

pikipiki na simu za mkononi ni miongoni mwa viashiria ambavyo havikuwepo katika utafiti wa 2007.

**Kuboresha Maisha na Ustawi wa Jamii**

201. Katika kuboresha maisha na ustawi wa jamii, viashiaria vikuu katika nguzo hii ni vile vinavyohusiana na elimu, afya na maji. Katika kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji wa MKUKUTA-II, utoaji wa elimu umeimarika hasa katika uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi zote. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika elimu ni pamoja na kuongezeka kwa uandikishaji katika ngazi ya vyuo vya ufundi na elimu ya juu. Kiwango cha kuhitimu elimu ya msingi kiliongezeka kutoka asilimia 54.8 mwaka 2012 hadi asilimia 55.3 mwaka 2013. Hata hivyo, uandikishaji katika ngazi ya elimu ya awali na msingi ulipungua, ikiashiria kwamba idadi ya wanafunzi waliofikia na kuvuka umri wa kuandikishwa iliendelea kupungua.

202. Mafanikio pia yamepatikana katika huduma ya afya. Kwa mujibu wa utafiti wa viashiria vya malaria na UKIMWI wa mwaka 2011/12, kiwango cha ugonjwa wa malaria kimepungua kutoka asilimia 18 mwaka 2007/08 hadi asilimia 9 mwaka 2011/12. Kiwango cha maambukizi ya UKIMWI katika kundi la watu wenye umri kati ya miaka 15-49 kilipungua kutoka asilimia 5.7 mwaka 2007/08 hadi asilimia 5.1 mwaka 2011/12. Idadi ya watu wanaopata maji safi na salama vijijini na mijini (ukiondoa Dar es salaam) ilifikia wastani wa asilimia 57 mwezi Desemba 2012 na asilimia 86 mwezi June 2013 kwa mtiririko huo. Hata hivyo, kiwango hicho kilikuwa chini ya lengo la MKUKUTA la asilimia 95 kwa wakazi wa mijini na 65 kwa wakazi wa vijijini.

203. Mafanikio yamepatikana pia katika kuboresha makazi. Matokeo ya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya yamwaka 2011/12 yanaonesha kwamba kumekuwa na ongezeko la familia zinazoishi katika nyumba zenye paa la bati kutoka familia 6 kati ya 10 mwaka 2006/07 hadi familia 7 kati ya 10 mwaka 2011/12. Vilevile, familia zinazoishi katika nyumba zenye ukuta wa matofali ya saruji au matofali ya kuchoma ziliongezeka kutoka asilimia 33 mwaka 2006/07 hadi asilimia 46 mwaka 2011/12.

**Utawala Bora na Uwajibikaji**

204. Katika kipindi cha mwaka 20012/13, Serikali iliendelea na juhudi zake za kupambana na rushwa, kujenga uwezo wa taasisi za umma katika kubresha utoaji wa huduma na uwajibikaji katika kusimamia fedha za umma, kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika utendaji wa Serikali na utoaji wa haki kwa wakati mbele ya sheria.

205. Katika kipindi cha miaka miwili, uwajibikaji katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa uliimarika. Mwaka 2011/12 idadi ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizopata hati safi ziliongezeka na kufikia asilimia 94.7 kutoka asilimia 85 mwaka 2010/11. Hati chafu zilipungua kutoka asilimia 15 hadi asilimia 5.3 katika kipindi hicho. Uwajibikaji pia umeimarika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo hati safi ziliongezeka kwa asilimia 24 katika kipindi cha mwaka 2010/11 na 2011/12. Hati chafu pia zimeendelea kupungua kutoka asilimia 21 mwaka 2010/12 hadi asilimai 4 mwaka 2011/12.

**Jedwali Na 9.3: Mwenendo wa Taarifa za Ukaguzi kwa Wizara, Taasisi za Serikali na Sekretarieti za Mikoa**

| **Aina ya taarifa** | **Hati safi** | | **Hati zenye mashaka** | | **Hati chafu** | | **Taarifa inayosubiriwa** | | **Jumla** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka | 2010/11 | 2011/12 | 2010/11 | 2011/12 | 2010/11 | 2011/12 | 2010/11 | 2011/12 | 2010/11 | 2011/12 |
| Wizara na Idara za Serikali | 50 | 87 | 10 | 6 | 0 | 0 | - | 0 | 60 | 93 |
| Sekretarieti za Mikoa | 19 | 21 | 2 | 0 | 0 | 0 | - | 0 | 21 | 21 |
| Jumla | 69 | 108 | 12 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 81 | 114 |
| Asilimia (%) | 85 | 94.7 | 15 | 5.3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 100 | 100 |

Chanzo: Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabua za Serikali

206.Katika mwaka 2012/13, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuleta usawa na haki mbele ya sheria. Katika kipindi hicho jumla ya kesi 94,872 zilisajiliwa katika mahakama za Wilaya ikilinganishwa na kesi 77,495 mwaka 2011/12. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 22. Vilevile, kesi zilizosajiliwa katika Mahakama za mwanzo pia ziliongezeka kutoka kesi 512,308 mwaka 2011/12 hadi kesi 650,181 mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la asilimia 27. Jumla ya kesi zilizosikilizwa na kutolewa hukumu nazo ziliongezeka kutoka kesi 510,996 mwaka 2011/12 hadi kesi 577,425 mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la asilimia 13.

# SEHEMU YA TATU

## SUALA MAALUMU KIMAENDELEO

## SURA YA 10

## MCHANGO WA GESI NA MAFUTA KATIKA UCHUMI

### Historia ya Utafutaji wa Mafuta na Gesi Nchini

207. Shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi nchini Tanzania zilianza takribani miaka 60 iliyopita. Utafutaji ulianza mwaka 1952 wakati *British Petroleum Company* (BP) na *Shell International Oil Company* (SHELL) walipoanza utafutaji wa mafuta katika miamba tabaka (*sedimentary basins*). Kwa kipindi kirefu na kwa nyakati tofauti, makampuni tofauti ya kimataifa ya mafuta yamekuwa yakifanya shughuli za utafutaji mafuta nchi kavu na kwenye maji ya kina kirefu. Mpaka sasa kiasi cha gesi iliyogunduliwa ni futi za ujazo trilioni 46.5 na hakuna ugunduzi wowote wa mafuta. Historia ya utafutaji mafuta na gesi imegawanyika kwa vipindi kama ifuatavyo:

#### a. Utafutaji Kabla ya 1980

208. Katika kipindi cha kabla ya mwaka 1964, eneo lote la mwambao lilitolewa kwa kampuni za SHELL na BP chini ya Sheria ya *"Mining Ordinance"* ambapo ilitolewa leseni moja na waliachia maeneo yote ilipofika mwaka 1964. Hizi zilikuwa ni kampuni za mwanzo kufanya utafiti na zilichoronga jumla ya visima vinne (4) katika maeneo ya Mafia, Zanzibar, Mandawa na Pemba.

209. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 1969 hadi mwanzoni mwa mwaka 1980, Kampuni ya AGIP/AMOCO ilipewa na Serikali eneo lote la mwambao chini ya Sheria ya "*Mining ordinance*" na baadae chini ya Mkataba wa Ugawanaji (PSA) ambao ulianza kutumika baada ya kuanzishwa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Kwa kipindi hicho, Kampuni ya AGIP ilichoronga visima vinne (4) maeneo ya Ras Machui, Songo Songo, Kisangire na Kisarawe. Mwaka 1974, eneo la Songo Songo liligunduliwa kuwa na gesi na mwaka huo huo Kampuni ilirudisha eneo hilo kwa Serikali na baadae ilirudisha maeneo mengine kwa utaratibu wa kimkataba. Aidha, Kampuni iliachia maeneo yote mwaka 1982 baada ya kuona kuwa gesi iliyogundulika haikuwa na tija kiuchumi. Baada ya kurudishwa kwa maeneo hayo, wataalamu wa TPDC wakishirikiana na Kampuni ya ONGC ya India walichoronga visima vitatu (3) maeneo ya Songo Songo na kuthibitisha uwepo wa gesi asilia kwa kiasi kikubwa.

**b. Utafutaji Miaka ya 1980-1990**

210. Katika miaka hii, kulikuwa na ugunduzi wa gesi eneo la Mnazi Bay uliofanywa na Kampuni ya AGIP mwaka 1982. Aidha, wawekezaji kadhaa wakiwemo AMOCO, TEXACO, SHELL na IEDC waliingia katika mikataba ya ugawanaji (PSA) ambapo SHELL Petroleum walipewa eneo la mwambao wa kati na Selous. Kampuni hii ilipewa vitalu vitano vyenye ukubwa wa eneo la kati ya kilometa za mraba 7,000 na 16,817. Kampuni hii ilichukua takwimu za mitetemo kwa kila kitalu na kuchoronga jumla ya visima vitano. Aidha, Kampuni ya AMOCO ilichimba visima viwili (2) wakati TEXACO ilichimba kisima kimoja (1).

211. Kampuni ya IEDC ambayo ni kampuni tanzu ya KUFPEC ilipewa leseni ya utafutaji na uzalishaji mafuta eneo la mwambao wa Kaskazini. Kampuni ilipewa kitalu kimoja chenye ukubwa wa kilometa za mraba 12,000. Kazi ilizofanya ni ukusanyaji wa taarifa za mitetemo na kuchoronga visima viwili. Kampuni zote zilisitisha utafutaji kutokana na ukata wa fedha. Kati ya mwaka 1981 hadi 1983, TPDC kwa kutumia fedha za ndani ilichoronga jumla ya visima saba (7)).

**c. Utafutaji Miaka ya 1990 – 1999**

212. Mwanzoni mwa awamu hii, Serikali ilikazania katika kuhakikisha inaimarisha mazingira ya kisera na kuvutia zaidi uwekezaji kwa kulegeza masharti ya mikataba. Hii iliwezesha Serikali kuanza kuangalia namna ya kuwezesha ugunduzi wa gesi ya Songo Songo kuanza kutumika kibiashara kama vile kuzalisha umeme. Katika kipindi hicho, Serikali iliingia mikataba na makampuni kadhaa yakiwemo; Antrim, SHELL, Ndovu Resource, Tullow Oil na Canop Oil. Hata hivyo, kipindi hiki kilitawaliwa na shughuli finyu za utafutaji rasilimali hizo.

**d. Utafutaji Miaka ya 2000 – 2013**

213. Katika kipindi hiki kulikuwa na ugunduzi mkubwa wa gesi baharini na nchi kavu ambapo gesi iligunduliwa maeneo ya Mkuranga (2007), Kiliwani (2008), Ntorya (2012) na bahari ya kina kirefu (2010 – 2013). Duru tatu (3) za ugawaji vitalu kwenye maji ya kina kirefu zilitangazwa kati ya mwaka 2000 na 2007 na moja ya nchi kavu iliyokuwa na vitalu sita (6) ilitangazwa mwaka 2006.

214. Mwaka 2000, zabuni ya kwanza ya baharini ilitangazwa ikiwa na vitalu sita (6) vya baharini vyenye wastani wa ukubwa wa kilometa za mraba 10,000. Zabuni moja tu ilipokelewa kutoka kampuni ya PETROBRAS ambayo ndio kampuni pekee iliyoomba. Kampuni hii ilipewa kitalu namba 5 na kusaini mkataba wa PSA mwaka 2004. Taarifa zilizokusanywa hadi sasa ni pamoja na takwimu za mitetemo ya 2D (*Two Dimensional*) kwa umbali wa kilomita 2,800 na 3D (*Three Dimensional*) kwa kilomita za mraba 1,125. Kampuni hii ya PETROBRAS ilifanikiwa kuchoronga kisima kimoja.

215. Mwaka 2001, Serikali ilitangaza zabuni ya pili ya baharini ambapo vitalu 11 vilitangazwa kunadiwa. Kila kitalu kilikuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 10,000. Zabuni mbili zilipokelewa kutoka kampuni ya SHELL na GLOBAL. Kampuni ya SHELL walipewa vitalu namba 9, 10, 11 na 12 wakati kampuni ya GLOBAL haikuonesha kuwa na uwezo wa kiutaalam na kifedha. Mpaka sasa katika eneo hilo la baharini hamna takwimu zilizokusanywa wala visima vilivyochorongwa kutokana na kutokamilika kwa mkataba.

216. Mwaka 2004, zabuni ya tatu ya baharini ilitangazwa ambapo vitalu saba (7) vilinadiwa vikiwa na ukubwa wa wastani wa kilomita za mraba 10,000. Katika zabuni hizo, kampuni tatu zilijitokeza ambazo ni OPHIR, STATOIL na PETROBRAS na walipewa vitalu na 1, 2 na 6. Takwimu zilizokusanywa hadi sasa ni mitetemo kilomita 12,626.025 za 2D na kilomita za mraba zipatazo 6,659 za 3D. Jumla ya visima vitano vilichorongwa vikiwemo vitatu vilivyochorongwa na OPHIR na visima viwili vilivyochorongwa na STATOIL.

217. Vitalu namba 3 na 4 vyenye wastani wa ukubwa wa kilomita za mraba 10,000 kwa kila kitalu vilitolewa kwa kampuni ya OPHIR ENERGY. Takwimu zilizokusanywa hadi sasa ni pamoja na za mitetemo ya 2D ambapo kilomita 4,824.925 zimekusanywa na takwimu za 3D zenye ukubwa wa kilomita za mraba 6,450. Visima vitatu vimechorongwa ambapo kitalu namba 3 kisima kimoja kimechorongwa wakati katika kitalu namba 4 visima viwili vimechorongwa.

218. Mwaka 2006, Serikali ilitoa agizo la kuharakisha utafutaji mafuta na gesi baharini ambapo TPDC iliruhusiwa kufanya mazungumzo ya moja kwa moja na kampuni zilizoonesha uwezo na nia ya kuwekeza. Katika kuharakisha utafutaji

baharini, mnamo mwaka 2007 zabuni ndogo ilitangazwa ambapo vitalu namba 7 na 8 vyenye ukubwa wa wastani wa kilomita za mraba 10,000 vilinadiwa. Vitalu hivi vilitolewa kwa kampuni za DOMINION kitalu namba 7 na PETROBRAS kitalu namba 8. Takwimu zilizokusanywa hadi sasa ni pamoja na mitetemo ya 2D kwa eneo la kilomita 4,315, mitetemo ya 3D kwa eneo la kilomita za mraba 1,235 na mpaka sasa hamna kisima ambacho kimeshachorongwa.

**e. Utafutaji Kuanzia 2014**

219. Mwaka 2013, Serikali ilizindua mchakato wa kuitisha zabuni ya utafutaji kwenye vitalu 7 vya bahari kuu ya kina kirefu na Ziwa Tanganyika. Vitalu hivyo ni namba 4/2A, 4/3A, 4/3B, 4/4A, 4/4B, 4/5A na 4/5B kwa baharini na kingine kaskazini mwa Ziwa Tanganyika. Uzinduzi huu ulifanyika nchini kwa mara ya kwanza.

**Sheria, Sera na Kanuni Katika Masuala ya Gesi na Mafuta Nchini**

220. Shughuli za utafutaji, uzalishaji na usambazaji wa gesi nchini zinafanywa kupitia Sera, Sheria na Kanuni mbali mbali kama ifuatavyo:

(i) Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Petroli ya mwaka 1980 (*Petroleum [Exploration and Production] Act 1980*);

(ii) Sheria ya Hifadhi ya Mazingira ya mwaka 2004 (*Environmental Management Act 2004);*

(iii) Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (*Income Tax Act 2004*);

(iv) Sera ya Nishati ya mwaka 2003 *(Energy Policy of 2003*);

(v) Sera ya Gesi Asilia ya mwaka 2013 (*Natural Gas Policy*); na

(vi) Mkataba wa Kugawana Mapato wa mwaka 2013 *(Production Sharing Agreement*);

**Maeneo Yaliyogunduliwa Mafuta na Gesi, Kiwango cha Uzalishaji na Matumizi**

**Maeneo Yaliyogunduliwa Gesi**

221. Maeneo ambayo yameshagunduliwa kuwa na gesi asilia ni pamoja na Songo Songo (1974), Mnazi Bay (1982), Mkuranga (2007), Kiliwani (2008), Ntorya (2012) na eneo la bahari ya kina kirefu (2010-2013) ambapo futi za ujazo trilioni 46.5 zimegundulika. Gesi asilia iliyogundulika baharini ni kiasi cha futi za ujazo trilioni 38.5 na nchi kavu ni futi za ujazo trilioni 8. Kiasi kilichohakikiwa ni futi za ujazo trilioni 1.169 na kinajumuisha gesi kutoka

Songo Songo (futi za ujazo bilioni 880), Kiliwani (futi za ujazo bilioni 27) na Mnazi Bay (futi za ujazo bilioni 262). Aidha, kulingana na matokeo ya utafutaji hadi kufikia sasa, Tanzania haijafanikiwa kugundua mafuta. Kielelezo kifuatacho kinaelezea ugunduzi huo.




**Kiwango cha Uzalishaji**

222.Mpaka sasa uzalishaji wa gesi asilia kwa visima vya Songo Songo ni takribani futi za ujazo milioni 96 hadi 102 kwa siku ambazo husafirishwa kwa bomba hadi Dar es Salaam. Uwezo wa bomba lililopo kwa sasa ni kusafirisha futi za ujazo milioni 105 kwa siku. Mitambo ya kusafishia gesi iliyopo Songo Songo inaweza kusafisha hadi futi za ujazo milioni 110 kwa siku. Hivyo, uwezo wa bomba kusafirisha futi za ujazo milioni 105 kwa siku ni kikwazo kwa mitambo hii kufikia uwezo wake wa juu. Vile vile, kutokana na hali ya mahitaji ya umeme Mtwara, uzalishaji wa gesi eneo la Mnazi Bay ambao ni futi za ujazo milioni 2 kwa siku, hutumika kwa kuzalisha umeme kukidhi mahitaji hayo.

**Matumizi ya gesi asilia**

223.Hadi mwaka 2013, asilimia 88 ya gesi asilia inayozalishwa nchini inatumika katika kuzalisha nishati ya umeme. Mitambo iliyopo inayotumia gesi asilia ina uwezo wa kuzalisha Megawati 554 lakini inazalisha Megawati 320. Aidha, gesi hii pia inatumika kwa matumizi mbalimbali kama nishati mbadala ambapo takriban viwanda 37 vinatumia gesi asilia, taasisi 2, nyumba 70 na magari zaidi ya 40.

**Gharama za Uwekezaji Katika Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi**

224.Gharama za utafutaji mafuta na gesi hutofautiana kulingana na hatua ambayo imefikiwa na mwekezaji na eneo la utafutaji. Kwa mfano, utafutaji mafuta baharini kwenye maji ya kina kirefu hugharimu fedha nyingi kiasi cha takriban shilingi bilioni 100 kwa kuchimba kisima kimoja ikilinganishwa na utafutaji nchi kavu ambao unagharimu kiasi cha takriban shilingi bilioni 25. Kutokana na ukubwa wa gharama hizo, Serikali inaingia mikataba na wawekezaji ambapo rasilimali inabaki kuwa ni mali ya Taifa. Serikali haina gharama wakati wa utafutaji na mgao hufuatana na mfumo wa ugawanaji (*production sharing*). Hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuhamasisha uwekezaji ni pamoja na uwepo wa Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Mafuta inayosimamia shughuli zote za utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi, Mikataba ya Ugawanaji inayosimamiwa na TPDC kwa niaba ya Serikali na Sera ya Gesi Asilia. Katika kuongeza uwekezaji zaidi, Serikali kwa hivi sasa inatayarisha Sera ya Mafuta, Sera ya Uwezeshaji Wananchi katika miradi ya Mafuta na Sheria ya Gesi Asilia.

**Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi**

225.Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) inatekeleza mradi wa ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asilia katika maeneo ya Madimba wilayani Mtwara Vijijini na Songo Songo Wilayani Kilwa na bomba la kusafirishia gesi hiyo kutoka Mtwara na Songo Songo hadi Dar es salaam kupitia Somanga Fungu. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2014.

226.Mitambo ya kusafisha gesi iliyopo Madimba ina uwezo wa kusafisha gesi kiasi cha futi za ujazo milioni 210 kwa siku na mitambo ya Songo Songo futi za ujazo milioni 140 kwa siku. Bomba la kusafirisha gesi litakuwa na urefu wa

kilomita 542. Katika hali ya kawaida ya uendeshaji, bomba hili litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kusafirisha kiasi cha futi za ujazo milioni 784 kwa siku. Uwezo huu unaweza kuongezeka mpaka futi za ujazo milioni 1,002 kwa siku kwa kufunga mitambo ya kuongeza msukumo wa gesi.

227. Mradi huu utakapokamilika utaunganisha maeneo yanayozalisha gesi asilia hususan Mnazi Bay, Songo Songo, Kiliwani, Mkuranga, Ntorya na gesi iliyogunduliwa katika eneo la bahari ya kina kirefu. Vile vile, bomba litakuwa na matoleo maeneo ya Mtwara, Lindi, Kilwa, Somanga Fungu na Mkuranga kwa ajili ya matumizi ya gesi asilia katika maeneo hayo.

228. Mabomba ya kutosheleza ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam yameshawasili nchini. Kufikia mwezi Machi, 2014, kazi ya kuunganisha mabomba kwa kuchomelea (*welding*) kwenye maeneo ya ujenzi ilikuwa imefikia kilometa 338. Aidha, jumla ya kilomita 203 zilikuwa zimechimbwa kwa ajili ya kuweka bomba (*Trenching*) na kilometa 158 tayari mabomba yalikuwa yamekwishawekwa kwenye njia yake (*Lowering – in*). Kazi ya kuweka mkongo wa mawasiliano sambamba na bomba (*Fiber Optic Cable - FOC*) ilikuwa imefanyika kwa kilometa 155. Zoezi la kufukia bomba pamoja na mkongo wa mawasiliano (*Backfilling*) lilikuwa limefanyika kwa umbali wa kilometa 154. Kazi ya kuyaongezea uzito (*Concrete coating*) mabomba yatakayojengwa baharini na maeneo ya mito ilikwishakamilika. Kazi ya ujenzi wa bomba la baharini lenye urefu wa kilomita 25.6 ilikuwa inaendelea na tayari kilometa 19 zilikwishaunganishwa.

229. Kwa upande wa mitambo ya kusafisha gesi asilia, maandalizi ya eneo la kujenga mitambo ya kusafisha gesi (Madimba na Songo Songo) yameanza. Kazi ya usanifu wa kina wa michoro ya miradi ya kusafisha gesi asilia imekamilika. Mitambo ya kuzalisha umeme, kusafisha maji kwa ajili ya matumizi ya kawaida (*domestic use*) na maji taka (*waste water treatment*) imeshawasili nchini. Kwa sasa kazi inayoendelea ni kukamilisha ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi na ununuzi wa vifaa vya ujenzi kutoka nchi mbalimbali. Zoezi la kusafirisha shehena ya mitambo iliyo tayari kutoka nchi za wazalishaji linaendelea. Vile vile, ujenzi wa kipande cha bomba cha kusafirisha gesi kutoka visimani (*raw gas trunk pipeline*) kwa eneo la Mnazi Bay hadi Madimba unaendelea.

**Mradi wa LNG (*Liquified Natural Gas*)**

230. Sehemu kubwa ya gesi iliyogunduliwa nchini hadi sasa iko baharini kwenye kina kirefu na inafikia kiasi cha futi za ujazo trilioni 38.5. Gesi hiyo imegunduliwa takribani umbali wa kilometa 80 mpaka 100 kutoka nchi kavu na kwenye kina cha urefu wa kati ya mita 1,500 na 3,000. Kutokana na mazingira hayo na wingi wa gesi hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wawekezaji ipo kwenye mchakato wa kuendeleza gesi hiyo kwa ajili ya matumizi ya ndani na pia kwa ajili ya kuuza nje ya nchi kama *Liquified Natural Gas (LNG).*

231. LNG ni gesi asilia iliyopozwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa hadi kufikia kiwango cha nyuzi joto -161 ambapo huwa rahisi kubeba na kusafirisha. Ili nchi iweze kunufaika kiuchumi ikiwa ni pamoja na kusimamia vizuri rasilimali ya gesi katika mradi wa LNG, Serikali imeamua kwamba mtambo wa uchakataji gesi utajengwa na kuwekwa nchi kavu na sio baharini.

232. Mradi wa LNG utakapoanza utakuwa na faida nyingi za kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kutoa ajira kwa watanzania na kuipatia nchi fedha za kigeni kutokana na mauzo ya gesi nje ya nchi. Faida nyingine za kiuchumi ni pamoja na kuiwezesha Serikali kuendeleza sekta ya umeme na viwanda ikiwa ni pamoja na kufanikisha uanzishwaji wa ukanda wa viwanda (*Industrial Park*) kwa ajili ya uwekezaji katika viwanda vya kemikali (*petrochemical*s), saruji, na mbolea. Hadi kufikia Desemba 2013, kampuni ambazo zilionesha nia ya kuwekeza katika mradi wa LNG ni pamoja na BG wakishirikiana na Ophir Energy na Statoil wakishirikiana na Exxon Mobil.

**Ushirikishwaji wa Wananchi Katika Shughuli za Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi**

233. Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) ndilo Shirika lenye dhamana ya kusimamia maslahi ya nchi kwenye shughuli za utafiti. TPDC kama Shirika la taifa, linawakilisha na kusimamia maslahi ya kitaifa katika sekta ya petroli (ambayo ni pamoja na gesi asilia). TPDC hupewa leseni na Serikali na inapaswa kutimiza masharti ya leseni ambayo ni pamoja na kutekeleza mpango kazi unaoidhinishwa pamoja na leseni hiyo. TPDC kwa kumtumia mkandarasi hutekeleza mpango kazi na pia huweza kushiriki kimtaji pale mafuta na gesi vitakapogunduliwa.

234.Katika zabuni za ugawaji vitalu na miradi ya kusambaza gesi, makampuni ya hapa nchini yanapewa vipaumbele maalum ili kuyawezesha kumiliki na kushiriki kikamilifu. Ingawa zabuni iko wazi kwa kampuni za ndani na nje kushiriki, utaratibu umewekwa unaotoa upendeleo kwa kampuni za ndani ikiwa kampuni hizo zitatimiza vigezo vilivyowekwa. Vile vile, ushirikiano wa ubia kati ya kampuni zinazomilikiwa na wazawa na zile za nje utapewa upendeleo ikiwa utatimiza vigezo vilivyowekwa.

235.Mwaka 2013, Serikali iliendelea kuwajengea wananchi uwezo wa kushiriki katika fursa mbalimbali zinahusiana na sekta ikiwa ni pamoja na kushiriki kama waajiriwa kwenye kampuni mbalimbali. Aidha, mikakati iliandaliwa ili kuongeza rasilimali watu ambapo watanzania kadhaa wanasomeshwa katika fani mbalimbali za mafuta na gesi katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Vile vile, makongamano mbalimbali ya kuelimisha umma juu ya fursa zilizopo katika sekta ya mafuta na gesi yanaendelea kufanyika ili kuihabarisha jamii juu ya umuhimu wa rasilimali hiyo na fursa mbalimbali zinazopatikana katika uendelezaji wa rasilimali hii. Kadhalika, mchakato wa maandalizi ya sera maalum ya ushirikishwaji wazawa (*Local Content Policy*) katika shughuli za gesi na mafuta unaendelea. Sera hii, pamoja na mambo mengine inatoa msisitizo kwa kampuni kununua na kutumia bidhaa za hapa nchini.

**Umuhimu na Mchango wa Mafuta na Gesi katika Uchumi**

236.Uwepo wa nishati ya gesi nchini na shughuli zinazohusiana na utafutaji, uchimbaji na usambazaji wa gesi asilia umekuwa na manufaa makubwa kwa Taifa. Manufaa hayo yanajumuisha kupunguza gharama za matumizi ya mafuta, kupunguza uchafuzi wa mazingira, kutoa ajira na kuongeza mapato kwa Serikali kuu na Halmashauri za Wilaya.

237.Uchumi wa Tanzania unakadiriwa kupoteza zaidi ya kiasi cha shilingi trilioni moja na nusu kwa mwaka kwa kutumia mafuta badala ya gesi asilia kwa mitambo ya kufua umeme. Matumizi ya gesi asilia hapa nchini yataokoa fedha hizo ambazo kwa sasa zinalipwa kwa fedha za kigeni. Kwa kutumia gesi asilia ambayo inasafirishwa mpaka Dar es Salaam kutoka Songo Songo na ile inayotumika Mtwara, nchi imeendelea kuokoa fedha za kigeni katika kuzalisha umeme na matumizi ya viwandani. Katika kipindi cha Julai 2004 hadi Desemba 2013, jumla ya futi za ujazo bilioni 196.6 za gesi asilia zenye thamani ya Dola

za Kimarekani milioni 322.4 zilitumika kuzalisha nishati iliyotumika katika uzalishaji umeme. Nishati hiyo kama ingezalishwa kwa kutumia mafuta ingegharimu kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni 6.4. Hii inatokana na utofauti mkubwa kati ya bei ya mafuta na gesi ambapo uzalishaji wa nishati kiasi cha mmBtu moja (1) kwa kutumia gesi asilia hugharimu wastani wa Dola za Kimarekani 1.6 wakati kwa kutumia mafuta hugharimu Dola za Kimarekani 32. Kwa sababu hiyo, kwa matumizi ya gesi asilia katika uzalishaji umeme Serikali imeokoa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 6.1 kutoka gesi ilipoanza kuzalishwa mpaka mwishoni mwa mwaka 2013.

238.Kwa upande wa matumizi ya viwandani, kuanzia Julai 2004 mpaka Desemba 2013, gesi asilia yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 238.8 ilitumika kama nishati mbadala kuendeshea mitambo ya viwanda hivyo. Kuzalisha nishati hiyo kwa kutumia mafuta kwa kipindi hicho chote ingegharimu Dola za Kimarekani milioni 713. Hivyo, kwa matumizi ya gesi asilia viwandani, kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 474.2 kimeokolewa. Vile vile, matumizi ya gesi badala ya mafuta kwenye taasisi, majumbani na katika magari yameokoa fedha za kigeni kwa kiasi kikubwa. Kuanzia Disemba 2009 mpaka Desemba 2013, gesi asilia yenye thamani ya Dola za Kimarekani 819,907 ilitumika kuzalisha nishati kiasi cha mmBtu 37,705 ambapo kama nishati ya mafuta ingetumika ingegharimu kiasi cha Dola za Kimarekani 981,718. Hivyo, katika kipindi husika, Serikali iliweza kuokoa kiasi cha Dola za Kimarekani 161,811 kwa matumizi ya gesi asilia katika taasisi, majumbani na katika magari.

239.Kupitia shughuli za gesi na mafuta, nchi ilipata mapato mbalimbali yakijumuisha mrabaha, kodi za mapato, kodi ya huduma na kodi ya ongezeko la thamani. Kati ya Julai 2004 hadi Desemba 2013, mapato ya Serikali kuu yaliyotokana na mauzo ya gesi ya Songo Songo yalifikia Dola za Kimarekani milioni 232.8 wakati kwa upande wa Mnazi Bay yalikuwa Dola za Kimarekani milioni 6.7. Kati ya hayo, mapato yaliyotokana na kodi ya ongezeko la thamani yalikuwa Dola za Kimarekani milioni 82.4 kwa upande wa Songo Songo na Dola milioni 1.036 kwa upande wa Mnazi Bay. Aidha, halmashauri za wilaya za Lindi na Mtwara vijijini zinapata asilimia 0.3 ya mauzo ya gesi kama kodi ya huduma. Kuanzia mwaka 2004 wakati mradi wa Songo Songo ulipoanza

kuzalisha gesi hadi kufikia mwishoni mwa 2013, halmashauri hizo zilipata zaidi ya shilingi milioni 885.

240.Miradi mbali mbali inayotokana na ugunduzi wa gesi asilia nchini imeajiri na inaendelea kuajiri wananchi wazawa kwa kiasi kikubwa. Serikali kupitia TPDC imeajiri wataalam katika fani tofauti wakiwemo; wanasheria, wahandisi, wachumi na wahasibu na sasa Serikali ina mkakati wa kuajiri watumishi zaidi kulingana na mahitaji. Mbali na ajira za moja kwa moja ambazo Serikali kupitia TPDC imekuwa ikitoa, zipo ajira katika miradi ya kampuni wezeshi katika huduma mbali mbali (*service companies*) zinazohitajika kwenye miradi ya gesi asilia. Mfano, kampuni za ulinzi, usafi pamoja na fursa kwa wafanya biashara wadogo wadogo wa vyakula.

241.Hadi Desemba 2013, kulikuwa na kampuni 18 zinazojishughulisha na utafutaji mafuta na gesi ambapo kila kampuni ina wastani wa kuajiri wafanyakazi 40 wa kudumu na mahitaji huongezeka pale shughuli za utafutaji zinapoongezeka. Pamoja na hayo, zipo kampuni nyingine zinazotoa huduma kwa kampuni za utafutaji ambazo zimeajiri jumla ya watanzania 427. Aidha, baadhi ya kampuni zimekuwa na utaratibu wa kutoa mafunzo ya kiutaalam kwa wafanyakazi wake. Kampuni ya Statoil kama mfano, imekuwa na utaratibu wa kuwapa mafunzo wafanyakazi mara tu baada ya kujiunga na kampuni hiyo na jumla ya wafanyakazi 55 tayari wameshapata mafunzo ya kiutaalam. Mafunzo haya ni muhimu kwa Taifa kwani litaweza kujitegemea kiutaalam hapo baadae. Mradi wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam pia umenufaisha jumla ya wafanyakazi (vibarua) zaidi ya 1,000 kwa siku katika maeneo bomba linapopita.

242.Matumizi ya gesi asilia nchini yamepunguza kwa kiasi kikubwa uchafuzi wa hali ya hewa unaotokana na matumizi ya mafuta katika uzalishaji umeme, viwandani na katika taasisi. Kiasi cha tani milioni 13.4 cha hewa chafu ($CO_2$) huzalishwa katika uzalishaji wa umeme kwa mitambo itumiayo mafuta aina ya *Jet 1* wakati matumizi ya gesi asilia huzalisha tani milioni 10.1 za $CO_2$. Hivyo, matumizi ya gesi asilia yamepunguza uchafuzi wa hewa kwa takriban tani milioni 3.3 za $CO_2$. Kwa upande wa viwandani, matumizi ya mafuta mazito (HFO) huzalisha $CO_2$ kiasi cha tani milioni 3.5 wakati matumizi ya gesi katika viwanda huzalisha tani milioni 2.1 za $CO_2$, hivyo punguzo la hewa chafu ni tani

milioni 1.4. Kuhusiana na matumizi ya LPG kwenye taasisi, $CO_2$ kiasi cha tani 2,215.43 huzalishwa ikilinganishwa na matumizi ya gesi asilia ambapo kiasi cha tani 1,860.35 za $CO_2$ huzalishwa ikiwa ni punguzo la hewa chafu kwa tani 355.08. Hivyo kwa wastani matumizi ya gesi asilia hupunguza hewa chafu kwa zaidi ya asilimia 25 ikilinganishwa na matumizi ya mafuta.

**Changamoto na mikakati iliyowekwa na Serikali kukabiliana nayo**

243. Sekta ya gesi na mafuta inakabiliwa na changamoto mbali mbali katika kutekeleza mipango yake. Changamoto na mikakati ya kukabiliana nazo zimejadiliwa kama ifuatavyo:-

**a. Tishio la Uharamia Baharini na Ziwa Tanganyika (Piracy) kwa meli za Utafutaji**

244. Kufuatia shughuli za utafutaji gesi na mafuta baharini, usalama wa utafutaji mafuta baharini unahatarishwa na kuwepo kwa maharamia wa Kisomali. Ili kukabiliana na changamoto hii, Jeshi likishirikiana na kampuni za utafutaji limejiimarisha zaidi katika kulinda meli za utafutaji.

**b. Tatizo la mpaka kati ya Tanzania na nchi jirani**

245. Upo mgogoro wa mpaka katika Ziwa Nyasa baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Malawi ambapo Serikali ya Malawi imeingia mikataba ya utafutaji mafuta na gesi kwa kugawa vitalu katika ziwa lote. Katika kutafuta muafaka, Serikali ya Malawi imeshauriwa kusitisha utafutaji kwanza mpaka suluhu itakapopatikana.

**c. Kushindwa kufanya kazi za Utafiti kwenye Hifadhi za Taifa**

246. Baadhi ya maeneo ya utafutaji gesi yako ndani ya hifadhi za taifa mfano Hifadhi ya Selous. Licha ya TPDC kuwa na leseni, haijaruhusiwa kutafuta mafuta katika maeneo hayo kwa kuwa yanalindwa na sheria za kimataifa. Wizara ya Maliasili na Utalii ipo kwenye mchakato wa kuandaa kanuni za utafutaji katika maeneo ya hifadhi ili kuiwezesha TPDC kufanya kazi zake inavyotakiwa.

**d. Miamba inayozalisha Gesi Asilia kuwa katika Mipaka ya Nchi mbili**

247. Jiolojia ya miamba haina mipaka kati ya leseni moja na leseni nyingine (ndani ya nchi), pia nchi moja na nchi nyingine mfano; Tanzania na Msumbiji, Tanzania na Malawi, Tanzania na Kenya, Tanzania na DRC. Hivyo ili kukabiliana na changamoto hii, mazungumzo ya uzalishaji wa pamoja (*unitization*) yatafanyika katika maeneo yenye muingiliano wa rasilimali za mafuta au gesi asilia.

**e. Ushiriki wa Nchi na Mtaji mkubwa unaohitajika katika uwekezaji**

248. TPDC inatakiwa iwekeze kwa kushiriki kimtaji katika miradi ya mafuta na gesi ili kuweza kupata faida zaidi lakini inashindwa kuwekeza kwa wakati katika miradi kutokana na ukosefu wa fedha. Katika kukabiliana na changamoto hii, TPDC imeanza kuwekeza kadri inavyopata mapato ya gesi kutoka kwenye mgao wake.

249. Vile vile, TPDC imetengewa maeneo yake ya utafutaji na uchimbaji wa gesi. Vitalu ilivyotengewa ni vya baharini kwenye kina kirefu ambako teknolojia yake ya utafiti na uchimbaji mafuta ni ya gharama kubwa. TPDC inakabiliwa na changamoto ya kupata fedha za kuwekeza katika vitalu hivyo na ili kuikabili changamoto hii, TPDC imejipanga kutafuta wawekezaji wa kuiwezesha kifedha na kitaalam (*Strategic partners*).

**f. Wataalam**

250. Nchi ina uhitaji mkubwa wa wataalam wa miamba wa kuendeleza utafutaji (*geoscientists–geologists, geophysicists, micropals*), wahandisi (*chemical processing, plant, pipeline, civil, production engineers*), wachumi, wanasheria kwa ajili ya mazungumzo ya mikataba, wahasibu na wakaguzi kwa ajili ya uhakiki wa gharama za utafutaji na uzalishaji na utunzaji wa taarifa (*Data Management*). Katika kuikabili changamoto hii, Serikali imeajiri wafanyakazi wenye fani mbali mbali, na ipo kwenye mchakato wa kuendelea kuajiri wataalam zaidi kulingana na mahitaji. Vile vile, Serikali inatekeleza mpango mkakati wa kuongeza wataalam wa mafuta na gesi kwa kusomesha watanzania zaidi ya 200 kwa kipindi cha miaka mitatu (2013 - 2015).

**g. Kujenga uwezo wa TPDC katika kusimamia mikataba ya PSA**

251. TPDC ina jukumu la kusimamia mikataba ya PSA *(Production Sharing Agreement)* kwa niaba ya Serikali lakini ina upungufu wa wataalam na vitendea kazi. Ili kuongeza uwezo wa kusimamia mikataba hiyo, TPDC inatarajia kuajiri wataalam wa kutosha ili kuiwezesha kusimamia vizuri mikataba hiyo, kuongeza vitendea kazi pamoja na kusomesha watumishi ili waweze kumudu kazi hizo kwa ufasaha.

**h. Uelewa wa Watanzania na matarajio ya wananchi**

252. Ugunduzi wa gesi umeibua mitazamo mbalimbali na kuamsha matarajio makubwa kwa wananchi (*public expectations*). Miundombinu ya miradi ya gesi huchukua kipindi kirefu kati ya miaka mitano mpaka saba toka kugunduliwa mpaka kuweza kutumika na hivyo kuibua mitazamo hasi kuhusu miradi hiyo. Katika kuikabili changamoto hii, Serikali imeandaa vipindi vya elimu kwa umma ambavyo vinaendelea kuelimisha wananchi kuhusiana na masuala ya gesi asilia.

**Matarajio**

253. Serikali imeweka vipaumbele na matarajio yake kama ifuatavyo:

a. Kuhakikisha kwamba gesi inayozalishwa hapa nchini inatumiwa kwa matumizi ya ndani kama vile kuzalisha umeme na inayobaki inauzwa nje kwa kukamilisha miundombinu ya kusafisha na kusafirisha gesi asilia itakayohudumia mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Miundombinu hii inatarajiwa kuanza kazi mwanzoni mwa mwaka 2015.

b. Kuhamasisha kuanzishwa kwa viwanda kama vya mbolea na shughuli zitakazoongezea thamani ya gesi asilia inayozalishwa hapa nchini. Kwa sasa mpango mkakati wa matumizi ya gesi asilia unatayarishwa ambapo mpango huo utaibua miradi mbalimbali ya matumizi ya ndani.

c. Kuongeza ushiriki wa wananchi katika mlolongo wa shughuli za gesi na mafuta. Hii ni kwa kuhakikisha kwamba wananchi wanawezeshwa kupitia Sera ya Ushiriki wa Wananchi katika Gesi na Mafuta (*Local Content Policy in Oil and Gas*) inayoandaliwa.

d. Kuongeza wataalam wazawa ambapo vyuo mbalimbali hapa nchini vimeanza na vingine vitaanza kutoa mafunzo kuhusiana na sekta hii.

Vyuo vikuu na vyuo vya ufundi ambavyo vimeanza kufundisha kozi hizo vinajumuisha Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Tumaini, Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, Chuo cha VETA-Mtwara na Chuo cha Madini Dodoma.

e. Kuvutia uwekezaji zaidi ambapo Serikali imeanza kugawa vitalu kwa zabuni katika maeneo ya baharini kwenye kina kirefu ambapo Zabuni ya Awamu ya Nne imetangazwa. Kampuni mbalimbali za Kimataifa zimejitokeza na zinaendelea kujitokeza kununua zabuni hizi. Kabla ya utangazaji wa zabuni hizi, mazingira ya kuhamasisha wawekezaji yalifanywa ikiwa ni pamoja na kupitishwa kwa Sera ya Gesi na marekebisho kwenye mwongozo wa mikataba ya ugawanaji (*Model Production Sharing Agreement-MPSA*).

# SEHEMU YA NNE

# MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI

# SURA YA 11

# KILIMO NA USHIRIKA

**Kiwango cha Ukuaji**

254.Mwaka 2013, shughuli za kiuchumi za kilimo zilikua kwa asilimia 4.3 kama ilivyokuwa mwaka 2012. Aidha, shughuli ndogo za kiuchumi za mazao; mifugo; na misitu na uwindaji zilikua kwa asilimia 4.5, 3.8 na 3.3 mwaka 2013 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.7, 3.1 na 2.4 mwaka 2012, kwa mtiririko huo. Kwa upande mwingine, shughuli za kilimo zilichangia asilimia 24.5 ya Pato la Taifa mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 24.7 mwaka 2012.

**Uzalishaji wa Mazao ya Chakula**

255.Mwaka 2013, uzalishaji wa mazao ya chakula hususan mahindi, mchele, mihogo, ndizi na viazi vitamu na mviringo uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2012. Kuongezeka kwa uzalishaji kulitokana na hali nzuri ya hewa katika baadhi ya maeneo yanayolima mazao hayo. Hata hivyo, uzalishaji wa ngano, mtama/ulezi, na maharage na mikunde mingine ulipungua mwaka 2013 ikilinganishwa na uzalishaji katika mwaka 2012. Uzalishaji wa mazao hayo ulipungua kutokana na kutokuwepo kwa mvua za kutosha katika baadhi ya mikoa inayolima mazao hayo. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya chakula ni kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 11.1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula (Tani 000)**

| Zao | 2011 | 2012 | 2013 | Badiliko (%) 2012/13 |
|---|---:|---:|---:|---:|
| Mahindi | 4,341 | 5,104 | 5,174 | 1.4 |
| Mchele | 1,461 | 1,170 | 1,307 | 11.7 |
| Ngano | 113 | 109 | 92 | -16.0 |
| Mtama na Ulezi | 1,119 | 1,052 | 1,041 | - 1.1 |
| Muhogo | 1,549 | 1,821 | 1,943 | 6.7 |
| Maharage na Mikunde mingine | 1,632 | 1,827 | 1,641 | - 10.2 |
| Ndizi | 1,048 | 842 | 1,307 | 55.1 |
| Viazi vitamu na mviringo | 1,710 | 1,418 | 1,879 | 32.6 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika

**Uzalishaji wa Mazao ya Biashara**

256. Mwaka 2013, uzalishaji wa tumbaku, sukari na mkonge uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2012. Ongezeko la uzalishaji wa tumbaku lilitokana na matumizi mazuri ya mbolea. Aidha, ongezeko la uzalishaji wa sukari lilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa miwa kwa wakulima wadogo na kwa mashamba ya kiwanda cha sukari cha Kagera na kuongezeka kwa uwezo wa uzalishaji katika kiwanda cha sukari cha Kilombero. Vile vile, kuongezeka kwa mkonge kulitokana na kuongezeka kwa bei na mahitaji yake katika soko la dunia pamoja na ushiriki wa wakulima wadogo.

257. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa pareto, pamba, kahawa, na korosho ulipungua mwaka 2013 ikilinganishwa na mwaka 2012. Kupungua kwa uzalishaji wa pamba kulitokana na kushuka kwa bei ya pamba katika msimu uliotangulia, kutopatikana kwa wakati na matumizi yasiyo sahihi ya viuwadudu. Aidha, kupungua kwa uzalishaji wa kahawa kulitokana na kuwepo kwa hali mbaya ya hewa katika kanda za uzalishaji wa kahawa. Vile vile, kupungua kwa uzalishaji wa korosho kulitokana na kutopatikana kwa mvua ya kutosha katika maeneo makuu ya uzalishaji.

**Jedwali Na. 11.2: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (Tani).**

| Zao | 2009 | 2010 | 2011 | 2012r | 2013p | Badiliko (%) 2012/13 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Pamba | 267,004 | 163,644 | 225,938 | 350,277 | 241,198 | 58.01 |
| Tumbaku | 60,900 | 130,000 | 126,624 | 74,240 | 85,877 | (5.23) |
| Sukari | 279,850 | 263,461 | 260,055 | 262,878 | 296,679 | 10.12 |
| Chai | 33,160 | 31,646 | 33,000 | 32,308 | 32,422 | (0.91) |
| Pareto | 3,320 | 5,000 | 5,700 | 6,100 | 4,100 | 7.02 |
| Kahawa | 40,000 | 60,575 | 33,219 | 71,200 | 48,000 | 97.34 |
| Mkonge | 26,363 | 24,091 | 33,406 | 35,580 | 37,368 | (30.12) |
| Korosho | 74,169 | 121,070 | 160,000 | 127,947 | 126,000 | (23.94) |

Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika

P - Matarajio; r- Zimerekebishwa

**Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta**

258. Mwaka 2013, uzalishaji wa mazao ya mafuta yakiwemo alizeti, karanga, ufuta na mawese uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2012. Ongezeko hilo

lilitokana na: Hali nzuri ya hewa katika maeneo yanayozalisha kwa wingi mazao hayo; jitihada za serikali za kuhakikisha upatikanaji wa ruzuku ya mbegu bora kwa wakulima; na Kuendelea kupanuka kwa wigo wa soko la mazao ya mafuta. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya mafuta ni kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 11.3: Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta (Tani)**

| Zao | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | Badiliko (%) 2012/13 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Alizeti | 162,019 | 348,877 | 786,902 | 1,125,000 | 2,625,000 | 133.3 |
| Karanga | 256,401 | 320,582 | 651,397 | 810,000 | 1,425,000 | 75.9 |
| Ufuta | 72,932 | 65,557 | 357,162 | 456,000 | 1,050,000 | 130.3 |
| Mawese | | 17,000 | 17,000 | 24,880 | 40,500 | 62.8 |
| Soya | 3,900 | 4,300 | 2,500 | 3,490 | 5830 | 67.0 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika

**Uwekezaji katika Shughuli za Kiuchumi za Kilimo**

259.Mwaka 2013, idadi ya matrekta makubwa yaliyoingizwa na sekta binafsi iliongezeka na kufikia matreka 916 ikilinganishwa na matrekta 782 mwaka 2012. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa fursa ya kupata mikopo ya kununua matrekta hayo kutoka Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, Benki ya Rasilimali Tanzania na benki nyingine. Vile vile, jumla ya matrekta madogo ya mkono 828 yaliingizwa nchini ikilinganishwa na matrekta madogo 949 yaliyoingizwa nchini mwaka 2012.

**Kilimo cha Umwagiliaji**

260. Mwaka 2013, eneo lenye jumla ya hekta 30,000 za umwagiliaji lilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu na kufanya eneo lililofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu kufikia hekta 473,254 kutoka hekta 443,254 mwaka 2012. Aidha, jumla ya hekta 365,811 za umwagiliaji ziliendelezwa ikilinganishwa na hekta 363,514 zilizoendelezwa mwaka 2012.

261.Mwaka 2013, uzalishaji na tija kutokana na umwagiliaji wa mazao ya mpunga, nyanya, mahindi na vitunguu uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2012. Uzalishaji wa zao la mpunga kutokana na umwagiliaji uliongezeka na kufikia tani 5.5 kutoka tani 2 kwa hekta mwaka 2012; mahindi tani 5 kwa hekta kutoka tani 4; na vitunguu tani 26 kutoka 20 kwa hekta. Aidha, uzalishaji na tija

katika zao la nyanya ulifikia tani 18 mwaka 2013. Ongezeko hili lilitokana na uboreshwaji wa miundombinu ya umwagiliaji na matumizi ya pembejeo kwenye maeneo yenye miundombinu. Vile vile, jumla ya vikundi vya umwagiliaji vilivyoundwa na kusajiliwa vilifikia 352 mwaka 2013 kutoka jumla ya vikundi 306 mwaka 2012. Vikundi hivi viliundwa na kusajiliwa ili kuhakikisha skimu za umwagiliaji zinakuwa endelevu. Aidha, mwaka 2013, jumla ya wakulima 1,910 na wataalam 335 wa ngazi mbalimbali walipatiwa mafunzo ya kuendeleza teknolojia sahihi za umwagiliaji na matumizi bora ya maji kwa umwagiliaji ikilinganishwa na wakulima 715 na wataalam 37 waliopatiwa mafunzo mwaka 2012.

**Huduma za Ugani na Mafunzo**

262.Mwaka 2013, jumla ya wakulima 20,518 na maafisa ugani 258 walishiriki katika mafunzo mbalimbali kuhusu teknolojia bora. Kati ya wakulima walioshiriki, wanaume walikuwa 14,277 na wanawake 6,241; na kwa upande wa maafisa ugani, wanaume walikuwa 189 na wanawake walikuwa 69. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu uzalishaji wa mbegu bora za mpunga, kanuni za kilimo bora, usindikaji, mnyororo wa thamani, upatikanaji wa masoko, matumizi ya simu za mkononi katika kupata taarifa za kilimo, mikopo na masuala ya uendelezaji wa vikundi. Vile vile, jumla ya mashamba darasa 13,023 yalianzishwa kuhusu mbinu za kilimo bora kwa mazao mbalimbali yanayolimwa nchini. Jumla ya wakulima 260,168 walishiriki kwenye mashamba darasa hayo ambapo wanawake walikuwa 106,488 na wanaume 153,680.

263.Mwaka 2013, jumla ya wakulima 120 na mabwana shamba 17 katika Halmashauri za Bunda na Ukerewe walipatiwa mafunzo ya kuanzisha na kusimamia mashamba darasa ya zao la muhogo. Aidha, mafunzo kuhusu kilimo bora, masoko na usindikaji wa mpunga yalitolewa kwa maafisa ugani 40 na wakulima wawezeshaji 10 kutoka skimu za umwagiliaji 20 nchini. Vile vile, vijana 300 kutoka wilaya za Sengerema, Bunda, Mvomero, Kilosa, Kyela na Mbarali walipatiwa mafunzo kuhusu uanzishwaji wa mashamba darasa ya mpunga. Aidha, mafunzo haya yalitolewa kwa mabwana shamba 42 kutoka Halmashauri za Mikoa ya Lindi, Mtwara na Morogoro. Sambamba na hilo, Serikali ilitoa mafunzo kwa maafisa ugani 14 na wakulima 84 toka skimu 14 kwenye Mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Ruvuma, Iringa, Morogoro, Manyara na Pwani ili kueneza matumizi sahihi ya mashine ya kupandikiza, kuvunia na kusindika mpunga.

**Shughuli za Utafiti**

264.Mwaka 2013, aina ya mbegu mpya 27 za mazao ziliidhinishwa kwa matumizi ya wakulima ikilinganishwa na mbegu 11 zilizoidhinishwa mwaka 2012. Kati ya mbegu zilizoidhinishwa mwaka 2013, saba zilikuwa za mahindi, nne za njugu mawe, nne za viazi vitamu, nne za tumbaku, nne za kahawa, mbili za soya, na mbili za mtama.

**Mfuko wa Pembejeo**

265.Mwaka 2013, mikopo 12 ya matrekta madogo ya mikono ilitolewa ikilinganishwa na mikopo minne mwaka 2012. Vile vile, jumla ya mikopo 81 ya matrekta makubwa ilitolewa ikilinganishwa na mikopo 115 mwaka 2012. Aidha, jumla ya mikopo 25 ilitolewa kwa ajili ya pembejeo za kilimo na mifugo ikilinganishwa na mikopo 23 iliyotolewa mwaka 2012 ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.7. Vile vile, mkopo mmoja ulitolewa kwa ajili ya zana za umwagiliaji maji ikilinganishwa na mikopo mitatu mwaka 2012 na mikopo miwili ya mitambo ya kuvunia ilitolewa katika mwaka 2013.

## MIFUGO

**Kiwango cha Ukuaji na Mchango Katika Ukuaji**

266.Mwaka 2013, shughuli ndogo za kiuchumi za mifugo zilikua kwa kiwango cha asilimia 3.8 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2012. Hali hii ilitokana na maeneo mengi ya ufugaji kupata mvua za wastani hivyo kusababisha kuwepo kwa maji na malisho bora kwa ajili ya mifugo na kuongezeka kwa thamani ya mifugo na bidhaa zake. Aidha, sekta hii ndogo ya mifugo ilichangia asilimia 4.4 katika Pato la Taifa mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2013.

**Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake**

267.Mwaka 2013, idadi ya mifugo nchini ilikadiriwa kufikia ng’ombe milioni 24.3, mbuzi milioni 16.3 na kondoo milioni 8.1 na nguruwe milioni 2.4 ikilinganishwa na ng’ombe milioni 22.8, mbuzi milioni 15.6 na kondoo milioni 7.0 na nguruwe milioni 2.01 . Aidha, idadi ya kuku ilikadiriwa kuwa milioni 66, ambapo kuku wa asili walikuwa milioni 36.5 na kuku wa kisasa milioni 29.5 ikilinganishwa na kuku wa asili milioni 35.5 na wa kisasa milioni 24.5 mwaka 2012.

268. Mwaka 2013, uzalishaji wa maziwa uliongezeka kwa asilimia 3.6 hadi lita bilioni 1.92 kutoka lita bilioni 1.85 mwaka 2012. Kati ya kiasi hicho, lita milioni 624 zilitokana na ng'ombe wa kisasa na lita bilioni 1.3 ng'ombe wa asili. Ongezeko la uzalishaji wa maziwa lilitokana na: kuongezeka kwa ukusanyaji wa maziwa kutoka kwenye kundi la ng'ombe wa asili; juhudi za uboreshaji wa kosaafu kwenye ng'ombe wa asili kupitia madume ya kisasa na uhamilishaji; na uboreshwaji wa vifaa vya kuhifadhia maziwa. Aidha, jumla ya dozi 168,000 za mbegu bora zilizalishwa kutoka kwenye Kituo cha Taifa cha uhamilishaji (NAIC) ambapo jumla ya ng'ombe 98,340 walihamilishwa ikilinganishwa na ng'ombe 81,300 waliohamilishwa mwaka 2012.

269. Mwaka 2013, usindikaji wa maziwa uliongezeka na kufikia lita 135,300 kwa siku sawa na ongezeko la asilimia 3.8 ikilinganishwa na lita 130,400 kwa siku mwaka 2012. Ongezeko hilo lilitokana kuongezeka kwa ukusanyaji na usindikaji katika viwanda vya Tanga fresh, Mara milk na Tan dairies.

270. Mwaka 2013, uzalishaji wa mayai uliongezeka na kufikia mayai bilioni 3.7 kutoka mayai bilioni 3.5 mwaka 2012. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ulaji wa mayai maeneo ya mijini na mayai ya kutotolesha vifaranga katika mashamba makubwa na ya kati.

**Jedwali Na. 11.4: Uzalishaji wa Mazao Yatokanayo na Mifugo**

| Aina ya Zao | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Uzalishaji Maziwa ('000' lita)** | | | | | | |
| Ng'ombe wa Asili | 980,000 | 1,012,436 | 997,261 | 1,135,422 | 1,255,938 | 1,297,775 |
| Ng'ombe wa Kisasa | 520,000 | 591,690 | 652,596 | 608,800 | 597,161 | 623,865 |
| Jumla | 1,500,000 | 1,604,126 | 1,649,857 | 1,738,683 | 1,853,099 | 1,921,640 |
| **Uzalishaji wa Nyama (Tani)** | | | | | | |
| N'gombe | 218,976 | 225,178 | 243,943 | 262,606 | 289,835 | 299,581 |
| Mbuzi/Kondoo | 81,173 | 82,884 | 86,634 | 103,709 | 111,106 | 115,652 |
| Nguruwe | 33,307 | 36,000 | 38,180 | 43,647 | 47,246 | 50,814 |
| Kuku | 77,250 | 78,168 | 80,916 | 93,534 | 84,524 | 87,408 |
| Jumla | 410,706 | 422,230 | 449,673 | 503,496 | 532,711 | 553,455 |
| **Uzalishaji Mayai ('000')** | | | | | | |
| Mayai | 2,690,000 | 2,806,350 | 2,917,875 | 3,339,566 | 3,494,584 | 3,725,200 |

Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

271.Mwaka 2013, ulaji wa mazao ya mifugo nchini kwa wastani ulikuwa kilo 12 za nyama, lita 45 za maziwa na mayai 75 kwa mtu kwa mwaka. Ulaji huu ni mdogo, ikilinganishwa na viwango vilivyopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO, 2011) vya kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka. Hivyo, Serikali inaendelea na juhudi za uhamasishaji ulaji wa mazao ya mifugo kupitia Wiki ya Maziwa na Unywaji wa Maziwa Mashuleni ambazo hufanyika mwezi Juni kila mwaka.

**Biashara ya Mifugo na Mazao Yake**

272.Mwaka 2013, idadi ya ng’ombe 1,215,541, mbuzi 960,199 na kondoo 209,292 wenye thamani ya shilingi bilioni 989.3 waliuzwa minadani ikilinganishwa na ng’ombe 1,105,037, mbuzi 872,908 na kondoo 190,265 wenye thamani ya shilingi bilioni 951.2 waliouzwa mwaka 2012. Vile vile, tani 126.2 za nyama ya ng’ombe, tani 66.78 za nyama ya mbuzi na tani 88.4 za nyama ya kondoo zenye thamani ya shilingi bilioni 28.8 ziliuzwa nje ya nchi mwaka 2013.

273.Mwaka 2013, jumla ya vipande milioni 2.9 vya ngozi za ng’ombe, milioni 3.4 vya mbuzi na vya kondoo 700,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 34.7 vilikusanywa ikilinganishwa na vipande milioni 2.8 vya ngozi za ng’ombe, milioni 2.7 vya mbuzi na 650,000 vya kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni 33 vilivyokusanywa katika mwaka 2012.

274.Mwaka 2013, usindikaji wa ngozi uliongezeka hadi vipande vya ngozi za ng’ombe 1,181,060, vya mbuzi na kondoo 2,582,525 vyenye thamani ya shilingi bilioni 63.6 kutoka vipande vya ngozi za ng’ombe 782,447, mbuzi 1,535,562 na kondoo 61,200 vyenye thamani ya shilingi bilioni 10.6 vilivyosindikwa mwaka 2012. Kuongezeka kwa usindikaji wa ngozi kulitokana na kuongezeka kwa ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi.

**Jedwali Na. 11.5: Ukusanyaji na Uuzaji wa Ngozi Ndani na Nje ya Nchi**

| A. UKUSANYAJI WA NGOZI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Ngozi za Ng'ombe** | **Ngozi za Mbuzi** | **Ngozi za Kondoo** | **Thamani Tshs.'000** |
| 2002 | 1,400,000 | 700,000 | 350,000 | 4,500,000 |
| 2003 | 1,400,000 | 800,000 | 460,000 | 5,500,000 |
| 2004 | 1,600,000 | 1,200,000 | 650,000 | 6,500,000 |
| 2005 | 1,600,000 | 1,500,000 | 750,160 | 5,500,000 |
| 2006 | 1,660,000 | 1,400,000 | 950,000 | 6,800,000 |
| 2007 | 1,980,000 | 1,520,000 | 1,200,000 | 8,700,000 |
| 2008 | 2,500,000 | 1,900,000 | 1,500,000 | 13,500,000 |
| 2009 | 1,650,000 | 2,990,000 | 1,250,000 | 10,900,000 |
| 2010 | 1,500,000 | 2,400,000 | 650,000 | 8,500,000 |
| 2011 | 2,500,000 | 2,400,000 | 200,000 | 16,100,000 |
| 2012 | 2,800,000 | 3,400,000 | 650,000 | 32,988,000 |
| 2013 | 2,900,000 | 3,600,000 | 700,000 | 34,673,500 |
| **B. UUZAJI NGOZI NJE** | | | | |
| **Mwaka** | **Ngozi za Ng'ombe** | **Ngozi za Mbuzi** | **Ngozi za Kondoo** | **Thamani Tshs.'000** |
| 2002 | 1,200,000 | 511,700 | 165,000 | 4,000,000 |
| 2003 | 1,300,000 | 600,000 | 300,000 | 4,600,000 |
| 2004 | 1,774,000 | 1,431,000 | 488,000 | 5,712,000 |
| 2005 | 1,400,000 | 1,200,000 | 597,155 | 4,025,400 |
| 2006 | 1,363,721 | 1,216,740 | 861,770 | 7,500,000 |
| 2007 | 1,700,000 | 1,055,000 | 925,530 | 16,200,000 |
| 2008 | 2,300,000 | 1,600,000 | 1,100,000 | 21,500,000 |
| 2009 | 982,668 | 2,700,000 | 769,936 | 12,800,000 |
| 2010 | 739,315 | 1,912,182 | 176,400 | 8,191,803 |
| 2011 | 1,719,506 | 2,111,176 | 83,600 | 17,400,000 |
| 2012 | 2,000,000 | 2,900,000 | 578,000 | 17,500,000 |
| 2013 | 1,269,060 | 2,582,525 | 522,500 | 63,600,000 |

Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

**Maendeleo ya Ushirika**

275.Mwaka 2013, Serikali ilichukua hatua madhubuti za kukabiliana na changamoto za ushirika nchini. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa vyama, ambapo mafunzo yalitolewa kwa Maafisa Ushirika 45 na kufanya ukaguzi katika Vyama vya Ushirika vya Msingi 252 na Vyama Vikuu Vitatu vya Singida, Tabora na Ruvuma. Aidha, Serikali imetunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6 ya mwaka 2013 ambayo imeanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Sheria hiyo imeainisha majukumu ya Tume hiyo ikiwa ni pamoja na usimamizi na udhibiti wa shughuli za Vyama vya Ushirika. Sheria mpya ya ushirika ilianza kutumika tarehe 1 Januari, 2014.

276.Mwaka 2013, Serikali ilifanya tathmini ya hali ya vyama vya ushirika na kubaini uwepo wa vyama vya ushirika mfu 360 ambavyo vilikuwa havitekelezi majukumu yao kwa mujibu wa sheria. Vyama hivyo vimefutwa katika Daftari la Usajili ili kubakiza vyama vinavyokidhi matakwa ya sheria. Hii ilifanya vyama vya ushirika kupungua kutoka 9,964 mwaka 2012 hadi 9,604 mwaka 2013. Aidha, idadi ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ilipungua kufikia 5,478 mwaka 2013 kutoka vyama 5,559 mwaka 2012. Vile vile, idadi ya wanachama ilipungua kufikia 935,121 mwaka 2013 kutoka 1,153,248 mwaka 2012.

**UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI**

Jedwali Na. 35

| Msimu[1] | Miwa | | | | Sukari | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wakulima | | | | | iliyotumika[3] | |
| | Umma (000 Tani) | Binafsi (000 Tani) | Jumla (000 Tani) | Bei[2] (Sh./Tani) | Iliyozalishwa Tani | Jumla Tani | Kilo kwa kila mtu[4] |
| 1977/78 | 1008 | 116 | 1124 | 96.20 | 132979 | 111546 | 6.69 |
| 1978/79 | 1169 | 197 | 1366 | 96.20 | 114267 | 127712 | 7.42 |
| 1979/80 | 1180 | 210 | 1390 | 101.20 | 122530 | 112282 | 6.34 |
| 1980/81 | 854 | 193 | 1047 | 106.20 | 114667 | 115961 | 6.37 |
| 1981/82 | 1135 | 203 | 1338 | 137.30 | 124326 | 120629 | 6.44 |
| 1982/83 | 1090 | 113 | 1203 | 170.00 | 101996 | 93179 | 4.84 |
| 1983/84 | 1372 | 160 | 1532 | 238.00 | 131525 | 108369 | 5.48 |
| 1984/85 | 1148 | 105 | 1253 | 323.70 | 108102 | 111433 | 5.48 |
| 1985/86 | 1003 | 104 | 1107 | 352.30 | 100287 | 95379 | 4.56 |
| 1986/87 | 991 | 72 | 1063 | 463.00 | 94815 | 109462 | 5.09 |
| 1987/88 | 997 | 102 | 1099 | 600.00 | 101266 | 96271 | 4.35 |
| 1988/89 | 787 | 91 | 878 | 750.00 | 96227 | 126771 | 5.29 |
| 1989/90 | 963 | 98 | 1061 | 1748.45 | 111236 | 190750 | 5.47 |
| 1990/91 | 1068 | 116 | 1184 | 2525.90 | 118560 | 212585 | 5.93 |
| 1991/92 | 967 | 114 | 1081 | 3476.85 | 108480 | 202478 | 6.07 |
| 1992/93 | 1098 | 273 | 1371 | 5267.67 | 121414 | 204126 | 6.11 |
| 1993/94 | 1105 | 362 | 1467 | 6200.00 | 123949 | 139829 | 5.38 |
| 1994/95 | 914 | 370 | 1284 | 8600.00 | 104624 | 238424 | 5.38 |
| 1995/96 | 997 | 372 | 1369 | 8900.00 | 116810 | 268910 | .. |
| 1996/97 | 951 | 347 | 1298 | 9500.00 | 116100 | 275700 | 5.54 |
| 1997/98 | 808 | 176 | 984 | 10500.00 | 116100 | 271790 | 5.70 |
| 1998/99 | 948 | 320 | 1268 | 12500.00 | 113622 | 101272 | 5.87 |
| 1999/00 | 907 | 341 | 1248 | 12500.00 | 116927 | 100127 | 6.70 |
| 2000/01 | 1050 | 284 | 1334 | 14000.00 | 135534 | 122534 | 10.00 |
| 2001/02 | 1134 | 389 | 1523 | 14700.00 | 164498 | 142398 | 10.10 |
| 2002/03 | 1402 | 411 | 1813 | 15000.00 | 190120 | 167300 | 10.42 |
| 2003/04 | 1672 | 670 | 2342 | 16800.00 | 223839 | 290711 | 10.90 |
| 2004/05 | 1594 | 752 | 2346 | 20568.00 | 229617 | 328005 | 10.90 |
| 2005/06 | 1545 | 956 | 2501 | 22383.00 | 263317 | 343292 | 12.00 |
| 2006/07 | 1430 | 611 | 2041 | 29000.00 | 192095 | 366708 | 12.00 |
| 2007/08 | 1967 | 799 | 2766 | 32767.00 | 265434 | 382518 | 13.00 |
| 2008/09 | 2056 | 693 | 2749 | 32770.51 | 279850 | 396113 | 13.40 |
| 2009/10 | 1972 | 598 | 2570 | 42046.00 | 263461 | 398070 | 13.68 |
| 2010/11 | 2357 | 661 | 3019 | 43865.00 | 304135 | 410259 | 12.00 |
| 2011/12 | 2036 | 680 | 2717 | 48833.00 | 262879 | 439307 | 12.00 |
| 2012/13 | 2242 | 711 | 2956 | 52167.00 | 296698 | 468000 | 12.00 |
| Badiliko (%) | | | | | | | |
| 11/12-12/13 | 0.10 | 0.05 | 0.09 | 0.07 | 0.13 | 0.07 | 0.00 |
| Ongezeko (%) | | | | | | | |
| 77/78-12/13 | 1.22 | 5.13 | 1.63 | 541.28 | 1.23 | 3.20 | 0.79 |

Chanzo: Bodi ya Sukari Tanzania

1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni

2 Bei ya Mimea ni ile iliyo na asilimia 10 za Sucrose

3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar

4 Ni kwa Tanzania bara

* Sukari yote huzalishwa na wakulima/mashirika binafsi

## PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 36

| Msimu [1] | Pamba yenye mbegu | | | | | Pamba iliyoondolewa mbegu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uzalishaji Kiasi (tani) | | | Bei ya wastani (Shs/Kilo) | | Kiasi (tani) | | | Mauzo nchini | | |
| | | | | | | | | | Kiasi (tani) | Bei ya wastani (Shs/tani) | |
| | AR | BR | Jumla | AR | BR | AR | BR | Jumla | Jumla [2] | AR | BR |
| 1976/77 | 176894 | 17800 | 194694 | 2.00 | 1.00 | 61549 | 6074 | 67623 | 8146 | 9487 | 7230 |
| 1977/78 | 153292 | 14790 | 168082 | 2.30 | 1.15 | 46555 | 5821 | 52376 | 14422 | 12186 | 9370 |
| 1978/79 | 152267 | 14248 | 166515 | 2.40 | 1.20 | 51072 | 4696 | 55768 | 14253 | 12340 | 8810 |
| 1979/80 | 162087 | 18367 | 180454 | 3.00 | 1.30 | 52546 | 3931 | 56477 | 17284 | 13750 | 11040 |
| 1980/81 | 166233 | 8344 | 174577 | 3.20 | 1.50 | 54189 | 2962 | 57151 | 15634 | 13750 | 11040 |
| 1981/82 | 126799 | 6127 | 132926 | 3.70 | 1.70 | 42439 | 2153 | 44592 | 14070 | 15480 | 11730 |
| 1982/83 | 124559 | 3351 | 127910 | 4.70 | 2.50 | 40521 | 2381 | 42902 | 12660 | 15420 | 11730 |
| 1983/84 | 136151 | 4647 | 140798 | 6.00 | 3.70 | 41779 | 2175 | 43954 | 11771 | 15867 | 12038 |
| 1984/85 | 152355 | 4490 | 156845 | 8.40 | 4.50 | 50858 | 1154 | 52012 | 16236 | 26000 | 17400 |
| 1985/86 | 97384 | 8515 | 105899 | 13.00 | 7.00 | 29715 | 17775 | 47490 | 13247 | 52250 | 37350 |
| 1986/87 | 210454 | 4115 | 214569 | 16.90 | 9.10 | 55108 | 2338 | 57446 | 11389 | 52250 | 37350 |
| 1987/88 | 252177 | 2738 | 254915 | 19.45 | 9.10 | 67057 | 659 | 67716 | 13247 | 81350 | 67250 |
| 1988/89 | 184524 | 4720 | 189244 | 22.35 | 10.00 | 61552 | 1880 | 63432 | 11084 | 175000 | 140000 |
| 1989/90 | 112333 | 572 | 112905 | 28.00 | 11.00 | 37652 | 192 | 37844 | 13184 | 225000 | 190000 |
| 1990/91 | 148124 | 1017 | 149141 | 41.00 | 14.00 | 48880 | 341 | 49221 | 300000 | 300000 | 240000 |
| 1991/92 | 26841 | 32 | 26873 | 70.00 | 28.00 | 90706 | 11 | 90717 | 14301 | 325000 | 255000 |
| 1992/93 | 281984 | 22000 | 303984 | 60.00 | 28.00 | 85784 | .. | 85784 | 4405 | 542916 | .. |
| 1993/94 | 125434 | .. | 125434 | 120.00 | .. | 42695 | .. | 42695 | .. | .. | .. |
| 1994/95 | 125434 | .. | 125434 | 120.00 | .. | 42695 | .. | 42695 | .. | .. | .. |
| 1995/96 | 221148 | .. | 221148 | 207.00 | .. | 84782 | .. | 84782 | .. | .. | .. |
| 1996/97 | 251751 | 74 | 251751 | 170.00 | .. | 85162 | 25 | 85187 | .. | .. | .. |
| 1997/98 | 202217 | .. | 202217 | 180.00 | .. | 67780 | .. | 67780 | .. | .. | .. |
| 1998/99 | 105853 | .. | 105853 | 185.00 | .. | 35480 | .. | 35480 | .. | .. | .. |
| 1999/00 | 100500 | .. | 100500 | 123.00 | .. | 33686 | .. | 33686 | .. | .. | .. |
| 2000/01 | 123558 | .. | 123558 | 180.00 | .. | 41415 | .. | 41415 | .. | .. | .. |
| 2001/02 | 148180 | .. | 148180 | 165.00 | .. | 49668 | .. | 49415 | .. | .. | .. |
| 2002/03 | 187908 | 781 | 188689 | 180.00 | 50 | 62983 | 262 | 63245 | .. | .. | .. |
| 2003/04 | 139756 | 213 | 139969 | 280.00 | 100 | 46843 | 72 | 46915 | .. | .. | .. |
| 2004/05 | 341589 | .. | 341589 | 250.00 | 0 | 114496 | .. | 114496 | .. | .. | .. |
| 2005/06 | 376591 | .. | 376591 | 220.00 | 0 | 126228 | .. | 126228 | .. | .. | .. |
| 2006/07 | 130585 | .. | 130585 | 350.00 | 0 | 43770 | .. | 43770 | .. | .. | .. |
| 2007/08 | 200662 | - | 200662 | 450 | | 70773 | - | 70773 | 37488 | .. | .. |
| 2008/09 | 368697 | 0 | 368697 | 480 | 0 | 123582 | 0 | 123582 | 66554 | .. | .. |
| 2009/10 | 267644 | 0 | 267644 | 480 | 0 | 54851 | 0 | 54851 | .. | .. | .. |
| 2010/11 | 163518 | 0 | 163518 | 900.00 | 0 | 54809 | 0 | 54809 | .. | .. | .. |
| 2011/12 | 225938 | .. | 225938 | 1000.00 | .. | 75731 | .. | 75731 | .. | .. | .. |
| 2012/13 | 351156 | .. | 351156 | 660.00 | .. | 117702 | .. | 117702 | - | - | - |
| Badiliko (%) 2011/12-2012/13 | 0.55 | | 0.55 | -0.34 | | 0.55 | | 0.55 | | | |
| Ongezeko (%) 77/78-12/13 | 0.99 | | 0.80 | 329.00 | | 0.91 | | 0.74 | -1.00 | -1.00 | -1.00 |

Chanzo: Bodi ya Mauzo ya Pamba

[1] Msimu ni kati ya Juni na Mei

[2] Ni jumla ya AR na BR

.. Takwimu hazikupatikana

## ENEO LILILOPANDWA MICHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA

Jedwali Na. 37

| Msimu [1] | Eneo lililopandwa (hekta): mashamba | | | Majani Mabichi yaliyopatikana (tani) | | | | | | Bei kwa mkulima (Shs/Kilo) | Mauzo[2] Nchini (tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Kiumilikaji: mashamba | | | Kikanda: mashamba | | | | |
| | Makubwa | Madogo | Jumla | Makubwa | Madogo | Jumla | Kaskazini | Kusini | Jumla | | |
| 1976/77 | 9023 | 9217 | 18240 | 59300 | 13679 | 72979 | 27841 | 45138 | 72979 | 0.90 | 2994 |
| 1977/78 | 9214 | 9334 | 18548 | 65933 | 22598 | 88531 | 32784 | 55747 | 88531 | 1.50 | 4168 |
| 1978/79 | 9268 | 9280 | 18548 | 60062 | 24230 | 84292 | 27177 | 57115 | 842292 | 1.50 | 3735 |
| 1979/80 | 9268 | 9289 | 18557 | 61294 | 21780 | 83074 | 27249 | 55825 | 83074 | 1.50 | 4376 |
| 1980/81 | 9268 | 9289 | 18557 | 59603 | 18800 | 78403 | 25267 | 53136 | 78403 | 1.50 | 5487 |
| 1981/82 | 9268 | 9289 | 18557 | 59603 | 18800 | 78403 | 25267 | 53136 | 78403 | 1.50 | 5487 |
| 1982/83 | 9268 | 9365 | 18633 | 56023 | 18540 | 74563 | 22622 | 51941 | 74563 | 1.50 | 6735 |
| 1983/84 | 9699 | 9177 | 18876 | 65309 | 18931 | 84240 | 22869 | 61371 | 84240 | 2.80 | 3763 |
| 1984/85 | 9699 | 9177 | 18876 | 51443 | 21493 | 72936 | 18346 | 54590 | 72936 | 2.80 | 4286 |
| 1985/86 | 9699 | 9177 | 18876 | 55680 | 21550 | 77230 | 22369 | 54861 | 77230 | 4.10 | 4714 |
| 1986/87 | 9699 | 9177 | 18876 | 52271 | 19201 | 71472 | 17564 | 53908 | 71472 | 4.90 | 6346 |
| 1987/88 | 9699 | 9177 | 18876 | 46752 | 17942 | 64694 | 12333 | 52361 | 64694 | 7.60 | 4556 |
| 1988/89 | 9699 | 9177 | 18876 | 45771 | 17851 | 63622 | 12749 | 50883 | 63632 | 9.90 | 4260 |
| 1989/90 | 9699 | 9177 | 18876 | 52194 | 18874 | 71068 | 18099 | 52969 | 71068 | 13.40 | 3559 |
| 1990/91 | 9699 | 9177 | 18876 | 70442 | 22434 | 92876 | 23531 | 69345 | 92876 | 17.00 | 3491 |
| 1991/92 | 9699 | 9177 | 18876 | 62994 | 20229 | 83223 | 19296 | 63927 | 83223 | 28.00 | 2750 |
| 1992/93 | 9699 | 9197 | 18896 | 80896 | 19934 | 100830 | 32218 | 68412 | 100630 | 45.00 | 3278 |
| 1993/94 | 10029 | 9197 | 19226 | 81159 | 21231 | 102390 | 32148 | 70242 | 102390 | 45.00 | 11124 |
| 1994/95 | 10149 | 9197 | 19346 | 93608 | 22641 | 116249 | 36825 | 79424 | 116249 | 50.00 | .. |
| 1995/96 | 10652 | 9332 | 19984 | 79968 | 13803 | 93771 | 25935 | 67836 | 93771 | 55.00 | 2350 |
| 1996/97 | 11113 | 9451 | 20564 | 83126 | 7803 | 90929 | 21992 | 68937 | 93771 | 55.00 | .. |
| 1997/98 | 11416 | 9451 | 20867 | 113448 | 7100 | 120548 | 30137 | 90411 | 120548 | 55.00 | .. |
| 1998/99 | 11416 | 9451 | 20867 | 98800 | 7000 | 105800 | 26450 | 79350 | 150800 | 55.00 | .. |
| 1999/00 | .. | .. | .. | 99848 | 6092 | 105940 | 24439 | 81502 | 105941 | 55.00 | .. |
| 2000/01 | 10811 | 10364 | 21175 | 109007 | 9728 | 118735 | 29419 | 89316 | 118735 | 65.00 | 2386 |
| 2001/02 | 10811 | 10364 | 21175 | 97297 | 13999 | 111296 | 22794 | 88502 | 111296 | 80.00 | 2683 |
| 2002/03 | 11097 | 9762 | 20889 | 100677 | 31718 | 132395 | 28679 | 103716 | 132395 | 85.00 | 3158 |
| 2003/04 | 11485 | 10801 | 22286 | 95986 | 31993 | 127979 | 26384 | 101595 | 127979 | 86.00 | 3225 |
| 2004/05 | 11271 | 11442 | 22713 | 94172 | 39246 | 133418 | 20649 | 112769 | 133418 | 86.00 | 4004 |
| 2005/06 | 11310 | 10977 | 22287 | 91337 | 31881 | 123218 | 29046 | 94172 | 123218 | 93.00 | 3881 |
| 2006/07 | 11271 | 11956 | 23227 | 109632 | 49024 | 158656 | 39673 | 118983 | 158656 | 100.00 | 4737 |
| 2007/08 | 11272 | 11449 | 22722 | 97310 | 51160 | 148470 | 33456 | 115015 | 148471 | 111.00 | 4253 |
| 2008/09 | 11271 | 11449 | 22722 | 100644 | 41167 | 141811 | 31677 | 110134 | 141811 | 118.00 | 4464 |
| 2009/10 | 11272 | 11449 | 22722 | 106021 | 44716 | 150737 | 33309 | 117428 | 150737 | 124.00 | 5084 |
| 2010/11 | 11272 | 11449 | 22722 | 95511 | 47616 | 143127 | 112368 | 30759 | 143127 | 152.00 | 6065 |
| 2011/12 | 11272 | 11449 | 22722 | 88582 | 52359 | 140941 | 27009 | 113932 | 140941 | 200.00 | 4839 |
| 2012/13 | 11272 | 11449 | 22722 | 113628 | 54872 | 168500 | 30997 | 137503 | 168500 | 206.00 | 5498 |
| Badiliko (%) | | | | | | | | | | | |
| 2011/12-2012/1 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.28 | 0.05 | 0.20 | 0.15 | 0.21 | 0.20 | 0.03 | 0.14 |
| Ongezeko (%) | | | | | | | | | | | |
| 76/77-2012/13 | 0.25 | 0.24 | 0.25 | 0.92 | 3.01 | 1.31 | 0.11 | 2.05 | 1.31 | 227.89 | 0.84 |

Chanzo: Bodi ya Chai Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Chai iliyotengenezwa

.. Takwimu hazikupatikana

## KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

**Jedwali Na. 38**

| Msimu[1] | Iliyonunuliwa (Tani) | | | | Bei (Sh./kilo) | | | Mauzo nchini[+] | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ARABICA | | ROBUSTA | JUMLA | ARABICA | | ROBUSTA | KIASI | THAMANI |
| | Laini | Ngumu | | | Laini | Ngumu | Maganda | (Tani) | (shs'000) |
| 1976/77 | 35263 | 2424 | 10995 | 48682 | 15.00 | 11.00 | 8.90 | 1625 | 9516 |
| 1977/78 | 38222 | 2851 | 12023 | 53096 | 10.89 | 17.50 | 5.27 | 758 | 6300 |
| 1978/79 | 33853 | 2551 | 12946 | 49350 | 9.07 | 14.16 | 4.64 | 587 | 8232 |
| 1979/80 | 30850 | 2968 | 14216 | 48034 | 11.42 | 13.32 | 5.55 | 336 | 5541 |
| 1980/81 | 52301 | 3223 | 11237 | 66761 | 12.36 | 10.50 | 4.50 | 687 | 7012 |
| 1981/82 | 36090 | 3753 | 10947 | 50790 | 14.90 | 10.50 | 5.93 | 997 | 13072 |
| 1982/83 | 38852 | 2216 | 12728 | 53796 | 15.17 | 10.55 | 10.55 | 1020 | 20170 |
| 1983/84 | 36436 | 1729 | 11509 | 49674 | 22.87 | 16.35 | 16.35 | 1730 | 25716 |
| 1984/85 | 36270 | 1974 | 10836 | 49080 | 29.68 | 15.07 | 15.07 | 895 | 36418 |
| 1985/86 | 41042 | 2820 | 11285 | 55147 | 45.80 | 20.90 | 20.90 | 1408 | 94117 |
| 1986/87 | 39060 | 2702 | 16975 | 58737 | 50.75 | 29.00 | 29.00 | 1146 | 96626 |
| 1987/88 | 32804 | 2514 | 10389 | 45707 | 66.00 | 37.70 | 37.00 | 1122 | 120638 |
| 1988/89 | 41230 | 2280 | 11620 | 55130 | 90.00 | 51.00 | 51.00 | 1220 | 229322 |
| 1989/90 | 34945 | 1702 | 16427 | 53074 | 165.00 | 66.50 | 55.00 | 783 | 144998 |
| 1990/91 | 31304 | 1416 | 11403 | 44123 | 165.00 | 66.50 | 60.50 | 783 | 151088 |
| 1991/92 | 37065 | 1926 | 8996 | 47987 | 230.00 | 100.00 | 70.00 | 1140 | 2558.76 |
| 1992/93 | 36901 | 2128 | 12217 | 51246 | 316.00 | 123.00 | 100.00 | 765 | 128200 |
| 1993/94 | 26361 | 2448 | 7577 | 36386 | 923.00 | 904.00 | 700.30 | .. | .. |
| 1994/95 | 27137 | 1542 | 7157 | 35836 | 1965.00 | 1481.10 | 1453.60 | .. | .. |
| 1995/96 | 35142 | 2096 | 9710 | 46948 | 1229.30 | 1301.60 | 1169.00 | .. | .. |
| 1996/97 | 32933 | 1279 | 9279 | 43491 | .. | .. | .. | .. | .. |
| 1997/98 | 19789 | 1894 | 9165 | 30848 | .. | .. | .. | .. | .. |
| 1998/99 | 23605 | 2590 | 13523 | 39718 | 1936.00 | 1064.00 | 1040.00 | .. | .. |
| 1999/00 | 18171 | 3593 | 1078 | 32842 | 1486.60 | 1894.80 | 476.47 | .. | .. |
| 2000/01 | 37176 | 3805 | 17007 | 57988 | .. | .. | .. | .. | .. |
| 2001/02 | 38000 | 3500 | 12000 | 53500 | .. | .. | .. | .. | .. |
| 2002/03 | 37294 | 4766 | 34368 | 76428 | .. | .. | .. | .. | .. |
| 2003/04 | 20716 | 1850 | 16138 | 38704 | 1800.00 | 1200.00 | 600.00 | 38704 | 46670 |
| 2004/05 | 23870 | 888 | 9133 | 33891 | 2593.50 | 1976.00 | 1235.00 | 33891 | 62566 |
| 2005/06 | 24116 | 1362 | 8856 | 34334 | 1200.00 | 420.00 | 270.00 | 33300 | 79304246 |
| 2006/07 | 33345 | 2417 | 19076 | 54838 | 2840.00 | 1796.00 | 1616.00 | 548 | 1298675 |
| 2007/08 | 26330 | 1588 | 15606 | 43524 | 2995.00 | 1875.00 | 1734.00 | 43523 | 89,099 |
| 2008/09 | 37207 | 1727 | 29643 | 68577 | 2887.00 | 2172.00 | 1836.00 | 68577 | 165615552 |
| 2009/10 | 22217 | 915 | 11467 | 34599 | 3988.00 | 2475.00 | 1563.00 | 34599 | 108741091 |
| 2010/11 | 30309 | 2013 | 24348 | 56670 | 4500.00 | 1300.00 | 1200.00 | 56670 | 264143599 |
| 2011/12 | 20775 | 941 | 11590 | 33306 | 8144.37 | 5436.40 | 3276.93 | 33306 | 212,292,594 |
| 2012/13 | 33204 | 1655 | 36150 | 71009 | 4850.00 | 3600.00 | 3200.00 | 71009 | 281781798 |
| Badiliko (%) | | | | | | | | | |
| 2011/12-12/13 | 0.60 | 0.76 | 2.12 | 1.13 | -0.40 | -0.34 | -0.02 | 1.13 | 0.33 |
| Ongezeko (%) | | | | | | | | | |
| 1976/77-12/13 | -0.1 | -0.3 | 2.3 | 0.5 | 322.3 | 326.3 | 358.6 | 42.7 | 29610.4 |

Chanzo: Bodi ya Kahawa Tanzania

+ Kahawa iliyosafishwa
1 Msimu ni kati ya Julai na Juni
2 Ni ya muda
.. Takwimu hazikupatikana

## ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA

**Jedwali Na. 39**

| Msimu[1] | Eneo (Hekta) | | | Katani iliyopatikana | | Mauzo nchini[+] | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uliokomaa | Usiokomaa | Jumla | Kiasi (tani) | Bei kwa Mkulima (shs/tani) | Kiasi (tani) | Thamani (Sh. milioni) |
| 1977/78 | 11626 | 38626 | 150252 | 91873 | 2474 | 25104 | 57.7 |
| 1978/79 | 107371 | 32589 | 139960 | 81384 | 2549 | 32023 | 95.6 |
| 1979/80 | 106866 | 26024 | 132890 | 85978 | 3135 | 35730 | 125.4 |
| 1980/81 | 99771 | 21642 | 121413 | 73753 | 3749 | 19687 | 68.0 |
| 1981/82 | 82257 | 17998 | 100255 | 60635 | 3784 | 30851 | 117.4 |
| 1982/83 | 85314 | 15720 | 101034 | 46187 | 4797 | 22384 | 94.9 |
| 1983/84 | 69799 | 13121 | 82920 | 38255 | 6410 | 12573 | 70.0 |
| 1984/85 | 62307 | 11796 | 74103 | 32247 | 7213 | 13075 | 88.3 |
| 1985/86 | 67606 | 13606 | 81212 | 30151 | 16099 | 19842 | 200.0 |
| 1986/87 | 67606 | 13606 | 81212 | 33170 | 19472 | 16477 | 407.0 |
| 1987/88 | 32932 | 20866 | 53798 | 33268 | 38750 | 20635 | 862.0 |
| 1988/89 | 47651 | 30584 | 78235 | 32265 | 64604 | 22661 | 1464.0 |
| 1989/90 | 48826 | 33780 | 82606 | 33743 | 94003 | 25563 | 2403.0 |
| 1990/91 | 49374 | 36240 | 85614 | 36001 | 89633 | 10398 | 932.0 |
| 1991/92 | 49374 | 36240 | 85614 | 24309 | 89203 | 17644 | 1582.2 |
| 1992/93 | 49374 | 36240 | 85614 | 21221 | 107079 | 18067 | 1517.6 |
| 1993/94 | 54485 | 24608 | 79093 | 29002 | 163540 | 17694 | 4031.0 |
| 1994/95 | 52953 | 25757 | 78710 | 24716 | 216026 | 18206 | 2629.0 |
| 1995/96 | 52018 | 27153 | 79171 | 28902 | 370807 | 18719 | 2549.0 |
| 1996/97 | 50459 | 28507 | 78967 | 25022 | .. | 18606 | 3374.0 |
| 1997/98 | 48745 | 29997 | 78742 | 22180 | .. | 18819 | .. |
| 1998/99 | 151869 | 33997 | 185666 | 23229 | .. | 6712 | 2146.0 |
| 1999/00 | 34645 | 7942 | 42587 | 41084 | .. | 16033 | 5617.8 |
| 2000/01 | 34645 | 11473 | 46118 | 23542 | 368077 | 7569 | 2786.0 |
| 2001/02 | 34645 | 11473 | 46118 | 23641 | 337732 | 4947 | 1671.0 |
| 2002/03 | 39462 | 10611 | 50073 | 23280 | 450000 | 6300 | 2835.0 |
| 2003/04 | 29493 | 12204 | 41697 | 26758 | 540000 | 6370 | 4027.0 |
| 2004/05 | 45079 | 14500 | 59579 | 27794 | 617342 | 8213 | 5070.0 |
| 2005/06 | 26384 | 13264 | 39649 | 30934 | 810000 | 10767 | 8613.0 |
| 2006/07 | 28273 | 13608 | 41882 | 33327 | 975000 | 11010 | 10152.0 |
| 2007/08 | 28577 | 15622 | 44199 | 34057 | 1000000 | 16997 | 15800.0 |
| 2008/09 | 35751 | 18023 | 53774 | 25996 | 1000000 | 11496 | 10100.0 |
| 2009/10 | 30556 | 11849 | 42405 | 24092 | 1200000 | 12761 | 10375.0 |
| 2010/11 | 31117 | 12169 | 43286 | 25090 | 1300000 | 11617 | 13154.0 |
| 2011/12 | 32601 | 14302 | 46902 | 36600 | 1500000 | 11511 | 14390.0 |
| 2012/13 | 33649 | 11994 | 45642 | 34874 | 1600 | 11466 | 16823.0 |
| Badiliko (%) 2011/12-12/13 | 3.2% | -16.1% | -2.7% | -4.7% | -99.9% | -0.4% | 16.9% |
| Ongezeko (%) 1977/78- 12/13 | 189.43% | -68.95% | -69.62% | -62.04% | -35.33% | -54.33% | 29055.98% |

Chanzo: Bodi ya Katani

\+ Katani aina ya Line fibre, Tow na Flume Tow

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

.. Takwimu hazikupatikana

## TUMBAKU ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

**Jedwali Na. 40**

| 2011 | 37,723,299.9 | 234,007,537,236.7 | 176,797,682.0 | 5,866,464,635.4 |
| 2012 | 41,291,250.6 | 254,612,571,950.4 | 163,114,349.4 | 6,812,426,813.1 |
| 2013p | 38,573,600.0 | 234,884,628,920.0 | 147,659,778.6 | 6,117,769,193.7 |
| **JUMLA** | **747,467,229.9** | **3,509,780,682,411.1** | **2,981,987,621.8** | **98,874,861,805.0** |

p: Takwimu za awali

Chanzo: Idara ya Uvuvi

### MWELEKEO WA MAUZO YA SANGARA NJE YA NCHI -1996-2013

Jedwali 51B

| Mwaka | Uzito | Thamani | | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| | Kg | T.sh | US $ | T.sh |
| 1996 | 20,296,124.4 | 19,338,404,278.7 | 52,277,681.3 | 1,185,728,961.9 |
| 1997 | 23,075,904.6 | 33,125,889,871.5 | 54,821,414.1 | 1,987,549,609.2 |
| 1998 | 36,386,241.0 | 43,258,023,811.9 | 65,727,795.0 | 2,595,481,431.8 |
| 1999 | 23,757,461.9 | 37,554,505,909.0 | 51,992,752.5 | 2,257,832,543.0 |
| 2000 | 30,831,841.0 | 36,401,237,005.8 | 45,903,212.8 | 2,184,070,656.4 |
| *2001 | 39,038,599.7 | 74,928,607,542.3 | 86,178,585.7 | 4,685,276,229.2 |
| *2002 | 29,479,322.7 | 83,005,557,292.2 | 88,231,655.1 | 4,980,333,437.5 |
| *2003 | 37,286,859.2 | 114,779,736,803.6 | 112,049,948.5 | 6,707,948,378.0 |
| 2004 | 30,312,898.3 | 82,356,866,789.0 | 76,261,406.4 | 5,171,324,343.0 |
| 2005 | 53,675,473.7 | 148,785,948,008.6 | 129,184,492.6 | 8,419,301,970.4 |
| 2006 | 39,472,977.7 | 156,160,190,326.6 | 126,829,665.7 | 5,491,786,878.8 |
| 2007 | 50,078,575.6 | 195,242,463,549.7 | 158,422,058.5 | 6,660,034,977.0 |
| 2008 | 38,721,422.2 | 180,366,779,818.2 | 153,740,732.3 | 5,412,912,979.2 |
| 2009 | 29,308,384.0 | 168,672,111,452.0 | 130,877,948.3 | 4,640,564,903.5 |
| 2010 | 27,229,470.7 | 194,012,069,313.9 | 139,666,995.1 | 4,509,670,993.8 |
| 2011 | 25,426,157.2 | 197,899,741,508.3 | 127,601,694.3 | 4,299,987,312.2 |
| 2012 | 28,951,094.7 | 220,149,518,645.6 | 141,189,161.6 | 4,967,311,025.1 |
| 2013p | 26,568,404.8 | 187,105,608,213.9 | 117,789,932.4 | 4,624,958,074.3 |
| **JUMLA** | **589,897,213.3** | **2,173,143,260,140.7** | **1,858,747,132.2** | **80,782,074,704.3** |

Chanzo: Idara ya Uvuvi

p: Takwimu za awali

## MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII 2006-2013

Jedwali 52

| Maelezo | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watalii | 644124 | 719031 | 770376 | 714367 | 782699 | 867994 | 1077058 | 1135884 |
| Idadi ya watalii hotelini | 592160 | 673722 | 723569 | 665000 | 719097 | 753818 | 974448 | 1075884 |
| Mapato ( US $ million) | 950 | 1198.76 | 1288.69 | 1159.82 | 1254.5 | 1324.8 | 1712.75 | 1806.3 |
| Wastani wa siku za kukaa watalii hotelini | 12 | 12 | 12 | 11 | 11 | 10 | 10 | 11 |
| Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa | 1551 | 2841 | 2091 | 2311 | 3281 | 3551 | 3841 | 3861 |
| siku(US $) | 1112 | 1322 | 1862 | 1942 | 2362 | 2472 | 2302 | 2352 |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Utalii

**IDADI YA WATALII WALIOINGIA NCHINI NA KIASI CHA FEDHA ZILIZOPATIKANA**

Jedwali Na. 53

| Mwaka | Idadi ya Watalii | Ongezeko kwa Mwaka (%) | Mapato (US $) Milioni | Ongezeko kwa Mwaka (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1995 | 293834 | 12.3 | 258.1 | 34.4 |
| 1996 | 326192 | 11.0 | 322.0 | 24.7 |
| 1997 | 360000 | 10.4 | 392.4 | 21.9 |
| 1998 | 482331 | 34.0 | 570.0 | 45.3 |
| 1999 | 628188 | 30.2 | 733.3 | 28.6 |
| 2000 | 501668 | -20.1 | 739.1 | 0.8 |
| 2001 | 525122 | 4.7 | 725.0 | -1.9 |
| 2002 | 575000 | 9.5 | 730.0 | 0.7 |
| 2003 | 576000 | 0.2 | 731.0 | 0.1 |
| 2004 | 582000 | 1.0 | 746.1 | 2.1 |
| 2005 | 612754 | 5.3 | 823.1 | 10.3 |
| 2006 | 644124 | 5.1 | 950.0 | 15.4 |
| 2007 | 719031 | 11.6 | 1198.0 | 26.1 |
| 2008 | 770376 | 7.1 | 1288.7 | 7.6 |
| 2009 | 714367 | -7.3 | 1159.8 | -10.0 |
| 2010 | 782699 | 9.6 | 1254.5 | 8.2 |
| 2011 | 867994 | 10.9 | 1324.8 | 5.6 |
| 2012 | 1077058 | 24.1 | 1372.8 | 3.6 |
| 2013 | 1135884 | 5.5 | 1806.3 | 31.6 |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

**IDADI YA WAGENI WALIOTEMBELEA VITUO VYA UTALII**

Jedwali Na. 55

| | 2008 | | 2009 | | 2010 | | 2011 | | 2012 | | 2013 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jina la Hifadhi** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** |
| ARUSHA | 39778 | 43484 | 40268 | 9235 | 34308 | 30162 | 33427 | 33922 | 28185 | 28898 | 30706 | 41224 |
| GOMBE | 1096 | 325 | 1202 | 432 | 1166 | 1001 | 1247 | 539 | 1056 | 327 | 996 | 775 |
| KATAVI | 3161 | 2250 | 1882 | 292 | 1484 | 1330 | 1631 | 1213 | 1465 | 1192 | 1703 | 2572 |
| KILIMANJARO | 155275 | 6954 | 41879 | 1183 | 50193 | 3545 | 54472 | 3231 | 42813 | 3019 | 50319 | 2935 |
| KITULO | 117 | 413 | 366 | 187 | 151 | 158 | 197 | 129 | 98 | 78 | 99 | 334 |
| LAKE MANYARA | 112687 | 46477 | 118565 | 16361 | 112982 | 48288 | 127428 | 51698 | 107991 | 47650 | 123502 | 64271 |
| MAHALE | 2888 | 191 | 810 | 58 | 865 | 44 | 995 | 75 | 806 | 24 | 1056 | 38 |
| MIKUMI | 21038 | 17629 | 25282 | 10616 | 18936 | 22872 | 20385 | 22937 | 17976 | 20253 | 15750 | 30138 |
| MKOMAZI | 433 | 552 | 647 | 263 | 566 | 572 | 472 | 516 | 556 | 533 | 550 | 1256 |
| RUAHA | 21832 | 12355 | 14125 | 3118 | 12623 | 8797 | 13846 | 9722 | 11004 | 7665 | 12616 | 9150 |
| RUBONDO | 721 | 490 | 472 | 153 | 501 | 381 | 506 | 472 | 525 | 461 | 450 | 458 |
| SAADANI | 2482 | 2293 | 2755 | 1335 | 2127 | 4442 | 2983 | 7681 | 2140 | 4644 | 3378 | 11331 |
| SERENGETI | 225606 | 218375 | 202537 | 58841 | 228644 | 69369 | 177730 | 169823 | 148278 | 309745 | 179282 | 273203 |
| TARANGIRE | 95760 | 43883 | 77739 | 10018 | 85778 | 34752 | 16591 | 47795 | 80821 | 37016 | 107567 | 58382 |
| UDZUNGWA | 2837 | 1731 | 3163 | 1395 | 2945 | 2707 | 3303 | 4034 | 2873 | 2536 | 3147 | 3984 |
| SAANANE | | | | | | | 194 | 4398 | 113 | 3383 | 163 | 4987 |
| **Jumla** | **685711** | **397402** | **531692** | **113487** | **553269** | **228420** | **455407** | **358185** | **446700** | **467424** | **531284** | **505038** |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii - Hifadhi za Taifa (TANAPA)

**WAGENI WALIOTEMBELEA VITUO VYA MAKUMBUSHO**

Jedwali Na.55A

| VITUO | 2003/04 | 2004/05 | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13[P] |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Amboni | 6457 | 5501 | 7595 | 4771 | 426 | 7782 | 10580 | 5392 | 9745 | 19413 |
| Tongoni | 0 | 98 | 382 | 306 | 60 | 511 | 598 | 362 | 108 | 871 |
| Isimila | 2480 | 1883 | 3579 | 2424 | 3307 | 0 | 2465 | 405 | 523 | 4158 |
| Kalenga | 670 | 635 | 1341 | 1112 | 1353 | 0 | 1026 | 793 | 423 | 4355 |
| Ngome Kongwe Bagamoyo | 0 | 0 | 0 | 368 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 214346 |
| Mbozi Kimondo | 9662 | 0 | 0 | 256 | 38 | | 733 | 836 | 4220 | 1907 |
| Kaole | 2158 | 3827 | 11907 | 18575 | 12938 | 10616 | 24529 | 14181 | 35348 | 35100 |
| Caravan Serai | 1369 | 0 | 5246 | 10793 | 1713 | 6328 | 14810 | 2983 | 4154 | 0 |
| Kunduchi | 0 | 0 | 139 | 325 | 164 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Engaruka | 53 | 340 | 265 | 730 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kilwa Kisiwani | 546 | 0 | 0 | 1439 | 425 | 538 | 2504 | 1285 | 2400 | 2679 |
| Kolo Kondoa | 253 | 561 | 0 | 419 | 64 | 0 | 437 | 420 | | 892 |
| Olduvai | 53235 | 35645 | 66239 | 57861 | 71553 | 85051 | 57467 | 44347 | 99534 | 52615 |
| Kwihara | 288 | 0 | 0 | 393 | 0 | 0 | 2403 | 2403 | 102 | 1288 |
| Makumbusho ya Mwl Nyerere | 684 | 1039 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ujiji | 1238 | 2569 | 1834 | 2812 | 803 | 2318 | 687 | 474 | 8432 | 4811 |
| **Jumla** | **79093** | **52098** | **98527** | **102584** | **92844** | **113144** | **118239** | **73881** | **164989** | **342435** |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

# SURA YA 13

## MADINI

### Kiwango cha Ukuaji

303. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe kwa mwaka 2013 kilikuwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2012. Hii ilitokana na kuwepo kwa ongezeko dogo la uzalishaji kufuatia kufungwa kwa migodi ya dhahabu ya Tulawaka na Resolute. Aidha, mchango wa shughuli za uchimbaji madini na mawe katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2012.

### Utafutaji Madini

304. Mwaka 2013, leseni 9,072 za utafutaji na uchimbaji wa madini mbalimbali zilitolewa ikilinganishwa na leseni 4810 zilizotolewa Mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 88.6. Kati ya hizo, leseni 736 zilikuwa za utafutaji, leseni 26 zilikuwa za uchimbaji mkubwa na wa kati, na leseni 8,310 zilikuwa za uchimbaji mdogo wa madini. Aidha, leseni 388 za biashara ya madini zilitolewa kwa watanzania.

### Uendelezaji wa Uchimbaji Mdogo wa Madini

305. Uendelezaji wa uchimbaji mdogo wa madini unalenga kubadili uchimbaji mdogo kuwa wa kisasa na kuweza kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Mwaka 2013, Serikali ilitenga maeneo tisa kwa ajili ya uchimbaji mdogo yenye ukubwa wa hekta 104,794.08. Aidha, Serikali imebainisha maeneo mengine matano ambayo yatatengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini. Maeneo hayo yapo Geita (2), Chunya (1), Kigoma (1) na Mtwara (1).

**Jedwali Na. 13.1: Maeneo Yaliyotengwa kwa Uchimbaji Mdogo katika mwaka 2013**

| Mahali | Wilaya | Ukubwa wa eneo (Hekta) |
|---|---|---|
| Dete-Mwalazi | Morogoro | 8,505.34 |
| Ilagala | Uvinza | 58,997.92 |
| Langweni (Mwanadilatu) | Mkuranga | 8,886.48 |
| Mbesa | Tunduru | 15,605.30 |
| Mihama | Misungwi | 4.19 |
| Mpambaa | Singida | 8,332.66 |
| Nyankunguru | Tarime | 49.18 |
| Vianzi (Mindevu) | Mkuranga | 600.01 |
| Winza | Mpwapwa | 3,813.00 |
| **Jumla** | | **104,794.08** |

Chanzo: Wizara ya Nishati na Madini

306. Mwaka 2013, jumla ya tani 5,474,775.40 za madini ya ujenzi, shaba na jasi zilizalishwa na wachimbaji wadogo zikiwa na thamani ya jumla ya shilingi milioni 56,510.1. Kutokana na uzalishaji huo, Serikali ilipata mrabaha wa shilingi milioni 1,707.1.

**Jedwali Na. 13.2: Uzalishaji na Mauzo ya Madini katika Migodi Midogo**

| Aina ya Madini | Uzito (Tani) | Thamani (TZS) | Mrabaha (TZS) |
|---|---|---|---|
| Ujenzi | 5,435,704.40 | 52,469,399,837.00 | 1,585,816,588.04 |
| Shaba | 208.00 | 104,000,000.00 | 121,251,000.00 |
| Jasi | 38,863.00 | 3,936,700,000.00 | |
| **Jumla** | **5,474,775.40** | **56,510,099,837.00** | **1,707,067,588.04** |

Chanzo: Wizara ya Nishati na Madini

**Uchimbaji na Uuzaji Madini**

**Almasi**

307. Mwaka 2013, uzalishaji wa almasi uliongezeka kwa asilimia 41.3 kufikia karati 179,633.21 kutoka karati 127,174.03 zilizozalishwa mwaka 2012. Ongezeko hili lilitokana na kukamilika kwa ukarabati wa mitambo ya uzalishaji katika migodi ya Williamson Diamond Limited na El- Hillal. Aidha, thamani ya mauzo ya almasi nje ya nchi ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 46.01 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 33.80 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 36.1. Ongezeko hili lilitokana na kuimarika kwa bei ya almasi katika soko la dunia na kuongezeka kwa kiasi cha almasi kilichouzwa nje.

**Dhahabu**

308. Mwaka 2013, uzalishaji wa dhahabu ulikuwa kilo 42,534.19 ikilinganishwa na kilo 39,012.14 zilizozalishwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 9.0. Aidha, thamani ya mauzo ya dhahabu nje ya nchi ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 1,735.8 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 2,161.5 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 19.7. Hii ilitokana na kupungua kwa kiasi cha dhahabu iliyouzwa nje na kushuka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia. Wastani wa bei ya dhahabu katika soko la dunia ilishuka kutoka Dola za Kimarekani 1,668.6 kwa wakia moja mwaka 2012 hadi kufikia wastani wa Dola za Kimarekani 1411.6 kwa wakia moja mwaka 2013.

**Vito vya thamani**

309. Mwaka 2013, jumla ya kilo 1,692,436 za vito vya thamani zilizalishwa ikilinganishwa na kilo 1,237,625.59 zilizozalishwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 36.8. Aidha, mauzo ya vito vya thamani nje yalikuwa Dola za Kimarekani milioni 62.5 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 32.6 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 91.7. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa kiasi kilichozalishwa na kuimarika kwa bei ya vito vya thamani katika soko dunia. Vile vile, katika jitihada za kukuza masoko ya vito vya thamani, Serikali iliandaa maonesho ya mnada wa madini ya vito jijini Arusha na kuhudhuriwa na watanzania 180 na wanunuzi wakubwa kutoka nje ya nchi.

**Madini Mengine**

310. Mwaka 2013, chumvi iliyozalishwa ilikuwa tani 36,031.67 ikilinganishwa na tani 34,016.57 zilizozalishwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Aidha, uzalishaji wa "Kaolin" ulipungua kwa asilimia 63.8 kutoka tani 1,421.58 mwaka 2012 hadi kufikia tani 906.97 mwaka 2013. Upungufu huu ulitokana na kusimama kwa uzalishaji katika baadhi ya maeneo yaliyokuwa ya hifadhi. Uzalishaji wa madini ya chokaa ulikuwa tani 3,552,880 ikilinganishwa na tani 1,224,475.09 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 190.6. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya chokaa hususan soko la ndani katika uzalishaji wa saruji.

**Thamani ya Mauzo ya Madini**

311. Mwaka 2013, thamani ya mauzo ya madini nje ilikuwa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 1,824.08 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 2,266.88 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 19.5. Upungufu huu ulitokana na kushuka kwa thamani ya mauzo ya dhahabu katika soko la dunia ambayo huchangia zaidi ya asilimia 90 ya mauzo ya madini nje.

## UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA

Jedwali Na.56

| MADINI | Kipimo | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Almasi | Carat | 303920 | 219639 | 272204 | 282786 | 237676 | 181874 | 80498 | 28378 | 127174 | 179633 |
| Dhahabu | Kg | 48176 | 52236 | 39750 | 40193 | 36434 | 39112 | 39448 | 37085 | 39012 | 42534 |
| Gemstones | Kg | 1613848 | 1936618 | 2493133 | 1286297 | 1858287 | 1068481 | 2646109 | 1241581 | 1237625 | 1692436 |
| Chumvi | Tani | 57062 | 135410 | 34798 | 35224 | 25897 | 27393 | 34455 | 32297 | 34016 | 36032 |
| Phosphate | Tani | 6570 | 7096 | 2881 | 8261 | 28684 | 752 | 17180 | 848512 | 570626 | 397020 |
| Limestone | 000 Tani | 1391 | 2780 | 1608 | 1322 | 1282000 | 1284000 | 1437 | 202 | 1224 | 35529 |
| Tin Ore | Tani | - | - | - | - | - | - | 3 | - | - | 2 |
| Gypsum | Tani | 59231 | 63377 | 32798 | 2730 | 55730 | 8105 | 26918 | 9288 | 91610 | 171567 |
| Makaa ya mawe | Tani | 65041 | 74800 | 17940 | 27198 | 15242 | 1 | 179 | 80710 | 78672 | 84772 |
| Pozolana | Tani | 152679 | 163499 | 129295 | 184070 | 260403 | 61501 | 60320 | 113489 | 75193 | 79452 |
| Kaolin | Tani | - | - | - | 1020 | 13926 | 18624 | 58 | 178 | 1422 | 907 |
| Madini ya fedha | Kg | 13216 | 12891 | 14906 | 12381 | 10388 | 8231 | 12470 | 10399 | 11227 | 12159 |
| Shaba | Pound | 9348181 | 7632959 | 7241639 | 7222390 | 6288503 | 4451697 | 11741898 | 7531164 | 12426025 | 12749548 |
| Bauxite | Tani | - | 1640 | 5373 | 5003 | 20601 | 122920 | 39326000 | 29520000 | 28433930 | 39977300 |

Chanzo: Wizara ya Nishati na Madini, Idara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

Carat = 0.205 gm

* Takwimu za awali

## MADINI YALIYOUZWA NCHI ZA NJE 2008 - 2013

Jedwali Na. 57

| **Aina ya madini** | **Kipimo** | **Kiasi kilichouzwa** | | | | | | **Thamani ('000 US $)** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2008** | **2009** | **2010** | **2011** | **2012** | **2013*** | **2008** | **2009** | **2010** | **2011** | **2012** | **2013*** |
| Almasi (Rough) | '000 Carats | 221 | 181 | 181 | 80 | 127 | 180 | 2238 | 22727 | 16294 | 7480 | 33826 | 46013 |
| Almasi (iliyokatwa) | '000 Carats | - | - | - | - | | | - | - | - | - | - | - |
| Almasi (Contruct goods) | '000 Carats | - | - | - | - | | | - | - | - | - | - | - |
| Dhahabu | '000 Gramu | 36392 | 39112 | 39112 | 37085 | 39012 | 42534 | 992802 | 1039456 | 1436233 | 1879622 | 2161520 | 1735708 |
| Mawe ya thamani | '000 Gramu | 1858107 | 1068481 | 1068481 | 1058580 | | 1086532 | 49850 | 20674 | 6119 | 6309 | 32570 | 62453 |
| Chumvi | Tani | 13523 | 18430 | 18430 | 32298 | 32004 | 33210 | 2380 | 1738 | 4038 | 3699 | 3408 | 3785 |
| Phosphate | Tani | 2684 | 752 | 752 | 848512 | 570626 | 397020 | 280 | 148 | 470 | 425 | 277 | 225 |
| Bati | Tani | - | - | - | - | 48 | | - | - | - | - | 732 | |
| Jasi | Tani | 2024 | 4226 | 9498 | 11820 | 71610 | | 650 | 84 | 126 | 99 | 215 | 231 |
| Grafiti | Tani | - | - | - | - | | | - | - | - | - | | |
| Fedha | 000Grams | 9835 | 8231 | 12040 | 10399 | 11227 | 11013 | 6680 | 4961 | 7673 | 11615 | 12682 | 17214 |
| Shaba | 0001b | 6288 | 4452 | 11742 | 7531 | 12426 | 12654045 | 21063 | 11499 | 36710 | 30202 | 44816 | 42134 |
| Madini ya viwandani | Tani | - | - | - | - | | | - | - | - | - | | |
| Bauxite | Tani | 20600 | 122920 | 39326000 | 37700000 | 28433930 | 39977300 | 480 | 2127 | 1050 | 1385 | 12479 | 35827 |
| Jumla ('000 US $) | | | | | | | | **1076423** | **1103414** | **1508713** | **1940836** | **2302525** | **1943590** |

Chanzo: Wizara ya Nishati na Madini, Idara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

* Takwimu za awali

# SURA YA 14

# VIWANDA NA BIASHARA

## Kiwango cha Ukuaji

312. Shughuli za kiuchumi za uzalishaji bidhaa za viwandani zilikua kwa asilimia 7.7 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2012. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kwa uzalishaji katika baadhi ya viwanda hususan vya rangi na dawa za pareto. Hata hivyo mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa uliongezeka mwaka 2013 kufikia asilimia 8.5 ikilinganishwa na asilimia 8.4 mwaka 2012.

## Viwanda Vidogo

313. Mwaka 2013, Serikali iliendelea kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwa kutoa mafunzo ya kilimo cha kisasa, ushauri, mitaji na huduma za kiufundi kwa wajasiriamali. Mkakati huo unazingatia umuhimu wa kuongeza thamani ya mazao na bidhaa kupitia program ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI).

314. Mwaka 2013, program ya MUVI uliwezesha jumla ya vikundi vya wakulima walioko vijijini 1,290 ikilinganishwa na vikundi 319 vilivyowezeshwa mwaka 2012. Programu hii iliweza kuongeza idadi ya wanachama wa vikundi kutoka 15,482 mwaka 2012 hadi 15,949 mwaka 2013. Aidha, idadi ya makampuni ya usambazaji wa mbegu bora zilizopatikana kiushindani yaliongezeka kwa asilimia 66.1 kutoka 20 mwaka 2012 na kufikia makampuni 59 mwaka 2013. Vile vile idadi ya wakulima wa mazao mchanganyiko wanaotumia mbegu bora kupitia shamba darasa iliongezeka kutoka 117 mwaka 2012 na kufikia 11,372 mwaka 2013.

## Gharama za Uzalishaji

315. Mwaka 2013, gharama za uzalishaji bidhaa ziliongezeka hadi shilingi milioni 3,719,077 kutoka shilingi milioni 3,541,978 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji viwandani hususan kupanda kwa gharama za usafirishaji na malighafi.

**Uzalishaji katika Baadhi ya Viwanda Nchini**

316. Mwaka 2013, uzalishaji wa baadhi ya bidhaa kama vile mabati, saruji, unga wa ngano, bia, sigara na konyagi uliongezeka. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa hizo katika soko la ndani. Uzalishaji wa chuma uliongezeka kutoka tani 46,690 mwaka 2012 hadi tani 48,312 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 3.5. Uzalishaji wa mabati uliongezeka kwa asilimia 4.8 kutoka tani 81,427 mwaka 2012 hadi tani 85,313 mwaka 2013. Aidha, uzalishaji wa saruji uliongezeka kutoka tani milioni 2.58 mwaka 2012 hadi tani milioni 3.06 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 18.9.

317. Uzalishaji wa unga wa ngano uliongezeka kutoka tani 443,731 mwaka 2012 hadi tani 479,140 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 8.0. Uzalishaji katika viwanda vya bia uliongezeka kutoka lita milioni 338.7 mwaka 2012 hadi lita milioni 359.7 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Uzalishaji wa sigara ulipanda kutoka sigara milioni 7,558 mwaka 2012 hadi sigara milioni 7,569 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 0.1. Uzalishaji wa konyagi uliongezeka kutoka lita milioni 16.8 mwaka 2012 hadi lita milioni 18.0 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 7.3.

318. Hata hivyo, uzalishaji katika baadhi ya viwanda ulipungua mwaka 2013. Uzalishaji wa rangi ulipungua kwa asilimia 4.5 kutoka uzalishaji wa lita milioni 34.9 mwaka 2012 hadi lita milioni 33.3 mwaka 2013. Uzalishaji wa dawa za pareto ulipungua kutoka tani 73 mwaka 2012 hadi tani 65 mwaka 2013, sawa na upungufu wa asilimia 11.0

**Maendeleo ya Teknologia kwa Wajasiriamali**

319. Mwaka 2013, jumla ya teknolojia mpya 86 ziligunduliwa kwa ajili ya matumizi ya miradi ya uzalishaji. Aidha, SIDO ilitengeneza mashine mpya za aina mbali mbali 1,143 na vipuri 3,682 zikiwemo mashine za kubangua korosho na karanga, kupukuchua na kukoboa mahindi na mpunga, na mashine za kusindika alizeti ikilinganishwa na mashine 604 na vipuri 2,472 vilivyotengenezwa mwaka 2012.

**Utoaji wa Elimu kwa Wajasiriamali Wanaosindika Mazao**

320.Mwaka 2013, Serikali kupitia SIDO ilitoa mafunzo kwa wajasiriamali mbalimbali kwa ajili ya kuendesha na kuendeleza shughuli za biashara na miradi ya uzalishaji mali. Jumla ya wajasiriamali 1,281 walipata elimu ya usindikaji wa nafaka na matunda. Aidha, kozi 220 zilitolewa ambapo wajasiriamali 4,451 walipatiwa mafunzo ya usindikaji wa mafuta ya alizeti, utengenezaji wa sabuni, mishumaa, chaki, mizinga ya kisasa ya nyuki na usindikaji wa asali. Vilevile, wajasiriamali wengine 63 walipatiwa ujuzi wa kusindika ngozi na bidhaa zake.

321.Mwaka 2013, wajasiriamali 6,143 walipatiwa mafunzo ya maarifa na stadi za kuimarisha shughuli za uzalishaji mali kupitia kozi 307 zilizotolewa. Aidha,Serikali kupitia SIDO iliendelea kutoa huduma za kuendeleza ujasiriamali ambapo wajasiriamali 20,475 walipata mafunzo mbalimbali na wajasiriamali 18,060 walipata huduma za ushauri na ugani. Aidha, wajasiriamali 992 waliwezeshwa kushiriki maonyesho ya bidhaa za wajasiriamali kwa kupatiwa mikopo 8,964 yenye thamani ya shillingi bilioni 7.539 kutoka Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali.

**Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa**

322.Mwaka 2013, nchi 32 zilishiriki katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara katika Viwanja vya Mwalimu J. K. Nyerere ikilinganishwa na nchi 11 zilizoshiriki mwaka 2012. Ongezeko hili linatokana na kukua kwa teknolojia, kutoa taaluma na fursa za biashara kwa wajasiriamali nchini. Aidha, idadi ya washiriki wa ndani kwa mwaka 2103 iliongezeka kwa asilimia 19.3 kufikia 1,600 ukilinganisha na washiriki 1,341 mwaka 2012. Hata hivyo, makampuni ya nje yaliyoshiriki mwaka 2013 yalipungua kwa asilimia 8 na kuwa 400 ikilinganishwa na makampuni ya nje 435 mwaka 2012.

323.Maonesho hayo hufanyiwa ukaguzi kila mwaka na yameweza kutambulika na shirika linalosimamia Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Duniani (UFI), hivyo kumepelekea kuimarika kwa ushiriki wa nchi za nje na makampuni kutoka ndani na nje ya nchi. Vile vile, maonesho hayo yamekuwa yakipata hati safi kutokana na ubora wa bidhaa zinazooneshwa na hivyo kuyafanya yawe na umaarufu mkubwa duniani katika kutangaza bidhaa na huduma mbalimbali za kitaifa na kimataifa.

324.Mwaka 2013, ahadi za mauzo ya nje zenye thamani ya Dola za Kimarekani 102.2 milioni zilipatikana ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 93.8 za mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 9.0. Vile vile, ahadi za ununuzi toka nje zilikuwa Dola za Kimarekani milioni 122.2, sawa na ongezeko la asilimia 6.0 ikilinganishwa na Dola milioni 115.3 mwaka 2012. Kuhusiana na bidhaa zilizoulizwa zaidi na wateja ni pamoja na asali, viungo kama hiliki na tangawizi na bidhaa za mikono. Aidha, bidhaa zilizonunuliwa zaidi ni pamoja na nguo, bidhaa za ngozi na samani.

325.Mwaka 2013, Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*TanTrade*) ilihamasisha wajasiriamali kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam na Maonesho ya Kisekta. Aidha, Serikali ilihamasisha na kuwawezesha wajasiriamali kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kimataifa kwenye nchi nyingine kama Kenya, Rwanda na Sudani.

## MATUMIZI YA SARUJI NCHINI

Jedwali Na. 58

| Mwaka | Kutoka Nje | Uuzaji nje | Utengenezaji | Tani | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Tani | Badiliko% |
| 1990 | 2544 | 131469 | 663900 | 534975 | -5.8% |
| 1991 | 2800 | 67766 | 1022580 | 957614 | 79.0% |
| 1992 | 3080 | 63065 | 677388 | 617403 | -35.5% |
| 1993 | 3600 | 102282 | 748850 | 650168 | 5.3% |
| 1994 | 3160 | 53706 | 686200 | 617272 | -5.1% |
| 1995 | 4000 | 72092 | 739156 | 671064 | 8.7% |
| 1996 | 1309 | 104811 | 725755 | 622253 | -7.3% |
| 1997 | 2804 | 100165 | 621159 | 523798 | -15.8% |
| 1998 | 14388 | 50718 | 777620 | 741290 | 41.5% |
| 1999 | 11418 | 29097 | 832602 | 814923 | 9.9% |
| 2000 | 7281 | 30497 | 833092 | 809882 | -0.6% |
| 2001 | 56395 | 53517 | 900430 | 903308 | 11.5% |
| 2002 | 149079 | 37203 | 1026082 | 1137958 | 26.0% |
| 2003 | 166446 | 34396 | 1186434 | 1318484 | 15.9% |
| 2004 | 125007 | 37655 | 1280851 | 1368203 | 3.8% |
| 2005 | 120200 | 40430 | 1375222 | 1454992 | 6.3% |
| 2006 | 92711 | 98 | 1421460 | 1514073 | 4.1% |
| 2007 | 101827 | 52170 | 1629890 | 1679547 | 10.9% |
| 2008 | 356468 | 99688 | 1755862 | 2012642 | 19.8% |
| 2009 | 516182 | 57569 | 1940845 | 2399458 | 19.2% |
| 2010 | 566828 | 189321 | 2312055 | 2689562 | 12.1% |
| 2011 | 768343 | 217944 | 2408765 | 2959164 | 10.0% |
| 2012 | 1013986 | 145793 | 2581398 | 3449591 | 16.6% |
| 2013* | 1218453 | 154481 | 2345647 | 3409619 | -1.2% |

Chanzo: Ofisi ya Taifa Takwimu

*     Takwimu za Awali

## UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI

Jedwali Na.59

| Aina ya Bidhaa | Kipimo | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | Badiliko(%) 2012/13 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Biskuti & tambi | Tani | 10912 | 10565 | 11273 | 15435 | 15200 | 7435 | 12053 | 16006 | 16100 | 0.6% |
| Unga wa ngano | Tani | 368019 | 434160 | 406336 | 287925 | 368885 | 444242 | 439926 | 443731 | 479140 | 8.0% |
| Konyagi | 000 Lita | 4489 | 5365 | 5622 | 4049 | 10201 | 11186 | 15432 | 16774 | 18005 | 7.3% |
| Bia | 000 Lita | 216604 | 299036 | 310194 | 291178 | 284906 | 242689 | 323393 | 338650 | 359713 | 6.2% |
| Chibuku | 000 Lita | 11106 | 11559 | 10320 | 10235 | 16141 | 21037 | 23474 | 22028 | 23674 | 7.5% |
| Sigara | Milioni | 4445 | 5095 | 5821 | 6101 | 5831 | 6181 | 6630 | 7558 | 7569 | 0.1% |
| Nguo | 000 $M^2$ | 99134 | 146600 | 139000 | 140531 | 91501 | 103177 | 101820 | 83592 | 97413 | 16.5% |
| Kamba za katani | Tani | 5943 | 5854 | 7012 | 7783 | 7913 | 6872 | 6976 | 7754 | 7542 | -2.7% |
| Nyavu za uvuvi | Tani | 274 | 119 | 156 | - | 64 | 247 | 164 | 295 | 270 | -8.5% |
| Mazulia | 000 $M^2$ | - | - | - | - | 37152 | - | - | - | - | |
| Tabaka za mbao | $M^2$ | 37941 | 44310 | 45147 | 44547 | 266 | - | 30589 | 35293 | 33447 | -5.2% |
| Dawa za pareto | Tani | 25 | 33 | 33 | 73 | - | 49 | 53 | 73 | 65 | -11.0% |
| Mbolea | Tani | - | - | | - | 25762 | - | 11200 | 0 | 11341 | |
| Rangi | 000 Lita | 16222 | 18402 | 17451 | 24857 | - | 28201 | 31211 | 34868 | 33312 | -4.5% |
| Bidhaa za petrol | 000 Tani | - | - | - | - | 1941 | - | 0 | 0 | 0 | |
| Saruji | 000 Tani | 1366 | 1422 | 1630 | 1756 | 34793 | 2313 | 2409 | 2581 | 3067 | 18.8% |
| Chuma | Tani | 41299 | 44482 | 52163 | 39969 | 34793 | 33384 | 39955 | 46690 | 48312 | 3.5% |
| Bati | Tani | 29737 | 29898 | 36492 | 31743 | 50664 | 71276 | 76912 | 81427 | 85313 | 4.8% |
| Aluminium | Tani | 183 | 105 | 110 | 105 | 58 | 59 | 33 | 23 | 37 | 60.9% |
| Radio | 000 namba | - | - | - | - | | - | 0 | 0 | 0 | |
| Betri | Milioni | 81 | 82 | 75 | 53 | 78 | 93 | 89 | 68 | 59 | -13.2% |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara

\- Hakuna uzalishaji

## VIWANDA- IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA

Jedwali Na. 60

| ISIC (Rev 3) | Shughuli | Walioajiriwa | | | | | | Wengine | | | | | | Jumla | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2008** | **2009*** | **2010**** | **2011**** | **2012**** | **2013**** | **2008** | **2009*** | **2010**** | **2011**** | **2012**** | **2013**** | **2008** | **2009*** | **2010**** | **2011**** | **2012**** | **2013**** |
| 151-4 | Vyakula | 43491 | 33859 | 44365 | 46584 | 48913 | 51358 | 299 | 2809 | 305 | 320 | 353 | 371 | 43790 | 36668 | 44670 | 46904 | 49266 | 51729 |
| 155 | Vinywaji | 5797 | 5195 | 5914 | 6209 | 6520 | 6846 | 49 | 192 | 50 | 52 | 58 | 61 | 5846 | 5387 | 5964 | 6262 | 6578 | 6906 |
| 160 | Tumbaku na Sigara | 6747 | 3815 | 6883 | 7227 | 7588 | 7968 | - | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6747 | 3815 | 6883 | 7227 | 7588 | 7968 |
| 171-2, | Ufumaji na Ushonaji | 11752 | 11845 | 11988 | 12588 | 13217 | 13878 | 231 | 291 | 236 | 247 | 273 | 287 | 11983 | 12136 | 12224 | 12835 | 13490 | 14165 |
| 191 | Ngozi, bidhaa za ngozi | 635 | 495 | 648 | 680 | 714 | 750 | 4 | 0 | 4 | 4 | 5 | 5 | 639 | 495 | 652 | 684 | 719 | 755 |
| 192 | Viatu | 803 | 648 | 819 | 860 | 903 | 948 | 5 | 6 | 5 | 5 | 6 | 6 | 808 | 654 | 824 | 865 | 909 | 954 |
| 201-202 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 755 | 1072 | 770 | 809 | 849 | 892 | 24 | 16 | 24 | 26 | 28 | 30 | 779 | 1088 | 795 | 834 | 877 | 921 |
| 210-221-222 | Karatasi, Uchapishaji | 5467 | 5860 | 5577 | 5856 | 6149 | 6456 | 90 | 405 | 92 | 96 | 106 | 112 | 5557 | 6265 | 5669 | 5952 | 6255 | 6568 |
| 241-2 | Utengenezaji wa Kemikali | 2886 | 3639 | 2944 | 3091 | 3246 | 3408 | 29 | 86 | 30 | 31 | 34 | 36 | 2915 | 3725 | 2974 | 3122 | 3280 | 3444 |
| 251 | Bidhaa za mpira | 1203 | 53 | 1227 | 1289 | 1353 | 1421 | 12 | 0 | 12 | 13 | 14 | 15 | 1215 | 53 | 1239 | 1301 | 1367 | 1436 |
| 252 | Bidhaa za Plastiki | 4112 | 4175 | 4195 | 4404 | 4625 | 4856 | 13 | 13 | 13 | 14 | 15 | 16 | 4125 | 4188 | 4208 | 4418 | 4640 | 4872 |
| 261-9 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 2461 | 2271 | 2510 | 2636 | 2768 | 2906 | 29 | 52 | 30 | 31 | 34 | 36 | 2490 | 2323 | 2540 | 2667 | 2802 | 2942 |
| 271-369 | Nyinginezo | 20096 | 18692 | 20500 | 21525 | 22601 | 23731 | 396 | 202 | 404 | 424 | 468 | 491 | 20492 | 18894 | 20904 | 21949 | 23069 | 24223 |
| | **Jumla** | **106205** | **91619** | **108340** | **113757** | **119445** | **125417** | **1181** | **4072** | **1205** | **1265** | **1395** | **1465** | **107386** | **95691** | **109545** | **115022** | **120840** | **126882** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Zimerekebishwa (Revised ) kutokana na utafiti

** Makisio (Estimates)

Viwanda rasmi vyenye wafanyakazi 10 na zaidi

Maelezo: *1. Uchambuzi wa Takwimu umetumia "International Standard Industrial Classification Revision 4 (ISIC Rev4)"*

*2. Takwimu za 2006 - 2009 zimerekebishwa kutokana na utafiti*

*3. Takwimu za 2010 - 2013 zimekadiriwa kwa kutumia takwimu za mwaka 2008 -2009 na Utafiti wa kila Robo Mwaka*

## VIWANDA: GHARAMA ZA KAZI

Jedwali Na. 61 (Sh.milioni)

| ISIC (Rev 3) | **Shughuli** | **Mishahara** | | | | | **Malipo Mengine** | | | | | **Jumla** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2009*** | **2010**** | **2011**** | **2012**** | **2013**** | **2009*** | **2010**** | **2011**** | **2012**** | **2013**** | **2009*** | **2010**** | **2011**** | **2012**** | **2013**** |
| 151-4 | Vyakula | 75131 | 53748 | 56435 | 59257 | 62220 | 30482 | 23350 | 24517 | 25743 | 27030 | 105613 | 77098 | 80953 | 85000 | 89250 |
| 155 | Vinywaji | 51012 | 37004 | 38854 | 40797 | 42836 | 17551 | 21052 | 22104 | 23210 | 24370 | 68563 | 58056 | 60958 | 64006 | 67206 |
| 160 | Tumbaku na Sigara | 8204 | 17725 | 18611 | 19541 | 20518 | 5324 | 9732 | 10218 | 10729 | 11266 | 13528 | 27456 | 28829 | 30271 | 31784 |
| 171-2, 181 | Ufumaji na Ushonaji | 10047 | 10469 | 10992 | 11542 | 12119 | 2540 | 4045 | 4248 | 4460 | 4683 | 12587 | 14514 | 15240 | 16002 | 16802 |
| 191 | Ngozi, Bidhaa za ngozi | 3477 | 488 | 512 | 538 | 565 | 813 | 113 | 118 | 124 | 131 | 4290 | 601 | 631 | 662 | 695 |
| 192 | Viatu | 239 | 1053 | 1105 | 1161 | 1219 | 197 | 404 | 425 | 446 | 468 | 436 | 1457 | 1530 | 1606 | 1687 |
| 201- 202 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 1995 | 775 | 814 | 855 | 897 | 1119 | 222 | 233 | 245 | 257 | 3114 | 997 | 1047 | 1100 | 1155 |
| 210-221-222 | Karatasi, Uchapishaji | 15895 | 18159 | 19067 | 20020 | 21021 | 9601 | 5857 | 6150 | 6457 | 6780 | 25496 | 24016 | 25217 | 26478 | 27801 |
| 241-2 | Utengenezaji wa Kemikali | 12135 | 7451 | 7824 | 8215 | 8626 | 7181 | 4317 | 4533 | 4760 | 4998 | 19316 | 11769 | 12357 | 12975 | 13624 |
| 251 | Bidhaa za Mpira | 304 | 5798 | 6088 | 6393 | 6712 | 3668 | 1446 | 1518 | 1594 | 1674 | 3972 | 7244 | 7607 | 7987 | 8386 |
| 252 | Bidhaa za Plastiki | 6020 | 6398 | 6718 | 7054 | 7406 | 1536 | 5347 | 5614 | 5895 | 6190 | 7556 | 11745 | 12332 | 12949 | 13596 |
| 261-9 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 18297 | 77022 | 80873 | 84917 | 89162 | 8279 | 8662 | 9095 | 9550 | 10028 | 26576 | 85684 | 89968 | 94467 | 99190 |
| 271-369 | Nyinginezo | 45540 | 44865 | 47108 | 49463 | 51936 | 14850 | 33211 | 34872 | 36615 | 38446 | 60390 | 78076 | 81980 | 86078 | 90382 |
| | **Jumla** | **248296** | **280954** | **295002** | **309752** | **325239** | **103141** | **117759** | **123647** | **129829** | **136320** | **351437** | **398713** | **418648** | **439580** | **461558** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Zimerekebishwa (Revised ) kutokana na utafiti

** Makisio (Estimates)

Viwanda rasmi vyenye wafanyakazi 10 na zaidi

Maelezo: *1. Uchambuzi wa Takwimu umetumia "International Standard Industrial Classification Revision 3 (ISIC Rev3)"*

*2. Takwimu za 2006 - 2009 zimerekebishwa kutokana na utafiti*

*3. Takwimu za 2010 - 2013 zimekadiriwa kwa kutumia takwimu za mwaka 2008 - 2009 na Utafiti wa kila Robo Mwaka*

## VIWANDA MUHTASARI WA MATOKEO

Jedwali Na. 62

(Tshs. Millioni)

| ISIC (Rev 3) | Shughuli | PATO | | | | GHARAMA | | | | Thamani Iliyoongezeka (Value Added) | | | | Uchakavu wa Mitambo (Depreciation) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2010** | 2011** | 2012** | 2013** | 2010** | 2011** | 2012** | 2013** | 2010** | 2011** | 2012** | 2013** | 2010** | 2011** | 2012** | 2013** |
| 151-4 | Vyakula | 1223445 | 1284618 | 1348849 | 1416291 | 695078 | 729832 | 766324 | 804640 | 528367 | 554786 | 582525 | 611651 | 33923 | 35619 | 37400 | 39270 |
| 155 | Vinywaji | 928737 | 975174 | 1023932 | 1075129 | 591932 | 621529 | 652606 | 685236 | 336804 | 353645 | 371327 | 389893 | 44556 | 46784 | 49124 | 51580 |
| 160 | Tumbaku na Sigara | 288987 | 303436 | 318608 | 334539 | 179901 | 188896 | 198341 | 208258 | 109086 | 114541 | 120268 | 126281 | 21753 | 22841 | 23983 | 25182 |
| 171-2, 181 | Ufumaji na Ushonaji | 209132 | 219588 | 230568 | 242096 | 119867 | 125860 | 132153 | 138761 | 89265 | 93728 | 98414 | 103335 | 22881 | 24025 | 25226 | 26487 |
| 191 | Ngozi, bidhaaa za ngozi | 9671 | 10155 | 10662 | 11195 | 6559 | 6887 | 7231 | 7592 | 3112 | 3268 | 3431 | 3603 | 306 | 321 | 337 | 354 |
| 192 | Viatu | 8967 | 9416 | 9887 | 10381 | 5459 | 5732 | 6019 | 6320 | 3508 | 3684 | 3868 | 4061 | 665 | 698 | 733 | 770 |
| 201-202 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 13315 | 13981 | 14680 | 15414 | 6808 | 7148 | 7506 | 7881 | 6507 | 6833 | 7174 | 7533 | 494 | 519 | 545 | 572 |
| 210-221-222 | Karatasi, Uchapishaji | 200607 | 210638 | 221170 | 232228 | 112829 | 118470 | 124394 | 130613 | 87779 | 92168 | 96776 | 101615 | 8895 | 9340 | 9807 | 10297 |
| 241-2 | Utengenezaji wa Kemikali | 289674 | 304158 | 319365 | 335334 | 168109 | 176515 | 185340 | 194607 | 121565 | 127643 | 134025 | 140726 | 7928 | 8325 | 8741 | 9178 |
| 251 | Bidhaa za mpira | 164445 | 172667 | 181300 | 190365 | 85572 | 89850 | 94343 | 99060 | 78873 | 82817 | 86958 | 91305 | 2385 | 2504 | 2630 | 2761 |
| 252 | Bidhaa za Plastiki | 471841 | 495433 | 520205 | 546215 | 327561 | 343939 | 361136 | 379193 | 144280 | 151494 | 159069 | 167022 | 9860 | 10353 | 10871 | 11414 |
| 261-9 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 379518 | 398494 | 418419 | 439340 | 243628 | 255809 | 268599 | 282029 | 135891 | 142685 | 149819 | 157310 | 31528 | 33105 | 34760 | 36498 |
| 271-369 | Nyinginezo | 1005953 | 1056250 | 1109063 | 1164516 | 669376 | 702845 | 737987 | 774887 | 336577 | 353405 | 371075 | 389629 | 35240 | 37002 | 38852 | 40795 |
| | **Jumla** | **5194293** | **5454007** | **5726707** | **6013043** | **3212678** | **3373312** | **3541978** | **3719077** | **1981614** | **2080695** | **2184729** | **2293966** | **220415** | **231436** | **243008** | **255159** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Zimerekebishwa (Revised ) kutokana na utafiti

** Makisio (Estimates)

Viwanda rasmi vyenye wafanyakazi 10 na zaidi

Maelezo: *1. Uchambuzi wa Takwimu umetumia "International Standard Industrial Classification Revision 4 (ISIC Rev4)"*

*2. Takwimu za 2008 - 2009 zimerekebishwa kutokana na utafiti*

*3. Takwimu za 2010 - 2013 zimekadiriwa kwa kutumia takwimu za mwaka 2008 - 2009 na Utafiti wa kila Robo Mwaka*

## VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA *

Jedwali Na. 63

| Jina la mkoa | Idadi ya Wafanyakazi | | | | Idadi ya Waajiriwa | | | | Mishahara (TShs. Milioni) | | | | Thamani Iliyoongezeka (TShs. Milioni) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2010** | 2011** | 2012** | 2013** | 2010** | 2011** | 2012** | 2013** | 2010** | 2011** | 2012** | 2013** | 2010** | 2011** | 2012** | 2013** |
| Dodoma | 235 | 216 | 227 | 238 | 234 | 208 | 218 | 229 | 584 | 542 | 569 | 598 | 8562 | 9213 | 9674 | 10157 |
| Arusha, Manyara | 15603 | 14312 | 15027 | 15787 | 15495 | 13759 | 14447 | 15169 | 22329 | 20720 | 21756 | 22844 | 356830 | 383946 | 403144 | 423301 |
| Kilimanjaro | 11780 | 10805 | 11345 | 11919 | 11699 | 10388 | 10907 | 11453 | 12308 | 11421 | 11992 | 12592 | 137290 | 147723 | 155109 | 162864 |
| Tanga | 10256 | 9407 | 9877 | 10377 | 10185 | 9043 | 9495 | 9970 | 12225 | 11344 | 11912 | 12507 | 237041 | 255055 | 267807 | 281198 |
| Morogoro | 8286 | 7600 | 7980 | 8384 | 8229 | 7307 | 7672 | 8056 | 21453 | 19907 | 20902 | 21947 | 288858 | 310810 | 326350 | 342668 |
| Pwani, | 24640 | 22600 | 23730 | 24930 | 24025 | 21333 | 22399 | 23519 | 133234 | 123634 | 129816 | 136306 | 624421 | 671873 | 705467 | 740740 |
| Dar es Salaam, Pwani*** | 62 | 57 | 60 | 63 | 61 | 55 | 57 | 60 | 79 | 73 | 77 | 81 | 435 | 468 | 492 | 516 |
| Lindi | 118 | 108 | 113 | 119 | 117 | 104 | 109 | 114 | 1512 | 1403 | 1473 | 1547 | 4139 | 4454 | 4677 | 4911 |
| Mtwara | 997 | 914 | 960 | 1009 | 990 | 879 | 923 | 969 | 534 | 495 | 520 | 546 | 7505 | 8075 | 8479 | 8903 |
| Ruvuma | 9282 | 8514 | 8940 | 9392 | 9218 | 8185 | 8594 | 9024 | 16578 | 15383 | 16152 | 16960 | 32645 | 35125 | 36882 | 38726 |
| Iringa | 2942 | 2698 | 2833 | 2977 | 2922 | 2594 | 2724 | 2860 | 6322 | 5867 | 6160 | 6468 | 22191 | 23877 | 25071 | 26324 |
| Mbeya | 243 | 223 | 234 | 246 | 241 | 214 | 225 | 236 | 533 | 494 | 519 | 545 | 2312 | 2488 | 2612 | 2743 |
| Singida | 823 | 755 | 793 | 833 | 818 | 726 | 762 | 800 | 1330 | 1234 | 1296 | 1360 | 4447 | 4785 | 5024 | 5275 |
| Tabora | 130 | 120 | 126 | 132 | 130 | 115 | 121 | 127 | 1037 | 963 | 1011 | 1061 | 1360 | 1464 | 1537 | 1614 |
| Rukwa | 692 | 635 | 667 | 700 | 687 | 610 | 641 | 673 | 1575 | 1462 | 1535 | 1611 | 5324 | 5729 | 6015 | 6316 |
| Kigoma | 2239 | 2053 | 2156 | 2265 | 2223 | 1974 | 2073 | 2177 | 10089 | 9362 | 9830 | 10321 | 19140 | 20595 | 21625 | 22706 |
| Shinyanga | 9702 | 8898 | 9343 | 9816 | 9634 | 8555 | 8983 | 9432 | 9757 | 9054 | 9506 | 9982 | 32941 | 35444 | 37216 | 39077 |
| Kagera | 7326 | 6719 | 7055 | 7412 | 7275 | 6460 | 6783 | 7122 | 13729 | 12740 | 13377 | 14046 | 102088 | 109846 | 115338 | 121105 |
| Mwanza | 3515 | 3224 | 3385 | 3556 | 3490 | 3099 | 3254 | 3417 | 10053 | 9328 | 9795 | 10284 | 82384 | 88644 | 93076 | 97730 |
| Mara | 673 | 617 | 648 | 681 | 668 | 593 | 623 | 654 | 5696 | 5285 | 5550 | 5827 | 11703 | 12592 | 13222 | 13883 |
| **Jumla** | **109545** | **100475** | **105500** | **110835** | **108340** | **96200** | **101010** | **106060** | **280954** | **260711** | **273747** | **287433** | **1981615** | **2132206** | **2238816** | **2350756** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Zimerekebishwa (Revised ) kutokana na utafiti

** Makisio (Estimates)

Viwanda rasmi vyenye wafanyakazi 10 na zaidi

## VIGEZO VYA UFANISI KATIKA SEKTA YA VIWANDA

Jedwali Na. 65

| Mwaka | Mchango katika Pato la Taifa % (Bei za 2001) | Ukuaji wa Sekta (Bei za 2001) | Mchango katika Mauzo nje % | Mchango katika Mauzo nje yasiyo Asilia (%) | Ongezeko la mauzo nje ya bidhaa za viwanda (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1998 | 8.37 | 5.5 | 6.10 | 15.40 | - |
| 1999 | 8.47 | 6.0 | 5.50 | 12.40 | -15.7% |
| 2000 | 8.46 | 4.8 | 6.50 | 11.71 | 44.2% |
| 2001 | 8.38 | 5.0 | 7.23 | 9.05 | 29.4% |
| 2002 | 8.40 | 7.5 | 7.40 | 8.52 | 17.3% |
| 2003 | 8.57 | 9.0 | 6.79 | 8.42 | 27.2% |
| 2004 | 8.69 | 9.4 | 8.28 | 9.37 | 31.4% |
| 2005 | 8.87 | 9.6 | 9.31 | 11.81 | 41.8% |
| 2006 | 9.02 | 8.5 | 11.24 | 13.81 | 25.4% |
| 2007 | 9.15 | 8.7 | 15.28 | 18.14 | 57.9% |
| 2008 | 9.36 | 9.9 | 20.73 | 28.48 | 139.9% |
| 2009 | 9.54 | 8.0 | 15.36 | 21.35 | -31.7% |
| 2010 | 9.61 | 7.9 | 22.29 | 30.34 | 90.3% |
| 2011 | 9.74 | 7.8 | 16.90 | 22.99 | -10.6% |
| 2012 | 9.85 | 8.2 | 17.61 | 24.91 | 20.4% |
| 2013 | 9.92 | 7.7 | 20.04 | 28.34 | 3.3% |

Chanzo: Wizara ya Fedha

## SURA YA 15

## UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

### UJENZI

#### Kiwango cha Ukuaji

326. Mwaka 2013, shughuli za ujenzi zilikua kwa asilimia 8.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.8 mwaka 2012. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi na ukarabati wa: barabara na madaraja ikiwemo barabara ya mabasi yaendayo kasi jijini Dar es Salaam; ujenzi unaondelea wa viwanja vya ndege; na majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi. Aidha, mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.3 ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 2012.

#### Mtandao wa Barabara

327. Mwaka 2013, mtandao wa barabara nchini ulikuwa na urefu wa jumla ya kilometa 87,581ikilinganishwa na kilometa 86,472, sawa na ongezeko la asilimia 1.3. Mchanganuo wa mtandao wa barabara katika mwaka 2013 unaonesha kuwa kilometa 12,786 ni barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani, zikijumuisha kilometa 5,823, sawa na asilimia 45.5 zilizo katika kiwango cha lami. Kilometa 22,214 ni barabara za mikoa zinazounganisha wilaya na miji mikuu, kati ya hizo kilometa 1,088 sawa na asilimia 4.9 ni za kiwango cha lami. Aidha, kilometa 58,037 ni barabara za wilaya zinazounganisha wilaya na vijiji pamoja na barabara viunganishi.

328. Katika mwaka 2013, jumla ya kilometa 1,072.34 zilijengwa au kukarabatiwa kwa kiwango cha lami ikilinganishwa na kilomita 820.35 mwaka 2012. Katika barabara zilizojengwa au kurabatiwa mwaka 2013, kilomita 816 zilijengwa kwa kiwango cha lami na kilomita 256.3 zilikarabatiwa kwa kiwango cha lami. Aidha, tathmini iliyofanyika mwaka 2013 juu ya ubora wa barabara ilionesha kwamba kilometa 6,005, sawa na asilimia 60.0 ya barabara kuu zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na asilimia 48.1 mwaka 2012. Vile vile, kilometa 3,340 sawa na asilimia 33.4 za barabara kuu zilikuwa na hali ya wastani mwaka 2013 ikilinganishwa na kilometa 4,015, sawa na asilimia 39.0 mwaka 2012. Aidha, kilometa 662, sawa na asilimia 6.6 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 1,320, sawa na asilimia 12.8 mwaka 2012. Kwa

ujumla hali ya ubora wa barabara kuu mwaka 2013 iliimarika kufuatia juhudi za Serikali katika kuimarisha miundombinu ya barabara.

329. Mwaka 2013, jumla ya kilometa 5,608, sawa na asilimia 26.1 za barabara za mikoa zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 6,689 mwaka 2012, sawa na asilimia 32.0. Aidha, kilometa 13,007 sawa na asilimia 60.5 zilikuwa na hali ya wastani ikilinganishwa na kilometa 14,780 mwaka 2012, sawa na asilimia 47.4. Vile vile, kilometa 2,874 sawa na asilimia 13.4 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 3,458 mwaka 2012, sawa na asilimia 16.5. Kiwango cha hali ya wastani wa barabara za mikoa kiliongezeka mwaka 2013 na wakati huo huo kiwango cha hali mbaya kilipungua kutokana na barabara zilizopandishwa madaraja na kuhamishiwa TANROADS. Jedwali Na. 15.1 linaonesha hali ya mtandao wa barabara kwa ujumla hadi kufikia mwishoni mwa Desemba 2013.

**Jedwali Na.15.1: Hali ya Mtandao wa Barabara Hadi Kufikia Desemba 2013**

| **Aina ya Barabara** | **Hali ya Barabara** | | | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Nzuri** | | **Wastani** | | **Mbaya** | | |
| | Km | % | Km | % | Km | % | Km |
| Barabara kuu Lami | 4,976 | 83.6 | 667 | 11.2 | 310 | 5.2 | 5,953 |
| Barabara kuu Changarawe/Udongo | 1,029 | 25.4 | 2,673 | 65.9 | 352 | 8.7 | 4,054 |
| **Jumla Ndogo-Barabara Kuu** | **6,005** | **60.0** | **3,340** | **33.4** | **662** | **6.6** | **10,007** |
| Barabara za Mkoa Lami | 456 | 54.0 | 196 | 23.2 | 193 | 22.9 | 844 |
| Barabara za Mkoa Changarawe/Udongo | 5,152 | 25.0 | 12,811 | 62.1 | 2,681 | 13.0 | 20,644 |
| **Jumla Ndogo-Barabara za Mkoa** | **5,608** | **26.1** | **13,007** | **60.5** | **2,874** | **13.4** | **21,488** |
| **Jumla Kuu** | **11,613** | **36.9** | **16,347** | **51.9** | **3,536** | **11.2** | **31,495** |

Chanzo: Wizara ya Ujenzi

## Matengenezo ya Barabara na Madaraja

330. Mwaka 2013, jumla ya kilometa 42,224, za barabara kuu na za mikoa zilifanyiwa matengenezo kupitia TANROADS ikilinganishwa na kilomita 28,282 mwaka 2012. Aidha, madaraja 1,856 yalifanyiwa matengenezo mwaka 2013 ikilinganishwa na madaraja 2,395 mwaka 2012.

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

331.Mwaka 2013, Mfuko wa Barabara ulikusanya mapato ya shilingi 448.3 bilioni ikilinganishwa na shilingi 404.6 bilioni zilizokusanywa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 10.8. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mapato yanayotokana na tozo ya mafuta ambayo yaliongezeka kwa asilimia 11.

332. Aidha katika mwaka 2013, Bodi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Wakala wa Barabara, ilihakikisha kwamba tozo za barabara zinakusanywa ipasavyo na kuwekwa kwenye akaunti ya Mfuko. Vile vile, katika juhudi za kuziba mianya ya uvujaji wa mapato Bodi ilishirikiana na taasisi zingine kama TRA, EWURA, SUMATRA n.k. katika hatua za kupunguza uvujaji wa mapato ikiwa ni pamoja na uchakachuaji wa mafuta yanapaswa kwenda nje ya nchi lakini huishia soko la ndani. Aidha, Bodi ilianza utaratibu wa kuwatumia Wahandisi Washauri kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa kiufundi na ubora wa kazi wakati miradi ya matengenezo ya barabara ikiwa inaendelea.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

333.Mwaka 2013, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilisajili makandarasi wapya 827 ikilinganishwa na makandarasi 813 mwaka 2012. Aidha, Bodi ilifanya ukaguzi katika miradi 2,687 ya ujenzi ikilinganishwa na miradi ya ujenzi 2,480 iliyokaguliwa mwaka 2012. Kati ya miradi iliyokaguliwa mwaka 2013, miradi 1,866 ilikuwa haina kasoro na miradi 821 ilikuwa na kasoro. Makandarasi katika miradi yenye mapungufu walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

334.Mwaka 2013, Bodi ya Usajili wa Makandarasi iliendesha kozi sita za mafunzo ya makandarasi katika mikoa ya Dar es Salaam (2), Kilimanjaro (1), Ruvuma (1), Mwanza (1) na Lindi (1), ambapo jumla ya washiriki 231 walihudhuria. Aidha, Bodi ilifanya mikutano ya majadiliano na wadau katika mkoa wa Dar es salaam ambapo jumla ya washiriki 810 walihudhuria.

335.Mwaka 2013, Serikali iliendelea kutekeleza mkakati wa kuendeleza makandarasi wazalendo kwa nia ya kukuza uwezo wa kutekeleza kazi za thamani kubwa za miundombinu. Utekelezaji huu uliendа sambamba na kuwaelimisha makandarasi kufanya kazi kubwa kwa ubia. Aidha, Bodi ilitoa vibali maalum vilivyowawezesha makandarasi wa madaraja ya chini kufanya kazi kwa ubia juu ya madaraja yao baada ya kuchunguzwa vigezo ambavyo

haviathiri thamani na viwango vya miradi. Vile vile, Bodi kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini na kampuni ya Symbioni ilitoa mafunzo ya usambazaji wa umeme vijijini kwa mafundi makandarasi wa umeme. Aidha, Bodi iliendelea na ufuatiliaji wa mradi wa ujenzi wa daraja la Mbutu unaotekelezwa na makandarasi wazalendo kwa mpango wa kusanifu na kujenga ili kuangalia ubora wa kazi.

**Bodi ya Usajili ya Wahandisi**

336.Mwaka 2013, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili wahandisi 1,100 na kampuni za ushauri 18 ikilinganishwa na wahandisi 1,009 na kampuni za ushauri 25 mwaka 2012, kama inavyoonekana katika jedwali 15.2. Hadi Desemba 2013, jumla ya wahandisi 13,148 walikuwa wamesajiliwa katika ngazi mbalimbali. Miongoni mwao, wahandisi 11,922 walikuwa wazalendo na wahandisi 1,226 wageni. Aidha, Bodi iliendeleza uanzishwaji wa kampuni nyingi za ushauri wa kihandisi katika mikoa.

**Jedwali Na: 15.2 Usajili wa Wahandisi Mwaka 2010 – 2013**

| **Aina za usajili** | **Usajili 2010** | **Usajili 2011** | **Usajili 2012** | **Usajili 2013** |
|---|---|---|---|---|
| Wahandisi Wasaidizi Wahitimu | 23 | 20 | 14 | 9 |
| Wahandisi Wasaidizi | 5 | 4 | 3 | 3 |
| Wahandisi Wahitimu | 411 | 594 | 586 | 716 |
| Wahandisi Wataalamu | 67 | 173 | 181 | 234 |
| Wahandisi Wataalamu wa Muda | 65 | 190 | 182 | 112 |
| Wahandisi Washauri | 9 | 24 | 37 | 19 |
| Wahandisi Washauri wa Muda | 2 | 12 | 6 | 7 |
| **JUMLA** | **582** | **1,017** | **1,009** | **1,100** |
| **Makampuni** | | | | |
| Makampuni ya Ushauri ya Kizalendo | 6 | 14 | 22 | 14 |
| Makampuni ya Ushauri ya Kigeni | 8 | 27 | 3 | 4 |
| **JUMLA** | **14** | **41** | **25** | **18** |

Chanzo: Wizara ya Ujenzi

337.Mwaka 2013, Bodi ilisimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi Wahitimu 178 ikilinganishwa na Wahandisi Wahitimu 133 waliopata mafunzo mwaka 2012. Jedwali Na. 15.3 linaonesha jumla ya Wahandisi Wahitimu waliojiunga na Mpango wa Mafunzo kwa vitendo kwa mwaka 2002/03-2013/14.

**Jedwali Na. 15.3: Takwimu za Wahandisi wahitimu waliojiunga na Mpango wa Mafunzo kwa vitendo 2002/2003 – 2013/2014**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya waliojiunga | Wanaogharimiwa na Serikali | Wanaogharimiwa na waajiri wao | Waliomaliza Mafunzo | Walioajiriwa kabla ya kumaliza | Walioa-hirisha | Waliomo katika Mafunzo hadi sasa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2002/03 | 120 | 110 | 10 | - | 60 | 8 | |
| 2003/04 | 169 | 162 | 7 | 20 | 95 | 9 | |
| 2004/05 | 212 | 195 | 17 | 10 | 120 | 15 | |
| 2005/06 | 167 | 137 | 30 | 121 | 81 | 12 | |
| 2006/07 | 218 | 113 | 105 | 78 | 85 | 20 | |
| 2007/08 | 159 | 128 | 31 | 136 | 34 | 12 | |
| 2008/09 | 265 | 156 | 109 | 140 | 79 | 41 | |
| 2009/10 | 263 | 104 | 159 | 176 | 60 | 12 | |
| 2010/11 | 224 | 44 | 180 | 218 | 70 | 15 | |
| 2011/12 | 294 | - | 294 | 263 | 100 | 3 | 291 |
| 2012/13 | 133 | - | 133 | 9 | 122 | - | 270 |
| 2013/14 | 178 | 81 | 97 | 209 | 127 | 6 | 172 |
| **Jumla** | **2,224** | **1,149** | **1,075** | **1,100** | **906** | **147** | **733** |

Chanzo: Bodi ya Usajili ya Wahandisi

## Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

338. Mwaka 2013, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili jumla ya wabunifu majengo 28 na wakadiriaji majenzi 29 ikilinganishwa na wabunifu majengo 18 na wakadiriaji majenzi 26 waliosajiliwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la wataalam kwa asilimia 29.5. Usajili huu unafanya jumla ya wataalamu waliosajiliwa na Bodi kufikia 599 hadi Desemba 2013. Kati yao, Wabunifu Majengo ni 358, Landscape Architect' 1, Wakadiriaji Majenzi 240 na "Building Surveyor"1. Aidha, kampuni 18 za wabunifu majengo na kampuni 9 za wakadiriaji majenzi zilisajiliwa na Bodi ikilinganishwa na kampuni 11 za wabunifu majengo na kampuni 9 za ukadiriaji majenzi zilizosajiliwa mwaka 2012. Hili ni ongezeko la kampuni 7 ambalo linafanya jumla ya kampuni zilizosajiliwa kufikia 292.

339. Mwaka 2013, Bodi ilisajili wataalam 53 wenye sifa za kati ikilinganishwa na wataalam 116 waliosajiliwa mwaka 2012. Hivyo, jumla ya wataalam wenye

sifa za kati walifikia 274 ikilinganishwa na wataalam 221 mwaka 2012. Kupungua kwa usajili kulitokana na wataalam 92 wa ngazi ya kati kuhitimu na kuwa katika ngazi ya juu. Serikali iliendelea na juhudi za kuhamasisha wahitimu wenye sifa zilizoainishwa kuzingatia matakwa ya Sheria Na.4 ya mwaka 2010 inayowataka kujitokeza na kusajiliwa na Bodi.

340. Katika mwaka 2013, Bodi ilifanya ukaguzi wa majenzi katika mikoa 25 ya Tanzania Bara ikilinganishwa na mikoa 21 mwaka 2012. Miradi ya ujenzi 2,752 ilikaguliwa ikilinganishwa na miradi 2,112 iliyokaguliwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 29.4. Lengo lilikuwa kuhakikisha kwamba shughuli zote za ujenzi zimebuniwa na kusimamiwa na kampuni za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi zilizosajiliwa na Bodi na zinakidhi na kufuata sheria Na.4 ya mwaka 2010. Aidha, jumla ya kampuni 65 za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi na waendelezaji 65 walilipishwa faini kwa kukiuka sheria. Vile vile, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi 6 na kampuni 6 za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi zilifutiwa usajili.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

341. Mwaka 2013, Baraza la Taifa la Ujenzi liliendelea kusambaza Sera ya Ujenzi pamoja na kutekeleza programu ya Sera ya Ujenzi kwa jumla ya wadau 4,000. Aidha, Baraza lilishirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa na mwekezaji binafsi *Lindi Express Limited* liliendelea na shughuli za ujenzi wa jengo la ghorofa 23 mtaa wa Samora jijini Dar es Salaam. Ujenzi wa jengo hilo uko katika hatua za mwisho kukamilika.

342. Mwaka 2013, Baraza liliendesha mafunzo kwa wadau 47 wa sekta ya ujenzi kuhusiana na shughuli za zabuni; menejimenti ya mikataba; usuluhishi wa migogoro; menejimenti ya madai; gharama za ujenzi wa barabara; shughuli za matengenezo pamoja na ukarabati wa majengo. Baraza liliandaa mafunzo maalum kwa ajili ya Mamlaka ya Bandari yanayojumuisha usimamizi wa miradi ya ujenzi na usuluhishi ambapo jumla ya wadau 12 walipatiwa mafunzo.

343. Mwaka 2013, Baraza lilifanya ukaguzi wa kiufundi katika miradi 191 chini ya Mfuko wa Barabara kwenye Halmashauri za wilaya na TANROADS za Mbeya, Iringa, Katavi na Rukwa. Aidha, ukaguzi wa kiufundi ulifanyika katika

matawi matatu ya benki ya NMB ya Mbagala, Kilosa na Usa river. Vilevile Baraza lilishughulikia usuluhishi wa migogoro ya miradi 57 ya ujenzi.

**Wakala wa Majengo Tanzania**

344.Mwaka 2013, Wakala wa Majengo Tanzania ulitekeleza miradi 19 ya maendeleo katika mikoa mbalimbali ikilinganishwa na miradi 23 mwaka 2012. Vilevile, Wakala uliendelea kusimamia miradi ya ujenzi wa nyumba za viongozi pamoja na ukarabati katika mikoa, miji na wilaya mbalimbali. Aidha, Wakala uliendelea na ujenzi na usimamizi wa mradi wa ujenzi wa zahanati za Mwangaza na Lindi. Vile vile, Wakala ulifanikiwa kusanifu na kusimamia jumla ya miradi ya ndani ya maendeleo 22 ambapo Idara ya Ushauri ilisanifu na kusimamia miradi 168. Miradi yote ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Wakala wa Ufundi na Umeme**

345.Katika mwaka 2013, Wakala wa Ufundi na Umeme ulitekeleza miradi 112 ya umeme; miradi 2 ya elektroniki; miradi 64 ya majokofu na viyoyozi; na miradi 72 ya ushauri ikilinganishwa na miradi 114 ya umeme; miradi 130 ya elektroniki; miradi 395 ya mabarafu na viyoyozi; na miradi 39 ya ushauri iliyotekelezwa mwaka 2012. Aidha, Wakala ulifanyia matengenezo magari 8,981 ikilinganishwa na magari 4,289 yaliotengenezwa mwaka 2012.

346.Katika mwaka 2013, Wakala ilitekeleza miradi ya maendeleo kwa kukarabati karakana ya Dodoma (awamu ya I); kukamilisha ujenzi wa ofisi za karakana ya mkoa wa Manyara (awamu I) Aidha, Wakala ulikamilisha ujenzi wa maegesho ya magari murahamba, kikumbitale na Senga katika kivuko cha Chato-Nkome (Geita); Msangamkuu na Msemo (Mtwara). Vilevile, Wakala ulinunua vivuko vipya vya Malagalasi (Kigoma) na Kilambo (Mtwara) na kukamilisha ukarabati mkubwa wa vivuko vya MV Sabasaba (Kisorya-Rugezi) na MV Chato (Geita) na kuendelea na ukarabati wa MV Geita na MV Kome I.

**MAENDELEO YA ARDHI**

**Upimaji wa Mipaka ya Vijiji**

**Mipaka ya Vijiji**

347.Katika mwaka 2013, jumla ya vijiji 145 vilipimwa mipaka yake ikilinganishwa na vijiji 256 viliyopimwa mwaka 2012. Upimaji huu wa mipaka

ya vijiji unawezesha upangaji wa matumizi ya ardhi, upimaji wa mashamba ya wanavijiji na utoaji wa hatimiliki za kimila.

**Jedwali Na. 15.4: Halmashauri za Wilaya ambazo Vijiji vilipimwa mipaka yake**

| Mwaka 2010 | | Mwaka 2011 | | Mwaka 2012 | | Mwaka 2013 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Wilaya** | **Idadi ya Vijiji** | **Wilaya** | **Idadi ya Vijiji** | **Wilaya** | **Idadi ya Vijiji** | **Wilaya** | **Idadi ya Vijiji** |
| Singida Vijijini | 35 | Bariadi | 99 | Same | 12 | Wanging' ombe | 22 |
| Bahi/Chamwino | 54 | Meatu | 29 | Longido | 10 | Mbinga | 68 |
| Tarime | 39 | Maswa | 52 | Arumeru | 28 | Nyasa | 29 |
| Rorya | 63 | Kishapu | 46 | Mbulu | 64 | Bagamoyo | 26 |
| Sengerema | 23 | Korogwe | 35 | Uyui | 66 | - | |
| Muleba | 98 | - | | Manyoni | 22 | - | |
| Misenyi | 73 | - | | Kiteto | 4 | - | |
| Karagwe | 45 | - | | Ulanga | 50 | - | |
| Ngara | 68 | - | | - | | - | |
| Kigoma Vijijini | 21 | - | | - | | - | |
| Kahama | 221 | - | | - | | - | |
| Bariadi | 22 | - | | - | | - | |
| Tabora Vijijini | 127 | - | | - | | - | |
| Babati | 5 | - | | - | | - | |
| Kilosa/Mahenge | 87 | - | | - | | - | |
| Shinyanga Vijijini/Kishapu | 226 | - | | - | | - | |
| **Jumla** | **1,207** | | **261** | | **256** | | **145** |

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mipaka ya Kimataifa**

348. Mwaka 2013, mpaka kati ya Tanzania na Burundi wenye urefu wa kilometa 448 ulifanyiwa ukaguzi. Ukaguzi huo ulifanyika katika wilaya ya Ngara – Tanzania na mikoa ya Makamba, Rutana, Ruyigi Cankunzo na Muyinga – Burundi ambako mpaka huo unapita. Aidha, kati ya Tanzania na Zambia alama 78 za kati zilisimikwa kati ya alama B576 na B579 katika kuimarisha mpaka wenye urefu wa kilometa 359 ulioko eneo la Tunduma na Nakonde. Kwa upande wa Tanzania na Msumbiji, alama 7 za mpaka wenye urefu wa kilometa 51 zilipimwa upya na alama 22 zilipimwa kwa kutumia picha za anga. Aidha,

Mkutano wa pamoja wa Kamati ya wataalamu kutoka Tanzania na Kenya ulifanyika kwa lengo la kukagua mpaka wenye urefu wa kilometa 726 katika eneo la Tarime/Kurya ambapo mpango kazi pamoja na bajeti iliandaliwa kwa ajili ya kuimarisha mpaka huo. Vilevile, Kamati ilifanya uhamasishaji kwa wananchi waishio mpakani juu ya umuhimu wa alama za mpaka.

349. Mwaka 2013, Kamati ya kitaifa ya wataalam inayoshughulika na mipaka ya kimataifa ilipitia andiko la Malawi lililohusu mpaka kati ya Tanzania na Malawi katika ziwa Nyasa. Kamati hiyo iliandaa majibu ya andiko hilo na kuyawasilisha kwenye jopo la usuluhishi la viongozi wastaafu wa nchi za SADC kwa hatua zaidi. Aidha, Tanzania ilipata nyaraka zaidi zitakazosaidia kutatua mgogoro huo kutoka Maktaba ya Umoja wa Mataifa huko Geneva Uswisi.

### Ukaguzi, Uhakiki na Utayarishaji wa Hatimiliki

350. Mwaka 2013, jumla ya milki 21,992 zilikaguliwa, kuhakikiwa na kuandaliwa hatimiliki katika kanda sita za ardhi ikilinganishwa na milki 23,610 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 6.9, kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 15.5. Aidha, ilani za ubatilisho 4,313 zilitumwa kwa wamiliki waliokiuka masharti ya upangaji wa ardhi ambapo Kanda ya Kusini Magharibi ilikuwa na ilani 1,487, Kanda ya Kati (1,321), Kanda ya Kusini (940), Kanda ya Kaskazini (514) na Kanda ya Mashariki (51).

**Jedwali Na.15.5: Utayarishaji wa Hatimiliki**

| Ofisi za Kanda | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kanda ya Mashariki | 13,269 | 15,561 | 5,848 | 7,745 | 1,0418 |
| Kanda ya Ziwa | 1,089 | 1,961 | 4,800 | 5,583 | 5,639 |
| Kanda ya Kusini Magharibi | 417 | 1,223 | 3,344 | 3,996 | 2,581 |
| Kanda ya Kaskazini | 817 | 1,400 | 4,400 | 4,204 | 1,948 |
| Kanda ya Kati | 132 | 600 | 451 | 687 | 328 |
| Kanda ya Kusini Mashariki | 59 | 425 | 805 | 1,395 | 1,078 |
| **Jumla** | **15,783** | **21,170** | **19,648** | **23,610** | **21,992** |

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji na Hati za Hakimiliki za Kimila**

351. Mwaka 2013, jumla ya vyeti 3,664 vya ardhi ya vijiji vilitolewa ikilinganishwa na vyeti 1,950 vilivyotolewa mwaka 2012. Aidha, jumla ya hatimiliki za kimila 8,730 zilitolewa ikilinganishwa na hatimiliki 21,169 zilizotolewa mwaka 2012.

**Usajili wa Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria**

352. Mwaka 2013, jumla ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 65,740 zilisajiliwa ikilinganishwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria 64,632 zilizosajiliwa mwaka 2012. Kati ya hizo, hatimiliki 23,241 na nyaraka 33,495 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334) ikilinganishwa na hatimiliki 27,452 na nyaraka 28,990 zilizosajiliwa mwaka 2012. Vile vile, nyaraka 7,148 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 117) ikilinganishwa na nyaraka 7,280 zilizosajiliwa mwaka 2012. Aidha, mwaka 2013, nyaraka 1,856 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali zinazohamishika (Sura ya 210) ikilinganishwa na nyaraka 910 zilizosajiliwa mwaka 2012.

353. Mwaka 2013, jumla ya taarifa za uthamini 6,067 ziliidhinishwa ambapo taarifa za uthamini wa kawaida zilikuwa 5,945 na taarifa za uthamini wa fidia zilikuwa 122. Aidha, uthamini wa mali za wananchi 23,508 walioathiriwa na miradi ya uwekezaji kama vile upanuzi wa migodi, maeneo ya barabara, njia za maji, umeme, gesi na maeneo ya huduma za jamii (shule na hospitali) ulitekelezwa.

**Upimaji wa Mashamba na Viwanja**

354. Mwaka 2013, jumla ya viwanja 68,800 na mashamba 711 yaliidhinishwa ikilinganishwa na viwanja 34,049 na mashamba 2,169 yaliyopimwa na kuidhinishwa mwaka 2012. Mchanganuo wa viwanja na mashamba yaliyoidhinishwa kimkoa ni kama unavyooneshwa katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 15.6: Upimaji wa Viwanja na Mashamba**

| Mikoa | Milki zilizoidhinishwa mwaka 2011 | | Milki zilizoidhinishwa mwaka 2012 | | Milki zilizoidhinishwa mwaka 2013 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Viwanja | Mashamba | Viwanja | Mashamba | Viwanja | Mashamba |
| Arusha | 1,294 | 144 | 1,799 | 84 | 3,225 | 11 |
| Pwani | 1,714 | 134 | 4,034 | 310 | 13,210 | 134 |
| Dar es Salaam | 2,425 | 0 | 3,781 | 0 | 13,359 | 0 |
| Dodoma | 345 | 13 | 501 | 0 | 618 | 1 |
| Geita | | | | | 1,731 | 0 |
| Iringa | 2,102 | 31 | 1,401 | 9 | 2,307 | 14 |
| Kagera | 236 | 108 | 3,290 | 35 | 346 | 15 |
| Kigoma | 448 | 0 | 7 | 7 | 133 | 1 |
| K/njaro | 1,043 | 95 | 2,087 | 195 | 2,914 | 21 |
| Katavi | | | | | 1961 | 0 |
| Lindi | 185 | 19 | 274 | 1 | 2,107 | 1 |
| Manyara | 1,075 | 2 | 1,901 | 0 | 907 | 2 |
| Mara | 818 | 22 | 625 | 14 | 978 | 7 |
| Mbeya | 1,361 | 40 | 1,708 | 76 | 572 | 8 |
| Morogoro | 1,988 | 20 | 2,805 | 1,042 | 3,542 | 444 |
| Njombe | | | | | 1,827 | 2 |
| Mtwara | 1,612 | 2 | 1,203 | 2 | 684 | 2 |
| Mwanza | 5,060 | 20 | 4,742 | 22 | 7,645 | 8 |
| Rukwa | 280 | 6 | 467 | 0 | 683 | 2 |
| Ruvuma | 549 | 1 | 158 | 315 | 0 | 15 |
| Shinyanga | 1052 | 6 | 975 | 0 | 1,324 | 0 |
| Singida | 848 | 0 | 120 | 0 | 356 | 0 |
| Simiyu | | | | | 673 | 0 |
| Tabora | 624 | 23 | 599 | 40 | 4,111 | 0 |
| Tanga | 1,729 | 20 | 1,572 | 17 | 3,587 | 23 |
| **Jumla** | **26,788** | **706** | **34,049** | **2,169** | **68,800** | **711** |

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya**

355.Mwaka 2013, jumla ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya wilaya za Ngorongoro, Tunduru, Mpanda, Muleba, Karagwe, Kyera na Ngara yaliundwa. Kuundwa kwa mabaraza hayo kunafanya kuwepo na jumla ya Mabaraza 49 tangu Sheria ya Mahakama za Ardhi ianze kutumika mwaka 2003. Aidha, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yaliendelea kushughulikia mashauri 18,263 ya ardhi na nyumba yaliyokuwepo mwaka 2012 na mengine 13,275 yaliyofunguliwa mwaka 2013. Vile vile, mashauri 13,268 yaliamuliwa na mashauri 18,270 yaliendelea kusikilizwa mwaka 2013.

**Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

356. Mwaka 2013, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilitayarisha mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 85 katika halmashauri za Newala, Rorya, Tarime, Mpanda na Muleba ikilinganishwa na vijiji 142 mwaka 2012. Katika vijiji hivyo, maeneo kwa ajili ya huduma za jamii pamoja na hifadhi za vyanzo vya maji, misitu, ufugaji, wanyamapori, kilimo cha umwagiliaji na mashamba makubwa yalitengwa kwa kuwashirikisha wananchi.

**MAENDELEO YA MAKAZI**

**Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara**

357. Mwaka 2013, Shirika la Nyumba la Taifa liliendelea na utekelezaji wa miradi 23 ya ujenzi wa nyumba za makazi yenye jumla ya nyumba 1,807 ikilinganishwa na miradi kumi ya ujenzi yenye jumla ya nyumba za makazi 823 mwaka 2012. Aidha, Shirika liliendelea na utekelezaji wa miradi minne ya majengo ya biashara kwenye maeneo mbalimbali nchini. Miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi iliyotekelezwa ilijumuisha nyumba za gharama nafuu 859 ambapo nyumba 193 zilikamilika na nyumba za gharama ya kati na juu 948 ambapo nyumba 456 zilikamilika. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2013, jengo moja la biashara lenye ghorofa 10 lilikamilika na ujenzi wa majengo mengine matatu unaendelea. Aidha, Shirika liliandaa mpango kabambe wa ujenzi wa nyumba katika maeneo ya Burka- Arusha (ekari 579.2), Usa River-Arusha (ekari 296), Uvumba – Dar es Salaam (ekari 202) na Kawe – Dar es Salaam (ekari 214).

**Jedwali Na.15.7: Miradi ya Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Majengo ya Biashara katika mwaka 2013**

| Miradi inayotekelezwa | Idadi ya Nyumba | | |
|---|---|---|---|
| | Gharama Nafuu | Gharama ya Kati na Juu | Miradi ya Majengo ya Biashara (Idadi ya Sakafu) |
| Na. 237 Kibada, Kigamboni - DSM | 193 | - | - |
| Medeli (Awamu ya II) - Dodoma | - | 150 | - |
| Na. 574 Mtaa wa Mindu, Upanga - DSM | - | 60 | - |
| Ubungo – DSM | - | 80 | - |
| Mchikichini – Ilala, DSM | - | 48 | - |
| Levolosi - Arusha | - | 98 | - |
| Chang'ombe (Awamu ya I) DSM | - | 20 | - |
| Na.1 Ufukoni/Alli Hassani Mwinyi, Upanga - DSM | - | - | 10 |
| **Jumla** | **193** | **456** | **10** |

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

## SURA YA 16

## MAWASILIANO NA UCHUKUZI

### Kiwango cha Ukuaji

358. Shughuli za kiuchumi za uchukuzi zilikua kwa asilimia 6.2 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2012. Kwa upande mwingine, shughuli za kiuchumi za mawasiliano zilikua kwa asilimia 22.8 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 20.6 mwaka 2012. Kupungua kwa shughuli za kiuchumi za uchukuzi kulitokana na kupungua kwa usafirishaji wa shehena za mizigo kwa njia ya anga na reli. Aidha, kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi za mawasiliano kulitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta hiyo na kuongezeka kwa matumizi ya simu za mkononi. Mwaka 2013, shughuli za kiuchumi za uchukuzi zilichangia asilimia 5.8 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2012. Pato la Taifa kutokana na shughuli za kiuchumi za mawasiliano liliongozeka na kuwa asilimia 2.4 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2012.

### UCHUKUZI

### Usafiri wa Barabara

359. Mwaka 2013, jumla ya leseni za usafirishaji 37,924 zilitolewa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) kwa mabasi ya abiria, sawa na ongezeko la asilimia 14.3 ikilinganishwa na leseni za usafirishaji 33,187 zilizotolewa mwaka 2012. Aidha, mwaka 2013, leseni 63,519 za magari ya mizigo zilitolewa ikilinganishwa na leseni 62,056 zilizotolewa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 2.3. Mchanganuo wa idadi ya leseni za usafirishaji zilizotolewa kwa vyombo vya usafirishaji kwa njia ya barabara unaonyeshwa katika jedwali Na. 16.1.

**Jedwali Na. 16.1: Idadi ya Leseni za Magari ya Abiria na Mizigo kwa kila Mkoa**

| Mkoa | Mwaka 2012 | | | Mwaka 2013 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Abiria | Mizigo | Jumla | Abiria | Mizigo | Jumla |
| Arusha | 5,278 | 5,795 | 11,073 | 5711 | 5667 | 11378 |
| Dar / Pwani | 9,685 | 30,506 | 40,191 | 10283 | 30759 | 41042 |
| Dodoma | 1,647 | 1,486 | 3,133 | 1887 | 1824 | 3711 |
| Iringa | 1,004 | 1,261 | 2,265 | 1140 | 1500 | 2640 |
| Kagera | 796 | 912 | 1,708 | 1040 | 962 | 2002 |
| Kigoma | 877 | 261 | 1,138 | 741 | 273 | 1014 |
| Kilimanjaro | 3,585 | 3,408 | 6,993 | 3955 | 4165 | 8120 |
| Lindi | 137 | 71 | 208 | 245 | 220 | 465 |
| Manyara | 196 | 399 | 595 | 577 | 491 | 1068 |
| Mara | 505 | 351 | 856 | 719 | 441 | 1160 |
| Mbeya | 1,420 | 2,500 | 3,920 | 1573 | 2363 | 3936 |
| Morogoro | 1,981 | 2,137 | 4,118 | 2295 | 2251 | 4546 |
| Mtwara | 319 | 464 | 783 | 269 | 365 | 634 |
| Mwanza | 2,621 | 4,868 | 7,489 | 2596 | 3563 | 6159 |
| Rukwa | 188 | 593 | 781 | 328 | 502 | 830 |
| Ruvuma | 396 | 449 | 845 | 669 | 572 | 1241 |
| Shinyanga | 286 | 1,046 | 1,332 | 725 | 1487 | 2212 |
| Singida | 680 | 1,256 | 1’936 | 722 | 1269 | 1991 |
| Tabora | 371 | 673 | 1,044 | 377 | 593 | 970 |
| Tanga | 1,177 | 3,610 | 4,787 | 1267 | 3692 | 4959 |
| Geita | 34 | 6 | 40 | 400 | 69 | 469 |
| Njombe | 3 | 1 | 4 | 236 | 339 | 575 |
| Katavi | 1 | 3 | 4 | 116 | 118 | 234 |
| Simiyu | - | - | - | 53 | 34 | 87 |
| **JUMLA** | **33,187** | **62,056** | **95,243** | **37,924** | **63,519** | **101,443** |

Chanzo: SUMATRA

360.Mwaka 2013, jumla ya ajali za barabarani 23,842 ziliripotiwa ikilinganishwa na ajali 23,578 zilizoripotiwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 1.1. Pikipiki ndizo zilizoripotiwa kuwa na ajali zaidi ikilinganishwa na vyombo vingine vya usafiri ikiwa zimechangia asilimia 28.7 ya ajali zote za barabarani kwa mwaka 2013. Hali ya ajali barabarani kwa kipindi cha mwaka 2012 hadi 2013 ni kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 16.2.

**Jedwali Na. 16.2: Ajali za Barabarani katika mwaka 2012 -2013**

| Aina ya Vyombo | 2012 | | 2013 | |
|---|---|---|---|---|
| | Ajali | % | Ajali | % |
| Mabasi ya Mjini | 1831 | 7.8 | 1630 | 6.8 |
| Mabasi Mengineyo | 731 | 3.1 | 723 | 3.0 |
| Malori | 2408 | 10.2 | 2125 | 8.9 |
| Pikipiki | 5763 | 24.4 | 6831 | 28.7 |
| Magari Mengineyo | 12845 | 54.5 | 12533 | 52.6 |
| **Jumla ya Ajali** | **23,578** | | **23,842** | |

Chanzo: Polisi-Usalama Barabarani

### Usafiri wa Majini

361. Mwaka 2013, SUMATRA ilifanya ukaguzi wa vyombo vidogo vya majini 6,355 ikilinganishwa na ukaguzi wa vyombo 4,519 mwaka 2012. Aidha, ukaguzi kwa vyombo vikubwa 168 vyenye uwezo wa kubeba tani 50 na zaidi ulifanyika mwaka 2013 ikilinganishwa na kaguzi 285 zilizofanyika mwaka 2012.

### Kampuni ya Reli Tanzania (TRL)

362. Kampuni ya Reli Tanzania ilisafirisha tani 154,341 za mizigo mwaka 2013 ikilinganishwa na tani 198,024 zilizosafirishwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 22.1. Aidha, abiria 492,872 walisafirishwa mwaka 2013 ikilinganishwa na abiria 505,223 waliosafirishwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 2.5. Kupungua kwa idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa kulitokana na uhaba na uchakavu wa mabehewa na vichwa vya treni. Vile vile, abiria wengine walitumia usafiri wa mabasi baada ya barabara ziendazo mikoani kuimarishwa au kukamilika.

### Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)

363. Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ilisafirisha jumla ya tani 218,285 za mizigo mwaka 2013 ikilinganishwa na tani 339,094 zilizosafirishwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 35.6. Aidha, mwaka 2013, TAZARA ilisafirisha abiria 703,349 ikilinganishwa na abiria 793,231 waliosafirishwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 10.5.

**Usafiri wa Anga**

**Mamlaka ya Usafiri wa Anga**

364.Mwaka 2013, watoa huduma wa Usafiri wa Anga wenye leseni walikuwa 42 ikilinganishwa na watoa huduma 54 waliokuwepo mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 22.2. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya watoa huduma kutokidhi masharti ya utoaji huduma za usafiri wa anga na hivyo kufutiwa leseni za kuendelea kutoa huduma hiyo.  Aidha, idadi ya abiria wanaowasili na kuondoka katika viwanja vya ndege nchini iliendelea kuongezeka kutoka abiria 4,068,982 mwaka 2012 hadi abiria  4,670,380  mwaka 2013, sawa na  ongezeko la asilimia 14.8. Ongezeko hili lilitokana na: Kampuni ya Fastjet kuanza kutoa huduma nchini; Kufunguliwa kwa kiwanja cha ndege cha Songwe- Mbeya; Kukarabatiwa kwa viwanja vya ndege katika mkoa wa Kigoma, Arusha, Mpanda, Musoma na Tabora; na kuongezeka kwa utalii nchini.

**Kielelezo Na. 16.1: Idadi ya Abiria Waliowasili na Kuondoka Nchini**




| | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kimataifa | 1,262,216 | 1,384,855 | 1,604,148 | 1,871,732 | 1,876,311 |
| Ndani ya nchi | 1,492,139 | 1,642,657 | 1,833,460 | 2,197,250 | 2,794,069 |
| Jumla | 2,754,355 | 3,027,512 | 3,437,608 | 4,068,982 | 4,670,380 |

Chanzo: TCAA

365.Mwaka 2013, safari za ndege ziliongezeka hadi kufikia 238,384 kutoka safari 227,708, mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 4.7. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa idadi ya safari katika ratiba ya wiki.

**Kielelezo Na. 16.2: Idadi ya Safari za Ndege Mwaka 2009-2013**




| | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kimataifa | 23,611 | 28,941 | 37,102 | 35,978 | 39,258 |
| Ndani ya nchi | 143,999 | 152,299 | 170,142 | 191,730 | 199,126 |
| Jumla | 167,610 | 181,240 | 207,244 | 227,708 | 238,384 |

Chanzo: TCAA

366.Mwaka 2013, tani 28,448 za mizigo zilisafirishwa kwa njia ya anga ikilinganishwa na tani 52,790 za mizigo zilizosafirishwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 46.1. Hii ilitokana na kupungua kwa uingizaji wa vifaa/mitambo kutoka nje ya nchi kwa ajili ya utafutaji na uchimbaji wa gesi asilia mkoani Mtwara na kupungua kwa mashirika ya ndege za kigeni nchini kama British Air na KLM.

**Kielelezo Na.16.3: Tani za Mizigo Zilizosafirishwa Mwaka 2009-2013**




| | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kimataifa | 24,705 | 25,837 | 37,084 | 45,980 | 26,524 |
| Ndani ya nchi | 2,532 | 3,024 | 2,517 | 6,810 | 1,924 |
| Jumla | 27,237 | 28,861 | 39,601 | 52,790 | 28,448 |

Chanzo: TCAA

**Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania**

367.Mwaka 2013, idadi ya safari za ndege katika viwanja vinavyosimamiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania ilikuwa 154,165 ikilinganishwa na safari 152,033 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Hii ilitokana na mashirika ya ndege kuongeza idadi ya miruko na mituo. Aidha, idadi ya abiria waliosafiri kupitia katika viwanja vinavyosimamiwa na Mamlaka iliongezeka kwa asilimia 13.0 kutoka abiria 2,895,869 mwaka 2012 hadi abiria 3,272,619 mwaka 2013. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji, biashara na utalii na pia uboreshwaji wa viwanja vya ndege nchini. Hata hivyo, mizigo iliyopitishwa katika viwanja vinavyosimamiwa na Mamlaka ilipungua kwa asilimia 13.2 kutoka tani 27,105 mwaka 2012 hadi tani 23,533.1 mwaka 2013. Upungufu huo ulitokana na idadi kubwa ya mizigo kusafirishwa kwa kutumia njia nyingine za usafiri.

**Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania**

368.Mwaka 2013, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilihudumia shehena yenye uzito wa tani milioni 13.713 ikilinganishwa na tani milioni 12.084 iliyohudumiwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 13.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shehena ya mizigo na matumizi ya kituo kimoja cha kufanya kazi ambapo wadau wote hufanya kazi katika jengo moja. Mwaka 2013, bandari ya Dar es salaam ilihudumia asilimia 91.4 ya shehena yote iliyopitia katika bandari zilizo chini ya Mamlaka.

**Jedwali Na. 16.3: Shehena Zilizosafirishwa (tani '000)**

| Kituo (Bandari) | 2011/2012 | 2012/2013 |
|---|---|---|
| **Bandari Kuu za Mwambao** | | |
| Dar es Salaam | 10,865.22 | 12,530.68 |
| Tanga | 644.61 | 457.54 |
| Mtwara | 235.17 | 203,.64 |
| **Jumla ndogo** | **11,744.99** | **13,191.86** |
| **Bandari Ndogo na Bandari za Maziwa Makuu** | | |
| Kilwa, Lindi na Mafia | 31.2 | 49.15 |
| Mwanza | 211.94 | 360. |
| Kigoma | 73.79 | 81.88 |
| Kyela | 22.09 | 29.61 |
| **Jumla ndogo** | **307.81** | **472.39** |
| **Jumla Kuu** | **12,084.00** | **13,713.39** |

Chanzo: TPA

369.Mwaka 2013, kitengo cha kupakua makasha (TICTS) kilihudumia makasha 399,000, sawa na ongezeko la asilimia 12.3 ikilinganishwa na makasha 355,105 yaliyohudumiwa mwaka 2012. Ongezeko hilo lilitokana na wateja wa nchi jirani kutumia bandari ya Dar es Salaam kufuatia kuongezeka kwa biashara ya kikanda. Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka ilihudumia jumla ya abiria 1,804,521 ikilinganishwa na abiria 1,913,479 waliohudumiwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 5.7.

**Jedwali Na 16.4: Idadi ya Abiria Waliohudumiwa 2009 - 2013**

| **Bandari** | **2008/09** | **2009/10** | **2010/11** | **2011/12** | **2012/13** |
|---|---|---|---|---|---|
| DSM | 829,417 | 892,465 | 1,008,731 | 1,342,875 | 1,373,146 |
| Tanga | 18,656 | 16,670 | 23,287 | 12,747 | 7,730 |
| Mwanza | 869,534 | 819,730 | 593,342 | 524,457 | 395,808 |
| Kigoma | 22,675 | 19,626 | 21,033 | 25,066 | 20,063 |
| Kyela | 14,484 | 12,607 | 9,913 | 8,334 | 7,774 |
| **Jumla** | **1,754,766** | **1,761,098** | **1,656,306** | **1,913,479** | **1,804,521** |

Chanzo: TPA

**Muda wa Meli Kukaa Bandarini**

370.Mwaka 2013, muda wa meli kukaa bandarini katika kitengo cha makasha ulipungua kutoka siku 8.5 hadi siku 4.0, sawa na kuongezeka kwa ufanisi kwa asilimia 52.9. Kwa upande wa mizigo ya kawaida, muda wa meli kukaa bandarini uliongezeka kwa asilimia 22.7 kutoka siku 4.4 hadi siku 5.4. Ongezeko hilo lilitokana na upungufu wa vifaa vya kuhudumia mizigo ya kawaida na pia kufungwa kwa gati Na.8 kwa ajili ya kupisha matengenezo ya kusimika vifaa vya kuhudumia meli. Aidha, muda wa meli kukaa bandarini katika kitengo cha mafuta (Kurasini Oil Jet) uliongezeka kwa asilimia 46.3 kutoka siku 4.1 hadi siku 6.0. Vile vile, muda wa meli kukaa bandarini katika kitengo cha mafuta (Single Point Mooring) uliongezeka kutoka siku 4.2 mwaka 2012 hadi siku 6.4 mwaka 2013. Kuongezeka kwa muda wa meli kukaa bandarini katika vitengo vya mafuta kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo: uhaba wa maeneo ya kuhifadhia shehena ya mafuta; Kampuni zinazoagiza shehena za mafuta kuchelewa kulipia shehena husika na; ucheleweshaji wa nyaraka kuhusu meli na shehena iliyobebwa.

**Shehena kwenda Nchi Jirani**

371.Mwaka 2013, jumla ya tani milioni 4.123 za mizigo ya nchi jirani zilihudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam, sawa na ongezeko la asilimia 6.0 ikilinganishwa na tani milioni 3.893 za mizigo zilizohudumiwa mwaka 2012. Shehena ya mizigo ya nchi jirani inayohudumiwa katika bandari ya Dar es salaam imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 16.2 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitano iliiyopita.

**Jedwali Na. 16.5: Shehena ya Nchi Jirani**

| Nchi | 2008/09 | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 |
|---|---|---|---|---|---|
| Zambia | 1,089,045 | 1,112,283 | 1,500,459 | 1,627,537 | 1,858,718 |
| DR Congo | 544,391 | 568,275 | 800,986 | 965,639 | 965,377 |
| Burundi | 256,089 | 327,468 | 384,648 | 336,410 | 308,180 |
| Rwanda | 136,560 | 261,068 | 301,778 | 436,029 | 636,998 |
| Malawi | 111,372 | 131,532 | 136,375 | 92,869 | 93,411 |
| Uganda | 28,133 | 32,612 | 45,453 | 74,670 | 190,876 |
| Nyinginezo | 166,093 | 8,319 | 303,571 | 360,059 | 70,148 |
| **JUMLA** | **2,331,683** | **2,441,557** | **3,473,269** | **3,893,213** | **4,123,708** |

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

### Uchukuzi kwenye Maziwa

#### Kampuni ya Huduma za Meli

372.Mwaka 2013, jumla ya abiria 279,987 walisafirishwa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ikilinganishwa na abiria 217,799 waliosafirishwa mwaka 20I2, sawa na ongezeko la asilimia 28.6. Ongezeko hilo lilitokana na uboreshwaji wa huduma zinazotolewa na Kampuni ya MSCL na pia kufanyiwa matengenezo meli ya MV Clarias. Hata hivyo, usafirishaji wa mizigo ulipungua kwa asilimia 26.2 kutoka tani 124,319 za mizigo zilizosafirishwa mwaka 2012, hadi tani 91,788 za mizigo zilizosafirishwa mwaka 2013. Sababu za kupungua kwa usafirishaji wa mizigo ni pamoja na kuimarika kwa barabara katika sehemu mbalimbali za nchi kulikosababisha baadhi ya wateja kutumia njia hiyo kusafirisha mizigo yao na pia kuzorota kwa usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli ya kati.

#### Kampuni ya Meli ya China na Tanzania

373.Mwaka 2013, Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP) ilisafirisha shehena jumla ya tani 330,000 ikilinganishwa na tani 334,000 za shehena zilizosafirishwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 1.2. Upungufu huo ulitokana na ushindani mkubwa kwenye soko la mizigo ambalo limetokana na ongezeko kubwa la meli mpya.

#### Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

374.Mwaka 2013, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ilianzisha vituo kumi na moja (11) vya hali ya hewa vinavyojiendesha vyenyewe katika maeneo ya

Moshi (Kisangesangeni, Maweni, Uparo, na Masila), Lindi, Nachingwea, Tunduru, Msata (Bagamoyo), Nzega (Tabora), Makete (Njombe), na Kisarawe. Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo ilinunua kompyuta kubwa kwa ajili ya kuchambua data za hali ya hewa ambapo taratibu za kuifunga ziko katika hatua za mwisho. Uchambuzi huo utasaidia kutoa utabiri katika maeneo madogo madogo ya nchi ikiwemo Ziwa Nyasa na Tanganyika.

**Huduma za Mawasiliano**

**Shirika la Posta Tanzania**

375. Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua ndani ya nchi 16,801,576 mwaka 2013, ikilinganishwa na barua 16,983,438 zilizosafirishwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 1.1. Aidha, katika kipindi hicho, barua 8,823,674 zilitumwa nje ya nchi ikilinganishwa na barua 9,001,302 zilizotumwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 2.0. Upungufu kwa maeneo yote mawili ulitokana na ukuaji wa matumizi ya TEHAMA ambapo watumiaji hupendelea zaidi mawasiliano kwa njia ya mtandao.

376. Idadi ya vifurushi vilivyosafirishwa ndani ya nchi mwaka 2013 ilikuwa 29,431 ikilinganishwa na vifurushi 26,685 vilivyotumwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 10.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa nyenzo za usafirishaji na kukua kwa biashara hususan iliyotokana na kusafirisha vifurushi vya matokeo ya Sensa ya watu na Makazi ya mwaka 2012. Aidha, vifurushi vilivyotumwa nje ya nchi mwaka 2013 vilikuwa 8,983 ikilinganishwa na vifurushi 8,709 vilivyotumwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 3.1.

377. Mwaka 2013, Shirika lilituma nchini rejesta 511,598 ikilinganishwa na rejesta 979,012 zilizotumwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 47.7. Upungufu huo ulitokana na kuwepo kwa kiasi kikubwa cha rejesta za Baraza la Mitihani (NECTA) zilizotumwa kwa mkupuo mwaka 2012, hali ambayo haikujirudia mwaka 2013. Aidha, rejesta zilizotumwa nje ya nchi mwaka 2013 zilikuwa 56,429 ikilinganishwa na rejesta 44,646 zilizotumwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 26.4. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa huduma baada ya kuunganishwa na huduma ya mtandao ya “track and Trace’’.

378. Mwaka 2013, jumla ya nyaraka na vipeto 620,478 zilitumwa kwa njia ya haraka (EMS) ikilinganishwa na nyaraka 682,979 zilizotumwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 9.2. Aidha, idadi ya nyaraka na vipeto vya haraka vilivyotumwa nje ya nchi mwaka 2013 ilikuwa 17,138 ikilinganishwa na nyaraka 34,028 zilizotumwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 49.6. kupungua kwa vifurushi na vipeto vilivyosafirishwa ndani na nje ya nchi kulitokana na kuongezeka kwa ushindani.

379. Mwaka 2013, huduma ya usambazaji wa barua za haraka ndani ya miji (Intracity) City Urgent Mail (Pcum) ilipungua ambapo barua/ nyaraka 80,409 zilipokelewa na kusambazwa ikilinganishwa na barua/nyaraka 109,296 zilizotumwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 26.4. Upungufu huo ulitokana na wateja kubadili mifumo ya utumaji nyaraka na hivyo kuacha matumizi ya mfumo huo.

380. Mwaka 2013, jumla ya miamala ya fedha iliyotumwa kupitia mtandao wa kompyuta (Electronic Money Transfer) ilikuwa 2,160 ikilinganishwa na miamala 14,080 iliyotumwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 84.7. Upungufu huo ulitokana na wateja kupendelea kutuma fedha kwa njia ya simu za viganjani. Aidha, mwaka 2013, miamala ya fedha 286 ilitumwa kupitia mfumo wa kimataifa wa utumaji fedha ikilinganishwa na miamala 601 iliyotumwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 52.4. Upungufu huo ulitokana na changamoto ya ushindani kutoka makampuni mengine ya kimataifa.

381. Mwaka 2013, utumaji wa fedha kwa hawala za posta ulishuka kwa asilimia 9.5 na kufikia hawala 684 ikilinganishwa na hawala 756 zilizotumwa mwaka 2012. Upungufu huo ulitokana na kuendelea kuimarika kwa mifumo ya utumaji fedha kwa kutumia mitandao ya kompyuta.

382. Mwaka 2013, wateja 182,526 walipata huduma ya kufanya malipo kwa uwakala ya “Post Giro” ndani ya nchi ikilinganishwa na wateja 176,017 waliohudumiwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 3.7. hii ilitokana na kuongezeka kwa wanahisa katika soko la hisa la Dar es salaam. Huduma hii hutumika kulipa pensheni za wastaafu na gawio za hisa za makampuni yaliyoorodheshwa katika soko la Hisa Dar es salaam.

**Mawasiliano kwa Njia ya Sauti na Takwimu**

383. Mwaka 2013, idadi ya makampuni yaliyokuwa yanayotoa huduma za mawasiliano kwa njia ya sauti yalikuwa 7 kama ilivyokuwa miaka miwili iliyopita. Makampuni hayo ni TTCL, Vodacom, Airtel, Tigo, Zantel, Benson Online na Devotel (Sasatel).

384. Hadi Desemba 2013, watumiaji wa simu za viganjani walikuwa 27,442,823 ikilinganishwa na watumiaji 27,219,283 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 1. Hata hivyo, idadi hii inajumuisha watumiaji wanaomiliki zaidi ya kadi moja ya mtandao wa simu. Kampuni ya simu ya Vodacom ndiyo yenye idadi kubwa ya wateja ambao ni asilimia 37.5 ya watumiaji wote wa simu za viganjani ikifuatiwa na Airtel asilimia 32.8. Aidha, watumiaji wa simu za mezani walipungua kwa asilimia 6.4 kutoka watumiaji 176,367 mwaka 2012 hadi watumiaji 164,999 mwaka 2013. Vile vile, idadi ya makampuni yanayotoa huduma za mawasiliano kwa njia ya takwimu (data) iliongezeka kutoka makampuni 84 mwaka 2012 hadi makampuni 91 mwaka 2013.

**Jedwali Na. 16.6: Idadi ya Wanaotumia Simu za Viganjani na Mezani**

| Kampuni za Simu | Idadi wa Wateja | | | Badiliko % |
|---|---|---|---|---|
| | 2011 | 2012 | 2013 | |
| VODACOM | 11,625,773 | 9,357,672 | 10,288,972 | 10% |
| TIGO | 5,450,766 | 6,370,796 | 6,297,288 | -1.2% |
| AIRTEL | 6,993,418 | 8,356,095 | 8,995,824 | 8% |
| ZANTEL MOBILE | 1,522,902 | 3,073,670 | 1,808,380 | -41% |
| ZANTEL FIXED | 1,699 | 10,219 | 6,064 | -41% |
| TTCL MOBILE | 66,214 | 55,515 | 51,831 | -7% |
| TTCL FIXED | 159,364 | 166,148 | 158,935 | -4.3% |
| BENSON ONLINE | 1,558 | 725 | 528 | -27% |
| SASATEL | 5,824 | 4,810 | - | - |
| **Jumla** | **25,827,518** | **27,395,650** | **27,607,822** | 1% |
| **Watumiaji wa Simu za Mkononi** | **25,666,455** | **27,219,283** | **27,442,823** | 1% |
| **Watumiaji wa Simu za Mezani** | **161,063** | **176,367** | **164,999** | -6.4% |

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

## Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

### Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

385. Mwaka 2013, Serikali ilianza utekelezaji wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Awamu ya III baada ya kumaliza awamu mbili za kwanza mwaka 2012. Awamu hii inahusu: ujenzi wa vituo mahiri vya kutunzia kumbukumbu (*Data Centres);* mtandao wa miundombinu ya itifaki ya kuunganisha huduma mbalimbali za mawasiliano *[Internet Protocol-Multiprotocol Label Switching (IP-MPLS)* Network]; upanuzi wa Mkongo Awamu ya I na II na kuunganisha Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**Uendelezaji wa Rasilimali Watu**

386.Mwaka 2013/14, Taasisi ya Nelson Mandela ya Arusha ilidahili wanachuo 120 ikilinganishwa na wanachuo 135 waliodailiwa mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 11.1. Kati ya hao waliodailiwa mwaka 2013, wanachuo 72 walikuwa wa shahada ya uzamili na wanachuo 48 walikuwa wa shahada ya uzamivu. Aidha, mwaka 2013, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilidahili jumla ya wanachuo 3,442 ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.1 ikilinganishwa na wanachuo 3,156 waliodahiliwa mwaka 2012. Idadi ya wanachuo 3,442 inajumuisha wanachuo 2,333 wa stashahada na wanachuo 1,109 wa shahada ya kwanza. Vile vile, mwaka 2013, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam ilidahili wanachuo wapya 1,371 ikilinganishwa na wanachuo 1,243 waliodailiwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 10.3. Kati ya wanachuo waliodahiliwa mwaka 2013/14, wanachuo 19 walikuwa wa cheti cha habari na mawasiliano, 872 wa stashahada ya uhandisi na 499 wa shahada ya uhandisi.

**Udhibiti wa Mionzi**

387.Mwaka 2013, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) ilipokea na kutathmini maombi 280 ya leseni za matumizi ya mionzi ikilinganishwa na maombi 195 yaliyopokelewa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 43.6. Maombi yote yalikubaliwa baada ya kukidhi matakwa na vigezo vya kinga na matumizi salama ya mionzi. Aidha, Tume ilifanya ukaguzi wa vituo 99 ambapo vituo 58 sawa na asilimia 58.5 vilikidhi matakwa ya sheria ya mionzi na kanuni zake. Vituo 5 vilifungiwa hadi virekebishe kasoro kubwa zilizooneka na vituo 36 vilipewa muda kurekebisha kasoro ndogondogo zilizoonekana kwa muda. Aidha, mwaka 2013, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilipima jumla ya sampuli 5,616 za vyakula ikilinganishwa na sampuli 1,650 zilizopimwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 70.6. Vile vile, Tume ilikagua migodi 7 ikilinganishwa na migodi 10 iliyokaguliwa mwaka 2012 na kuthibitisha kuwa kiasi cha mionzi ya gesi ya Radon katika migodi hiyo kipo katika kiwango kinachokubalika.

**Vyombo vya Habari**

388.Mwaka 2013, jumla ya majarida na magazeti 35 yalisajiliwa, ikilinganishwa na usajili wa magazeti na majarida 28 mwaka 2012, sawa na ongezeko la

asilimia 25.0. Hata hivyo, jumla ya magazeti 550 yaliyosajiliwa hapo awali yapo katika mchakato wa kufutwa kwa sababu mbalimbali, ikiwemo ya kutochapishwa kwa muda mrefu. Aidha, hadi kufikia Desemba 2013, vituo 2 vya radio na kituo 1 cha runinga vilisajiliwa.

**Jedwali 16.7: Idadi ya Vituo vya Radio na Televisheni**

| Mwaka | Vituo vya Radio | Vituo vya Televisheni |
|---|---|---|
| 2005 | 35 | 11 |
| 2006 | 11 | 14 |
| 2007 | 01 | 01 |
| 2008 | 04 | 00 |
| 2009 | 02 | 00 |
| 2010 | 07 | 00 |
| 2011 | 13 | 00 |
| 2012 | 0 | 00 |
| 2013 | 02 | 01 |

Chanzo: Idara ya Habari

## SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jedwali Na. 67

| Maelezo | Kipimo | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urefu wa Reli | kms. | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 |
| Magari ya Moshi: | Namba | 103 | 99 | 99 | 84 | 45 | 43 | 25 | 22 | 20 | 45 |
| Mvuke | Namba | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Dizeli | Namba | 102 | 98 | 98 | 83 | 45 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mainlain | | 77 | 73 | 73 | 62 | 5 | 5 | 21 | 19 | 16 | 38 |
| Shunting | | 25 | 25 | 25 | 21 | 40 | 38 | 4 | 3 | 4 | 7 |
| Jumla ya mabehewa: | Namba | 1592 | 1951 | 1828 | 1912 | 1648 | 1357 | 1071 | 1326 | 1162 | 1200 |
| Abiria | Namba | 83 | 82 | 54 | 102 | 45 | 68 | 50 | 53 | 36 | 91 |
| Mizigo ya kawaida | Namba | 1104 | 1464 | 1369 | 1369 | 1190 | 1093 | 648 | 658 | 635 | 681 |
| Mafuta | Namba | 164 | 164 | 164 | 208 | 244 | 178 | 179 | 335 | 208 | 178 |
| Mifugo | Namba | 69 | 69 | 69 | 76 | 18 | 39 | 88 | 88 | 80 | 39 |
| Mengineyo | Namba | 172 | 172 | 172 | 157 | 151 | 105 | 106 | 192 | 203 | 211 |
| Uchukuzi | Namba | | | | | | | | | | |
| Abiria | 000 | 464 | 514 | 594 | 524 | 392 | 285 | 284 | 227 | 339 | 373 |
| Mizigo | Tani'000 | 1002 | 1169 | 775 | 714 | 429 | 237 | 265 | 138 | 154 | 185 |

Chanzo: Shirika la Reli Tanzania

## RELI YA UHURU - TAZARA

Jedwali Na. 68

| Maelezo | Kipimo | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urefu wa Reli Kuu | Km | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 |
| Magari ya Moshi | Namba | 58 | 58 | 21 | 19 | 10 | 16 | 15 | 13 | 13 | 15 |
| Reli Kuu | Namba | 42 | 42 | 15 | 14 | 8 | 11 | 10 | 9 | 9 | 11 |
| Ya kujongeza | Namba | 16 | 16 | 6 | 5 | 2 | 5 | 5 | 4 | 5 | 4 |
| Mabehewa ya abiria | Namba | 75 | 75 | 66 | 71 | 62 | 53 | 36 | 36 | 35 | 52 |
| Abiria | Namba | 61 | 61 | 52 | 59 | 53 | 44 | 31 | 30 | 30 | 45 |
| Chakula | Namba | 5 | 5 | 6 | 8 | 4 | 3 | 2 | 3 | 2 | 3 |
| Vifurushi | Namba | 9 | 9 | 8 | 4 | 5 | 6 | 3 | 3 | 3 | 4 |
| Mabehewa ya mizigo | Namba | 1556 | 1518 | 1455 | 1458 | 1371 | 1412 | 1620 | 930 | 858 | 1391 |
| Mizigo ya kawaida | Namba | 1354 | 1364 | 1297 | 1295 | 1217 | 1174 | 1381 | 795 | 765 | 1229 |
| Mifugo | Namba | 2 | 16 | 20 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mafuta | Namba | 83 | 81 | 72 | 81 | 114 | 196 | 197 | 93 | 59 | 104 |
| Barafu | Namba | 3 | 8 | 3 | 10 | 4 | 7 | 7 | 7 | 0 | 5 |
| Mengineyo | Namba | 22 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1 |
| Breki | Namba | 64 | 26 | 44 | 46 | 17 | 16 | 16 | 16 | 16 | 35 |
| Ballast | Namba | 28 | 21 | 17 | 18 | 17 | 17 | 17 | 17 | 17 | 17 |
| Uchukuzi mizigo (Tani) | 000 | 298 | 470 | 555 | 569 | 525 | 333 | 540 | 248 | 259 | 245 |
| Abiria | 000 | 390 | 611 | 1063 | 1000 | 1177 | 923 | 758 | 414 | 678 | 654 |

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Uhuru

\+ Urefu ni km. 1860.54, km 974.814 zikiwa nchini Tanzania

\- Takwimu hazikupatikana

## USAFIRISHAJI KWA MELI: DAR ES SALAAM

Jedwali Na. 69

| Maelezo | Kipimo | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 2898 | 3895 | 4154 | 3038 | 697 | 1842 | 1274 | 1232 | 1600 | 742 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 5848 | 11506 | 18257 | 16588 | 7260 | 17472 | 18721 | 24240 | 24496 | 13359 |
| Jumla ya abiria | 000 | 525 | 1072 | 664 | 714 | 310 | 141 | 228 | 312 | 375 | 347 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000wt | 4179 | 4307 | 6320 | 5703 | 2316 | 4946 | 4954 | 5432 | 10122 | 5547 |
| **Bidhaa zilizopakuliwa** | **000wt** | **3390** | **3599** | **5292** | **4932** | **2136** | **4382** | **4559** | **4816** | **9018** | **3899** |
| Za kawaida | 000wt | 1928 | 2107 | 3164 | 2762 | 1053 | 2430 | 2159 | 2474 | 5021 | 2682 |
| Saruji | 000wt | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mafuta | 000wt | 1382 | 1311 | 1909 | 2054 | 1013 | 1852 | 2400 | 2342 | 3997 | 1217 |
| Mengineyo1 | 000wt | 80 | 181 | 219 | 116 | 70 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Bidhaa zilizopakiwa** | **000wt** | **874** | **1016** | **1398** | **887** | **181** | **565** | **466** | **648** | **1120** | **414** |
| Za kawaida | 000wt | 581 | 654 | 971 | 713 | 153 | 466 | 419 | 557 | 1033 | 391 |
| Mafuta | 000wt | 32 | 35 | 34 | 48 | 28 | 24 | 47 | 59 | 72 | 23 |
| Mengineyo1 | 000wt | 10 | 19 | 22 | 0 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mabadilishano | 000wt | 251 | 308 | 371 | 126 | - | 68 | 0.1 | 32 | 15 | 0 |

Chanzo: Mamlaka ya Bandari

1 Kama vile mbolea, mollasses, tallow fats n.k

\- Takwimu hazikupatikana

## USAFIRISHAJI KWA MELI: TANGA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

| Maelezo | Kipimo | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 185 | 215 | 281 | 242 | 95 | 144 | 215 | 201 | 232 | 92 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 440 | 628 | 964 | 551 | 133 | 671 | 1059 | 1005 | 1378 | 700 |
| Jumla ya abiria | 000 | 4 | 6.4 | 6.6 | 7.1 | 8.3 | 0 | 228 | 312 | 2865 | 0 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000wt | 162 | 289 | 519 | 542 | 178 | 359 | 529 | 508 | 608 | 271 |
| Bidhaa zilizopakuliwa | 000wt | 127 | 165 | 307 | 330 | 836 | 213 | 357 | 373 | 1217 | 199 |
| Za kawaida | 000wt | 113 | 111 | 195 | 242 | 817 | 147 | 313 | 365 | 436 | 3171 |
| Mafuta | 000wt | 14 | 54 | 112 | 88 | 19 | 66 | 44 | 8 | 615 | 2186 |
| Bidhaa zilizopakiwa | 000wt | 104 | 134 | 212 | 212 | 66 | 145 | 171 | 134 | 166 | 985 |
| Za kawaida | 000wt | 104 | 134 | 212 | 212 | 66 | 145 | 171 | 507 | 166 | 912 |
| Mafuta | 000wt | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mabadilishano | 000wt | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

## USAFIRISHAJI KWA MELI: MTWARA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

| Maelezo | Kipimo | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 85 | 215 | 281 | 99 | 36 | 32 | 58 | 129 | 498 | 339 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 106 | 628 | 964 | 251 | 131 | 31 | 455 | 307 | 1557 | 1245 |
| Jumla ya abiria | 000 | 10 | 6.4 | 6.6 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000 | 169 | 289 | 519 | 112 | 82 | 95 | 107 | 112 | 178 | 144 |
| Bidhaa zilizopakuliwa | 000wt | 44 | 165 | 307 | 53 | 26 | 23 | 39 | 44 | 309 | 894 |
| Za kawaida | 000wt | 30 | 111 | 195 | 47 | 22 | 23 | 36 | 35 | 55 | 274 |
| Mafuta | 000wt | 14 | 54 | 112 | 6 | 4 | 0 | 3 | 9 | 254 | 620 |
| Bidhaa zilizopakiwa | 000wt | 75 | 134 | 212 | 59 | 56 | 72 | 68 | 71 | 113 | 70 |
| Za kawaida | 000wt | 75 | 134 | 212 | 59 | 56 | 72 | 68 | 71 | 113 | 70 |
| Mafuta | 000wt | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mabadilishano | 000wt | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

## HUDUMA ZA POSTA

**Jedwali Na. 70**

| Maelezo | Kipimo | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ofisi ndogo Posta | Namba | 136 | 162 | 162 | 167 | 202 | 171 | 105 | 65 | 74 |
| Franchised Post Offices | Namba | 92 | 91 | 86 | 113 | 81 | 81 | 151 | 112 | 89 |
| Ofisi kamili | Namba | 157 | 129 | 113 | 172 | 170 | 170 | 163 | 147 | 160 |
| **Jumla** | **Namba** | **385** | **382** | **361** | **452** | **453** | **422** | **419** | **324** | **323** |
| Masanduku binafsi | 000 | 172 | 172 | 173 | 174 | 117 | | 146 | 162 | 173 |
| Masanduku yaliyokodishwa | 000 | 147 | 146 | 150 | 130 | 87 | 120 | 130 | 140 | 148 |
| Maombi yasiyotimizwa | 000 | 0 | 0 | 0 | 5 | 4 | 0 | 21 | 28 | 25 |
| Mifuko pekee iliyokodishwa | Namba | 214 | 203 | 217 | 182 | 62 | 183 | 361 | 278 | 212 |
| **Barua zilizotumwa bila vifurushi** | Mill. | **0** | **28** | **24** | **15** | **14** | **29** | **27** | **15** | **26** |
| Nchini | Mill. | | 20 | 17 | 10 | 14 | 19 | 19 | - | - |
| Nje ya nchi | Mill. | | 8 | 7 | 5 | | 11 | 8 | - | - |
| **Regista na barua za amana** | 000 | **489** | **1003** | **530** | **307** | **377** | **480** | **347** | **397** | **398** |
| Nchini | 000 | | 915 | 452 | 147 | 0 | 305 | 293 | - | - |
| Nje ya nchi | 000 | | 40 | 37 | 136 | 0 | 154 | 34 | - | - |
| Vifurushi nchini | 000 | 48 | 36 | 29 | 18 | 9 | 15 | 10 | 15 | 29 |
| Vifurushi vya nje | 000 | 7 | 12 | 12 | 6 | 2 | 7 | 11 | 12 | 9 |
| Leseni za kuuza stamp | Namba | 10099 | 12824 | 6324 | 6242 | 6256 | 25145 | 28257 | 33311 | 2637 |
| **Huduma za haraka, barua na vifurushi** | " | | | | | | | | | |
| Ndani ya nchi | " | 297061 | 312110 | 262381 | 216762 | 493709 | 283711 | 501635 | 404453 | 620478 |
| Nje ya nchi | " | 37331 | 36930 | 12289 | 14650 | 4012 | 18766 | 16965 | 24347 | 17130 |
| EMS Money Fax | " | 300357 | 533821 | 379084 | 366382 | 23165 | 82002 | 36357 | 2940 | 550 |
| EMS Fax (Fax message received) | " | 22968 | 23328 | 14659 | 121901 | 103558 | 31594 | 1595 | 876187 | 544 |
| **Overnight Mail Services** | " | | | | | | | | | |
| Mifuko ya barua iliyosafirishwa | " | 70086 | 101486 | 75900 | 85595 | 68912 | 76983 | 115403 | 50082 | 87051 |
| vifurushi vya magazeti vilivyosafirishwa | " | 21692 | 28753 | 20314 | 12754 | 13934 | 2752 | 12040 | 10652 | 18784 |
| **Huduma za gari ndogo** | | | | | | | | | | |
| Jumla ya barua zilizosafirishwa | " | 5993 | 3690 | 6542 | 4328 | 268 | 0 | 193 | 24095 | 849 |
| Amana za haraka zilizotolewa | " | 207997 | 210440 | 214558 | 0 | 20057 | 8169 | 4717 | 3087 | 2034 |
| Amana za haraka zilizolipwa | | 147020 | 233325 | 132030 | 93508 | 23069 | 11881 | 17397 | 516 | 555 |
| **Amana za haraka za nje ya nchi:** | | | | | | | | | | |
| Zilizotumwa | " | 1586 | 1788 | 1519 | 1354 | 1030 | 1027 | 998 | 369 | 478 |
| Zilizopokelewa | " | 1001 | 1105 | 686 | 671 | 150 | 150 | 217 | 77 | 83 |
| Amana za posta zilizouzwa | " | 8277 | 8029 | 9152 | 8062 | 8831 | 1924 | 633 | 414 | 684 |
| Amana za posta zilizolipwa | " | 7565 | 7639 | 4615 | 5709 | 5490 | 3262 | 1662 | 252 | 166 |
| **Benki ya Akiba (Transactions)** | | | | | | | | | | |
| Uwekaji amana (Deposit) | " | 66885 | 42255 | 25382 | 24574 | 9535 | 18863 | 13438 | 6260 | 21491 |
| Uchukuaji amana (Withdrawal) | " | 55392 | 32294 | 19534 | 21122 | 11663 | 23025 | 72358 | 17527 | 37556 |

Chanzo: Shirika la Posta

## SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)+

Jedwali Na.73

| Maelezo | Kipimo | 2004 | 2005 | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tani-Kilometa: | | | | | | | | | | | |
| Zilizokuwepo | 000 | 91769 | 33198 | 42627 | 32533 | - | 5313 | 9482 | 1662 | 1932 | 6154 |
| Zilizotumika | 000 | 58579 | 18121 | 22085 | 18480 | - | 1508 | 2888 | 268 | 815 | 2503 |
| Matumizi | % | 47.25 | 54.6 | 51.8 | 56.7 | - | 28.4 | 30.5 | 16 | 42 | 41 |
| Viti-kilometa: | | | | | | | | | | | |
| Vilivyokuwepo | 000 | 343250 | 334427 | 365265 | 306461 | 469426 | 41396 | 59724 | 7140 | 15131 | 54665 |
| Vilivyotumika | 000 | 164553 | 185085 | 221307 | 190006 | 129000 | 16469 | 30527 | 2946 | 10209 | 27279 |
| Matumizi | % | 47.9 | 55.3 | 60.6 | 62.0 | 27.5 | 39.8 | 51.1 | 41 | 67 | 50 |
| Abiria ++ | 000 | 271 | 197 | 224 | 190 | 188 | 27 | 41 | 9 | 11 | 35 |
| Mizigo ya ziada | Tani | NA | NA | NA | 103 | 30 | 9 | 8 | 2 | 0.3 | 45 |
| Mizigo mingine | Tani | 1506 | 1200 | 1502 | 1123 | 1044 | 54 | 145 | 4 | 4.7 | 35 |
| Shehena za Posta | Tani | 235 | 214 | 299 | 241 | 162 | 11 | 30 | 0 | 0 | 25 |

Chanzo: Shirika la Ndege Tanzania

+ Zinahusu "scheduled traffic" tu

++ Abiria waliolipa nauli kamili

- Takwimu hazikupatikana

## SURA YA 17

## NISHATI

### Kiwango cha Ukuaji

389. Mwaka 2013, shughuli za kiuchumi za umeme na gesi zilikua kwa asilimia 4.4 ikilinganishwa na asilimia 6.0 mwaka 2012. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa ufuaji wa umeme wa maji kutokana na uchakavu wa mitambo. Aidha, uzalishaji wa umeme wa mafuta ambao ni wa gharama umepungua kufuatia jitihada za serikali za kuelekeza uwekezaji zaidi katika uzalishaji wa umeme wa gesi kufuatia kugunduliwa kwa gesi huko Mtwara na Lindi ambayo ndiyo chanzo cha uhakika zaidi na cha gharama nafuu. Aidha, shughuli za kiuchumi za umeme na gesi zilichangia asilimia 1.8 katika Pato la Taifa mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 1.9 mwaka 2012.

### Ufuaji wa Umeme

390. Mwaka 2013, uwezo wa uzalishaji umeme ulikuwa MW 1,583.53 ikilinganishwa na MW 1,451.59 mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 9.1. Katika kipindi hicho, mahitaji ya juu ya umeme yalifikia MW 898.72 ikilinganishwa na MW 851.30 mwaka 2012. Umeme uliozalishwa katika Gridi ya Taifa na vyanzo vingine ulikuwa saa za gigawati 5,997.41 sawa na ongezeko la asilimia 10.1 ikilinganishwa na saa za gigawati 5,449.68 zilizozalishwa mwaka 2012. Kati ya hizo, saa za gigawati 3,092.03 zilizalishwa kwenye Gridi ya Taifa na saa za gigawati 2,726.89 zilizalishwa kutoka kwenye vituo nje ya Gridi ya Taifa. Aidha, umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali nchini mwaka 2013, ulikuwa saa za gigawati 4,825.08 ikilinganishwa na saa za gigawati 4,401.35 zilizouzwa mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 9.6. Hata hivyo, kiasi cha umeme uliopotea kutokana na uchakavu wa mitambo ya kusafirisha na kusambaza umeme ulikuwa saa za gigawati 1,139.51 sawa na asilimia 19 ya umeme wote uliozalishwa mwaka 2013 ikilinganishwa na saa za gigawati 1,048.33 sawa na asilimia 19.8 ya umeme uliozalishwa katika gridi mwaka 2012. Mwaka 2013, idadi ya wateja waliounganishiwa umeme nchini iliongezeka kutoka wateja 88,469 mwaka 2012 hadi kufikia wateja 143,114 sawa na ongezeko la asilimia 61.8. Ongezeko hilo lilitokana na wateja wengi kuunganishiwa umeme kufuatia kushuka kwa gharama za kuunganishia wateja umeme mijini na vijijini kwa wastani wa kati ya asilimia 30 na asilimia 77 kwa mtiririko huo.

391.Mchanganuo wa umeme uliozalishwa unaonesha kuwa ufuaji wa umeme wa maji ulipungua kwa asilimia 2.8 kutoka saa za gigawati 1,766.6 mwaka 2012 hadi kufikia saa za gigawati 1,717.3 mwaka 2013.

## UWEZO WA MITAMBO YA UMEME NA KIASI CHA UMEME ULIOTENGENEZWA KWA VITUO

Jedwali Na. 74

| Kituo | 2010 | | 2011 | | 2012* | | 2013* | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uwezo **MW** | Uliotengenezwa **GWH** | Uwezo **MW** | Uliotengenezwa **GWH** | Uwezo **MW** | Uliotengenezwa **GWH** | Uwezo **MW** | Uliotengenezwa **GWH** |
| **GRIDI YA TAIFA** | | | | | | | | |
| Kidatu (Morogoro) | 204.0 | 1110.58 | 204.0 | 759.34 | 204.0 | 710.72 | 204.0 | 558.34 |
| Mtera | 80.0 | 433.31 | 80.0 | 229.25 | 80.0 | 261.71 | 80.0 | 166.68 |
| Hale (Tanga) | 21.0 | 48.96 | 21.0 | 2.55 | 21.0 | 31.89 | 21.0 | 36.11 |
| New pangani | 68.0 | 207.94 | 68.0 | 197.32 | 68.0 | 147.43 | 68.0 | 137.2 |
| Nyumba ya Mungu (Moshi) | 8.0 | 30.17 | 8.0 | 29.35 | 8.0 | 21.53 | 8.0 | 21.53 |
| Kihansi | 180.0 | 867.32 | 180.0 | 772.85 | 180.0 | 590.93 | 180.0 | 795.17 |
| Uwemba Min Hydro | 0.8 | 3.00 | 0.8 | 1.92 | 0.8 | 2.3 | 0.8 | 2.3 |
| **Jumla Hydro** | **561.8** | **2701.28** | **561.8** | **1992.58** | **561.84** | **1766.51** | **561.84** | **1717.33** |
| Ubungo Diesel | 0.00 | 0.00 | 34.37 | - | - | - | - | - |
| Ubungo GTS | | | | | 105 | 244.67 | 105 | 479.05 |
| Ubungo-Watsila | 100.00 | 669.83 | 102.00 | 631.35 | 102 | 667.57 | 102 | 522.12 |
| Tegeta-Watsila | 43.65 | 243.73 | 45.00 | 320.23 | 45 | 286.67 | 45 | 313.43 |
| Dodoma (Zuzu) | 7.44 | 1.07 | 7.44 | 5.41 | 7.4 | 4.9 | 7.4 | 6.71 |
| Mbeya Iyunga | 13.90 | 0.00 | 13.90 | - | - | - | - | - |
| Musoma | 2.56 | 0.00 | 2.56 | - | 0 | - | 0 | - |
| Mwanza Nyakato | 12.50 | 0.00 | 12.50 | - | 0 | - | 63 | 53.39 |
| Tabora | 10.20 | 0.00 | 10.20 | - | 0 | - | 0 | - |
| **Jumla Thermal** | **190.25** | **914.63** | **227.97** | **956.99** | **259.40** | **1203.81** | **322.40** | **1374.70** |
| **JUMLA GRIDI** | **752.05** | **3615.91** | **789.81** | **2949.57** | **821.24** | **2970.32** | **884.24** | **3092.03** |
| **MATAWI MENGINE - ISOLATED STATIONS** | | | | | | | | |
| Bukoba | 2.56 | 0.15 | 2.56 | 2.78 | 2.56 | 0.16 | 2.56 | 0.59 |
| Kigoma | 6.25 | 21.22 | 12.00 | 21.14 | 12 | 23.4 | 12.31 | 24.04 |
| Kilwa /Masoko | 1.50 | 1.36 | 1.50 | - | 1.5 | 0 | 0 | 0 |
| Lindi | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mafia | 0.85 | 2.70 | 0.85 | 3.15 | 0.848 | 0 | 2.13 | 4.45 |
| Mtwara | 1.14 | 0.00 | 18.00 | 59.21 | 18 | 64.13 | 21.8 | 68.6 |
| Njombe | 1.28 | 0.00 | - | - | - | - | - | - |
| Songea | 6.43 | 18.76 | 6.43 | 17.62 | 6.428 | 20.59 | 8.1 | 22.69 |
| Sumbawanga | 1.50 | 0.00 | 5.00 | 2.42 | 5 | 10.85 | 6.25 | 13.94 |
| Mpanda | 1.66 | 6.96 | 2.30 | 6.90 | 2.296 | 8.28 | 2.6 | 8.58 |
| Ikwiriri | 0.85 | 2.82 | 8.45 | 0.27 | 0.848 | 0 | 0 | 0 |
| Tunduru | 2.07 | 3.75 | 2.07 | 3.64 | 2.068 | 3.72 | 1.98 | 3.75 |
| Masasi | 4.50 | 10.12 | 4.50 | - | 4.5 | 0 | 0 | 0 |
| Liwale | 0.60 | 0.97 | 1.00 | 1.20 | 1 | 1.05 | 0.85 | 1.35 |
| Ngara | 0.95 | 2.78 | 0.95 | 2.78 | 0.952 | 3.15 | 0.95 | 2.92 |
| Biharamulo | 0.95 | 3.30 | 0.95 | 3.38 | 0.952 | 3.71 | 0.85 | 4.14 |
| Mbinga | 2.26 | 3.10 | 2.26 | 3.07 | 2.256 | 4.01 | 2.75 | 4.63 |
| Ludewa | 1.28 | 0.82 | 1.28 | 0.80 | 1.276 | 0.88 | 1.27 | 0.96 |
| Somanga | | | 7.50 | 3.35 | 7.5 | 11.8 | 7.5 | 11.53 |
| Kasulu | | | | | 0.25 | 2.17 | 2.5 | 3.15 |
| Kibondo | | | | | 0.25 | 1.54 | 2.5 | 2.27 |
| Loliondo | | | | | 0.5 | 0.24 | 5 | 0.64 |
| Namtumbo | | | | | | | 0.4 | 0.28 |
| **JUMLA - MATAWI MENGINE** | **36.63** | **78.81** | **77.60** | **131.71** | **70.98** | **159.68** | **82.30** | **178.51** |
| **IPP Thermal** | | | | | | | | |
| Import from Songas | | | 189.00 | 1312.02 | 189 | 1465.06 | 189 | 1313.92 |
| Import from IPTL | | | 103.00 | 305.35 | 103 | 432.43 | 103 | 409.46 |
| Symbion Gas Plant/JET A1 | | | 112.50 | 346.40 | 120 | 315.83 | 120 | 283.67 |
| Agrreko-Ubungo | | | 50.00 | 36.16 | 50 | 89.62 | 50 | 233.25 |
| Agrreko-Tegeta | | | 50.00 | 54.69 | 50 | 96.27 | 50 | 235.92 |
| Symbion - Dodoma | | | 55.00 | 7.90 | 55 | 95.39 | 55 | 79.96 |
| Symbion - Arusha | | | 50.00 | | 50 | 55.62 | 50 | 78.76 |
| SPP | | | 17.49 | 12.36 | | 14.13 | 3.5 | 32.24 |
| | | | **626.99** | **2074.88** | **617.00** | **2564.35** | **620.50** | **2667.18** |
| **JUMLA KUU - TANESCO** | **788.68** | **3694.72** | **867.41** | **3081.28** | **892.22** | **3130.00** | **966.54** | **3270.54** |
| **KUTOKA VYANZO VINGINE (Uganda, TANWAT, Zambia, GTS Songas, IPTL, Kiwira Coal Mine, Kilombero-Ilovo)** | | **1443.04** | | **2074.89** | | **2725.71** | | **2726.71** |
| **JUMLA YA UMEME ULIOTENGENEZWA** | | **5137.76** | | **5156.17** | | **5855.71** | | **5997.25** |

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

* Takwimu za Awali

## MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI

Jedwali Na. 75 GWH

| Mwaka | Tanzania Bara | | | Zanzibar | Jumla | Umeme uliopotea | Jumla ya umeme uliotengenezwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wateja wadogo (D1) | Wateja wa Kati (T1) | Wateja Wakubwa (T2,T3 & T8) | T5 | | | |
| 2011 | 329 | 1271 | 2118 | 277 | 3994.7 | 1158.7 | 5153.4 |
| 2012 | 321 | 1480 | 2302 | 299 | 4401.4 | 1048.3 | 5449.7 |
| 2013 | 281 | 1747 | 2560 | 219 | 4807.1 | 1139.5 | 5997.4 |

Chanzo: Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

## MAUZO YA UMEME KWA MIKOA

Jedwali Na. 76

| Mkoa | Umeme uliouzwa (GWh) | | |
|---|---|---|---|
| | 2011 | 2012 | 2013 |
| Ilala | 595.9 | 629.6 | 730.9 |
| Kinondoni Kaskazini | 511.6 | 580.2 | 770.0 |
| Kinondoni Kusini | 233.0 | 238.5 | 257.2 |
| Temeke | 323.6 | 364.1 | 392.1 |
| Pwani | 115.5 | 141.2 | 170.7 |
| Dodoma | 86.2 | 93.8 | 104.9 |
| Morogoro | 163.3 | 206.5 | 221.0 |
| Singida | 23.4 | 29.2 | 32.0 |
| Tanga | 218.7 | 244.4 | 264.2 |
| Kilimanjaro | 117.9 | 134.3 | 144.1 |
| Arusha | 239.8 | 285.4 | 315.8 |
| Manyara | 19.9 | 22.9 | 24.2 |
| Mtwara | 29.6 | 34.0 | 35.0 |
| Lindi | 14.4 | 14.5 | 18.2 |
| Ruvuma | 21.2 | 23.3 | 26.8 |
| Mbeya | 131.6 | 149.6 | 153.2 |
| Iringa | 91.7 | 102.0 | 105.3 |
| Rukwa | 18.7 | 18.1 | 20.1 |
| Mwanza | 200.5 | 223.7 | 231.1 |
| Kagera | 29.2 | 54.8 | 52.7 |
| Mara | 109.3 | 110.2 | 125.0 |
| Tabora | 94.8 | 103.1 | 108.7 |
| Shinyanga | 309.8 | 279.3 | 280.4 |
| Kigoma | 17.9 | 20.4 | 23.1 |
| **Jumla Tanzania Bara** | **3717.51** | **4102.80** | **4606.43** |
| **Zanzibar** | 277.24 | 298.55 | 218.65 |
| **JUMLA** | **3994.75** | **4401.35** | **4825.08** |

Chanzo: Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

**Utafutaji Mafuta na Gesi**

**Gesi Asilia**

392. Mwaka 2013, jumla ya futi za ujazo ($c^3$sgf) trilioni 12 za gesi asilia ziligundulika katika kina kirefu cha maji baharini. Hii inafanya kiasi cha gesi iliyogundulika kufikia futi za ujazo trilioni 46.5. Aidha, jumla ya futi za ujazo bilioni 35.9 za gesi asilia zilizalishwa mwaka 2013 ikilinganishwa na futi za ujazo bilioni 33.2 zilizozalishwa mwaka 2012. Kati ya kiasi hicho kilichozalishwa, futi za ujazo bilioni 28.6 zilitumika kuzalisha umeme na futi za ujazo bilioni 7.1 zilitumika viwandani. Vile vile, katika kipindi hicho, mkataba mmoja wa utafutaji na uzalishaji mafuta ulisainiwa. Mwaka 2013, shughuli za ukusanyaji wa takwimu za mitetemo ya miamba na uchorongaji wa visima katika maeneo ya nchi kavu na baharini ziliendelea ambapo visima vinne vya utafutaji wa mafuta vilichorongwa katika maji ya kina kirefu baharini ikilinganishwa na visima 11 vilivyochimbwa mwaka 2012.

393. Mwaka 2013, mapato yaliyotokana na mauzo ya gesi asilia yalikuwa Dola za Kimarekani 52,175,264 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 36,551,396 zilizopatikana mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 42.7. Ongezeko hili lilitokana na Kampuni ya *Pan Africa Energy Tanzania Ltd* inayojishughulisha na uzalishaji gesi asilia katika eneo la Songo Songo kumaliza kurejesha gharama za uwekezaji na hivyo mgawanyo wa faida ya mauzo ya gesi asilia kuongezeka.

**Jedwali Na. 17.1: Uzalishaji wa Gesi Asilia - Songo Songo**

| | **(Futi za ujazo)** | | |
|---|---|---|---|
| **Mwezi** | **Kiasi kilichozalishwa** | ***Process Fuel*** | **Gesi iliyochomwa *(Flared gas)*** |
| Januari | 3,085,000,000 | 9,000,000 | 5,400,000 |
| Februari | 2,769,000,000 | 8,300,000 | 3,100,000 |
| Machi | 3,037,434,446 | 9,204,855 | 3,420,000 |
| Aprili | 2,840,405,322 | 9,573,897 | 3,350,000 |
| Mei | 2,794,570,828 | 9,446,763 | 4,850,000 |
| Juni | 2,933,000,000 | 8,100,000 | 3,200,000 |
| **Jumla Ndogo (Jan-Jun 2013)** | **17,459,410,596** | **53,625,514** | **23,320,000** |
| Julai | 3,042,000,000 | 8,400,000 | 3,400,000 |
| Agosti | 2,932,000,000 | 8,100,000 | 3,400,000 |
| Septemba | 2,920,000,000 | 8,500,000 | 3,300,000 |
| Oktoba | 3,033,000,000 | 7,800,000 | 3,400,000 |
| Novemba | 2,809,000,000 | 7,600,000 | 3,300,000 |
| Desemba | 3,022,000,000 | 7,800,000 | 3,400,000 |
| **Jumla ndogo (Jul-Dec, 2013)** | **17,758,000,000** | **48,200,000** | **20,200,000** |
| **2013** | 35,217,410,596 | 101,825,514 | 43,520,000 |
| **2012** | 36,233,010,000 | 118,370,000 | 50,510,000 |
| **2011** | 30,970,500,000 | 101,200,000 | 50,900,000 |
| **2010** | 27,633,000,000 | 84,000,000 | 43,000,000 |
| **2009** | 23,593,000,000 | 103,000,000 | 46,000,000 |
| **2008** | 20,084,000,000 | 84,000,000 | 48,000,000 |
| **2007** | 19,705,000,000 | 86,000,000 | 55,000,000 |
| **2006** | 17,907,000,000 | 89,000,000 | 60,000,000 |
| **2005** | 14,704,000,000 | 93,000,000 | 86,000,000 |
| **2004** | 4,659,000,000 | 55,000,000 | 175,000,000 |
| **Jumla Kuu** | **230,705,920,596** | **915,395,514** | **657,930,000** |

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

**Jedwali Na. 17.2: Uzalishaji na Matumizi ya Gesi Asilia - Mnazi Bay katika mwaka 2013**

| Mwaka | Uzalishaji | Matumizi katika mtambo wa kusafishia | Gesi iliyouzwa kwa ajili ya kuzalisha umeme |
|---|---|---|---|
| **Mwezi** | **Futi za ujazo** | **Futi za ujazo** | **Futi za ujazo** |
| 13-Jan | 50,183,383 | 1,549,287 | 49,964,659 |
| 13-Feb | 49,479,294 | 1,128,618 | 48,434,214 |
| 13-Mar | 59,776,242 | 1,588,722 | 55,445,615 |
| 13-Apr | 60,179,298 | 1,421,228 | 56,473,841 |
| 13-May | 62,363,693 | 1,317,633 | 58,261,921 |
| 13-Jun | 58,943,058 | 1,293,449 | 55,371,221 |
| 13-Jul | 59,569,149 | 1,272,976 | 56,138,019 |
| 13-Aug | 59,522,374 | 1,310,054 | 57,398,260 |
| 13-Sep | 60,120,038 | 1,242,544 | 57,925,219 |
| 13-Oct | 64,583,723 | 1,285,485 | 62,764,980 |
| 13-Nov | 65,392,683 | 1,293,098 | 62,879,630 |
| 13-Dec | 65,829,948 | 1,531,286 | 62,587,277 |

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

**Jedwali Na. 17.3: Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Gesi ya Songo songo na Mnazi Bay (Dola za Marekani)**

| Mwaka | Songo Songo - | Mnazi Bay | Jumla |
|---|---|---|---|
| July - Des. 2004 | 2,411,281 | - | 2,411,281 |
| Jan - Des. 2005 | 9,019,384 | - | 9,019,384 |
| Jan - Des. 2006 | 14,966,409 | - | 14,966,409 |
| Jan - Des. 2007 | 16,861,492 | 305,236 | 17,166,727 |
| Jan - Des. 2008 | 19,521,646 | 388,449 | 19,910,095 |
| Jan - Des. 2009 | 21,403,804 | 396,109 | 21,799,913 |
| Jan - Des. 2010 | 25,607,621 | 1,080,131 | 26,687,753 |
| Jan - Des. 2011 | 38,337,903 | 1,444,856 | 39,782,759 |
| Jan - Des. 2012 | 35,026,145 | 1,525,251 | 36,551,396 |
| Jan - Des. 2013 | 50,582,385 | 1,592,879 | 52,175,264 |
| **Total** | **233,738,070** | **6,732,911** | **240,470,981** |

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

**Uagizaji na Mwenendo wa Bei za Mafuta**

394. Mwaka 2013, mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam yalikuwa lita za ujazo milioni 4,662.3 ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 3,661.7 zilizoingizwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 27.3. Kati ya lita hizo, mafuta yaliyosafirishwa nchi za jirani yalikuwa lita za ujazo milioni 1,887.8 sawa na asilimia 40.5 ya mafuta yote yaliyoagizwa.

395. Mwaka 2013, mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia zilikuwa zikipanda na kushuka kulingana na nguvu ya soko. Kiwango cha juu cha bei kilikuwa mwezi Februari ambapo bei ya mafuta ya dizeli ilikuwa Dola za Kimarekani 964 kwa tani; mafuta ya taa/ndege ilikuwa Dola za Kimarekani 1,050 kwa tani; na petroli ilikuwa Dola za Kimarekani 1,099 kwa tani. Kwa ujumla, wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwaka 2013 zilishuka kwa asilimia 2.99 kwa mafuta ya Dizeli; asilimia 2.12 kwa mafuta ya taa/ndege; na asilimia 2.75 kwa mafuta ya petroli ikilinganishwa na wastani wa bei za mafuta hayo mwaka 2012 kama inavyoonekana katika jedwali Na 17.4. Aidha, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) iliendelea kutoa bei za ukomo ambapo wastani wa bei za mafuta nchini ulikuwa shilingi 2,090 kwa lita moja ya mafuta ya petroli, shilingi 2,005 mafuta ya dizeli na shilingi 1,997 mafuta ya taa ikilinganishwa na shilingi 2,112 kwa lita moja ya mafuta ya petroli, shilingi 2,022 mafuta ya dizeli na shilingi 2,014 mafuta ya taa mwaka 2012.

**Jedwali Na. 17.4: Bei za Mafuta kwenye Soko la Dunia - Dola za Kimarekani kwa Mita za Ujazo (Fob)**

| Aina ya Mafuta | Petroli | | Dizeli | | Mafuta ya Taa | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwezi** | **2012** | **2013** | **2012** | **2013** | **2012** | **2013** |
| Januari | 975 | 1026 | 945 | 920 | 995 | 1004 |
| Februari | 1,058 | 1099 | 982 | 964 | 1,039 | 1050 |
| Machi | 1,148 | 1008 | 1,010 | 892 | 1,071 | 963 |
| Aprili | 1,150 | 933 | 982 | 844 | 1,045 | 908 |
| Mei | 959 | 944 | 912 | 846 | 974 | 904 |
| Juni | 892 | 966 | 811 | 865 | 863 | 915 |
| Julai | 968 | 1000 | 862 | 897 | 918 | 953 |
| Agosti | 1,087 | 1016 | 951 | 900 | 1,014 | 978 |
| Septemba | 1,077 | 964 | 961 | 895 | 1,040 | 970 |
| Octoba | 1,014 | 945 | 940 | 898 | 1,020 | 964 |
| Novemba | 932 | 928 | 910 | 896 | 978 | 963 |
| Desemba | 955 | 954 | 904 | 917 | 973 | 994 |
| **Wastani wa bei (USD/MT)** | **1,017.95** | **990** | **930.84** | **903** | **994.09** | **973** |
| **Wastani wa ongezeko la bei kwa mwaka** | | **(27.95)** | | **(27.84)** | | **(21.09)** |
| **Wastani wa ongezeko kwa mwaka kwa asilimia (%)** | | **-2.75%** | | **-2.99%** | | **-2.12%** |

Chanzo: EWURA

**Jedwali Na.17.5: Ukomo wa Bei za Rejareja za Mafuta kwa Dar es Salaam**

| Mwezi | Bei za Mafuta TZS/Lts | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Petroli | | Dizeli | | Mafuta Ya Taa | |
| | 2012 | 2013 | 2012 | 2013 | 2012 | 2013 |
| Januari | 1,956 | 1,993 | 1,977 | 1,967 | 1,963 | 1,973 |
| Februari | 1,991 | 2,005 | 1,977 | 1,964 | 1,951 | 1,953 |
| Machi | 2,144 | 2,052 | 2,095 | 1,974 | 2,056 | 1,991 |
| Aprili | 2,231 | 2,087 | 2,098 | 1,970 | 2,068 | 2,023 |
| Mei | 2,183 | 2,073 | 2,044 | 1,934 | 2,068 | 2,023 |
| Juni | 2,189 | 2,057 | 2,004 | 1,892 | 2,068 | 1,951 |
| Julai | 2,179 | 2,083 | 2,041 | 1,993 | 2,028 | 1,994 |
| Agosti | 2,009 | 2,096 | 1,943 | 2,037 | 1,926 | 1,962 |
| Septemba | 2,300 | 2,154 | 2,142 | 2,060 | 1,993 | 2,001 |
| Oktoba | 1,994 | 2,146 | 1,950 | 2,064 | 1,993 | 2,027 |
| Novemba | 2,049 | 2,102 | 1,989 | 2,066 | 2,026 | 2,018 |
| Desemba | 2,119 | 2,114 | 1,999 | 2,101 | 2,023 | 2,049 |
| Wastani | 2,112 | 2,090 | 2,022 | 2,005 | 2,014 | 1,997 |

Chanzo: EWURA

**Nishati Mbadala**

**Maporomoko Madogo ya Maji**

396.Mwaka 2013, Serikali iliendelea na kazi za utafiti wa masoko, upembuzi yakinifu wa mradi, uchambuzi wa athari za mazingira na jamii ikijumuisha upimaji wa kina cha maji katika vyanzo sita (6) vya kuzalisha umeme kutokana na maporomoko madogo ya maji. Vyanzo hivyo ni: Lingatunda (Songea Vijijini); Macheke (Ludewa); Luswisi (Ileje); Mwoga (Kasulu); Darakuta (Babati) na Nole/Ihalula (Njombe). Kwa pamoja vyanzo hivyo vina uwezo wa kuzalisha jumla ya MW 9.1 na kuweza kuunganisha jumla ya wateja 27,000.

**Jedwali Na: 17.6 Hali ya Maporomoko Madogo ya Maji Nchini**

| Jina la Mradi | Sehemu ulipo mradi | Mwendelezaji | Kiwango cha upatikanaji) *(KW)* | Hali ya mradi kimaendeleo |
|---|---|---|---|---|
| Isoko | Ileje | Njombe Roman Catholic Church | 200 | Uzalisha ji |
| Mbingu | Kilombero | Roman Catholic Mbingu Sisters' Convent | 850 | Sababu za kiufundi |
| Lugarawa | Ludewa | Njombe Roman Catholic Church | 150 | Uzalishaji |
| Mavanga | Ludewa | Njombe Roman Catholic Church | 140 | Uzalishaji |
| Kinko | Lushoto | Kinko Community (CBO) | 10 | Sababu za kiutawala |
| Bulongwa | Makete | Bulongwa Lutheran Hospital | 150 | Uzalishaji |
| Ikonda | Makete | Njombe Roman Catholic Church | 60 | Uzalishaji |
| Kitai | Mbinga | Kitai Prisons | 45 | Uzalishaji |
| Ndolage | Muleba | Ndolage Hospital | 110 | Uzalishaji |
| Hagafiro | Njombe | Mr. John Fute | 28 | Uzalishaji |
| Matembwe | Njombe | Njombe Roman Catholic Church | 150 | Uzalishaji |
| Hanga | Songea Rural | Songea Roman Catholic Church | 55 | Uzalishaji |
| Mawengi | Njombe | Njombe Roman Catholic Church | 300 | Uzalishaji |
| Igominyi | Njombe | Igominyi *Community* | 10 | Ujenzi |
| Wangama | Njombe | Wangama *Community* | 48 | Ujenzi |
| Limage | Njombe | Limage *Community* | 10 | Ujenzi |
| Magoda | Njombe | Magoda *Community* | 25 | Ujenzi |

Chanzo: MEM

### Nishati ya Mionzi ya Jua

397.Katika mwaka 2013, Serikali imewezesha utekelezaji wa miradi ya nishati ya mionzi ya jua kwa ajili ya kuhamasisha wananchi ambapo, miradi midogo ya nishati ya jua ilitekelezwa katika Halmashauri tatu (3) za Geita, Tandahimba na Bunda kwenye hospitali, shule, vituo vya afya na nyumba za wafanyakazi kwenye Halmashauri hizo.

### Tungamotaka (*Biomass*)

398.Mwaka 2013, Mkakati wa kuendeleza tungamotaka uliandaliwa, ambapo maeneo kadhaa yaliainishwa ili kuhakikisha nishati ya tungamotaka inazalishwa na kutumika kwa uendelevu kwa kuongeza matumizi mazuri ya nishati,

kuhamasisha ongezeko la matumizi ya nishati mbadala na kuweka muundo mzuri wa kitaasisi na kisera katika kuendeleza nishati ya tungamotaka. Jumla ya miradi saba ya tungamotaka iliainishwa ikiwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa kW 51,500 kwa mchanganuo kama inavyoonekana katika jedwali Na. 17.8. Aidha, jumla ya mitambo 8,799 itumiayo tungamotaka kwa ajili ya kuzalisha *biogas* ilijengwa katika Mikoa 11 ya Tanzania Bara na mtambo mmoja Zanzibar ikilinganishwa na mitambo 2,409 iliyojengwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 73.

**Jedwali Na: 17.7 Hali ya Miradi ya Nishati ya Tungamotaka**

| Jina la Mradi/Mwendelezaji | Sehemu | Kiwango cha upatikanaji (*Potential Capacity) (kW)* |
|---|---|---|
| TPC | Moshi | 15000 |
| TANWAT | Njombe | 2750 |
| Kagera  Sugar | Kagera | 5000 |
| Katani Ltd | Hale | 150 |
| Kilombero Sugar Ltd | Kilombero | 10600 |
| Kilombero Sugar Ltd | Mtibwa | 8000 |
| Mufindi Paper Mill | Mufindi | 10000 |

Chanzo: MEM

**Jotoardhi**

399.Utafiti wa awali wa jotoardhi ulionesha kwamba kiwango kilichopo cha nishati ya jotoardhi ni zaidi ya MW 650. Mwaka 2013, Serikali ilianzisha Kampuni iitwayo *Tanzania Geothermal Development Company (TGDC)* kwa lengo la kushughulikia utafiti hadi uzalishaji wa umeme utokanao na nishati ya jotoardhi nchini. Mchakato wa kutafuta wataalam mbalimbali wakiwemo Wajiolojia, Wajiokemia, Wajiofizikia na Wahandisi Nishati unaendelea.

# SURA YA 18

## MAJI

### Utangulizi

400.Mwaka 2013, kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi za usambazaji maji ilipungua kidogo na kuwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2012. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na uchakavu wa miundombinu ya maji. Hata hivyo Serikali iliendelea na jitihada za kuboresha miundombinu ya maji ikiwemo kuchimba visima na upanuzi/ukarabati wa mitambo ya maji ya Ruvu juu na Ruvu chini. Mchango wa shughuli za usambazaji maji katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 0.3 kwa mwaka wa tatu mfululizo.

### Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

401.Mwaka 2013, usimamizi wa rasilimali za maji uliendelea kuboreshwa kwa kufuatilia mwenendo wa maji chini na juu ya ardhi, ambapo jumla ya vituo 64 vya kupima mwenendo na hali ya maji vilikarabatiwa. Ukarabati wa vituo hivyo ulifanyika katika mabonde ya Pangani, Rufiji, Wami/Ruvu, Ziwa Nyasa, Ruvuma, Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa. Aidha, ujenzi wa vituo vipya 28 ulifanyika katika bonde la Ziwa Nyasa. Vilevile, ujenzi wa uzio kwa ajili ya vituo vitatu vya hali ya hewa na uzio kuzunguka visima virefu sita ulifanyika katika bonde la Mto Ruvuma.

402. Mwaka 2013, Serikali iliendelea kuchukua hatua za kukabiliana na uchafuzi wa maji na vyanzo vyake, ikiwa ni pamoja na utatuzi wa migogoro katika matumizi ya maji kwa kutumia Sheria ya Maji Na. 11 ya mwaka 2009. Sambamba na hatua zilizochukuliwa, jumla ya migogoro 25 ya watumia maji iliripotiwa kwa ajili ya kupatiwa suluhu kwenye Bodi za Maji za Mabonde ya Rufiji (4), Pangani (13), Wami/Ruvu (4), Ziwa Nyasa (2) na Ruvuma (2). Kati ya hiyo, migogoro 12 ilitatuliwa kwenye mabonde ya Wami/Ruvu (4), Rufiji (2), Pangani (4), Ruvuma (1) na Ziwa Nyasa (1). Aidha, jumla ya vibali 421 vya kutumia maji vilitolewa mwaka 2013 kwenye mabonde ya Rufiji (92), Pangani (107), mifereji ya ardhini (15), Ziwa Rukwa (52), Wami/Ruvu (28), Ziwa Nyasa (73), Ruvuma (19) na Ziwa Victoria (35). Vile vile, jumla ya vibali 13 vya kutiririsha maji vilitolewa katika Bonde la Ziwa Victoria (11) na Pangani (2).

403. Mwaka 2013, sampuli 6,769 kutoka vyanzo mbalimbali vya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani (4,819), umwagiliaji (1,158) na viwanda (792) zilikusanywa na kufanyiwa utafiti wa kimaabara, ikilinganishwa na sampuli 6,219 mwaka 2012. Kati ya sampuli 4,819 zilizochukuliwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, asilimia 89.1 zilikuwa na viwango vinavyokubalika kwa matumizi husika. Sampuli ambazo hazikukidhi zilitokana na maji ya vyanzo hivyo kuwa na vimelea vya vijidudu, chumvichumvi, madini ya chuma na *floride*. Aidha, kati ya sampuli 792 za majitaka toka viwandani na mitambo ya kusafishia majitaka zilizofanyiwa uchunguzi wa kimaabara, sampuli 609, sawa na asilimia 76.9 zilikidhi viwango vya kumwagwa bila kuleta athari kwenye mazingira.

**Huduma ya Maji Vijijini**

404. Mwaka 2013, miradi 225 ya kusambaza maji vijijini ilikamilika kwenye vijiji 243 ambapo jumla ya wakazi 2,598,500 wa vijiji hivyo walinufaika kwa kupata huduma ya maji safi na salama. Aidha, jumla ya miradi 763 ya usambazaji wa maji vijijini inaendelea kujengwa. Utekelezaji wa mradi wa maji kwa vijiji kumi kwa kila Halmashauri upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji 248 katika vijiji 270 ulikamilika mwaka 2013. Vile vile, mwaka 2013 jumla ya vituo 10,393 vya kuchotea maji vinavyohudumia watu 2,598,250 vilijengwa

405. Idadi ya wakazi wa vijijini waliopata huduma ya maji iliongezeka kutoka watumiaji 15,200,000 mwaka 2012 hadi kufikia jumla ya watumiaji 17,798,250 mwaka 2013, ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.1. Uwiano wa wakazi waliopata huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini ilikuwa asilimia 58 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 57 mwaka 2012.

**Huduma za Maji Mijini**

406. Mwaka 2013, taarifa za Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira zimejumuisha miji mikuu ya mikoa mipya iliyoanzishwa ambayo ni Simiyu (Bariadi), Geita, Katavi (Mpanda) na Njombe. Kutokana na hali hiyo takwimu za mwaka 2012 nazo zimebadilika kwa kujumuishwa na miji hiyo.

407. Mwaka 2013, uzalishaji wa maji katika miji mikuu ya mikoa uliongezeka hadi kufikia mita za ujazo milioni 131.45 kutoka mita za ujazo milioni 124.48 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Katika kipindi hicho, Mamlaka

23 za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji mikuu ya mikoa zilitoa huduma ya maji kwa kiwango cha wastani wa asilimia 80 ya wakazi wa mijini ikilinganishwa na wastani wa asilimia 86 ya wakazi wa mijini mwaka 2012.

408. Mwaka 2013, idadi ya wakazi wanaoishi katika Jiji la Dar es Salaam wanaopata huduma ya maji safi na salama iliongezeka hadi wastani wa asilimia 68 ya wakazi wote ikilinganishwa na wastani wa asilimia 67.0 mwaka 2012. Kiwango hiki cha upatikanaji wa maji safi na salama katika jiji la Dar es salaam ni cha chini ikilinganishwa na miji mikuu ya mikoa kutokana na ongezeko kubwa la wakazi, shughuli za kiuchumi pamoja na uchakavu wa miundombinu inayosambaza maji Dar es salaam. Katika kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji katika jiji la Dar es salaam, mwaka 2013 Serikali iliendelea kukamilisha upanuzi na ujenzi wa bomba kuu la maji kutoka Ruvu Juu na Ruvu Chini. Aidha, mwaka 2013, Serikali iliendelea kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam kwa kutekeleza Mpango Maalum wa Kuboresha Huduma ya Maji safi na Usafi wa Mazingira.

409. Mwaka 2013, mamlaka za maji katika miji mikuu ya mikoa zilikusanya jumla ya shilingi bilioni 71.88 ikilinganishwa na makusanyo ya shilingi bilioni 57.52 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 25.0. Ongezeko hilo lilitokana na wateja wapya wapatao 330,983 waliounganishwa katika mfumo wa maji, ikilinganishwa na wateja 309,257 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 7. Pamoja na ongezeko la mapato, huduma ya maji mijini inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya maji na kasi kubwa ya ongezeko la wakazi mijini.

## UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYO NA MAJI MIJINI

Jedwali Na. 77

| Mamlaka | Uzalishaji wa Maji (Mita za ujazo) | Mapato (TShs) | Uzalishaji wa Maji (Mita za ujazo) | Mapato (TShs) | Uzalishaji wa Maji (Mita za ujazo) | Mapato (TShs) | Uzalishaji wa Maji (Mita za ujazo) | Mapato (TShs) | Wastani wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2010 | | 2011 | | 2012 | | 2013 | | |
| Arusha | 14721190 | 4228767804 | 13130365 | 4439919207 | 14154190 | 4805714687 | 14535621 | 8007740391 | 78 |
| Babati | 1150694 | 412582337 | 1102056 | 545791770 | 1109955 | 578144517 | 1373450 | 760951113 | 84 |
| Bukoba | 2290311 | 781849481 | 2379843 | 856364230 | 2812072 | 1130847335 | 3013875 | 1235958118 | 76 |
| Dodoma | 9667795 | 4080208091 | 9891546 | 5319580534 | 10433535 | 6218098840 | 11163384 | 7000211337 | 87 |
| Iringa | 4229160 | 2129065911 | 4901651 | 2543391568 | 7230917 | 3221320841 | 5840161 | 3728711681 | 96 |
| Kigoma | 3117511 | 502410725 | 4684263 | 815222870 | 5148765 | 1540273313 | 4449503 | 2659869782 | 71 |
| Lindi | 328902 | 203796544 | 268133 | 175506149 | 302159 | 322656268 | 678758 | 348652297 | 70 |
| Mbeya | 11236254 | 3339539484 | 10793446 | 3772790461 | 12788166 | 4366757972 | 13949166 | 6337499404 | 97 |
| Morogoro | 8900610 | 3801407363 | 8800245 | 4730546495 | 8799500 | 5442333000 | 9583006 | 5476458042 | 94 |
| Moshi | 9102782 | 3102872040 | 9189308 | 3710388357 | 9417445 | 3815735410 | 9496538 | 4061210145 | 100 |
| Mtwara | 1659664 | 972731617 | 2285218 | 1253598238 | 2070828 | 1168445202 | 2937422 | 1417894479 | 92 |
| Musoma | 3848175 | 1247335118 | 3717139 | 1354049964 | 3840910 | 1470169446 | 3754128 | 1730601178 | 82 |
| Mwanza | 23492486 | 7304948210 | 22966066 | 9461022328 | 22912029 | 12025412228 | 24078295 | 14067535585 | 94 |
| Shinyanga | 3491099 | 1506671775 | 2983817 | 1963006961 | 3009409 | 2099942920 | 3178653 | 2466577091 | 78 |
| Singida | 1527053 | 500960728 | 1326238 | 580684186 | 1414895 | 727162830 | 2091692 | 954136220 | 89 |
| Songea | 2361703 | 734974362 | 2669799 | 986463073 | 2700505 | 985786335 | 2729923 | 1411191264 | 93 |
| Sumbawanga | 1763680 | 402940915 | 1669100 | 456552113 | 1708956 | 617133945 | 1667890 | 630860514 | 62 |
| Tabora | 4149561 | 1340824081 | 3767712 | 1393944777 | 4013737 | 2127947751 | 4295009 | 2113370179 | 86 |
| Tanga | 9513697 | 3696449819 | 9929713 | 4403689730 | 10613741 | 4859604244 | 10136529 | 6806849948 | 99 |
| Mpanda | | | | | | | 1105950 | 196336208 | 52 |
| Bariadi | | | | | | | 154148 | 36688067 | 40 |
| Njombe | | | | | | | 1114593 | 363505746 | 53 |
| Geita | | | | | | | 119979 | 62619565 | 54 |
| **Jumla** | **116552327** | **40290336405** | **116455658** | **48762513011** | **124481714** | **57523487084** | **131447673** | **71875428354** | **80** |

hanzo: Wizara ya Maji

# SURA YA 19

## ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

### Elimu ya Awali

410. Mwaka 2013, madarasa ya elimu ya awali yalikuwa na mikondo 39,037 ikilinganishwa na mikondo 36,786 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Idadi ya mikondo katika shule za Serikali ilikuwa asimilia 91.1 ya mikondo yote. Aidha, idadi ya mikondo kwa shule za Serikali iliongezeka kutoka mikondo 34,628 mwaka 2012 hadi mikondo 35,557 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 2.7 wakati shule zisizo za Serikali iliongezeka kutoka mikondo 2,158 mwaka 2012 hadi mikondo 3,480 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 61.2. Ongezeko la idadi ya madarasa katika shule za awali zisizo za Serikali lilitokana na sekta binafsi kupewa fursa ya kushiriki na kuchangia katika utoaji wa elimu. Vile vile, ongezeko hilo lilichangiwa na utekelezaji wa agizo la Serikali lililoitaka kila shule ya msingi inayoanzishwa kuwa na madarasa ya elimu ya awali.

411. Mwaka 2013, idadi ya wanafunzi katika elimu ya awali ilikuwa 1,026,466 ikilinganishwa na wanafunzi 1,034,729 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 0.8. Kati ya hao, wasichana walikuwa 513,668, sawa na asilimia 50.04 ya wanafunzi wote na wavulana walikuwa 512,798. Idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali ilikuwa 969,683 ambapo wasichana walikuwa 485,963 na wavulana 483,720. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule zisizo za Serikali ilikuwa 56,783 ambapo wasichana walikuwa 27,705 na wavulana walikuwa 29,078. Kushuka kwa uandikishaji katika elimu ya awali kulitokana na uelewa mdogo wa wazazi, walezi na wadau wa elimu juu ya umuhimu wa elimu ya awali. Vile vile, kushuka kwa uandikishaji kulitokana na uwezo mdogo wa kuchangia gharama zisizo za moja kwa moja, kama vile gharama za sare, chakula na michango mingine.

412. Mwaka 2013, uwiano wa mwalimu mwenye sifa kwa wanafunzi katika shule za awali za Serikali ulikuwa 1:199 ikilinganishwa na 1:124 mwaka 2012 wakati kiuhalisia uwiano unaokubalika ni 1:25. Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika madarasa ya awali katika shule za Serikali uliimarika katika mkoa wa Dar es Salaam (1:34) na Kilimanjaro (1:50) wakati Rukwa, Simiyu na

Shinyanga ilikuwa na uwiano wa 1:405, 1:339 na 1:189 kwa mtawalia. Mikoa mingine yenye uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 100 au zaidi ni Dodoma, Geita, Katavi, Mara, Mbeya, Mwanza, Singida, Tabora na Tanga. Uchache wa idadi ya walimu katika elimu ya awali ulitokana na uhamasishaji mdogo katika elimu ya awali pamoja na kuwepo kwa vyuo vichache vinavyotoa mafunzo ya ualimu ngazi ya elimu ya awali**.** Aidha, uwiano huo wa mwalimu mwenye sifa kwa wanafunzi katika shule za awali unatokana na waalimu wanaofundisha shule za awali tu tofauti na ilivyokuwa huko nyuma ambapo uwiano huo ulikuwa unajumuisha waalimu wanafundisha shule za awali na wale wanaofundisha shule za msingi**.**

**Elimu ya Msingi**

413. Mwaka 2013, idadi ya shule za msingi za Serikali na zisizo za Serikali iliongezeka hadi shule 16,343 kutoka shule 16,331 mwaka 2012. Kwa upande wa shule za Serikali, idadi iliongezeka kutoka shule 15,525 mwaka 2012 hadi shule 15,576 mwaka 2013. Aidha, idadi ya shule zisizo za Serikali ilipungua hadi shule 767 kutoka shule 806 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 4.8. Kupungua kwa idadi ya shule za msingi zisizo za Serikali kulitokana na wamiliki kushindwa kumudu gharama za uendeshaji.

414. Mwaka 2013, idadi ya wanafunzi katika elimu ya msingi ilikuwa 8,231,913 ikilinganishwa na wanafunzi 8,247,172 mwaka 2012. Kati ya hao, wasichana walikuwa 4,165,626, sawa na asilimia 50.6 ambapo wavulana walikuwa 4,066,287. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali iliongezeka hadi wanafunzi 8,033,926 kutoka wanafunzi 8,019,748 mwaka 2012 ambapo wasichana walikuwa 4,068,354 na wavulana 3,965,572. Idadi ya wanafunzi katika shule zisizo za Serikali ilikuwa 197,987 ikilinganishwa na wanafunzi 227,424 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 13. Kati ya hao, wasichana walikuwa 97,272 na wavulana walikuwa 100,715. Upungufu wa idadi ya wanafunzi katika shule za msingi zisizo za Serikali ulitokana na gharama kubwa za kusomesha wanafunzi. Vile vile, idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza iliongezeka hadi wanafunzi 1,430,231 mwaka 2013 kutoka wanafunzi 1,404,998 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 1.8.

415. Mwaka 2013, uwiano kati ya wanafunzi wote waliokuwa shule za msingi na idadi ya watoto wenye umri wa kuwa shule za msingi (Miaka 7-13) ulipungua

kutoka asilimia 92.0 mwaka 2012 hadi asilimia 89. Baadhi ya mikoa iliyokuwa na uwiano wa juu ni Mara (asilimia 99.6), Iringa (asilimia 99.7) na Geita (asilimia 99.5). Mikoa iliyokuwa na uwiano wa chini ni Kigoma (asilimia 72.9), Dar Es Salaam (asilimia 73.9) na Katavi (asilimia 73.2). Aidha, kiwango cha jumla cha uandikishaji wa wanafunzi wote kilipungua hadi asilimia 96.2 mwaka 2013kutoka asilimia 98.4 mwaka 2012. Vile vile, kiwango halisi cha uandikishaji wa wanafunzi wa umri wa kuwa shule (miaka 7-13) kilipungua kutoka asilimia 92.0 mwaka 2012 hadi asilimia 89.7 mwaka 2013. Kushuka kwa uandikishaji wa wanafunzi wa shule za msingi kunasababishwa na uhamasishaji hafifu kwa wazazi na walezi kuhusu umuhimu wa kuwaandikisha watoto wenye umri wa kwenda shule. Sababu nyingine ni uhaba wa miundombinu, mazingira magumu kwa baadhi ya shule za msingi, umbali mrefu kati ya shule na makazi ya wanafunzi, umasikini wa wazazi au walezi na ukosefu wa chakula kwa wanafunzi katika shule nyingi za msingi. Aidha, kwa maeneo ya wafugaji, wavuvi na wachimbaji madini watoto wengine wanakwenda tafuta ajira za muda na wengine wanawasaidia wazazi wao kuchunga mifugo yao.

416.Idadi ya walimu wenye sifa katika shule za Serikali iliongezeka kutoka walimu 174,834 mwaka 2012 hadi walimu 187,566 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Ongezeko hilo limesababisha uwiano wa walimu wenye sifa kwa wanafunzi kuimarika kutoka uwiano wa 1:47 mwaka 2012 hadi 1:44 mwaka 2013. Kigezo stahili cha uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi katika shule za msingi ni 1:40. Ongezeko hili la walimu wenye sifa lilitokana na jitihada za Serikali za kuongeza ajira za walimu wenye sifa ili kukabiliana na changamoto ya idadi kubwa ya wanafunzi katika elimu ya msingi.

417.Idadi ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2013 ilikuwa 844,921. Kati yao, wavulana walikuwa 398,814 na wasichana walikuwa 446,107. Jumla ya wanafunzi waliofaulu walikuwa 427,606 ambapo ufaulu huu ni sawa na asilimia 50.6 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani ikilinganishwa na mwaka 2012 ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 30.7. Kati yao, wavulana walikuwa 409,575 na wasichana walikuwa 455,959. Jumla ya wanafunzi waliofaulu walikuwa 265,873 wavulana 145,649 na wasichana 120,224.

418. Mwaka 2013, mkoa wa Dar es salaam ndio ulikuwa na kiwango cha juu cha ufaulu kwa asilimia 72.49 ukifuatiwa na Iringa (asilimia 64.7), Kilimanjaro (asilimia 60.04) na Njombe (asilimia 57.7). Aidha, mikoa iliyokuwa na kiwango cha chini cha ufaulu ni Simiyu (asilimia 32.24); Tabora (asilimia 35.14); na Mara (asilimia 35.4). Halmashauri zilizokuwa na kiwango cha juu cha ufaulu ni Biharamulo (asilimia 85.59); Arusha Manispaa (asilimia 85.55); Kinondoni Manispaa (asilimia 84.66). Halmashauri zilizokuwa na kiwango cha chini cha ufaulu zilikuwa Tunduru (asilimia 20.66); Kondoa (asilimia 21.40); Meatu (asilimia 23.41); Iramba (asilimia 24.56); na Nzega (asilimia 24.93). Ufaulu huu unaonesha kuwa shule za msingi za halmashauri za mijini zilifanya vizuri zaidi ikilinganishwa na shule za halmashauri za vijijini. Kutofautiana kwa ufaulu kulitokana na kuwepo kwa mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia katika Halmashauri za miji/Jiji ikilinganishwa na shule za halmashauri za vijijini.

**Elimu ya Sekondari**

419. Idadi ya shule za sekondari katika mwaka 2013 iliongezeka hadi shule 4,576 kutoka shule 4,528 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 1.1. Kati ya hizo, shule 3,528 zilikuwa za Serikali na shule zisizo za Serikali zilikuwa 1,048. Idadi ya shule za sekondari za Serikali iliongezeka kutoka shule 3,508 mwaka 2012 hadi shule 3,538 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 0.6. Aidha, shule za sekondari zisizo za Serikali ziliongezeka kutoka shule 1,020 mwaka 2012 hadi shule 1,048 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 2.7. Ongezeko hili lilitokana na utekelezaji madhubuti wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) uliopelekea kuongezeka kwa mahitaji ya nafasi za elimu ya sekondari.

420. Idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari kidato cha kwanza hadi cha sita ilipungua kwa asilimia 4.3 kutoka wanafunzi 1,884,272 mwaka 2012 hadi 1,804,056 mwaka 2013. Kati ya hao, wasichana walikuwa 864,865 sawa na asilimia 47.9 na wavulana walikuwa 939,191 sawa na asilimia 52.1 ikilinganishwa na wasichana 873,799 (asilimia 49.4) na wavulana 1,010,473 (asilimia 51.6) mwaka 2012.

421. Kiwango cha jumla cha uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita kilipungua kutoka asilimia 36.9 mwaka 2012 hadi asilimia 32.1 mwaka 2013. Vile vile, kiwango halisi cha uandikishaji kilipungua kutoka

asilimia 34.3 mwaka 2012 hadi asilimia 28.1 mwaka 2013. Kushuka kwa kiwango cha uandikishaji kulitokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaokatisha masomo kutoka asilimia 4.4 mwaka 2012 hadi asilimia 13.8 mwaka 2013. Aidha, ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaokatiza masomo lilitokana na ufaulu hafifu wa mtihani wa kidato cha pili. Aidha, uandikishaji wa wanafunzi kidato cha kwanza ulipungua kwa asilimia 1.5 kutoka wanafunzi 522,379 wakiwemo wavulana 264,196 na wasichana 258,183 mwaka 2012 hadi wanafunzi 514,592 wakiwemo wasichana 257,127 na wavulana 257,465 mwaka 2013. Kushuka kwa uandikishaji wa wanafunzi kidato cha kwanza kunatokana na ufaulu mdogo wa wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi.

422.Idadi ya walimu wenye sifa katika shule za sekondari iliongezeka kutoka walimu 55,110 mwaka 2012 hadi walimu 65,513 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 18.9. Ongezeko hilo lilisababisha uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika shule za Serikali kuimarika kutoka 1:29 mwaka 2012 hadi 1:28 mwaka 2013. Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika shule za sekondari uko juu katika mikoa ya Geita (1:43), Kagera, Kigoma na Mara zenye uwiano wa 1:33. Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi ni mkubwa katika shule za Serikali (1:28) ikilinganishwa na uwiano kwa shule zisizo za serikali (1:25). Kuimarika kwa uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi kulitokana na jitihada za Serikali kuendelea kuajiri walimu wenye sifa.

**Elimu ya Ualimu**

423.Mwaka 2013, idadi ya vyuo vya ualimu vilivyosajiliwa ilikuwa 126 ikilinganishwa na vyuo 105 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 20.0. Kati ya hivyo, vyuo vya Serikali vilikuwa 34 sawa na ilivyokuwa mwaka 2012 na visivyo vya Serikali viliongezeka kufikia vyuo 92 kutoka vyuo 71 mwaka 2012. Ongezeko la vyuo vya ualimu visivyo vya Serikali lilitokana na jitihada Serikali za kuboresha mazingira ya uwekezaji na hivyo kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika elimu.

424.Mwaka 2013, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali ilipungua kwa asilimia 17.6 kufikia wanachuo 35,645 kutoka wanachuo 43,258 mwaka 2012. Kati ya wanachuo hao, wavulana walikuwa 20,769 (asilimia 58.3) na wasichana walikuwa 14,876 (asilimia 41.7). Mafunzo wanayopata vyuoni ni ya ngazi ya elimu maalum ambayo ilikuwa na

jumla ya wanachuo 159 (wasichana 107, wavulana 52); Cheti (tarajali) wanachuo 22,975 (wasichana 10,120, wavulana 12,855); Stashahada (tarajali) wanachuo 11,519 (wasichana 4,331, wavulana 7,188) na Stashahada (mafunzo kazini) wanachuo 992 (wanawake 318, wanaume 674).

425. Mwaka 2013, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu vya Serikali ilikuwa 24,072 ikilinganishwa na wanachuo 26,626 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 9.6. Kati ya wanachuo hao, wasichana walikuwa 9,934 (asilimia 58.7) na wavulana walikuwa 14,138 (asilimia 41.3). Aidha, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu visivyo vya Serikali ilikuwa 11,573 mwaka 2013 ikilinganishwa na wanachuo 16,632 mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 30.4. Kati ya wanachuo hao, wasichana walikuwa 4,942 (asilimia 42.7) na wavulana walikuwa 6,631 (asilimia 58.3). Udahili wa wanafunzi katika vyuo vya ualimu ulishuka kutokana na kutopatikana kwa wahitimu wa kidato cha sita wenye sifa za kujiunga na mafunzo ya stashahada katika masomo ya sayansi na hisabati.

**Elimu ya Watu Wazima na Mfumo Usio Rasmi**

426. Mwaka 2013, idadi ya wananchi walioshiriki katika Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Waliokosa (MEMKWA) wenye umri wa miaka 11 hadi 18 ilipungua kwa asilimia 29.7 kutoka washiriki 76,867 mwaka 2012 hadi 54,029. Kati ya hao, wanaume walikuwa 28,836 sawa na asilimia 53.4 na wanawake walikuwa 25,193, sawa na asilimia 46.6 ikilinganishwa na washiriki wanaume 41,241 (asilimia 53.7) na wanawake 35,626 (asilimia 46.3) mwaka 2012. Idadi ya washiriki wa MEMKWA imeendelea kupungua kutokana na wazazi kuhamasika kuandikisha wanafunzi katika darasa la kwanza hasa watoto wa rika lengwa (miaka 7) katika shule za msingi.

427. Mwaka 2013, idadi ya wananchi walioshiriki katika Mpango wa Uwiano kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) ilipungua kwa asilimia 6.9 kutoka washiriki 907,771 mwaka 2012 hadi washiriki 845,380. Kati ya hao, wanaume walikuwa 401,260, sawa na asilimia 47.5 na wanawake walikuwa 444,120, sawa na asilimia 52.9 ikilinganishwa na washiriki wanaume 434,466 (asilimia 47.9) na wanawake 473,305 (asilimia 52.1) mwaka 2012.

**Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

428.Mwaka 2013, Serikali iliendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za elimu ili kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora kwa wanafunzi katika shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Mwaka 2012/2013, jumla ya shule/vyuo/taasisi/asasi 6,404 za elimu zilikaguliwa ikilinganishwa na shule/vyuo/taasisi/asasi 6,081 zilizokaguliwa mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 5.3. Aidha, idadi ya shule/vyuo/taasisi/asasi zilizokaguliwa ilikuwa asilimia 33.5 ya lengo lililokusudiwa la kukagua shule/vyuo/taasisi/asasi 19,095. Malengo ya ukaguzi hayakufikiwa kutokana na upungufu wa vitendea kazi hususan vyombo vya usafiri kuwawezesha wakaguzi kuzifikia shule/taasisi/asasi/vyuo vinavyotoa elimu nchini.

**Jedwali 19.1: Ukaguzi wa Taasisi za Elimu katika mwaka 2013**

| Taasisi/Shule/Vituo /Vyuo | Idadi ya Taasisi/ Asasi June, 2013 | Idadi iliyolengwa kukaguliwa | Idadi halisi iliyokaguliwa | Kiwango cha utekelezaji (% ya idadi iliyokaguliwa) |
|---|---|---|---|---|
| Elimu ya Awali | 14,283 | 6,166 | 2,026 | 32.9 |
| Shule ya Msingi | 16442 | 7,165 | 2,682 | 37.4 |
| Elimu ya Ufundi | 319 | 88 | 15 | 17.0 |
| Elimu ya Maalumu | 242 | 87 | 11 | 12.6 |
| Elimu ya Watu Wazima | 12,124 | 3,663 | 777 | 21.2 |
| Shule za Sekondari | 4576 | 1,815 | 833 | 45.9 |
| Vyuo vya Ualimu | 119 | 111 | 60 | 54.1 |
| **Jumla Kuu** | **48,105** | **19,095** | **6,404** | **33.5** |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

**Elimu ya Ufundi na Mafunzo**

429.Mwaka 2012/2013, idadi ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ilikuwa 324 ikilinganishwa na vyuo 248 mwaka 2011/2012 sawa na ongezeko la asilimia 30.2. Kati ya vyuo hivyo, vyuo 229 ni vya Serikali wakati vyuo 94 vinamilikiwa na sekta binafsi. Aidha, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo iliongezeka kufikia wanafunzi 113,080 mwaka 2012/2013 kutoka wanafunzi 112,447 mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 0.6. Kati

yao, wanafunzi 59,847 (asilimia 52.9) walikuwa wanaume na wanafunzi 53,233 (asilimia 47.1) walikuwa wanawake.

**Elimu ya Ufundi Stadi**

430. Mwaka 2012/2013, idadi ya vyuo vya ufundi stadi ilikuwa 744 ikilinganishwa na vyuo 750 mwaka 2011/2012, sawa na upungufu wa asilimia 0.8. Kati ya hivyo, vyuo 144 ni vya Serikali na vyuo 600 vinamilikiwa na sekta binafsi. Hii inaonyesha kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa elimu ya ufundi stadi. Kupungua kwa idadi ya vyuo kulitokana na baadhi ya vyuo hivyo kushindwa kufikia vigezo vya ubora vilivyowekwa na hivyo kuzuiliwa kuendesha mafunzo. Aidha, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi iliongezeka kwa asilimia 19.2 kufikia wanafunzi 144,628 mwaka 2012/2013 kutoka wanafunzi 121,348 mwaka 2011/2012. Kati yao, wanaume walikuwa 77,855 sawa na asilimia 53.8 ya wanafunzi wote wakati idadi ya wanawake ilikuwa 66,773 sawa na asilimia 46.2 ya wanafunzi wote waliosajiliwa mwaka 2012/2013.

**Elimu ya Juu**

431. Mwaka 2012/13, idadi ya vyuo vikuu ilikuwa 50 ikilinganishwa na vyuo 45 mwaka 2011/12. Kati ya hivyo, vyuo vikuu vya Serikali vilikuwa 14, sawa na asilimia 28, ambapo vyuo vikuu binafsi vilikuwa 36 sawa na asilimia 72. Aidha, idadi ya wanafunzi wote waliokuwa katika vyuo vikuu vya Serikali na visivyo vya Serikali iliongezeka kwa asilimia 22.6 kutoka wanafunzi 166,484 mwaka 2011/2012 hadi wanafunzi 204,175 mwaka 2012/13. Kati ya hao, wanafunzi wa kike walikuwa 74,498 sawa na asilimia 36.5 ya wanafunzi wote katika mwaka 2012/13.

432. Mwaka 2012/2013, idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu vya Serikali iliongezeka kwa asilimia 12.2 kufikia wanafunzi 128,471 kutoka wanafunzi 114,531 mwaka 2011/2012. Kati ya hao, wanafunzi 42,534 sawa na asilimia 33.1 ni wa kike. Aidha, idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu visivyo vya Serikali iliongezeka kwa asilimia 15.9 kutoka wanafunzi 51,953 mwaka 2011/2012 hadi wanafunzi 60,207 mwaka 2012/13. Kati ya hao, wanafunzi 24,794, sawa na asilimia 41.2 ni wa kike.

433. Mwaka 2012/2013, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu ilitoa mikopo kwa wanafunzi 96,625 yenye thamani ya shilingi bilioni 335.07 ikilinganishwa na wanafunzi 94,773 waliopata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 317.79 mwaka 2011/2012. Aidha, kasi ya urejeshwaji mikopo iliendelea kuongezeka ambapo mwaka 2012/2013, Bodi ya Mikopo ilikusanya shilingi bilioni 14.85 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11.508 zilizokusanywa mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 29.0. Kwa ujumla, urejeshwaji wa mikopo hadi Desemba, 2013 ulikuwa asilimia 67.8 ambapo jumla ya shilingi bilioni 43.01 zilirejeshwa kati ya shilingi bilioni 63.44 zinazostahili kurejeshwa kwa kipindi hicho.

434. Changamoto zinazohusiana na mikopo ya elimu ya juu ni pamoja na: Kutokueleweka vema kwa sera ya uchangiaji wa gharama za elimu ya juu; mtazamo potofu kuwa fedha zinazotolewa na Serikali ni ruzuku badala ya mkopo; baadhi ya vyuo vikuu hususan vya binafsi kupandisha ada ya mafunzo kwa lengo la kupata fedha zaidi; baadhi ya waajiri kutokutoa ushirikiano katika kutoa taarifa za wafanyakazi waliosomeshwa kwa fedha za mkopo; na ugumu wa kuthibitisha taarifa za waombaji ili kubaini uwezo wao wa kumudu au kutokumudu gharama za elimu ya juu.

## SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 80 (Namba)

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1986 | 10789 | 9855 | 8401 | 8679 | 2363 | 2276 | 42363 |
| 1987 | 11626 | 10870 | 9528 | 9162 | 2313 | 2322 | 45821 |
| 1988 | 14258 | 11195 | 10373 | 9180 | 2313 | 2240 | 49559 |
| 1989 | 16034 | 14815 | 11275 | 10018 | 2980 | 2360 | 57482 |
| 1990 | 18654 | 16340 | 14199 | 11157 | 3777 | 2859 | 66986 |
| 1991 | 18892 | 18679 | 15459 | 13915 | 3646 | 3355 | 73946 |
| 1992 | 19299 | 19443 | 17044 | 14864 | 4136 | 3874 | 78660 |
| 1993 | 20267 | 20110 | 17597 | 16713 | 4261 | 4016 | 82964 |
| 1994 | 21589 | 19823 | 17513 | 16474 | 4179 | 3863 | 83441 |
| 1995 | 25200 | 22237 | 19118 | 17067 | 4541 | 3903 | 92066 |
| 1996 | 28289 | 23874 | 20197 | 16468 | 4528 | 4035 | 97391 |
| 1997 | 32043 | 29748 | 23810 | 19697 | 6412 | 4846 | 116556 |
| 1998 | 37094 | 31218 | 24925 | 21182 | 5163 | 4748 | 124330 |
| 1999 | 39144 | 36682 | 28589 | 23996 | 6305 | 5248 | 139964 |
| 2000 | 43643 | 36734 | 31132 | 25456 | 6654 | 6143 | 149762 |
| 2001 | 47204 | 45078 | 30531 | 29188 | 7198 | 6601 | 165800 |
| 2002 | 56101 | 50371 | 36989 | 29045 | 7711 | 7126 | 187343 |
| 2003 | 52863 | 60643 | 36906 | 35653 | 7780 | 6885 | 200730 |
| 2004 | 98738 | 67294 | 46546 | 36385 | 8353 | 7572 | 264888 |
| 2005 | 134963 | 109398 | 46188 | 46489 | 9710 | 8444 | 355192 |
| 2006 | 196391 | 151448 | 72167 | 42584 | 18211 | 9691 | 490492 |
| 2007 | 401011 | 218060 | 105770 | 70796 | 21789 | 11668 | 829094 |
| 2008 | 395930 | 332393 | 175353 | 95214 | 25240 | 11743 | 1035873 |
| 2009 | 480529 | 308131 | 159789 | 167355 | 31201 | 12695 | 1159700 |
| 2010 | 382207 | 398870 | 293519 | 279995 | 26065 | 20674 | 1401330 |
| 2011 | 403873 | 396724 | 380528 | 279117 | 30265 | 25164 | 1515671 |
| 2012 | 457321 | 386250 | 355740 | 343376 | 31206 | 28859 | 1602752 |
| 2013 | 444532 | 506036 | 193901 | 302963 | 30581 | 26698 | 1504711 |
| Badiliko (% ) | | | | | | | |
| 2012 - 2013 | -2.8 | 31.0 | -45.5 | -11.8 | -2.0 | -7.5 | -6.1 |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

**IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA**

Jedwali 80A

| | 2010 | | | 2011 | | | 2012 | | | 2013 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Waume | Wake | Jumla | Waume | Wake | Jumla | Waume | Wake | Jumla | Waume | Wake | Jumla |
| **I. Elimu ya Awali** | | | | | | | | | | | | |
| Jumla ya Wanafunzi walioandikishwa mwaka I&II | 461628 | 463837 | 925465 | 538478 | 530730 | 1069208 | 530425 | 504304 | 1034729 | 512798 | 513668 | 1026466 |
| Walioandikishwa Mwaka I&II madarasa ya Awali shule za Serikali | 440202 | 443465 | 883667 | 502187 | 494894 | 997081 | 504935 | 480125 | 985060 | 483720 | 485963 | 969683 |
| Walioandikishwa Mwaka I&II madarasa ya Awali shule zisizo za Serikali | 21426 | 20372 | 41798 | 36291 | 35836 | 72127 | 25490 | 24179 | 49669 | 29078 | 27705 | 56783 |
| Jumla ya Walimu wenye Sifa | 359 | 1269 | 1628 | 286 | 1225 | 1511 | 256 | 1200 | 1456 | 1656 | 3205 | 4861 |
| Madarasa ya Awali Shule za Serikali | 128 | 1205 | 1333 | 149 | 1409 | 1558 | 175 | 1464 | 1639 | 243 | 1401 | 1644 |
| Madarasa ya Awali Shule za Zisizo za Serikali | 487 | 2474 | 2961 | 435 | 2634 | 3069 | 431 | 2664 | 3095 | 1899 | 4606 | 6505 |
| **II. Elimu ya Msingi** | | | | | | | | | | | | |
| Jumla ya wanafunzi wote walioandikishwa Darasa la I-VII | 4203269 | 4216036 | 8419305 | 4159740 | 4203646 | 8363386 | 4086280 | 4160892 | 8247172 | 4066287 | 4165626 | 8231913 |
| Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za serikali Darasa la I-VII | 4127500 | 4139526 | 8267026 | 4076899 | 4123752 | 8200651 | 3970502 | 4049246 | 8019748 | 3965572 | 4068354 | 8033926 |
| Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa la I-VII | 75769 | 76510 | 152279 | 82841 | 79894 | 162735 | 115778 | 111646 | 227424 | 100715 | 97272 | 197987 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi | 82170 | 83686 | 165856 | 86098 | 89351 | 175449 | 87601 | 93386 | 180987 | 91253 | 98234 | 189487 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi za serikali | 78331 | 80750 | 159081 | 81262 | 85849 | 167111 | 82541 | 89445 | 171986 | 85525 | 93797 | 179322 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi za binafsi | 3839 | 2936 | 6775 | 4836 | 3502 | 8338 | 5060 | 3941 | 9001 | 5728 | 4437 | 10165 |
| **III. Elimu ya Sekondari** | | | | | | | | | | | | |
| Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI | 910171 | 728528 | 1638699 | 986993 | 802554 | 1789547 | 1010473 | 873799 | 1884272 | 939191 | 864865 | 1804056 |
| Wanafunzi wanaosoma katika shule za serikali, kidato I-VI | 792974 | 608356 | 1401330 | 854739 | 660932 | 1515671 | 875480 | 727272 | 1602752 | 796895 | 707816 | 1504711 |
| Wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI | 117197 | 120172 | 237369 | 132254 | 141622 | 273876 | 134993 | 146527 | 281520 | 142296 | 157049 | 299345 |
| Idadi ya walimu katika shule za serikali | 19666 | 10586 | 30252 | 26635 | 13299 | 39934 | 33643 | 17826 | 51469 | 37291 | 20737 | 58028 |
| Idadi ya walimu katika shule za binafsi | 8155 | 2110 | 10265 | 9722 | 2490 | 12212 | 10881 | 2736 | 13617 | 12261 | 3118 | 15379 |
| Jumla ya Walimu katika shule za Sekondari | 27821 | 12696 | 40517 | 36357 | 15789 | 52146 | 44524 | 20562 | 65086 | 49552 | 23855 | 73407 |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

## IDADI YA TAASISI ZA ELIMU

Jedwali 80 B

| Aina ya Taasisi | 2009 | | 2010 | | | 2011 | | | 2012 | | | 2013 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Binafsi** | **Jumla** | **Serikali** | **Binafsi** | **Jumla** | **Serikali** | **Binafsi** | **Jumla** | **Serikali** | **Binafsi** | **Jumla** | **Serikali** | **Binafsi** | **Jumla** |
| Shule za Msingi | 426 | 15727 | 15265 | 551 | 15816 | 15412 | 589 | 16001 | 15525 | 806 | 16331 | 15576 | 767 | 16343 |
| Shule za Sekondari | 819 | 4102 | 3397 | 869 | 4266 | 3425 | 942 | 4367 | 3508 | 1020 | 4528 | 3528 | 1048 | 4576 |
| Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari) | 43 | 77 | 34 | 58 | 92 | 34 | 69 | 103 | 34 | 71 | 105 | 34 | 92 | 126 |
| Elimu ya Ufundi na Mafunzo | | | | | | 103 | 569 | 672 | 109 | 641 | 750 | 113 | 631 | 744 |
| **Jumla** | **1288** | **19906** | **18696** | **1478** | **20174** | **18974** | **2169** | **21143** | **19176** | **2538** | **21714** | **19251** | **2538** | **21789** |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

## MAFUNZO YA WALIMU KATIKA VYUO VYA UALIMU

Jedwali 80C

| KIWANGO | 2009 | | | 2010 | | | 2011 | | | 2012 | | | 2013 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Waume** | **Wake** | **Jumla** | **Waume** | **Wake** | **Jumla** | **Waume** | **Wake** | **Jumla** | **Waume** | **Wake** | **Jumla** | **Waume** | **Wake** | **Jumla** |
| Stashahada (Pre-Service) | 5646 | 3642 | 9288 | 8695 | 5982 | 14677 | 7222 | 4360 | 11582 | 7552 | 4808 | 12360 | 7188 | 4331 | 11519 |
| Astashahada (In - service) | 1489 | 679 | 2168 | 1873 | 1191 | 3064 | 1071 | 551 | 1622 | 729 | 327 | 1056 | 674 | 318 | 992 |
| Daraja A | 11078 | 12797 | 23875 | 9145 | 9296 | 18441 | 11905 | 12137 | 24042 | 14044 | 11582 | 25626 | 12855 | 10120 | 22975 |
| Elimu maalum | 5 | 21 | 26 | 338 | 128 | 466 | 187 | 265 | 452 | 17 | 34 | 51 | 52 | 107 | 159 |
| Mafunzo Kazini B/C-A | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **18218** | **17139** | **35357** | **20051** | **16597** | **36648** | **20385** | **17313** | **37698** | **22342** | **16751** | **39093** | **20769** | **14876** | **35645** |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

**IDADI YA WANAFUNZI NA WAKUFUNZI KATIKA VYUO VIKUU KWA MWAKA 2012/2013**

Jedwali 80D

| JINA LA CHUO | UMILIKI | Idadi ya Wanafunzi | | | Idadi ya Walimu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KE | ME | JUMLA | ME | KE | JUMLA |
| Aga Khan UUniversity (AKU) | Binafsi | 51 | 45 | 96 | 11 | 16 | 27 |
| TABORA) | Binafsi | 91 | 197 | 288 | - | - | - |
| Ardhi University (ARU) | Serikali | 1181 | 2732 | 3913 | 186 | 47 | 233 |
| Catholic University of Health and Allied Science (CUHAS) | Binafsi | 438 | 845 | 1283 | 87 | 19 | 106 |
| Dar Es SalaamUniversity College of Education (DUCE) | Serikali | 1296 | 2092 | 3388 | 121 | 68 | 189 |
| EcknifordeTanga University ( ETU) | Binafsi | 482 | 647 | 1129 | 14 | 7 | 21 |
| Hubert Kairuki Memorial Univesity (HKMU) | Binafsi | 55 | 73 | 128 | 24 | 16 | 40 |
| International Medical and Technology University (IMTU) | Binafsi | 446 | 542 | 988 | 58 | 28 | 86 |
| Iringa University College (IUCO) | Binafsi | 1923 | 2338 | 4261 | 87 | 36 | 123 |
| (JKUAT- ARUSHA) | Binafsi | 93 | 133 | 226 | 42 | 17 | 59 |
| Jordan University College (JUCO) | Binafsi | 889 | 1465 | 2354 | 59 | 10 | 69 |
| Josiah Kibira University College (JOKUCO) | Binafsi | 104 | 276 | 380 | 8 | 3 | 11 |
| Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC) | Binafsi | 602 | 857 | 1459 | - | - | - |
| Kampala International University (KIU) | Binafsi | 1236 | 1657 | 2893 | 89 | | 125 |
| Mount Meru University (MMU) | Binafsi | 649 | 1045 | 1694 | 63 | 33 | 96 |
| Mzumbe University (MU) | Serikali | 3535 | 4309 | 7844 | 218 | 74 | 292 |
| Bussiness Studies (MUCCOBS) | Serikali | 1968 | 2516 | 4484 | - | - | - |
| Mkwawa University College of Education (MUCE) | Serikali | 959 | 1609 | 2568 | 83 | 31 | 114 |
| Makumira University College (MUCO) | Binafsi | 1059 | 2132 | 3191 | 52 | 14 | 66 |
| Muhimbili University of Allied Science (MUHAS) | Serikali | 1082 | 1987 | 3069 | 96 | 43 | 139 |
| Muslim University of Morogoro (MUM) | Binafsi | 1050 | 1670 | 2720 | 42 | 4 | 46 |
| Mbeya University of Science and Technology (MUST) | Serikali | 509 | 2645 | 3154 | 140 | 18 | 158 |
| Mwenge University College of Ecudation (MWUCE) | Binafsi | 719 | 1254 | 1973 | 77 | 25 | 102 |
| Nelson Mandela African Insitute of Technology (NM-AIST) | Serikali | 43 | 166 | 209 | 36 | 11 | 47 |
| The Open University of Tanzania (OUT) | Binafsi | 18372 | 43488 | 61860 | 227 | 127 | 354 |
| Ruaha University College (RUCO) | Binafsi | 1746 | 3565 | 5311 | 78 | 44 | 122 |
| St. Augustine University of Tanzania (SAUT) | Binafsi | 7209 | 6746 | 13955 | 203 | 100 | 303 |
| Sebastian Kulowa Univesity College (SEKUCO) | Binafsi | 907 | 542 | 1449 | 48 | 18 | 66 |
| (SFUCHAS) | Binafsi | 83 | 226 | 309 | 11 | 5 | 16 |
| (SJCOAST) | Binafsi | 56 | 110 | 166 | - | - | - |
| St. Joseph College of Engineering and Technology (SJOCET) | Binafsi | 350 | 1994 | 2344 | 93 | 32 | 125 |
| St. Joseph Collegy of Information Technology (SJOCIT) | Binafsi | 137 | 635 | 772 | 18 | 3 | 21 |
| St. Joseph College of Management and Finance (SJCoMF) | Binafsi | 3 | 19 | 22 | 6 | 1 | 7 |
| St. John's University fo Tanzania (SJUT) | Binafsi | 3685 | 3745 | 7430 | 79 | 33 | 112 |
| Stefano Moshi Memorial University College (SMMUC) | Binafsi | 146 | 42 | 188 | - | - | - |
| Stela Maris Mtwara University College (SMMUCO) | Binafsi | 793 | 1665 | 2458 | - | - | - |
| Sokoine University of Agriculture (SUA) | Serikali | 2600 | 5473 | 8073 | - | - | - |
| State University of Zanzibar (SUZA) | Serikali | 536 | 355 | 891 | 76 | 42 | 118 |
| Theofilo Kisanji University (TEKU) | Binafsi | 2881 | 4702 | 7583 | 47 | 12 | 59 |
| Tumaini University Dar Es Salaam College (TUDARCO) | Binafsi | 1026 | 1005 | 2031 | 38 | 18 | 56 |
| The United African University of Tanzania (UAUT) | Binafsi | 0 | 9 | 9 | 14 | 1 | 15 |
| University College of Education Zanzibar (UCEZ) | Binafsi | 763 | 644 | 1407 | - | - | - |
| University of Dodoma (UDOM) | Serikali | 5009 | 9250 | 14259 | 457 | 141 | 598 |
| Universifty of Dar Es Salaam (UDSM) | Serikali | 5444 | 9315 | 14759 | 927 | 253 | 1180 |
| University of Arusha (UoA) | Binafsi | 1128 | 1623 | 2751 | 8 | 2 | 10 |
| University of Bagamoyo (UoB) | Binafsi | 113 | 185 | 298 | 41 | 7 | 48 |
| Zanzibar University (ZU) | Binafsi | 1051 | 1107 | 2158 | 25 | 5 | 30 |
| **Jumla kuu** | | **74,498** | **129,677** | **204,175** | **3,989** | **1,364** | **5,389** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

- Takwimu hazikupatikana

## SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 81 (Namba)

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1986 | 12625 | 12389 | 11895 | 10073 | 730 | 567 | 48279 |
| 1987 | 15709 | 15526 | 13188 | 12245 | 801 | 756 | 58225 |
| 1988 | 18007 | 18897 | 15326 | 14358 | 966 | 702 | 68256 |
| 1989 | 20789 | 19279 | 18415 | 14759 | 1045 | 716 | 75003 |
| 1990 | 23585 | 21870 | 17599 | 17685 | 1481 | 1094 | 83314 |
| 1991 | 27554 | 25143 | 19237 | 17371 | 1922 | 1639 | 92866 |
| 1992 | 29027 | 27044 | 19378 | 17891 | 2018 | 1758 | 97116 |
| 1993 | 25703 | 27651 | 21894 | 18367 | 2223 | 2097 | 97935 |
| 1994 | 28657 | 26971 | 22784 | 19809 | 2573 | 2011 | 102805 |
| 1995 | 28498 | 26242 | 24098 | 21199 | 2334 | 1938 | 104309 |
| 1996 | 28002 | 25807 | 22494 | 20318 | 3168 | 2243 | 102032 |
| 1997 | 29768 | 27461 | 22406 | 20627 | 3408 | 3381 | 107051 |
| 1998 | 27125 | 24756 | 22029 | 20409 | 4826 | 3428 | 102573 |
| 1999 | 28333 | 25747 | 23120 | 20255 | 5667 | 4493 | 107615 |
| 2000 | 30789 | 26601 | 23469 | 20430 | 5894 | 5011 | 112194 |
| 2001 | 36305 | 30820 | 25004 | 20762 | 5892 | 5116 | 123899 |
| 2002 | 41593 | 34209 | 27540 | 20681 | 6418 | 5534 | 135975 |
| 2003 | 46891 | 38506 | 26385 | 21650 | 6430 | 4859 | 144721 |
| 2004 | 48752 | 46167 | 33240 | 24476 | 8847 | 6229 | 167711 |
| 2005 | 45276 | 46321 | 32063 | 29248 | 9183 | 7046 | 169137 |
| 2006 | 46968 | 48013 | 42878 | 29796 | 9569 | 7956 | 185180 |
| 2007 | 47437 | 46927 | 41340 | 35746 | 11299 | 8667 | 191416 |
| 2008 | 42971 | 43232 | 43177 | 35980 | 12576 | 8594 | 186530 |
| 2009 | 44255 | 36384 | 37064 | 34061 | 11851 | 9096 | 172711 |
| 2010 | 56620 | 57876 | 50778 | 46820 | 12269 | 13006 | 237369 |
| 2011 | 63282 | 67205 | 65859 | 54521 | 11083 | 11926 | 273876 |
| 2012 | 65058 | 69403 | 64453 | 61209 | 9684 | 11713 | 281520 |
| 2013 | 70060 | 77407 | 67998 | 65637 | 8592 | 9651 | 299345 |
| Badiliko (% ) | | | | | | | |
| 2012 - 2013 | 7.7 | 11.5 | 5.5 | 7.2 | -11.3 | -17.6 | 6.3 |

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

# SURA YA 20

# AFYA

## Utangulizi

435.Mwaka 2013, Serikali iliendelea na uratibu na utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii ili kuwapunguzia wananchi tatizo la maradhi. Hii inalenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya zenye ubora na viwango stahiki na zinazowafikia wananchi wote kwa wakati. Aidha, katika mwaka 2013 Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) uliendelea kutekelezwa kulingana na mpango kazi wake. Vilevile, mitaala ya kufundishia watalaam mbalimbali wa kada za afya ilipitiwa na kuboreshwa ili iendane na wakati na mahitaji. Huduma za afya ya uzazi na mtoto ziliendelea kupewa kipaumbele ili kuhakikisha vifo vya akina mama na watoto vinapungua kwa kiasi kikubwa. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kuhakikisha kuwa mifumo ya ukusanyaji wa takwimu sahihi za sekta ya afya inaendelea kuimarishwa.

## Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya

436.Mwaka 2013, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya iliendelea kuvijengea uwezo wa kutoa huduma vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, Serikali katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi iliendelea kuongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya, kutoka vituo 6,663 mwaka 2012 hadi kufikia vituo 6,878 mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 3.2.

437.Mwaka 2013, jumla ya mahudhurio ya wagonjwa wa nje yalikuwa ni 52,458,810 ikilinganishwa na 50,806,868 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Kati ya mahudhurio hayo, 42,682,479 sawa na asilimia 81.4 yalikuwa katika zahanati, 6,873,056 sawa na asilimia 8.6 vituo vya afya, na 2,903,275 sawa na asilimia 5.5 yalikuwa katika hospitali. Ongezeko la mahudhurio ya wagonjwa kwenye zahanati lilitokana na ongezeko la zahanati kufuatia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi ya kuwa na zahanati katika kila kijiji ili kumnufaisha mwananchi na huduma muhimu za afya.

**Ukaguzi wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii**

438. Mwaka 2013, Serikali iliendelea kufanya ukaguzi wa vituo vya afya na vyuo vya ustawi wa jamii. Ukaguzi huo ulifanyika katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ilihusisha mikoa ya Mtwara, Lindi, Manyara, Katavi, Kagera, Iringa, Njombe na Pwani. Awamu ya Pili ilihusisha mikoa ya Arusha, Kigoma na Mwanza. Aidha, ilani na maelekezo mbalimbali yalitolewa ili kuboresha huduma.

**Matibabu nje ya nchi**

439. Mwaka 2013, jumla ya wagonjwa 488 walipelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kupata matibabu kutokana na matatizo mbalimbali ya kiafya yaliyoshindikana kupatiwa tiba hapa nchini kutokana na uhaba wa vifaa vya kisasa. Kati ya hao, wagonjwa wenye matatizo ya moyo walikuwa 212, saratani 45, figo 35 na magonjwa mengine 196.

**Elimu ya Afya kwa Wananchi**

440. Mwaka 2013, huduma za elimu ya afya kwa umma ziliendelea kutolewa kupitia vipindi vya redio, magazeti, vipeperushi, machapisho, mitandao ya simu, tovuti, magari ya kuelimisha na mabango yanayotoa elimu ya afya. Lengo kubwa lilikuwa ni kuwapa wananchi uwezo wa kutambua na kuzingatia mitindo bora ya maisha, hivyo kuepuka tabia hatarishi kwa afya kama matumizi ya tumbaku, unywaji wa pombe kupita kiasi, lishe duni, kutofanya mazoezi na msongo wa mawazo zinazopelekea magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama kisukari, matatizo ya moyo na saratani. Vile vile, vituo vya kutolea huduma ya afya viliendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza afya, kubadili tabia hatarishi kwa afya, kujikinga na maradhi, na kutumia huduma za afya pale inapobidi.

441. Mwaka 2013, Serikali iliendelea kusimamia na kuratibu ongezeko la wataalam kutoka vyuo vya afya. Idadi ya wataalam wa afya iliendelea kuimarika kutokana na ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo vya afya, kutoka wanafunzi 7,458 mwaka 2011/12 hadi wanafunzi 7,959 mwaka 2012/13. Ongezeko hili linaendana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi unaohitaji ongezeko la wataalam wa afya ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la zahanati na vituo vya afya nchini.

**Afya ya Uzazi na Mtoto**

442.Mwaka 2013, Serikali kwa kushirikiana na wadau iliendelea kutekeleza mpango mkakati wa kupunguza kasi ya vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto. Aidha, Serikali ilidhibiti kwa kiasi kikubwa milipuko ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo. Vile vile, Serikali iliendelea kukusanya sampuli za vipimo vya magonjwa ya ulemavu wa ghafla na vipimo vya surua kutoka wilayani kwa wagonjwa waliohisiwa kuwa na magonjwa hayo na kupimwa maabara. Vipimo vya magonjwa ya ulemavu wa ghafla na surua vilionesha kuwa salama, hali inayoonesha kuimarika kwa udhibiti wa magonjwa hayo hapa nchini.

443.Mwaka 2013, Serikali iliendelea kutoa huduma za uzazi wa mpango kwa kununua na kusambaza dawa na vifaa tiba kwa ajili ya kuwahudumia wananchi. Aidha, Serikali ilinunua na kusambaza vifaa katika vituo vya afya katika mikoa 16 nchini ili kumsaidia mtoto mchanga kupumua baada ya kuzaliwa. Vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na; *'Ambubags'* na *'Masks'* 7,153, '*penguine suckers'* 9,550, na '*Neonatalie model* 3,267. Lengo ni kuboresha upatikanaji wa vifaa hivyo muhimu kwa ajili ya kumsadia mtoto mchanga mwenye matatizo ya kupumua.

444.Mwaka 2013, Serikali ilianzisha mpango unaoitwa *'Option B plus'* unaolenga kuwapatia dawa za kupunguza makali ya VVU kwa wakati, kwa wajawazito wenye maambukizi ya VVU. Hii ni katika kutekeleza Mpango wa kutokomeza maambukizi mapya ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Aidha, mafunzo na warsha zilitolewa kwa watoa huduma na viongozi wa ngazi mbalimbali za mikoa na wilaya. Lengo lilikuwa ni kuwawezesha kuandaa mipango endelevu ya kutokomeza maambukizi mapya na kuiingiza katika mipango kabambe ya afya katika Halmashauri husika.

445.Mwaka 2013, Serikali katika kutekeleza mpango mkakati wa kitaifa wa kuzuia na kudhibiti saratani ya shingo ya kizazi, ilianzisha vituo 130 vya uchunguzi wa awali na matibabu ya ugonjwa huo katika mikoa 17 Tanzania Bara. Aidha, mwongozo wa kujumuisha katika vituo vya tiba ulizinduliwa na kituo cha mfano cha kutoa huduma kwa mfumo wa *'One Stop Centre'* kilizinduliwa katika Hospitali ya Amana.

**Mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria**

446. Mwaka 2013, Serikali ilitoa mafunzo kuhusu ugawaji na matumizi ya vyandarua vyenye viuatilifu vya muda mrefu kwa walimu wa shule za msingi na sekondari 4,481 na Maafisa elimu wa kata 426 wa mikoa ya majaribio ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Aidha, jumla ya vyandarua vyenye viuatilifu vya muda mrefu 179,359 viligawiwa kwa wanafunzi wa shule za msingi wa darasa la 1, 3, 5 na 7 na sekondari kidato cha I, III na IV katika mkoa wa Ruvuma (Songea mjini 30,725; Songea vijijini 22,764; Namtumbo 27,679 na Mbinga 62,795).

**Mpango wa Damu Salama**

447. Mwaka 2013, Serikali kupitia Mpango wa Damu Salama wa Taifa ulikusanya jumla ya chupa 120,000 za damu salama sawa na asilimia 60 ya lengo lililowekwa la kukusanya jumla ya chupa 200,000. Aidha, jumla ya hospitali 209 zilipewa damu salama kutoka katika vituo vya kanda vya damu salama. Vile vile, elimu iliendelea kutolewa kwa wananchi juu ya umuhimu wa tabia ya uchangiaji wa damu.

**Magonjwa ya kuambukiza na ya mlipuko**

448. Mwaka 2013, Serikali iliendelea na ufuatiliaji wa magonjwa ya kuambukiza na matukio ya kiafya yanayotokea katika jamii. Aidha, elimu ilitolewa kwa wataalamu wa afya ili kuimarisha uwezo wao katika kufanya ufuatiliaji wa magonjwa na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko. Vile vile, ulifanyika uimarishaji wa utambuzi na upokeaji wa taarifa za magonjwa ya mlipuko yaliyopo na yanayojitokeza katika maeneo mbalimbali kupitia mwongozo wa *'Integrated Disease Surveillance and Response (IDSR)'*. Katika kipindi hicho, Serikali ilikabiliana na magonjwa ya mlipuko wa Homa ya Dengue (Dar es Salaam), Homa ya uti wa mgongo (Rukwa), Surua (Mwanza, Mbeya, Arusha na Ruvuma) na Kipindupindu (Dar es Salaam, Tanga na Mbeya). Aidha, vifaa kinga na tiba kwa ajili ya matumizi wakati wa dharura vilitolewa kwa mikoa na wilaya. Seti ya vifaa kinga 15,000 ilipelekwa kwenye ofisi za kanda za MSD kwa ajili ya kusambazwa kwenye vituo vya afya.

**Chakula na Lishe**

449. Mwaka 2013, Serikali iliendelea kuimarisha juhudi za kukabiliana na utapiamlo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano ili kupunguza kasi ya maradhi na vifo vya watoto. Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa na kuchapisha mwongozo wa taifa kuhusu ulishaji watoto wachanga na wadogo. Aidha, Serikali iliendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu ulishaji

wa watoto kupitia vipindi 12 vya redio na nane vya televisheni. Vile vile, elimu ilitolewa kwa njia ya matangazo mafupi kupitia redio, televisheni na kusambaza vipeperushi. Katika kipindi hicho, Serikali kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe na wadau wengine hususan Mamlaka ya Chakula na Dawa ilikamilisha mchakato wa mapitio ya sheria inayodhibiti uuzaji na usambazaji wa maziwa na vyakula vya watoto wachanga ili kulinda afya na lishe za watoto. Sheria hii ilichapishwa katika Gazeti la Serikali la mwezi Machi 2013.

450.Mwaka 2013, Serikali kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania iliwapatia ‘chakula dawa’ watu wenye virusi vya UKIMWI na utapiamlo. Watu wenye virusi vya UKIMWI na watoto wenye umri chini ya miaka mitano walipimwa hali zao za lishe na waliobainika kuwa na utapiamlo waliingizwa kwenye programu ya chakula dawa. Programu hii inatekelezwa katika vituo vyote vya matunzo na tiba katika mikoa ya Arusha, Dodoma na Singida. Aidha, watoa huduma 2,530 walipata mafunzo ya jinsi ya kuchukua vipimo na kutoa chakula dawa kwa wagonjwa. Jumla ya watu 26,868 wanaoishi na virusi vya UKIMWI na watoto wadogo chini ya umri wa miaka mitano wenye utapiamlo walipata matibabu ya utapiamlo kwa kutumia chakula dawa. Watoa huduma waligawiwa machapisho mbalimbali (vijitabu na vipeperushi) pamoja na vitendea kazi kama vile utepe wa kupimia mzingo wa mkono kwa ajili ya kutambua hali ya lishe.

**Huduma za Ustawi wa Jamii**

451.Mwaka 2013, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi kwa wazee na watu wenye ulemavu. Huduma zilizotolewa ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa chakula, malazi na matibabu kwa watu wenye ulemavu wanaotunzwa na kulelewa katika makazi 17. Jumla ya wazee na watu wenye ulemavu wanaohudumiwa ni 1,135, wakiwemo wanaume 528 na wanawake 607 ambao walipatiwa huduma za msingi za chakula, malazi na mavazi. Aidha, Serikali iliratibu huduma za matunzo katika makazi 24 yanayoendeshwa na mashirika yasiyo ya kiserikali.

452.Mwaka 2013, Serikali iliendelea kutoa hifadhi, kutunza na kuwafanyia watoto marekebisho ya tabia katika mahabusu za watoto za Mbeya, Tanga, Dar Es Salaam, Moshi, Arusha na shule ya Maadilisho Irambo. Jumla ya watoto 617 walikinzana na sheria ikilinganishwa na watoto 578 mwaka 2012. Aidha, watoto hawa walipewa huduma za elimu ya msingi na ya ufundi katika fani mbalimbali kulingana na mahitaji yao.

## IDADI YA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Jedwali Na. 84

| Aina ya Vituo | 2011 | | | 2012 | | | 2013 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Binafsi | Serikali | Jumla | Binafsi | Serikali | Jumla | Binafsi | Serikali | Jumla |
| Zahanati | 1289 | 3843 | 5132 | 1358 | 4322 | 5680 | 1444 | 4469 | 5913 |
| Vituo vya Afya | 230 | 454 | 684 | 244 | 498 | 742 | 222 | 489 | 711 |
| Hospitali | 128 | 108 | 236 | 129 | 112 | 241 | 140 | 114 | 254 |
| **Jumla** | **1647** | **4405** | **6052** | **1731** | **4932** | **6663** | **1806** | **5072** | **6878** |

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

## HUDUMA ZA AFYA:  WALIOFAULU MAFUNZO

Jedwali 85

| Kada | Sehemu | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Waliofaulu Mafunzo ya Afya ya miaka miwili katika Ngazi ya Cheti** | | | | | | | | |
| Health Records | Kilimanjaro | 20 | 20 | 22 | 24 | 33 | 23 | 32 |
| Laboratory Assistant | Singida | 47 | 50 | 63 | 107 | 93 | 69 | 61 |
| Laboratory Assistant | Mvumi | 40 | 41 | 44 | 49 | 64 | 19 | 56 |
| Laboratory Assistant | Nkinga | 29 | 30 | 34 | 33 | 41 | 31 | 0 |
| Laboratory Assistant | Kolandoto | - | - | - | 42 | 54 | 70 | 69 |
| Laboratory Assistant | Litembo | - | - | - | 41 | 44 | 51 | 0 |
| Pharmaceutical Assistant - KSP | Kilimanjaro | 19 | 24 | 34 | 29 | 33 | - | - |
| Clinical Assistants | Songea | 40 | 45 | 47 | 63 | 69 | 57 | 43 |
| Clinical Assistants | Sumbawanga | 41 | 43 | 50 | 55 | 48 | 50 | 44 |
| Clinical Assistants | Masasi | 31 | 39 | 54 | 57 | 59 | 58 | 46 |
| Clinical Assistants | Kigoma | 29 | 27 | 37 | 40 | 41 | 36 | 20 |
| Clinical Assistants | Maswa | 39 | 41 | 83 | 66 | 81 | 91 | 0 |
| Clinical Assistants | Musoma | 35 | 35 | 47 | 58 | 50 | 41 | 40 |
| **Waliofaulu Mafunzo ya Afya ya miaka mitatu katika Stashahada** | | | | | | | | |
| Dental Therapy | Mbeya | 13 | 15 | 12 | 17 | 21 | 14 | 17 |
| Dental Therapy | Tanga | 20 | 15 | 15 | 21 | 23 | 17 | 14 |
| Dental Laboratory Technologists | Dar es salaam | 5 | 5 | 5 | 4 | 5 | - | - |
| Medical Laboratory Technicians | Dar es salaam | 35 | 37 | 54 | 55 | 57 | 52 | 53 |
| Medical Laboratory Technicians | Iringa | 15 | 14 | 46 | 54 | 55 | 51 | 0 |
| Medical Laboratory Technicians | Mwanza | 25 | 27 | 32 | 29 | 33 | 30 | 45 |
| Pharmaceutical Technician | Dar es salaam | 20 | 19 | 24 | 27 | 29 | 31 | - |
| Pharmaceutical Technician | Mwanza | 23 | 31 | 26 | 34 | 42 | 33 | 44 |
| Physiotherapy | Kilimanjaro | 17 | 18 | 17 | 28 | 26 | 15 | 14 |
| Optometry-KCMC | Kilimanjaro | 15 | 16 | 13 | 11 | 16 | 6 | - |
| Health Officers | Kagera | 33 | 35 | 50 | 36 | 65 | 36 | 62 |
| Health Officers | Kwimba | 31 | 33 | 49 | 41 | 43 | 38 | 30 |
| Health Officers | Mpwapwa | 15 | 16 | 21 | 29 | 31 | 32 | 36 |
| Health Officers | Tanga | 17 | 16 | 20 | 28 | 35 | 25 | 0 |
| Health Officers | Dar es salaam | 21 | 22 | 24 | 34 | 40 | 28 | 76 |

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

## IDADI YA VITANDA KATIKA HOSPITALI ZOTE NCHINI

Jedwali Na. 87

| Aina ya Huduma / Mwaka | Mmiliki | | | | | | | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | | Mashirika ya Kujitolea/Dini | | Mashirika ya Umma | | Binafsi | | | |
| | 2012 | 2013 | 2012 | 2013 | 2012 | 2013 | 2012 | 2013 | 2012 | 2013 |
| Hospitali | 15,697 | 16,726 | 14,677 | 14,843 | 800 | 920 | 1,187 | 1,133 | 32,361 | 33,622 |
| Vituo vya Afya | 8,766 | 9,168 | 5,286 | 5,791 | 271 | 294 | 800 | 880 | 15,123 | 16,133 |
| **Jumla** | **24,463** | **25,894** | **19,963** | **20,634** | **1,071** | **1,214** | **1,987** | **2,013** | **47,484** | **49,755** |

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

## SURA YA 21

## MAENDELEO YA JAMII

### Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

453. Mwaka 2013 Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilitoa mafunzo ya Ufundi Stadi ya muda mrefu na mfupi kwa wananchi 41,681 ikilinganishwa na wananchi 17,896 mwaka 2012. Kati ya hao, wanawake walikuwa 17,959 na wanaume walikuwa 23,722. Mafunzo yaliyotolewa yalikuwa katika fani za kilimo, ufundi na ujasiriamali. Aidha, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 25 vilitoa mafunzo ya mchepuo wa VETA.

454. Mwaka 2013, wanachuo 3,309 walihitimu mafunzo katika vyuo tisa vya Maendeleo ya Jamii nchini katika ngazi mbalimbali. Katika ngazi ya shahada ya uzamili, wanachuo 6 walihitimu ambapo wanawake walikuwa 3 na wanaume 3. Aidha, wanafunzi 173 walihitimu katika ngazi ya shahada ikilinganishwa na wanafunzi 150 waliohitimu mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 15.3. Kati ya wahitimu hao, wanaume walikuwa 82 na wanawake 91. Katika ngazi ya Stashahada, jumla ya wanachuo 612 walihitimu ikilinganishwa na wanachuo 557 waliohitimu mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Kati ya hao, wanaume walikuwa 190 na wanawake 422. Katika ngazi ya cheti, wanachuo 2,516 walihitimu ikilinganishwa na wahitimu 2,073 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 21.3. Kati ya hao wanaume walikuwa 660 na wanawake 1,856. Kwa ujumla ongezeko la wahitimu lilitokana na jitihada za Serikali kuhamasisha umuhimu wa elimu.

### Jinsia na Maendeleo ya Wanawake

455. Mwaka 2013, Serikali iliendelea na mpango wa uingizaji wa masuala ya jinsia katika mipango, mikakati, sera na programu mbalimbali za kisekta. Katika kutekeleza mpango huo, masuala ya jinsia yalizingatiwa na wizara zinazotekeleza mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Aidha, Kamati ya kitaifa ya kuzuia na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu wa ngozi iliendelea kuratibu na kusimamia shughuli za kuzuia na kudhibiti vitendo vya ukatili dhidi yao. Vilevile, Serikali iliratibu maandalizi ya taarifa ya 7 na 8 ya Mkataba wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake. Maandalizi ya taarifa hiyo yaliwashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na watendaji wa madawati

ya Jinsia kutoka wizara mbalimbali, idara na wakala, asasi za kijamii 31 na maofisa maendeleo ya jamii 18.

**Benki ya Wanawake**

456.Benki ya wanawake Tanzania ilitoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake na wanaume nchini ambapo jumla ya shilingi milioni 9,163.9 zilitolewa kwa wateja 9,380. Kati ya hao, wanawake walikuwa 7,395, sawa na asilimia 79. Vile vile, Benki iliendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na uendeshaji wa biashara kwa wateja 8,858. Aidha, Benki ilipanua wigo wa shughuli zake kwa kufungua tawi eneo la Kariakoo, Mtaa wa Aggrey. Aidha, Benki ilifungua vituo vya kutolea mikopo katika Mikoa ya Dar es Salaam (Kawe, Airwing, Mbezi Luis, Tabata, Mbande, Makongo, Tegeta, Jet, Uamsho, Buza, Kurasini, Kijichi, Kipunguni, Kigamboni, Kongowe, Kibamba, Mabibo, Mbezi Kati, Polisi Ufundi, Banana, Ubungo, Kibangu na Kitunda); Pwani (Kibaha); Dodoma (Airport, Chamwino, Ipagala, Posta, Hazina Kikuyu, Kizota, Savanna Kikuyu, Chang'ombe, Mnadani, Veyula, Mpwapwa, Kongwa na Mbande); na Mwanza (Nyakato, Igogo, Nyegezi, Pansiansi, Igoma, Kisesa, Magu, Misungwi na Kitangiri).

**Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake**

457.Mwaka wa fedha 2013/14, Serikali ilitenga shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Katika kipindi cha Julai – Desemba 2013, Wizara ilikuwa imepokea shilingi 515,628,846 kutoka Wizara ya Fedha. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, shilingi 347,000,000 sawa na 62% zilipelekwa katika halmashauri 31 za Kilindi, Muheza, Ikungi, Meatu, Msalala, Shinyanga Manispaa, Songea manispaa, Mkuranga, Makete, Ukerewe, Nanyumbu, Mtwara Mikindani, Tandahimba, Masasi, Gairo, Kilosa, Mbeya Jiji, Babati Mji, Kilwa, Lindi Manispaa, Lindi H/W, Moshi Manispaa, Kilolo, Iringa H/W, Chemba, Bahi, Mpwapwa, Longido, Monduli, Mpanda Mji na Mbinga kwa ajili ya kuwakopesha wanawake wajasiriamali kuendeshea biashara zao. Aidha, shilingi 103,125,769 zilitumika kwa ajili ya ufuatiliaji katika mikoa 9 ya Arusha, Manyara, Singida, Pwani, Tanga, Katavi, Rukwa, Morogoro na Kagera.

**Maendeleo ya Watoto**

458.Mwaka 2013, Serikali ilizindua rasmi Mtandao wa Mawasiliano wa Kusaidia Watoto ambao unafanya kazi kwa majaribio katika wilaya za Temeke,

Magu, Kasulu, Hai, Bukoba Vijijini na Musoma Mjini. Aidha, Mtandao huo unatarajiwa kuenezwa katika wilaya zote nchini. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa masuala ya watoto iliandaa na kuzindua Mpango Kazi wa Taifa wa miaka mitatu wa Kushughulikia Tatizo la Ukatili Dhidi ya Watoto (2013 – 2016). Lengo la Mpango Kazi huo ni kuhakikisha kuwa taasisi zote za kiserikali na zile zisizo za kiserikali zinatekeleza shughuli mbalimbali ambazo zitalenga kuondoa tatizo la ongezeko la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto hapa nchini.

**Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

459. Mwaka 2013, mashirika yasiyo ya kiserikali 617 yalipatiwa usajili chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005 ikilinganishwa na mashirika 692 yaliyosajiliwa mwaka 2012. Usajili huo mpya unafanya mashirika hayo kufikia 6,377 mwishoni mwaka 2013. Kati ya mashirika hayo yaliyosajiliwa mwaka 2013, mashirika 591 yalipatiwa cheti cha usajili na mengine 26 yalipatiwa cheti cha ukubalifu. Aidha, usajili huo unayawezesha mashirika husika kutambulika kisheria na kuongeza uhuru wa kujumuika katika jamii.

460. Mwaka 2013, mashirika yasiyo ya kiserikali yaliendelea kushiriki na kutoa mchango katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika kutathmini mchango wa mashirika hayo katika maendeleo ya nchi, Serikali iliandaa Taarifa ambayo ilionesha kuwa mashirika hayo yaliwekeza jumla ya shilingi milioni 524,526.5 katika nyanja mbalimbali ikiwemo kilimo, elimu, maji, afya, UKIMWI na Virusi Vya UKIMWI, mazingira, utawala bora, jinsia na ustawi kwa mwaka husika.

461. Mwaka 2013, uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali uliendelea kuimarishwa kwa kuwatumia maafisa maendeleo ya jamii wa wilaya na mikoa kutoa maoni ya maombi ya usajili wa mashirika hayo yaliyopo katika maeneo yao. Miongoni mwa vigezo vinavyotumika ili kupata usajili ni pamoja na kuhakikisha kuwa mashirika hayo yanakuwa na ofisi. Aidha, uwepo wa maafisa hao umesaidia kusogeza huduma za ushauri kuhusu usajili na uendeshaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali karibu na wananchi.